

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Thelathini - Tarehe 21 Julai, 2004

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira kwa Mwaka Ulilioishia Tarehe 30 Juni, 2003 (*The Annual Report and Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the year ended 30th June, 2003*).

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa Mwaka wa fedha Uliopita, Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 286

Matumizi ya Jina la Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA aliuliza:-

Kwa kuwa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere alifanya mambo mengi na makubwa na mema ndani na nje ya nchi kama vile kuwaunganisha Watanzania kujiona wamoja, kuweka misingi ya maendeleo kama shughuli za uchumi, elimu, afya, miundombinu lakini zaidi alikuwa Kiongozi Mashuhuri wa karne katika harakati za Ukombozi wa Afrika, kupinga unyanyasaji, ubaguzi, ukandamizaji wa aina yoyote popote duniani na hivyo kujijengea umaarufu ndani na nje ya Taifa letu:-

(a) Je, isingekuwa jambo la busara na la hekima kuhakikisha kuwa Jina hilo (Nyerere) linatajwa kila siku ndani na nje ya nchi kwa kuvipa jina lake vitu kama *Dar es Salaam International Airport* ikaitwa *Nyerere International Airport (NIA)* na *University of Dar es Salaam* kuitwa *Nyerere University*?

(b) Je, kuna utaratibu gani unaotumika katika uchongaji na uchoraji wa Sanamu ya Mwalimu Nyerere ili zionyeshe sura yake kamili kuliko ilivyo sasa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA aliijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi wakati nikijibu Swalii Na. 259 la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Wawi kuwa, kutunza kumbukumbu za nchi hususan za Waasisi wa Taifa ni jambo la msingi. Aidha, kwa sasa Serikali inaanadaa utaratibu wa Sheria utakaojenga mazingira ya kuwa na utamaduni wa kudumu wa kuthamini, kutunza na kudhibiti kumbukumbu za Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa ili kuhakikisha kuwa hazina waliyonayo viongozi wetu hawa haipotei na inakuwepo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Mapendelekezo ya Mheshimiwa Eliachim Simpasa, ni mazuri na Serikali imeyapokea na itayawasilisha kwa wadau mbalimbali likiwemo Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kupitia Muswada na kutunga Sheria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo ambayo Muswada utazingatia ni matumizi ya Jina la Baba wa Taifa. Muswada huu utaweka utaratibu wa matumizi sahihi ya majina ya Waasisi wa Taifa letu kwa kuhakikisha kwamba, majina yao hayatumiki kibiashara, hayadhalilishwi na hadhi yao haipotei. (*Makofii*)

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Serikali bado hajawa na utaratibu wa ithibati unaoongoza uchoraji wa picha au uchongaji wa sanamu, hivyo kupelekea watu mbalimbali wa ndani na nje ya nchi kuchora na kuchonga sanamu za Mwalimu Nyerere zisizoonyesha sura yake kamili. Utaratibu wa kuchora picha au kuchonga sanamu unatokana na fikra, uelewa na ujuzi katika fani ya sanaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inaandaa utaratibu wa Sheria, italifanyia kazi jambo hili ili pawepo na ithibati ya uchoraji picha na uchongaji sanamu zinazoonyesha sura sahihi za viongozi wetu kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi kwa Taifa letu na vizazi vijavyo.

MHE. ELIACHIM J. SIMPASA: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri lakini niulize maswali mawili madogo.

(a) Katika haya aliyotuahidi na najua utaratibu wa Serikali inaweza kuchukua muda sana, je, anatuhakikishia kwamba inaweza kuchukua muda mfupi iwezekanavyo sheria hiyo kuletwa na utaratibu uweze kuwekwa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sahihi za Mwalimu na Viongozi wengine?

(b) Kwa kuwa sasa kuna sanamu nimeziona mahali fulani na wenzetu wameziona ambazo kwa kweli hazifanani na hata picha kwenye noti ya Sh.1,000/= mimi sijui kama na yenyewe iko sawasawa, je, sasa kama ni sanamu mbaya mbaya ambazo tumeziona zinaweza kubomolewa ili tusahihishe makosa?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJEMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naamini haitachukua muda mrefu kwa sababu *process* ya kutayarisha Muswada ilishaanza. Nina imani pengine kabla ya mwaka huu wa 2204 kwisha au mapema mwaka 2005, sheria hii itapitishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sanamu, muda mfupi baada ya kifo cha Baba wa Taifa wataalam mbalimbali walialikwa kukagua sanamu ya Baba wa Taifa iliyotengenezwa na Mtaalam kutoka Urosi. Wataalam walioalikwa walitoka Baraza la Sanaa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Wizara ya Mambo ya Nje. Wataalam hao walifikia uamuzi kuwa sanamu haikuwa sahihi na sura ya Baba wa Taifa haikuwa sahihi. Hata hivyo, kulikuwa na sanamu iliyochongwa kule Tanga. Sanamu hiyo vile vile haikuwa sahihi na ilivunjwa na ikachongwa upya. Kwa hiyo, Serikali inapenda kuona kwamba, sura za viongozi wetu zinachongwa au zinachorwa kwa usahihi.

Na. 287

Ujenzi wa Kiwanda cha Mbolea za Chumvichumvi

MHE. PAUL P. KIMITI (k.n.y. MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tatu imejenga heshima kubwa kwa Makampuni na Mashirika ya Kitaifa/Kimataifa kuwekeza katika Taifa letu. Je, kumekuwa na ugumu gani katika kuyashawishi Mashirika/Makampuni hayo ili yakubali kujenga kiwanda cha kisasa cha mbolea nchini kwetu?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ya Awamu ya Tatu imejenga heshima kubwa kwa makampuni na Mashirika ya Kitaifa kuwekeza katika Taifa letu kwa ujumla. Kama inavyojulikana, ushawishi huu upo katika kuweka mazingira mazuri ya kiuchumi ili wanaofikiria kuwekeza waone urahisi wa kufanya hivyo. Katika kipindi kilichopita, hakuna mwekezaji makini aliyejitokeza aidha kufufua kiwanda cha zamani cha mbolea Tanga au kujenga kiwanda kipyä mahali pengine. Serikali inaendelea kuhamasisha makampuni ambayo yamekuwa yakifanya biashara ya mbolea ili yaweze kuwekeza katika uzalishaji wa mbolea nchini hasa ikizingatiwa kuwa nchi yetu inazo malighafi za mbolea ikiwemo gesi asili ya Songo Songo na machimbo ya madini ya *phosphate*. Malighafi hizo zinaweza kutumika kutengeneza mbolea ambazo zinaweza kufaa sana kwa udongo wa nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwekeza au kutowekeza litachukua sura kamili pale mwekezaji atakapojuwa faida ya kuwekeza katika mradi husika na baada ya kufanya upembuzi yakinifu na upembuzi huo kukubalika katika Mabenki yanayokopesha kwa vile wawekezaji wengi hutumia fedha za Mabenki kuanzisha miradi kama hiyo.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Waziri atakubaliana nami kwamba, moja ya matatizo ambayo Makampuni mengi na wawekezaji wengi wanayapata ni masharti magumu wanayopewa ili kuingia katika Mikataba hii?

Kiwanda cha Mbolea cha Tanga ambacho kimekuwepo kwa siku nyingi kingekuwa ni mfano mzuri wa kumpa mtu yejote hata kwa mpango wa dola moja, kwa nini tuisitumie nafasi hiyo ili angalau tukampata mwekezaji ambaye alionekana angeweza kupatikana ili kiwanda hiki kwa kushirikiana na Kiwanda cha Minjingu, kiendelee kutoa mbolea kwa ajili ya matumizi ya nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, hata ingebidi kukitoa Kiwanda cha Tanga bure tungekitoa lakini tumejitahidi kama tulivyojitahidi na Kiwanda cha *Southern Paper Mill* zaidi ya miaka 15, hatukupata mwekezaji yejote aliyejitokeza wala aliyetamani kuzalisha kwa kutumia

mitambo iliyokuwepo. *PSRC* ikaona matangi yanaharibika, mitambo inazidi kuoza, wakakiuza kiwanda hicho kwa *Kampuni ya Gulf Bulk Petroleum Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Spika, Serikali bado ina wazo la kutafatuta mwekezaji makini haswa kama nilivyosema katika swalii msingi kwamba tunayo gesi ya *Songosongo* na pia tunayo *phosphate* ya *Minjingu* ambayo tunaweza kuitumia kama malighafi ya kuanzisha Kiwanda hicho.

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa mwekezaji aliyenunua Kiwanda cha *Mbolea Tanga* amenunua eneo kubwa sana la zaidi ya heka 60 na heka hizi ziko mjini na kwa kuwa yeye kazi yake ni kuuza mafuta, je, Serikali haioni kwamba ingekuwa jambo la busara kama eneo hili lingegawiwa akachukua eneo tu ambalo linatosheleza kazi ambayo angehitaji kufanya? (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, aliyenunua Kiwanda cha zamani cha *Mbolea cha Tanga* amenunua *non-core assets*. Ukinunua *non-core assets*, mali ambayo siyo ya msingi, huna masharti ya kukiendeleza kiwanda kile. Ananunua eneo lile kwa madhumuni ya kufanya shughuli nyingine ndio maana huyu bwana anaendesha shughuli ya mafuta. Lakini kama alinunua eneo kubwa heka 60 ambazo yeye hazitumii, utaratibu upo wa kuwezesha sehemu moja ya eneo lile likatengwa kwa ajili ya shughuli nyingine na yeye akabakia na eneo ambalo kwa kweli anahitaji. Kinachotakiwa ni *Manispaa ya Tanga* iwasilishe maombi yake kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili waweze kuffikiriwa.

Na. 288

Vitambulisho vya Uraia

MHE. PARSEKO V. KONE (k.n.y. MHE. DR. BATILDA S. BURIAN) aliuliza:-

Kwa kuwa suala la vitambulisho vya uraia limekuwa likiulizwa Bungeni mara kwa mara na kwa kuwa majibu yanayotolewa hayatoi msimamo wa uhakika juu ya jambo hilo. Je, Serikali kwa mara nyingine tena, inatoa tamko gani la uhakika na kuuarifu umma wa *Tanzania* kwamba ni lini hasa vitambulisho vya uraia vitatolewa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, suala la kuwepo kwa vitambulisho vya uraia limekuwa likiulizwa mara kwa mara Bungeni, hii inatokana na umuhimu wa vitambulisho hivi kwa Taifa letu. Serikali inatambua umuhimu wa vitambulisho hivi katika ulinzi na usalama wa Wananchi, hasa ikizingatiwa kwamba,

vitambulisho vitasaidia kuwabaini wageni na kuwadhibiti. Serikali inayo azma ya kutengeneza vitambulisho vya uraia kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoeleza katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara yetu, hivi sasa Serikali imeamua kufanya upembuzi yakinifu kuhusu mradi huu kabla ya kutafuta mzabuni mwengine baada ya kuachana na mzabuni wa awali. Zoezi hili litafanyika ili kujiridhisha katika maeneo muhimu ya gharama zinazohitajika, pamoja na kujua mfumo mzuri wa utekelezaji na uendeshaji wa mradi. Ukosefu wa upembuzi yakinifu ndio uliosababisha mzabuni wa awali kubadilisha badilisha vigezo hadi tukatofautiana naye.

Hivyo, kutokana na ukweli huo, Serikali haijawa katika hali ya kuweza kutangaza kwa uhakika tarehe ya kupatikana kwa vitambulisho hivyo.

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba aueleze umma wa Tanzania hivi kuwapa vitambulisho ni hiari, hisani au ni haki ya raia wa Tanzania, kama ni haki Serikali itakubali kwamba haki inayoleweshwa ni haki inayokataliwa?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, vitambulisho ni jambo la muhimu katika nchi yetu, ni jambo ambalo linamtofautisha kwa urahisi raia na asiyekuwa raia. Ni jambo la muhimu na ndio maana Serikali tunakazana sana tupate vitambulisho kwa sababu ya umuhimu huo na kama nilivyoeleza, mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, tunafanya upembuzi yakinifu. Juzi mmepitisha hapa katika bajeti yetu Sh.163 milioni kwa ajili ya kazi hii. Kwa hiyo, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Watanzania kwamba, sasa hivi Serikali inakazana kabisa kabisa ili tupate vitambulisho kwa sababu ya umuhimu nilioutaja.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na napenda nimshukuru Waziri kwa majibu yake, nina swali dogo la nyongeza.

Kwa vile mwaka huu nchi yetu inaingia kwenye Daftari la Wapiga Kura na Daftari hilo linatengeneza vitambulisho na kuna nchi nyingi ambazo zinatumia Vitambulisho hivyo vya Kura kuwa kama multipurpose Identity Cards ili kupunguza gharama. Je, Serikali iko tayari kama hatua ya awali kuunganisha kazi hiyo ya vitambulisho iwe pamoja na vitambulisho vitakavyotolewa katika kadi za wapiga kura? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba mtu akishaandikishwa katika Daftari la Wapiga Kura na kupewa kile kipande cha kupigia kura moja kwa moja kinakuwa ndicho kitambulisho cha uraia. Haya ni mazoezi mawili tofauti. Awali tulitaka tuyauanganishe, yaende sambamba lakini tulivyofika katikati ikaonekana gharama zake ni kubwa sana. Wenzetu wa Tume ya

Uchaguzi wakawa na haraka wakasema mwakani kuna uchaguzi na ni hitaji la Kikatiba ikaonekana basi wao kwa fedha zilizopo watangulie. Nataka nikubali kwamba, baadhi ya taarifa ambazo wenzetu wa Tume ya Uchaguzi watazikusanya na sisi tutazitumia wakati tunaandaa kitambulisho cha uraia.

Na. 289

Uharibifu wa Mazingira Kutokana na Wakimbizi

MHE. MARGARETH J. BWANA (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA) aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imekuwa kimbilio la wakimbizi ambao kwa kiwango kikubwa sana wamechangia uharibifu wa mazingira katika Mikoa ya Rukwa, Kigoma, Tabora na Kagera na kwa kuwa kupokelewa kwa wakimbizi nchini Tanzania kunafanyika kwa niaba ya Umoja wa Mataifa:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kufanya tathmini ya gharama za uharibifu wa mazingira kwenye Mikoa inayohusika?

(b) Je, isingekuwa jambo la busara na la haki kwa Serikali kulipwa fidia itakayopelekwa kwenye Mikoa hiyo kwa lengo la kuanza kufufua mazingira ambayo uharibifu wake ni mkubwa?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Tanzania imekuwa kimbilio la wakimbizi ambao wamechangia uharibifu wa mazingira hasa katika Mikoa ya Rukwa, Kigoma, Tabora na Kagera. Nakubaliana pia na Mheshimiwa Mbunge kuwa, iko haja ya kufanya tathmini ya kiwango cha uharibifu wa mazingira uliofanyika na gharama ya kukarabati mazingira hayo yaliyoharibika. Mikoa ya Kigoma na Kagera iliwihi kufanya tathmini ya aina hii na Serikali ikishirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ilianzisha mradi wa hifadhi ya mazingira ulioitwa *Special Programme on Rehabilitation of Refugee Affected Area (SPRAA)*. Hivi sasa Wizara yangu tayari imeiandikia Mikoa yenye wakimbizi kufanya tathmini mpya ya uharibifu wa mazingira na kuandika michanganuo ya miradi ya hifadhi ya mazingira. Michanganuo hiyo itatumwa kujenga hoja kwa Jumuiya ya Kimataifa kusaidia kugharamia miradi hiyo kama ilivyofanywa kwa Mikoa ya Kigoma na Kagera huko nyuma.

(b) Mheshimiwa Spika, Mikataba ya Kimataifa kuhusu wakimbizi haina kipengele cha fidia ya hasara inayosababishwa na wakimbizi bali inahimiza Mataifa kusaidiana katika kubeba mzigo (*Burden Sharing*) wa kuhudumia wakimbizi ikiwa ni

pamoja na urekebishaji wa uharibifu wa mazingira unaotokana na ujio wa wakimbizi katika nchi zinazohifadhi wakimbizi. Tunatumia kipengele hiki katika kujenga hoja kwa Jumuiya ya Kimataifa ili iwajibike katika kufufua mazingira yaliyoharibiwa na wakimbizi katika nchi yetu.

MHE. MARGARETH J. BWANA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kama Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba kwa vile katika baadhi ya maeneo wanayotoka hawa wakimbizi katika hizo nchi zao ni shwari, je, kuna utaratibu wowote ule ambao unaweza kufanyika wakimbizi hao wakapelekwa kwenye maeneo hayo badala ya kuendelea kuletwa katika nchi zetu na kuendelea kufanya uharibifu kama wanavyoendelea kufanya hivi sasa?

(ii) Napenda nijue kama kuna utaratibu wowote aidha Serikali inaweza kuufanya wanapokuja wakimbizi katika nchi yetu wakaweza kugawanywa katika nchi za *East Africa* ili na wao waweze kuona na kupata uzoefu wa matatizo mbalimbali tunayopambana nayo hapa kwetu Tanzania ili kilio chetu kiwe kikubwa ili waweze kusaidia kufikia ufumbuzi wa pamoja kama nchi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kuhusu wakimbizi kurudi kwa sababu huko wanakotoka sasa nchi zao ni shwari, sina hakika sana na hilo kwa sababu kwa mfano, Burundi ambako tuna wakimbizi wengi sasa hivi hali inaendelea kuwa shwari lakini sio katika Mikoa yote, uko Mkoa mmoja ambao bado una matatizo. Kwa hiyo, wakimbizi wa Burundi sasa hivi wanarudi. Zamani walikuwa wanarudi kwa kutumia njia mbili, sasa hivi tumeshafungua njia nne wanarudi na wanaendelea kurudi lakini hali haijatulia sana kiasi hicho lakini tuna mategemeo kwamba, jinsi hali inavyotulia ndivyo wakimbizi wa Burundi watakavyozidi kurudi. Lengo letu sisi hali ikitulia mwaka huu wa 2004, wakimbizi wa Burundi wote warudi kwao.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunao wakimbizi kutoka *Congo DRC*. Kwa kipindi kirefu hali iliendelea kutulia, wale Wapinzani walishakubaliana na kwa kweli tulishaanza mazungumzo Serikali ya Tanzania na Congo waanze kurudi. Sasa juzi tena kule Congo Mashariki mmesikia yametokea tena yale yaliyotokea, kumetokea mapigano, imeturudisha nyuma kidogo katika mazungumzo na Congo katika kuwarejesha wakimbizi wa Congo. Lakini ombi letu, ushuwari upatikane warudi wote ili mzigo huu tuondokane nao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuwagawanya wakimbizi katika nchi za Afrika Mashariki, hawa nao tayari wanao. Uganda wanao wakimbizi kwa hiyo wana mgao wao tayari, Kenya wana wakimbizi kwa hiyo wana mgao tayari. Kwa hiyo, nchi za Afrika Mashariki zote tunahangaika na mzigo huu lakini *inshallah*, nchi zao zitatulia, watarudi kwao ili na sisi tuweze kupumua.

MHE. LEPHY B. GEMBE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swalı dogo la nyongeza. Kwa kuwa inaonekana Mkoa wa Rukwa haujafanyiwa tathmini hata ile moja ukifananisha na Mikoa mingine. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuupa Mkoa wa Rukwa kipaumbele cha kwanza ili na wao angalau wafanyiwe tathmini hiyo ili madhara yake yaweze kubainika?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, katika tathmini ambazo zimewahi kufanywa kuhusu athari za wakimbizi, Mkoa wa Rukwa ulikuwa haujafanyiwa tathmini hiyo na ndio maana hata katika ule mradi wa awali niliousema, Mkoa wa Rukwa haukuwemo. Lakini sasa hivi tunapozungumza, tayari tathmini inafanyika katika Mkoa wa Rukwa na tumewahimiza wamalize haraka ili waandike mchanganuo ili mpango unaokuja sasa wa kusaidia maeneo yaliyoathirika na wakimbizi na Mkoa wa Rukwa vile vile uingizwe.

Na. 290

Kusambaza Umeme Vijijini

MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. STEPHEN M. KAHUMBI) aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Umeme inaagiza umeme uteremshwe katika vijiji vinavyopitiwa na njia ya umeme; na kwa kuwa katika Wilaya nyingine umeme umevitwa na kupelekwa kwenye vijiji zaidi ya maili 30 hivi, wakati Wilaya nyingine kama Nzega, umeme hautoki na kwenda vijiji hata vilivyo umbali wa maili tano tu:-

(a) Je, kama viro vigezo vinavyofuatwa, Bukene ambao ni mji mkubwa hata kuzidi miji ya Makao Makuu ya Wilaya nyingine hapa nchini na pia kuna Shule za Sekondari mbili, Seminar moja, Vituo vya Afya vitatu, Vituo vya Polisi viwili na Stesheni ya Garimoshi, inapungukiwa na nini kukidhi haja ya kupatiwa umeme?

(b) Kwa kuwa nimekuwa naahidiwa tu kuwa tutapatiwa umeme na mfano halisi ni wa barua DO/MRE/BUNGE/9 ya tarehe 29 Mei, 2000, je, ahadi ya mwisho leo inasemaje?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Stephen M. Kahumbi, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Stephen Kahumbi kwamba, Mji wa Bukene unatimiza vigezo muhimu vya kuuwezesha na kuhitaji kupatiwa umeme. Ni kweli pia kwamba, kuitia Mheshimiwa Stephen Kahumbi, tuliwaahidi Wananchi wa Bukene kuhusu uwezekano na upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali kutekeleza ahadi hii iko pale pale. Tumechelewa kutokana na uwezo mdogo wa fedha ukilinganisha na mahitaji mkubwa ya umeme nchi nzima. Gharama za kupeleka umeme Mji wa Bukene pamoja na vitongoji vyake inakadiriwa kuwa Sh.800 milioni. Baada ya muda si mrefu, Serikali itaanziwa Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund*). Mradi wa umeme Bukene utatekelezwa chini ya mpango wa umeme vijijini katika mpango mzima wa nishati vijijini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, ndiye aliyetuhimiza tuweke umeme wa nguvu za juu pale Stesheni ya Garimoshi ya Bukene. Amekuwa mtetezi mkubwa wa Wananchi wa Bukene. Yeye pamoja na Mheshimiwa Lucas Selelili, wamekuwa chachu ya maendeleo ya Nzega. (*Makofî*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameshatamka kwamba, upo mpango huo maalum katika bajeti ya Wizara wa kueneza umeme katika maeneo ya Vijijini na kwa kuwa katika swali la pili tumetaka kupata tamko la mwisho. Je, Mheshimiwa Waziri, yupo tayari kutuambia kwamba mpango huo utatoa kipaumbele cha kwanza katika Vijiji hivyo na maeneo hayo yaliyotamkwa katika swali la msingi?

Pli,kwa kuwa tuna utaratibu wa kupeleka umeme wa *grid* katika maeneo ya Mji wa Songea. Je, Mheshimiwa Waziri, yuko tayari kutoa tamko kwamba Vijiji vyote vitakavyopitiwa na mpango huo wa *grid* kama vile Peramiho, Madaba na maeneo mengine, yatapatiwa umeme katika mpango huo? (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri, yapo maswali mawili, la kwanza ni sahihi, lakini la pili ni jipya. Jibu lile la kwanza. (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa tamko kwamba, kipaumbele cha kwanza kitatolewa katika kupeleka umeme katika Makao Makuu ya Wilaya ambazo hazina umeme kabisa. Wilaya hizo ni pamoja na Simanjiro, Kasulu, Kibondo, Bukombe, Nkasi, Ludewa, Ngorongoro, Kilolo, Namtumbo, Uyui, Kilindi na Mbinga. (*Makofî*)

Na. 291

Umeme Vijijini

MHE. PAUL P. KIMITI aliuliza:-

Kwa kuwa sera yetu ya kusambaza umeme hadi Vijijini inaweza kukwama kutokana na ubinafsishaji ambao mwekezaji anaangalia faida ya muda mfupi kuliko ya muda mrefu:-

(a) Kwa kutambua hilo, je, isingekuwa vizuri Serikali ikaanzisha Mfuko Maalum wa kuwezesha utekelezaji wa mpango huo, hasa kwa wenyewe kipato kidogo na Wananchi Vijijini ambao hawawezi kubeba mzigo huo wa gharama?

(b) Kwa kuwa hali ya umeme bado itaendelea kuwa kitendawili kwa muda mrefu hasa tukiendelea kutegemea mvua, je, isingefaa tuanze kufikiria umeme wa *Biogas* na baadaye wa *Nuclear Power*?

(c) Je, ni nini hatma ya umeme unaotoka nchi jirani?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (k.n.y. WAZIRI WA NISHATI NA MADINI): alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Paul Kimiti kuhusu malengo yanayoweza kutofautiana ya mwekezaji na yale ya Taifa kuhusu kusambaza umeme, hasa Vijijini. Malengo ya Taifa ni ya maendeleo, ambayo ni ya muda mrefu na yale ya mwekezaji ambayo ni faida ni ya muda mfupi. Changamoto iliyo mbele yetu ni kutumia faida za uwekezaji kukidhi lengo letu la maendeleo. Tumechelewa kwa makusudi kuirekebisha *TANESCO* ili tuwe na uhakika zoezi hili kama litakidhi matarajio yetu yaliyo katika Sera ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Paul Kimiti, kuhusu umuhimu wa kuanzisha Mfuko Maalum wa Nishati Vijijini. Mheshimiwa Paul Kimiti na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba, tarehe 15 Februari, 2004, Wizara ya Nishati na Madini iliendesha semina ya kuanzishwa kwa Mfuko wa Nishati Vijijini. Serikali inakamilisha taratibu za kuanzisha Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency*) na Mfuko wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Fund*). Wakala huo na Mfuko huo utaanzhishwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Nachukua nafasi hii, kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa dhati kabisa kwa mawazo, ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wakichangia katika semina niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Paul Kimiti kuhusu umuhimu wa kuendeleza nishati mbadala ikiwa ni pamoja na gesi asilia (ambayo sasa imefika Dar es Salaam) na inatoa *megawatt* 75, makaa ya mawe, nishati ya upepo, nyuklia, nishati ya juu, bayogesi, joto ardhi (*geothermal*) na mabaki ya mazao na miti na taka za Mijini.

Mheshimiwa Spika, ukame umetufundisha mengi, mojawapo ni kwamba, vyanzo vingi vya umeme ni suala lisilo na mjadala. Kwa maana hiyo umeme toka nchi jirani utafsiriwe kama chanzo mbadala na umeme kwenda nchi jirani, utafsiriwe kama biashara.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Kimiti amefanya mambo mengi kuhusiana na maendeleo ya Sumbawanga Mjini, Mkoa wa Rukwa na Taifa kwa ujumla. Tunamshukuru. (*Makofsi*)

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuzingatia majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri, atakubaliana nami kwamba kwa sababu Mfuko huo wa kusaidia Umeme Vijiji unaanzishwa katika mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, je, angeona kwamba heshima hiyo hiyo aliyosema Vijiji vinavyofuatana na Wilaya ya Sumbawanga Mjini kama Ntendo, Matanga, Pito, Senga, Hasese, Ulinzi, Isese na Milanzi, wakapewa kipaumbele kupewa msaada katika mwaka huu wa fedha?

Mheshimiwa Spika, la pili, umeme kutoka nchi jirani tunafahamu wote unategemea uhusiano unaokuwepo kati ya nchi na nchi. Je, nini hatima ya Serikali na mstakabali wa Serikali kama mahusiano hayo yatavunjika hasa kwa Mikoa kama Kagera na Rukwa ambao wanategemea moja kwa moja umeme kutoka Zambia na Uganda, tutafanya nini?

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kuhusu kupewa kipaumbele kwa Vijiji alivyovitaja kama viro karibu na ile Miji ya Wilaya ambazo haijapata umeme, basi nina uhakika vitapatiwa umeme. Kama haviko, basi kama nilivyosema, kipaumbele kwanza ni Miji ambayo iko katika Wilaya ambazo hatujapeleka umeme.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu umeme au nishati kutoka nchi jirani, napenda kusema kwamba, nishati kutoka nchi jirani katika mahusiano ya Kimataifa ni kitu kinachoziunganisha nchi badala ya kuzigawa nchi. Hata katika wakati wa vita baridi bado Ulaya Magharibi ilikuwa inapata gesi kutoka Urusi na nchi za Mashariki. Kwa hiyo, hili lisionekane kama ni tatizo, ionekane kwamba ni faida katika mahusiano ya Kimataifa.

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu na mimi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa nchi yetu imejaliwa kuwa na jua na mionzi ya jua kwa wingi sana na kwa kuwa suala la umeme wa jua ni ghali sana kutokana na kodi. Sasa kama mkakati ni kueneza umeme Vijijini, je, Serikali inaweza kufikiria kupunguza kodi za *solar* ili umeme huu uweze kusambazwa Vijijini? (*Makofi*)

SPIKA: Hilo nalo ni swali jipya sijui kama Waziri ana majibu, bora lije katika sura ya kawaida.

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *research* imeonesha ng'ombe anaweza kutoa kinyesi kati ya tani sita mpaka kumi na tano kwa mwaka. Je, kwa sababu Serikali ina *deficit budget*, kwa nini isikae Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, kutafuta njia ya kuachia ng'ombe kuzurura ovyo ili wakusanye haya mavi halafu wafanye *biogas*? (*Kicheko*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mwuliza swali la nyongeza, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kuhusu umuhimu wa *biogas* katika maendeleo ya nishati. Lakini atakubaliana nami kwamba,

nishati hii inafaa kwa matumizi madogo madogo tu kama vile ndani ya nyumba au viwanda vidogo vidogo sana. Kwa maana ya maendeleo, napenda kuthibitisha kwamba, hakuna nchi duniani iliyoendelea kwa matumizi ya *biogas* tu. (*Kicheko*)

Na. 292

Tatizo la Mitambo ya TTCL Kamachumu

MHE. RUTH B. MSAFIRI aliuliza:-

Kwa kuwa Kamachumu ipo mitambo ya *TTCL* na kwa kuwa Kituo hicho kimekuwa kikisumbuliwa na kupigwa radi mara kwa mara inyeshapo mvua na kusababisha uharibifu wa mitambo na simu, hali inayoleta hasara na bila shaka kuwakera wateja wa shirika:-

- (a) Je, Serikali ina taarifa ya tatizo hilo?
- (b) Je, kutokana na taarifa hiyo ni hatua zipi zinachukuliwa ili kuondokana na tatizo hilo?
- (c) Je, kwa nini Serikali haifungi mtambo imara wa kuzuia radi?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la mitambo ya Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), kupigwa radi hasa katika Mikoa ya Kagera na Mbeya linafahamika. Hatua zinazochukuliwa ili kuondokana na tatizo hili ni kuweka mitambo ya kunyonya nguvu za radi (*Earthing Systems*) na kuzipeleka ardhini ili mitambo ya simu isiathirike. Upimaji wa mitambo hiyo hufanywa mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa ipo katika hali nzuri ya kiutendaji kazi. Ikibainika kuwa mitambo hiyo haifanyi kazi kama inavyotakiwa, uboreshaji (*Earthing Improvement*) hufanyika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, uboreshaji huo hivi sasa unafanyika katika vituo vyote Mkoani Kagera na kazi hiyo imeshakamilika katika kituo cha Kamachumu.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza na pia namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri yanayoonesha jitihada za Wizara za kila wakati kufanya uangalizi na kuona jinsi ya kurekebisha mitambo inayosababisha madhara lakini napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu na Wizara inakiri na kwa kweli inapotokea mvua kunyesha mitambo huwa inaleta matatizo na simu vile vile zinaleta matatizo, kitu ambacho kinasababisha hasara kwa wale watumia simu. Je, Serikali inawafidia kwa namna yoyote kama wamechelewa kuchomoa simu zao na zikapigwa na radi?

Pili, kwa kuwa uharibifu wa mitambo na simu mara kwa mara kwa vyovyote vile ni hasara kwa Shirika. Je, Shirika lenyewe limewahi kufanya tathmini likaona linapata hasara kwa kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, suala la radi linatokea sana katika Mikoa inayozunguka bonde la ufa na ni suala la *nature*, hatuwezi kuliepuka lakini napenda niseme kwamba, Kampuni ya Simu Tanzania, hajatoa fidia isipokuwa tunafanya *replacement* ya mitambo pale shughuli hizi zinapotokea na bila ya kumdai mwenye simu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tathmini ya hasara, haijafanyika, labda nichukue wazo la Mheshimiwa Mbunge kwamba, niwaombe Kampuni ya Simu, waone uwezekano. Lakini hata kama watafanya ile tathmini ya hasara, masuala haya yataendelea tu kutokea katika Mikoa ile ambayo lipo bonde la ufa.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namwomba Waziri kwa kuwa tatizo hili la Muleba ni sawa na linalotokea Mbozi. Je, atakuwa tayari kutufikiria Wilaya ya Mbozi maana hasara tunazopata ni kubwa, mimi mwenyewe nimekwishapoteza vichwa vya simu vinne kwa radi, atakuwa tayari kuwaambia watu wa simu watusaidie mtambo huo wa kukamata radi? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, Mikoa yote inayozunguka bonde la ufa Mbeya ikiwemo masuala haya yapo na radi zinatokea Tukuyu, Rungwe na sehemu nyingine na kila inapotokea na mitambo kuharibika, Kampuni ya Simu inafanya *replacement* bila kudai chochote. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutaendelea kufanya hivyo.

Na. 293

Huduma za Simu Sikonge

MHE. AZIZA S. ALI (k.n.y. MHE. SAID J. NKUMBA) aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Sikonge wanaendelea kusubiri ahadi ya Serikali aliyoitao Mgomea mwenza kwenye uchaguzi wa mwaka 2000 ya kuwapatia huduma ya simu lakini mpaka sasa ahadi hiyo hajatekelezwa:-

- (a) Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

(b) Je, Serikali imefikia hatua gani ya kuwasiliana na Kampuni ya Simu za Mkononi ili kufikisha mitambo ya simu hizo Sikonge?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mji wa Sikonge kwa hivi sasa unahudumiwa na mtambo wa simu za kukoroga wenyewe uwezo wa kuhudumia jumla ya wateja 100 na hadi mwezi Machi, 2004 wateja 79 wameunganishwa. Pia Mji huo umeunganishwa na Tabora kupitia mtambo wa *analogue* wa radio wenyewe njia moja (*Single Channel VHF Radio*). Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*), ina mpango wa uboreshaji wa huduma zake kwa kuondoa mtambo huu wa zamani na kuwekwa mpya unaotumia teknolojia ya kisasa (*Digital*). Utekelezaji wake utafanyika Kampuni itakapoongeza uwezo wa kifedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu ya *Celtel* imefanya tathmini ya awali ya soko (*Field Marketing Survey*) katika Jimbo la Sikonge. Aidha, tathmini hiyo ilibaini kuwa Mji huo una rasilimali nyingi na wakazi wa maeneo hayo wanao uwezo mkubwa wa kutumia huduma za simu za mkononi. Hii ni hatua ya awali kabisa ambayo itaisaidia kampuni kufikia uamuvi wa kujenga kituo cha kutolea huduma za simu za mkononi (*Base Trans-receiver Station*), ambao hutegemea mambo mengine mengi ikiwemo, tathmini ya kiufundi, uagizaji na uingizwaji wa bidhaa muhimu za ujenzi na vifaa na fedha za kufanya kazi hiyo.

Kwa upande wa Kampuni ya *Vodacom*, hivi sasa inafanya tathmini ya soko nchi nzima ili kubaini maeneo ya kuweka mitambo yao ya mawasiliano. Kufuatia uchunguzi wa awali, ujenzi wa mitambo ya mawasiliano utaanza kufanywa katika maeneo yale yakayooonekana kuvutia zaidi na ambayo yanaweza kuunganishwa kwenye mtandao kirahisi zaidi. Maeneo mengine, yatawekewa mitambo baadaye kutokana na ubora, kipaumbele (*priority*) na upatikanaji wa njia za simu.

Zoezi hili litaendelea nchi nzima hadi kila sehemu ipate huduma za *Vodacom*. Hivyo, mipango ya *Vodacom* kupeleka mawasiliano ya simu za mkononi Sikonge itajulikana punde tathmini itakapokamilika katika kipindi kifupi kijacho.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa umuhimu wa simu za mikononi na simu za kawaida katika Wilaya ya Sikonge ni muhimu kutokana na mazao ambayo yanalinwa pale ya tumbaku, ambao unafanana kabisa na umuhimu wa sehemu za Kilolo hasa kule Ilula na sehemu nyingine ambako wanalima mazao yanayofanana.

Je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Sikonge, Kilolo na Ilula, kuhusu uwezekano wa kupatiwa simu hizo kabla ya kwisha mwaka huu wa 2004? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Sikonge tayari nimeshawaeleza juhudhi za Serikali yao katika kuwapelekea mawasiliano ya simu katika Mji wa Sikonge. Napenda kuchukua nafasi hii, niwaambie Wananchi wa Kilolo na Ilula kwamba, Mbunge wao tumeshazungumza naye na tumemwunganisha na Makampuni ya Simu ya TTCL na CelteL kwa lengo la kupata simu katika maeneo yao na Mheshimiwa Mbunge ameahidiwa na wenyе kampuni kwamba, watapeleka simu Kilolo na Ilula. Nawaomba Wananchi wa Kilolo na Ilula, wamuunge mkono Mbunge wao, kwa juhudhi hizo anazozifanya. (*Makofi*)

Na. 294

Shule chache za Serikali kwa Watoto Wenyе Ulemavu

MHE. MARGARETH A. MKANGA aliuliza:-

Kwa kuwa shule kwa watoto wenyе ulemavu zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Utamaduni ni chache hapa nchini hivyo kusababisha watoto hao kushindwa kusoma kwenye Shule za Elimu Maalum zinazoendeshwa na Mashirika au watu binafsi kutokana na kushindwa kumudu gharama au umbali wa kufikia shule hizo na kwa kuwa elimu ni haki ya msingi ya mtoto, je, Serikali ina mipango gani madhubuti ya kuhakikisha kuwa watoto hao wanapatiwa elimu?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalı la Mheshimiwa Mwalimu Margareth Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tangu miaka ya 1950, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mashirika ya Kidini na taasisi za kujitolea imekuwa ikitoa elimu kwa watoto wenyе ulemavu kupitia Mfumo ya Shule Maalum za Walemavu peke yao, shule za mchanganyiko (wenye ulemavu wakipatiwa huduma za bweni na vitengo vya wenyе ulemavu vya kutwa). Mpaka sasa Wizara yangu imeweza kufungua shule na vitengo vya wenyе ulemavu wa aina mbalimbali 176 vyenye jumla ya wanafunzi 5,365 na walimu 1,033.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda sasa kujibu swalı la Mheshimiwa Margareth Mkanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili kutoa nafasi zaidi kwa watoto wenyе ulemavu, mipango madhubuti imeandaliwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza utoaji wa Elimu Jumuisho (*Inclusive Education*), ambapo watoto wenyе ulemavu wataandikishwa na kusomeshwa katika shule za msingi za kawaida zilizo karibu na kwao katika madarasa mchanganyiko na wanafunzi wasio na ulemavu.

(b) Kutoa mafunzo ya elimu maalum katika ngazi ya Cheti na Stashahada kwa walimu wa kutosha wa kuweza kutumia mbinu shirkishi ili kuwasaidia wanafunzi wenyewe ulemavu katika mfumo wa Elimu Jumuisho.

(c) Kununua na kusambaza vifaa maalum vya kufundishia na kujifunzia katika shule na vitengo vya wenyewe ulemavu.

(d) Kufungua shule zaidi za kuhudumia watoto wenyewe ulemavu wa aina zote katika kila Wilaya ifikapo 2006.

(e) Kuingiza kipengele cha elimu maalum katika Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Daraja la IIIA.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya wanafunzi wenyewe ulemavu yanazingatiwa pia katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES). Katika mwaka wa kwanza wa MMES, jumla ya Sh. 1,231,400,000/= zimetengwa kwa ajili ya kukarabati shule nane za sekondari zenye wanafunzi wenyewe ulemavu na kuchangia ujenzi wa shule mpya mbili za wenyewe ulemavu. Aidha, Serikali itatoa ruzuku ya maendeleo kwa mwenye shule asiyeh Serikali, atakayeidhinishwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya ujenzi wa shule za wanafunzi wenyewe ulemavu kwa kiwango sawa na ile inayotolewa kwa ajili ya Sekondari za Serikali zinazojengwa kwa nguvu za Wananchi yaani shilingi milioni sana kwa darasa na shilingi milioni tisa kwa nyumba ya mwalimu. Aidha, shule hizo zitapewa ruzuku ya uendeshaji ya Sh. 15,000/= kwa mwanafunzi.

MHE. MARGARETH A. MKANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Nishukuru kwa mipango ambayo imefanuliwa na Wizara kuhusu swali langu, lakini niulize mingi nimeisikia hapa ni mipango itakuwa. Je, kwa sasa hivi ni mbinu gani inatumika kusudi kuweza kusawazisha masuala haya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Margaret Mkanga ni kwamba, mipango imekuwa ikifanyika na pengine matokeo ya mipango hiyo haionekani. Sasa hivi mbinu inayotumika ni kwamba, tumejifunza, sasa tutafanya kwa vitendo kuliko kwa maneno.

Na. 295

Umuhimu wa Michezo Mashulenii

MHE. BAKARI M. MBONDE aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali inafahamu umuhimu wa michezo katika shule za sekondari na za msingi:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi na za kimaendeleo zilizoifanya Serikali ifute mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA?

(b) Je, Serikali sasa ina mikakati gani ya kuimarisha na kuendeleza michezo katika shule hizo kote nchini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCAD D. NTAGAZWA - k.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa Waraka wa Elimu Na. 3 wa Mwaka 2001, ilisitisha michango na mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISETA kutokana na sababu kuu mbili ambazo ni:-

(i) Mashindano hayo yalikuwa yanachukua kati ya siku 60 mpaka 75 kutokana na zile siku 194 zilizopangwa na Afisa Elimu Kiongozi kwa ajili ya vipindi vyaa masomo madarasani.

(ii) Wazazi kuchangishwa fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia michezo hiyo na hivyo kuwa kero. Aidha, iligundulika kuwa sehemu kubwa ya fedha hizi zilikuwa zinatumika kwa utawala na mambo mengine na siyo kuendeleza michezo kwa faida ya wanafunzi.

(b) Mheshimiwa Spika, Waraka wa Elimu Na. 3 wa Mwaka 2001 pia ulitoa utaratibu wa kufuata ili kuboresha na kuendeleza michezo shulenii. Mojawapo ya taratibu hizo ni Wakuu wa Shule na Vyuo, Walimu Wakuu na Maafisa Elimu kuendesha mashindano ya michezo baina ya vyuo na shule zao kwa ratiba ambazo hazivurugi siku 194 za masomo darasani. Ratiba hizo lazima ziidhinishwe na Wakurugenzi wa Idara ya Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari au Elimu ya Ualimu, baada ya kuridhika kuwa haziingiliani na siku 194 za vipindi madarasani zilizopangwa na Afisa Elimu Kiongozi.

MHE. MARIA D. WATONDOHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa michezo inamwongezea nguvu mwanafunzi na aweze kujifunza zaidi na kwa kuwa kwa utaratibu ule wazazi walikuwa wala hawachangii sana na wala tulikuwa hatupati matatizo.

Je, Serikali itakuwa tayari kutazama upya ili angalau *inter-school competition* ziwepo? (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCAD D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Spika, katika jibu la msingi nimeeleza utaratibu uliowekwa na ule Waraka Na. 3 wa Mwaka 2001, unaoelekeza mashindano na maandalizi yake yafanyike baina ya shule na shule. Kwa hiyo, baina ya shule na shule naamini ndiyo Kiingereza *inter-school*. Kwa hiyo, utaratibu umekwishawekwa.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wake umekwisha. Sasa tunaendelea na kazi nyingine, kwanza, matangazo ya vikao vya leo ambavyo ni vingi kidogo. Kamati zifuatazo zimepangiwa kufanya vikao leo:-

Kwanza, ni Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, watakuwa na Kikao kuanzia saa 5.00 asubuhi chumba namba 219 ghorofa ya pili. Kamati nyingine ni ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake anasema kutakuwa na Kikao leo tarehe 21 Julai, 2004 kuanzia saa 5.00 vilevile asubuhi chumba namba 231.

Kamati nyingine ni ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mwenyekiti wake amepanga kikao kifanyike leo saa 5.00 asubuhi chumba namba 428 ghorofa ya nne. Halafu Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, anaomba kikao kifanyike saa 4.30 asubuhi, yaani mara baada ya kipindi hiki cha maswali chumba namba 227 ghorofa ya pili. Hizo ndiyo Kamati zinazokutana.

Sasa vikao visivyokuwa vya Kamati, cha kwanza ni Umoja wa Wabunge Wanawake (*TWPG*), Mheshimiwa Anne Makinda, Mwenyekiti wake anaomba kikao kifanyike leo saa 7.00 mchana chumba namba 227 ghorofa ya pili. *APNAC Tanzania*, Mwenyekiti wake, mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anaomba Wabunge ambao ni Wajumbe wa *APNAC Tanzania*, wafanye kikao leo saa 7.00 mchana baada ya kuahirisha Bunge, kwa kuwa ni wengi basi watabaki humu humu ndani ya Ukumbi wa Bunge. Mwisho wa matangazo. Katibu tuendelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe, iliyochambua kwa makini malengo na makusudio ya Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kuafiki na kuipitisha kifungu kwa kifungu. Mchango uliotolewa na Kamati kwa ujumla pamoja na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hiyo umesaidia sana kuiboresha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kutoa hotuba yangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutuongoza kwa ufanisi na kutekeleza majukumu yake mbalimbali yakiwemo wa kikanda na Kimataifa na hivyo kuijengea heshima kubwa nchi yetu. Nampongeza pia Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kwa kumsaidia Rais kwa ufanisi na busara. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Frederick Sumaye, Waziri Mkuu, kwa hotuba yake iliyotoa dira ya mijadala wetu hapa Bungeni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu walionitangulia, kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika Bunge la Afrika amba ni Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe. Aidha, pongezi nyingi nazitoa kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhamwe, kwa kuteuliwa kwake kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira, Mheshimiwa Dr. Pius Y. Ng'wandu, Mbunge wa Maswa, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Tume ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kwake kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa *SADC (SADC Parliamentary Forum)* na ninawataenia kila la kheri katika majukumu hayo mapya.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nikushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe, kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza Bunge letu kwa busara na hekima kubwa. Aidha, pamoja Wenyeviti wote wa Bunge wanaokusaidia wakati haupo Bungeni. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine, kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Bariadi Magharibi, kwa kuchaguliwa hivi karibuni kuitia Chama chetu cha CCM na kujiunga nasi katika Bunge hili Tukufu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kwake na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Mbunge na papo hapo kumpa pole kwa ajali iliyomfika alipokuwa akija kuhudhuria Mkutano huu wa Bajeti. Nawapa pole Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kushambuliwa na majambazi na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, aliyepeata ajali walipokuwa njiani kuja Dodoma kuhudhuria Bunge la Bajeti.

Aidha, nawapa pole Waheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na Baba yao Mpewda, Mzee Omar Kigoda, Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao wapendwa. Mwenyezi Mungu,

aziweke roho zao mahali pema peponi. Vile vile, nawapeni pole Wananchi wote ambao kwa njia moja au nyingine, waliathirika na ajali, majanga au misiba. Wote hao nawatakieni kila la heri katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kumkumbuka na kumwombea dua mwenzetu ambaye amelitumikia Taifa kupitia Bunge hili, Marehemu Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, aliyeitwa mbele za haki tarehe 24 Juni, 2004 akiwa hapa Mjini Dodoma katika shughuli za Bunge. Nawapa pole familia yake na Wananchi wa Jimbo lake la Mbeya Vijijini na namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke mahali pema peponi roho yake. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyoolewa majukumu ya Wizara yangu ni kusimamia suala zima la utoaji haki, udumishaji wa haki za binadamu na kuishauri Serikali katika masuala ya Sheria kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na kuweka mazingira mazuri ya maendeleo na hasa wakati huu baada ya nchi yetu kuingia katika mfumo wa uchumi wa soko huria na utandawazi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imejizatiti kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa kuongozwa na Dira ya Haki kwa Wote na kwa Wakati unaofaa. Lengo la Dira hii ni kuleta maendeleo ya Haki ya Kijamii, Usawa na Utawala wa Sheria kutokana na kuwepo kwa huduma bora za kisheria zitakazopatikana kwa wote na kwa muda muafaka. Wizara yangu inao Mkakati wa Kujenga Mfumo wa Sheria ambao utakidhi mahitaji mapya ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na maendeleo ya kisayansi ndani ya nchi na kutokana na mahusiano na nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuelezea mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2003/2004, napenda kutumia fursa hii, kulishukuru Bunge lako Tukufu na Serikali kwa ujumla, kwa kutambua umuhimu wa Sekta ya Sheria katika utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini na katika kuendeleza na kudumisha Utawala wa Sheria na Utawala Bora nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, pamoja na mahitaji makubwa ya rasilimali inayohitajika katika kuboresha na kuimarisha huduma katika Sekta hii, Serikali imekuwa ikiongeza kiwango cha mgao wa Bajeti kwa Sekta ya Sheria. Mathalani, kiwango cha Bajeti ya Sekta hii kimeongezeka kutoka Sh.16.8 bilioni mwaka 2001/2002 hadi kufikia Sh.31.0 bilioni katika Mwaka huu wa Fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea hali ya kiwango cha mgao wa Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya Sekta, nachukua fursa hii kuelezea hali ya utekelezaji wa mpango katika mwaka wa fedha wa 2003/2004. Katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2003, Wizara yangu ilitekeleza shughuli zake kwa kuzingatia Mkakati wa Kupunguza Umaskini kwa kuimarisha na kuharakisha utoaji haki kwa wote na kwa wakati ili kuwawezesha Wananchi kutekeleza majukumu yao kwa amani na utulivu na kudumisha Utawala Bora. Hali ya utekelezaji kwa maeneo muhimu ambayo Wizara ilipanga kuyafanya ilikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani, Wafungwa na Mahabusu Magerezani, katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004, Mahakama imefanya vikao 11 vya Mahakama ya Rufaa ikilinganishwa na vikao vinane ilivyofanya mwaka 2002/2003, Mahakama Kuu, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imefanya vikao 65 katika Kanda kumi na moja ikilinganishwa na vikao 59 katika mwaka 2002/2003. Hivyo, kesi za mauaji zilizofunguliwa Mahakama Kuu ziliwa 915 ambapo kati ya hizo, kesi 620 zilishughulikiwa na kutolewa maamuzi. Kesi za rufaa za jinai zilizofunguliwa Mahakama Kuu ziliwa 992 na kati ya hizo, kesi 460 zilishughulikiwa na kutolewa maamuzi. Aidha, Mahakama za Mahakimu Wakazi, Wilaya na Mahakama za Mwanzo zilifanya vikao vyao vya kila siku. Katika kuimarisha utendaji, Ofisi zote za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilikaguliwa na maofisa wa ngazi za juu kutoka Makao Makuu ya Wizara. Ukaguzi huo umesaidia kuboresha huduma na ufanisi wa ofisi hizo za Kanda.

Mheshimiwa Spika, kutokana na msongamano wa Mahabusu katika Magereza na mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu, Wizara yangu ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kutatua tatizo hili. Hatua hizo ni pamoja na: -

- Kuimarisha Vikao vya Kamati za Kusukuma Kesi kwa kuundwa Kamati ya Kitaifa inayowahusisha Watendaji Wakuu wa Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Polisi na Magereza. Kamati hii itakuwa na wajibu wa kutoa taarifa za usukumaji wa kesi kwa Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Inspekte Jenerali wa Polisi na Kamishna Mkuu wa Magereza;
- Kufanya ziara katika Magereza ili kusikiliza matatizo ya Wafungwa na Mahabusu na kuchukua hatua ipasavyo;
- Kuharakisha huduma za utoaji haki Mahakamani na kuhimiza ufanisi na kuajiri Mahakimu zaidi, kuboresha ufanisi wa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu kuongeza kasi ya Vikao zaidi vya kushughulikia mashauri mbalimbali; na
- Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kufanyiwa marekebisho ambapo sasa mashauri ya Kujamiana na Maherimu (*Incest*), ambayo siku hizi yameongezeka sana yatakuwa yakisikilizwa na Mahakama za Wilaya badala ya mashauri hayo kusikilizwa na Mahakama Kuu. Hatua hii itachangia kupunguza mlundikano wa kesi za aina hiyo Mahakama Kuu na pia itawezesha mashauri ya aina hiyo yasikilizwe mapema.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha juhudzi za kutanzua tatizo la msongamano wa Mahabusu na Wafungwa, Wizara yangu, Wizara ya Mambo ya Ndani na Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa pamoja tulikutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama,

chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa John Samwel Malecela, Mbunge wa Mtera, tarehe 5 Aprili, 2004, kujadili kwa pamoja Taarifa Maalum ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuhusu Hali ya Magereza. Kikao hicho kwa pamoja kilipendelekeza iundwe Kamati Maalum ya kushughulikia tatizo hilo. Pendeleko hili tayari nimekwisha lifikisha ngazi za juu zaidi na linafanyiwa kazi. Nami nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hizi kwa hatua waliyoichukua ya kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo. Aidha, natumaini kwamba kuanza kutumika kwa Sheria ya *Community Service Act, 2002* kutachangia sana kupunguza tatizo hili la msongamano wa Wafungwa na Mahabusu Magerezani.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, nilieleza kuwa, Mahakama ya Ardhi ilikwisha anzishwa rasmi kisheria tarehe 4 Mei, 2001. Ninafurahi kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa Mahakama hii imeanza kufanya shughuli zake rasmi tarehe 1 Oktoba, 2003 baada ya kukamilika kwa taratibu zote za kuanzisha Masjala za kisheria katika Kanda kumi za Mahakama Kuu. Aidha, Mahakama hii katika Mwaka wa Fedha 2003/2004, ilisajili mashauri ya ardhi 139 na mashauri 40 yamekwisha tolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, nilikwisha kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Mahakama ya Biashara ilianzishwa kwa lengo la kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani na hasa kesi za kibashara. Mahakama hii imekuwa na utaratibu mzuri wa usajili wa mashauri, usikilizaji, maamuzi na utunzaji wa kumbukumbu za mashauri. Aidha, Majaji wa Mahakama hiyo wanao utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za mashauri. Kila mwezi, Jiji wa Mahakama hii hujaza fomu maalumu ya kuthibisha mashauri aliyopokea, aliyoyaamua na ambayo hayajatolewa uamuzi.

Mahakama hii imekuwa Mahakama ya mfano kwenye nchi za Jumuia ya Ushirikiano Kusini mwa Afrika (*SADC*) na inastahili pongozi na kuigwa na Masjala nyingine za Mahakama Kuu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004, ilisajili jumla ya mashauri 90 ya biashara na kulikuwa na bakaa la mashauri ya nyuma 162, hivyo kufanya jumla ya mashauri ya biashara 252. Kati ya mashauri hayo, Mahakama hii iliamua mashauri 187, ikiwa ni asilimia 74.2 ya mashauri yote. Kwa mantiki hii, Mahakama ya Biashara inapaswa kupongezwa kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya toka izinduliwe.

Mheshimiwa Spika, aidha, vitendea kazi vilinunuliwa na kusambazwa katika Mahakama zote hapa nchini na hivyo kuimarisha uendeshaji wa kesi. Ukaguzi wa Mahakama uliimariswa na kufanya katika Kanda zote na utaendelea kuimarishwa. Jumla ya magari 20 yameagizwa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukaguzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Wizara, kwa kupitia Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu iliendela na shughuli za usajili wa vizazi, vifo, ndoa na wadhamini na kufanya ukaguzi wa Wilaya mbali mbali kwa ajili ya kuimarisha shughuli za usajili na ukusanyaji wa mapato. Wizara, kwa kupitia Idara hii iliendelea na uenezaji wa Mradi wa Usajili wa Vizazi na Vifo katika Wilaya zote za Mkoa wa Mbeya, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto na Elimu (*UNICEF*). Kutokana na ufinyu wa Bajeti,

mradi huu haukuweza kuenezwa katika Mikoa ya Kagera, Kigoma, Mtwara, Ruvuma, Rukwa na Lindi. Aidha, katika kuimariswa usajili wa vizazi na vifo katika ngazi ya vijiji, Idara hii kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la *Plan International - Tanzania*, walitoa elimu ya kuhamasisha Wananchi katika Mikoa ya Pwani, Morogoro na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, ili juhudhi hizi zilete mafanikio, nachukua fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kupitia Halmashauri zao za Jiji, Manispaa, Wilaya na Miji, wawahimiza na kuwashauri wananchi wasajili, Vizazi, Ndoa na Vifo. Kwani usajili huo una manufaa makubwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na uthibitisho wa umri, uthibitisho wa ndoa, uthibitisho wa uraia na haki zinazoambatana na usajili huo na pia katika masuala ya ufuatiliaji wa mirathi. Pale ambapo zoezi la usajili wa Vizazi, Ndoa na Vifo limefanyika kikamilifu, linasaidia sana kupatikana kwa takwimu za idadi ya watu katika eneo hilo kwa urahisi na hivyo kurahisisha upangaji Mipango ya Maendeleo kwa nia ya kufikisha huduma mbalimbali za kijamii.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria iliendelea na shughuli za utafiti wa Sheria na kufanya mapitio ya Sheria mbali mbali ambazo haziendi na wakati huu wa mageuzi yanayotokana na teknolojia, kiuchumi na kijamii. Tume ilifanya utafiti na mapitio ya Sheria 4 za *Kisekta* ambazo ni Sheria za Sekta ya Usalama Barabani (*Road Traffic*), Utalii, Mtiririko wa Utendaji Haki, Polisi na Magereza. Utafiti na mapitio ya Sheria za Usalama Barabarani na Utalii zimekamilika na taarifa ya mwisho imewasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, jumla ya Miswada 31 ilipitishwa na Bunge, Sheria Mama 22 na Sheria ndogo ndogo 444 zilihakikiwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu pia kuwa, zoezi lililoanza mwaka 1992 la kurekebu sheria mbalimbali za nchi za tangu ukoloni na kuzichuja hadi kufikia 424 limeshakamilika. Jumla ya Matoleo ya Sheria hizi (*The Revised Edition of the Laws of Tanzania*) ni 600 ambayo yamegawanyika katika juzuu kumi za Sheria Mama na juzuu kumi za Sheria Ndogo na juzuu moja ya Rejeo la Sheria. Sheria hizi nilizindua mwezi Desemba, 2003. Hivi sasa zinasambazwa kwenye Idara na Taasisi za Serikali. Baada ya zoezi hilo kukamilika, Mheshimiwa Rais atashauriwa kutangaza kuanza kutumika kwa Sheria hizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, kazi hiyo muhimu ya kuzichuja na kuzichapisha Sheria hizo ilifadhiliwa na Serikali ya Sweden kwa gharama ya Dola za Kimarekani 1.2 milioni. Kwa niaba ya Serikali yetu, nachukua nafasi hii kwa mara nyingine tena kuishukuru Serikali ya Sweden kwa kuweza kufadhili kazi hii. Kabla ya kazi hiyo, Sheria zetu zilikuwa zimetapaka katika vipande mbali mbali kutokana na ukweli kwamba kila mwaka Sheria zinatungwa na kurekebisha au kufutwa ili kukidhi matakwa ya jamii na Taifa letu kwa wakati. Hatua hii itarahisisha sana upatikanaji wa Sheria hizo kwa watafiti wa Sheria, Wanataluma wa Sheria, Majaji, Mahakimu, Mawakili na Wanasheria wa kada zote na wananchi wote kwa ujumla kwa ajili ya matumizi yao. Hii itachangia katika uboreshaji wa huduma za utoaji haki katika Mahakama zetu, ushauri wa kisheria na uhakika zaidi wa maamuzi na ushauri wa kisheria katika kada zote za Wanasheria na kufahamika kwa urahisi na Wananchi wanaofuatilia masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, sambamba na zoezi hili, Sheria Mama mbili zilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Sheria hizo ni Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sheria Na. 8 ya Mwaka, 2001 na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Sheria Na. 7 ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake yaliyotolewa kwa Sheria Na. 16 ya Mwaka 2001. Pamoja na kutafsiri Sheria Mama hizo, pia kuna Sheria ndogo ambazo kutokana na umuhimu wake kwa jamii zimetafsiriwa katika lugha ya kiswahili. Sheria hizi ni pamoja na: Msamaha wa Kodi kwa Ongezeko la Thamani lililotolewa likiwa amri kwa Tangazo la Serikali Na. 389 la Mwaka 2003, na Kanuni za Usalama Barabarani zilizohusu usajili wa magari) kwa Tangazo la Serikali Na. 25 la Mwaka 2001. Shughuli za utafiti wa kisheria katika mwenendo wa kesi za jinai na mapitio ya Sheria za Kisekta za Madini na Utalii ziliendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieleza Bunge juu ya utafiti kuhusu Sheria za Ndoa, Watoto na Mirathi uliofanywa na Tume ya Kurekebisha Sheria. Bunge hili Tukufu linaelewa kuwa Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 imekuwa ikitumika takriban miaka thelethini na tatu sasa. Sheria hii imeonyesha mafanikio na vilevile imeonyesha mapungufu kadhaa ambayo ndiyo yamesababisha Sheria hiyo kuangaliwa upya. Baada ya kukamilisha uchambuzi, Wizara ilipeleka mapendekezo Serikalini kwa ajili ya kufanya maamuzi kuhusu kuboresha ama kutunga Sheria kuhusu masuala hayo. Masuala muhimu yatakayozingatiwa ni umri na utaratibu wa kufunga na kusajili ndoa, hadhi ya mahusiano ya mume na mke walioishi muda mrefu bila kufunga ndoa, muundo na majukumu ya Baraza la Usuluhishi wa Ndoa, umiliki wa mali, malezi na matunzo ya watoto.

Sheria ya Watoto, itazingatia haki za watoto kama zilivyoainishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki ya Mtoto, Itifaki ya Nyongeza Kuhusu Uuzaji Watoto, Ukahaba na Upigaji Picha za Udhalilishaji, Itifaki ya Nyongeza Kuhusu Kuwahusisha Watoto Kwenye Migogoro ya Kivita, Mkataba wa Shirika la Kazi la Dunia Kuhusu Kupiga Vita Utumikishaji wa Watoto katika Kazi za Hatari, Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto pamoja na Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania. Sheria ya Mirathi na Urithi itazingatia mfumo wa usimamizi wa mirathi na urithi, haki sawa ya watoto wa jinsia zote kurithi, haki ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa kurithi pamoja na mfumo rahisi wa kuandika wasia.

Mheshimiwa Spika, suala la uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Serikali imeona ni vyema kulifanyia utafiti na kupata maoni ya Wananchi juu ya uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi, mfumo wa Mahakama ya Kadhi, uteuzi wa Makadhi na Kadhi Mkuu pamoja na mamlaka ya Mahakama ya Kadhi. Hivyo, Wizara yangu imeona ni vyema kujumuisha suala la Mahakama ya Kadhi, pamoja na masuala ya mirathi, ndoa na watoto katika kuyashughulikia.

Kutokana na ukweli kwamba, masuala ya ndoa, watoto, mirathi na kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi nchini, yanahu su maslahi na imani za Watanzania wengi, Serikali imeona ni busara kuwashirikisha Wananchi wengi zaidi ili kupata maoni yatakayowezesha kufanya maamuzi ambayo yatazingatia maslahi yao na ya Taifa kwa

ujumla. Hivyo, Serikali imeamua kuandaa na kuchapisha Waraka wa Serikali (*White Paper*), utakaowezesha kupata maoni hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuishauri Serikali juu ya uendeshaji wa Serikali kwa kufuata Utawala wa Sheria, kanuni na taratibu, kuishauri Serikali kuhakikisha kuwa utaratibu uliopo wa wananchi kuchagua viongozi wao kwa misingi ya demokrasia unadumishwa, pia imeendelea kushauri juu ya ushirikiano baina ya Serikali yetu na Serikali nyingine na Mashirika ya Kimataifa na kuishauri Serikali juu ya Mikataba ya Kimataifa kati ya Serikali yetu na Taasisi za Kimataifa na binafsi.

Kwa misingi hiyo, Wizara ilishughulikia mashauri ya madai na kuiwakilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ya kisheria yanayoikabili Serikali. Katika Mwaka wa Fedha wa 2003/04, mashauri ya madai mia mbili arobaini na tano yailifunguliwa dhidi ya Serikali. Mashauri hayo yanahusu madai dhidi ya Wizara na Idara za Serikali zifuatazo: Ardhi, Maliasili na Utalii, Ujenzi (*TANROADS*), Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo na Idara ya Polisi. Kati ya hayo, mashauri thelathini yalishughulikiwa na kumalizika. Vile vile, Mikataba thelathini ilishughulikiwa. Aidha, Wizara iliendelea kuiwakilisha Serikali katika majadiliano mbali mbali ya Kimataifa ambayo Tanzania inawakilishwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika utangulizi, eneo lingine muhimu ambalo linashughulikiwa na Wizara ni lile linalohusu masuala ya Katiba na Haki za Binadamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004, rasimu ya Muswada wa mabadiliko ya Kumi na Nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeandalowi. Muswada huo utafikishwa kwenye Bunge hili hivi karibuni. Muswada huu ni muhimu kwa sababu pamoja na mabadiliko ya mambo mengine, yapo masuala mengi yanayohusu uwakilishi wa Wananchi katika hatua ya kupanua demokrasia.

Vile vile, Mawakili wamesimamia na kuitetea Serikali katika mashauri mawili yanayohusu malalamiko ya ukiukaji wa haki za binadamu katika Mkoa wa Mara, ambayo yalifunguliwa na Wananchi kwenye Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mashauri hayo ambayo ni ya ukikwaji wa haki za binadamu yanahusu malalamiko juu ya kuhamishwa kwenye eneo la mgodi wa dhahabu bila kulipwa fidia kamili (*Fair Compensation*) na malalamiko ya Wananchi kuchomewa nyumba zao huko Serengeti. Tumeweza pia kuwasilisha utetezi wa Serikali kwenye shauri moja ambalo mwananchi ametumia haki yake kufungua malalamiko kwenye Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu (*African Commission for Human and Peoples' Rights*). Mwananchi huyo anadai kuwa hakupewa haki ya kusikilizwa katika shauri lake lililohusu masuala ya uraia. Aidha, Wizara imeshughulikia mashauri manane yaliyowasilishwa katika Mahakama Kuu dhidi ya Sheria zilizotungwa na Bunge kwa maelezo kwamba, Sheria hizo zinakiuka Katiba ya Nchi na walalamikaji wakiomba zitenguliwe. Mashauri hayo yote yanahusiana na masuala ya uraia na uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia ina wajibu wa kutekeleza majukumu ya nchi yanayotokana na Mikataba na Kanuni zinazohusu Haki za Binadamu kama zilivyoainishwa na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika. Moja ya majukumu hayo ni

kutoa taarifa za utekelezaji wa Mikataba inayohusika. Kwa mwaka uliopita, Wizara imeandaa taarifa kuhusu Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi wa Kitabaka (*Convention on the Elimination of all forms of Racial Discrimination*) na kueleza hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa kuondoa aina zote za ubaguzi nchini. Aidha, tumeandaa rasimu nyingine kwa mujibu wa Mkataba wa Haki za Binadamu Barani Afrika ambayo itajadiliwa na Wadau kabla hajawasilishwa kwenye Tume ya Haki za Binadamu ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imeendela na shughuli zake kuhusu kuhamasisha na kulinda haki za binadamu na misingi ya Utawala Bora. Katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitoa elimu kwa umma kwa kutembelea Vijiji katika Wilaya 23 za Tanzania Bara na kukutana rasmi na Sekretarieti za Wilaya na Viongozi wengine wa Umma katika Wilaya husika. Jumla ya malalamiko 2,578 yalipokelewa na Tume na kati ya hayo malalamiko 327 yameshughulikiwa na Wananchi waliostahili haki walipata. Malalamiko 2,251 yaliyobakia yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Tume ilitembelea na kukagua Magereza 24 na vituo vya Polisi 33 katika baadhi ya Wilaya za Tanzania Bara kwa ajili ya kuona hali ya wafungwa na mahabusu. Halikadhalika, Tume ilifanya uzinduzi rasmi wa Taarifa yake ya Ukaguzi wa Magereza Tanzania Bara kwa mwaka 2002/2003, mwezi Februari, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2003/2004, nilielezea hatua ambazo zinachukuliwa ili kuimarisha hali na hadhi ya ofisi na majengo ya Mahakama hapa nchini. Napenda kulielezea Bunge lako Tukufu kuwa, awamu ya kwanza ya ukarabati wa jengo la Forodhani litakalokuwa Mahakama ya Rufaa iliyohusisha paa la jengo, umekamilika. Mkandarasi *B&S International Engineering and Contractors A/S* atakayetekeleza awamu ya pili itakayohusu jengo zima amekwisha kutiliana saini mkataba na Serikali. Mkandarasi huyu anatarajia kukamilisha kazi za awamu hiyo katika kipindi cha wiki ishirini na mbili. Hivyo, ukarabati wa jengo hilo utakuwa umekamilika ifikapo Januari, 2005.

Kukamilika kwa jengo hilo kutapunguza uhaba wa ofisi kwa Majaji katika jengo la Mahakama Kuu. Aidha, ukarabati wa jengo la masjala ya Mahakama Kuu ya Mwanza na ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya ya Kongwa na Mbarali upo katika hatua za mwisho. Pia taratibu za kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Ludewa zipo katika hatua za mwisho. Taratibu za kupata michoro na ukadiriaji wa gharama na uteuzi wa mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Mahakama Kuu katika Masjala ya Moshi, Sumbawanga na Iringa zimekamilika. Aidha, kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Mwanza ya Manzese kilikwisha patikana na taratibu za kuanza ujenzi zinaandalialiwa.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilielezea umuhimu wa kuwa na Sera ya Sekta ambayo ndiyo mwongozo wa kutekeleza majukumu mbalimbali ya Sekta. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, maandalizi ya utayarishaji wa Sera ya Taifa ya Sekta ya Sheria yalikwisha kuanza. Rasimu ya Mwongozo wa Sera (*Legal Sector Concept Paper*) imekwisha jadiliwa na Wadau wote wa Sekta ya Sheria na kutolewa

maoni. Aidha, rasimu ya hadidu za rejea (*terms of reference*), zitakazotumika katika utayarishaji wa Sera hiyo zimeanza kutayarishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu iliendelea kutekeleza Programu ya Kurekebu Sekta ya Sheria (*The Legal Sector Reform Programme*), iliyotokana na taarifa ya Tume ya Bomani ya mwaka 1996. Taarifa hii iliwasilishwa Serikalini mwaka 1997 ambapo mapendekezo yake yote yalikubalika kutekelezwa. Kutokana na ghamama za utekelezaji wa Programu hiyo kuwa kubwa, Mkakati wa Muda wa Kati wa kutekeleza Programu hiyo uliandaliwa na kuzinduliwa mwaka 1999. Mkakati huu ultathminiwa na kuhuishwa kwa lengo la kuimarisha usimamiaji, uwajibikaji na uratibu. Lengo la msingi ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji pamoja na kuwezesha Sekta kuhimili mabadiliko ya kiuchumi na kijamii. Aidha, miradi iliyobuniwa kwa lengo la kutekeleza Mpango wa Kurekebu Sekta ya Sheria iliendelea kutekelezwa. Miradi hiyo ni *Quick Start* na *Capacity Building*, pamoja na maandalizi ya Mradi wa *Tanzania Accountability Transparency and Integrity Project (ATIP)*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Quick Start* uliobuniwa mwaka 2001 ambao ulikuwa wa majaribio, ulikuwa na lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa Mpango wa Kurekebu Sekta ya Sheria. Mradi huu umegharamia maeneo sita ikiwa ni pamoja na tafiti tano. Tafiti hizi ni muhimu na zitasaidia kuboresha utekelezaji wa mpango wa utendaji katika asasi za kisheria. Tafiti hizi zimejadiliwa katika warsha na mikutano mbalimbali ya Wadau ili kuhakikisha kuwa mabadiliko ya Sekta ya Sheria yanahuishwa na kusaidia kasi ya mageuzi nchini. Lengo la Wizara ni kuainisha na kuhuisha tafiti hizi ili yatokanayo yatekelezwe kwa pamoja kwa madhumuni ya kuongeza kasi ya mageuzi na ufanisi katika Sekta ya Sheria. Tafiti ni hizi zifuatazo:-

- Utafiti wa kwanza ni kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sheria na kuhuisha kanuni na taratibu zinazoongoza taasisi za kisheria ili zikidhi mabadiliko yanayoendelea nchini kwa lengo la kutoa haki sawa kwa wote. Lengo la utafiti huu ni kuondoa urasimu katika kutoa haki, kuboresha huduma na kuongeza uwajibikaji na usimamizi;
- Utafiti wa pili ni wa namna ya kuboresha usimamizi na mgawanyo wa kazi katika asasi za kisheria ili kuwezesha taasisi kusimamia utekelezaji wa malengo na majukumu. Utafiti umekamilika na unafanyiwa kazi. Madhumuni yake ni kuboresha usimamizi na uwajibikaji katika asasi za kisheria;
- Utafiti wa tatu ni wa namna ya kutenganisha majukumu ya kutoa haki na ya kiutawala kwa nia ya kuongeza ufanisi katika kutoa haki. Lengo ni kuboresha utekelezaji wa majukumu ya msingi (*core functions*), ya asasi za kisheria ili kuongeza kasi ya utoaji haki. Mapendekezo ya awali yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwisho wa mwezi huu;
- Utafiti wa nne ni wa kuangalia kanuni na taratibu zinazoongoza mifuko maalumu (*retention schemes*) ya asasi za kisheria kwa lengo la kuboresha usimamizi na kuhakikisha kuwa ada za huduma za kisheria haziathiri haki sawa kwa wote. Lengo ni kuhakikisha kuwa huduma za kisheria zinalingana na malipo (*value for money*) na uwezo wa wote; na

- Utafiti wa tano ni kwa ajili ya maandalizi ya mkakati wa muda mrefu wa mafunzo katika asasi za Sekta ya Sheria wenyе lengo la kuhuisha mafunzo na wajibu wa mtumishi katika kutekeleza malengo na majukumu ya asasi husika kwa kuzingatia mageuzi yaliyopo nchini na kimataifa. Aidha, utafiti unaangalia namna ya kuboresha taasisi za mafunzo ya Sheria nchini kwa ajili ya mafunzo endelevu kwa watumishi wa asasi za kisheria.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Quick Start* pia unagharimia uboreshaji wa mfumo wa kusimamia haki za Watoto Watukutu. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa hivi sasa Idara ya Mahakama inapitia na kuhakiki michoro ya ukarabati wa Mahakama ya Watoto Kisitu na ujenzi wa Mahakama za Watoto Mtwara na Mbeya ili kuona kama michoro inazingatia vigezo muhimu vya Mahakama za Watoto kwa lengo la kuongeza idadi ya Mahakama za watoto nchini. Aidha, mafunzo yanayolenga kubadili mwelekeo katika usimamizi wa haki za watoto Watukutu yametolewa kwa Majaji, Wasajili wa Mahakama Rufani, Mahakama Kuu, Mahakimu, Makarani wa Mahakama, Mapolis, Maofisa Magereza na Maafisa Ustawi wa Jamii. Washiriki wa mafunzo haya waliainisha matatizo yaliyopo katika mfumo mzima wa utoaji haki kwa Watoto Watukutu ambayo Idara ya Mahakama kwa kushirikiana na Wadau imendaa mpango wa kuyatatuu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pia taarifa ya majaribio ya uboreshaji wa Mahakama za Mwanzo na za Wilaya katika Mikoa ya Arusha na Manyara yanayotekelawa chini ya Mradi wa *Quick Start*. Wilaya zote za Mkoa wa Manyara zimekamilisha taratibu za kuteua Washauri wa Majengo (*Consulting Engineers*) na kazi sasa inaendelea vizuri. Hatua hiyo imekamilika katika Wilaya za Monduli, Arusha na Arumeru. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa kipekee wananchi wa Wilaya ya Mbulu kwa kujitolea kukarabati na kuziwekea mipaka Mahakama zilizopo Wilayani na pia kwa wananchi wote wa Mikoa hii pamoja na uongozi mzima wa Mikoa ya Arusha na Manyara kwa kujitolea nguvu zao katika maandalizi ya ujenzi wa Mahakama hizo na ushirikiano waliouonyesha kwa Wizara yangu hususan kwa Idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Capacity Building* ambao ulimalizika mwezi Januari 2004 na ambao uligharamiwa na Benki ya Dunia, lengo lake lilikuwa kuimarisha na kujenga uelewa wa namna ya kuendesha mfumo wa mageuzi wa kurekebu Sekta ya Sheria ili kuimarisha uongozi na usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati wa Kurekebu Sekta ya Sheria. Katika kufanikisha matayarisho hayo, Mradi ultoa fursa kwa Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji kutembelea nchi za India, Malaysia na Jamhuri ya Afrika ya Kusini kujifunza mbinu za kufanikisha mageuzi katika Sekta ya Sheria. Vile vile, chini ya mradi huo, Warsha ya Kitaifa iliendeshwa ambapo Mkakati wa Muda wa Kati wa kurekebu Sekta ya Sheria (*Medium Term Strategy for the Legal Sector Reform Programme*) ulijadiliwa na kuhuishwa. Aidha, Mradi huu umegharamia utaratibu wa kuanzisha mfumo wa mawasiliano na elimu kwa njia ya majarida na asasi za vyombo vya habari kama redio na televisheni ili kuhamasisha jamii.

Mheshimiwa Spika, chini ya maandalizi ya mradi wa *Tanzania Accountability Transparency and Integrity Project (ATIP)*, kwa upande wa Sekta ya Sheria, imeandalisha taarifa ya awali ya hali ya majengo ya Mahakama inayoainisha mahitaji ya ukarabati na ujenzi na tayari viwanja kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama ya Rufaa vimepatikana. Hivi sasa unaandalisha Mpango wa Ujenzi na Uboreshaji wa Majengo ya Mahakama ambao utajadiliwa na warsha ya Wadau hivi karibuni. Lengo ni kushirikisha Wadau katika kuainisha mahitaji ya kipaumbele na yale ya kijamii, na majukumu ya utekelezaji na hatimaye kuwa na mpango unaotekelzeza. Aidha, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Kisutu ambayo ndiyo kioo cha Mahakama za Wilaya, itapewa kipaumbele katika Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mradi huu wa *Tanzania Accountability Transparency and Integrity Project (ATIP)* yanajumuisha pia Mpango wa kuanzisha *Law School* ambao ulijadiliwa katika kikao cha Wadau mwezi Aprili, 2004 kwa lengo la kuhuisha jukumu la kila mdau na mwelekeo mzima wa kuanzisha *Law School*. Naomba nililieleze Bunge lako Tukufu kuwa *Law School* ina umuhimu wa kipekee kwa taaluma ya wanasheria kwa kuwa itasaidia kuboresha maadili na mazoezi ya vitendo kwa wahitimu wa fani ya Sheria kabla ya kuajiriwa au kujajiri na kuwezesha kuwapo kwa fursa ya majadiliano ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zoezi la kuimarisha majengo ya Mahakama chini ya mradi huu wa *ATIP* litachukuwa muda mrefu kukamilika, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athuman Janguo, Mbunge wa Kisarawe, iliiagiza Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuandaa Mpango Endelevu wa Mahakama za Mwanzo. Wizara yangu ilianda Mpango huo na kuuwakilisha Wizara ya Fedha ambayo imetoa fedha za utekelezaji wa mpango huo. Lengo la Mpango huo, ambao utekelezaji wake umegawanywa katika awamu tano ni kuimarisha majengo na vitendea kazi vingine katika Mahakama za Mwanzo zote katika mikoa ya Tanzania Bara. Mpango huu Endelevu wa Mahakama za Mwanzo unatarajiwa kugharimu kiasi cha Sh. 54.22 bilioni. Kwa kuanzia, Wizara ya Fedha imetenga kiasi cha Sh. 1.0 bilioni kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo kwa Mwaka huu wa Fedha. Kutokana na umuhimu wa Mpango Endelevu wa Mahakama za Mwanzo utekelezaji wake utasimamiwa na Kamati ndogo ya Wataalam kutoka Wizara yangu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ujenzi na Idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika kuinua viwango vya utendaji kazi na kuongeza ufanisi, Watumishi walipatiwa mafunzo ya aina mbalimbali yanayohusu uboreshaji utendaji katika Sekta ya Sheria. Mafunzo yaliyotolewa yalikuwa ya muda mrefu, muda mfupi, semina na warsha ndani na nje ya nchi. Kwa upande wa Mahakama idadi ya watumishi waliopata mafunzo ya muda mrefu ni 81 na muda mfupi ni 106 na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali watumishi waliopata mafunzo ya muda mrefu ni 11 yakihu shahada za uzamili katika Sheria na muda mfupi ni 32 katika taaluma za Kisheria. Mawakili 79 walipata mafunzo ya kompyuta. Aidha, watumishi wa kada nyingine 38 walipata mafunzo mbali mbali ya muda mfupi ikiwa ni pamoja na haki za kikatiba. Katika kuinua ufanisi na utendaji Mahakamani, Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu ziliongezewa nguvu kwa kuteuliwa Majaji wawili wa Mahakama ya Rufaa na Majaji watatu wa

Mahakama Kuu, Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeongezewa nguvu kwa kuruhusiwa kuajiri Mawakili ishirini.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ambacho kilianzishwa mwaka 1992, kilianza kutoa mafunzo rasmi ya Cheti cha Stashahada na Cheti cha Sheria mwaka 2000/2001. Madhumuni ya Chuo hiki ni kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Idara ya Mahakama na Taasisi nyingine zinazohusiana na utoaji haki kwa lengo la kuinua na kuboresha viwango vya kazi na ujuzi katika Sheria. Walengwa wakuu ni Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama. Uwezo wa Chuo hiki ni kufundisha jumla ya Wanafunzi 131 wa Stashahada na Cheti kwa mwaka ikilinganishwa na maombi 720 yaliyopokelewa na Chuo ambao wana uwezo wa kuchukua mafunzo hayo. Kutokana na tatizo la majengo, hasa madarasa na mabweni, limekuwa kikwazo kuongeza wanafunzi katika Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii pia kuelezea ushiriki wa Wizara yangu katika kushughulikia masuala ya kitaifa yanayohusiana na vita dhidi ya rushwa na kupunguza umasikini. Masuala haya yote ni muhimu katika kufanikisha kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Katika kupambana na suala la rushwa, Wizara yangu katika Mwaka wa Fedha 2003/2004, iliendesha warsha tatu kwa watumishi wake. Semina hizo zilikuwa muhimu kwa Sekta hii ya Sheria ambayo ni mhimili wa utoaji wa haki. Aidha, Wizara iliendesha semina moja ya kujadili mapitio ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini kwa kuwashirikisha Wadau mbali mbali. Michango ya Wadau hao itatusaidia sana katika utekelezaji wa jukumu letu la utoaji wa haki na kusimamia Sheria hapa nchini. Wizara pia iliendesha warsha ya kuandaa Mpango wa Kupambana na Ukimwi katika Sekta ya Sheria. Mpango huu utawasilishwa wenye Tume ya Kupambana na Ukimwi (*TACAIDS*), kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieza kwa kirefu Bunge lako Tukufu, juu ya matatizo yanayoikabili Sekta ya Sheria. Katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2003/2004, pamoja na mafanikio yake, Sekta ya Sheria kwa ujumla wake imeendelea kukabiliwa na matatizo ambayo yanaathiri kasi na ufanisi wa utendaji. Matatizo hayo yametokana hasa na ufinyu wa Bajeti ya Serikali. Ufinyu huo wa Bajeti umeendelea kuathiri utoaji na usimamizi wa haki na utawala wa Sheria. Baadhi ya athari zilizokuwepo ni ubovu na uchakavu wa vitendea kazi, uchakavu, uhaba na ukosefu wa majengo ya Mahakama na ofisi na uhafifu wa mawasiliano na miundo mbinu kwa Sekta nzima ya Sheria. Vile vile, Sekta ya Sheria imeendelea kuwa na upungufu wa watumishi hasa Majaji, Mawakili wenye uzoefu na Mahakimu. Aidha, pamoja na kuwa Wilaya zote zina Bodi za Mahakama, Bodi hizo zimekuwa hazifanyi vikao vyake kulingana na utaratibu uliowekwa kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea mafanikio na matatizo katika kipindi cha mwaka 2003/2004, sasa napenda nielezee Mpango na Malengo ya mwaka 2004/2005. Pamoja na Wizara kuendelea kulenga kutekeleza Dira yake ya Haki kwa Wote na kwa Wakati, kauli mbiu ya mwaka 2004/2005 ni Kuboresha Mfumo wa Sekta ya Sheria. Lengo kuu la kauli mbiu hiyo ni kuharakisha utoaji haki kwa Wananchi kwa nia ya kupunguza umaskini na kuendelea kuimarisha utawala bora. Hivyo katika kuhakikisha

kwamba haki inapatikana kwa wote na kwa wakati, tutazingatia taratibu tulizojiwekea katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nilielezea juu ya umuhimu wa kuwa na Sera ya Sekta ya Sheria na kwamba Wizara ilikuwa katika maandalizi ya uandaaji wa Sera hiyo. Katika Mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara itaendelea kutoa umuhimu katika uandaaji wa rasimu ya Sera hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nzungumzie mipango na malengo ya Sekta ya Sheria katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Sekta ya Sheria imepanga kuboresha huduma zake za kisheria ili kuendelea kuchangia katika vita ya kupunguza umaskini na vita dhidi ya rushwa. Ili kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri nchini, mambo yafuatayo yamepangwa kutekelezwa:-

- Kwanza, muundo wa Idara ya Mahakama unatarajiwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuwa na Maafisa Utawala (*Court Administrators*) ili kusimamia masuala ya utawala katika kuimarisha mgawanyo wa kazi na madaraka. Aidha, mhimili huu utaitwa kwa jina ambalo litatoa maana ya hadhi yake badala ya Idara.

- Pili, katika kuimarisha na kuboresha huduma za uendeshaji kesi za jinai nchini, Wizara inaandaa mpango utakao wawezesha Mawakili wa Serikali kuendesha kesi hadi ngazi za Mahakama za Wilaya. Kwa kuanzia, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itafungua Ofisi zake katika Wilaya ishirini hadi ifikapo mwaka 2009. Katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara itafanya maandalizi ya awali ya kuchagua Wilaya za kuanzia. Aidha, ukaguzi wa Ofisi za Kanda utaimarishwa kwa kuongeza mzunguko wa ukaguzi hadi mara tatu kwa Mwaka huu wa Fedha.

- Tatu, katika kuharakisha usikilizwaji wa mashauri (*fair and timely disposition of cases*), Idara ya Mahakama imeweka mkakati wa kusikiliza na kumaliza mashauri kati ya sita na saba katika kila mashauri 10 yanayopelekwa na kuandikishwa Mahakamani. Ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi, Idara ya Mahakama imeweka mkakati wa kuajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hamsini na tano.

- Nne, utaratibu wa kila Jaji na Hakimu kujipangia kalenda ya kusikiliza kesi kwa wiki, mwezi na mwaka utaendelea kutumika. Aidha, Idara ya Mahakama itaendelea kuwaajiri kwa mikataba Mahakimu Wastaifu wa Mahakama za Mwanzo kuendelea kutoa huduma ya kupunguza mlundikano wa mashauri katika Mahakama hizo.

- Tano, Idara ya Mahakama itaimarisha upatikanaji wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya ofisini, usafiri na majengo ya Mahakama.

- Sita, Mahakama ya Biashara itafungua Masjala ya kuandikisha mashauri ya biashara katika Kanda za Mahakama Kuu za Mwanza, Mbeya na Tanga.

- Saba, Wizara itaendelea kufanya mabadiliko katika Sheria za Mienendo ya Mashauri ya Madai na Jinai ili kuboresha upatikanaji haki kwa wakati.
- Nane, Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu itaimarishwa kwa lengo la kuboresha huduma za usajili na utunzaji takwimu za vizazi, ndoa, vifo, mirathi na udhamini wa mali. Pia, Idara hii kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto na Elimu (*UNICEF*), itaananza mradi wa usajili wa vizazi, ndoa na vifo katika Mikoa ya Ruvuma na Mtwara. Juhudi zinaendelea ili kusambaza mradi huu katika Mikoa yote iliyosalia hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Spika, hapo awali nililielezea Bunge lako Tukufu juu ya umuhimu wa kuwepo kwa Kanuni zitakazoweka utaratibu wa kisheria wa kuteua Wazee wa Baraza. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wanatambua umuhimu na mchango wa Wazee wa Baraza katika utoaji haki hapa nchini. Sheria ya Mahakama ya Mwaka 1984 inampa Waziri wa Sheria uwezo wa kuandaa na kutangaza Kanuni hizo. Maandalizi ya Kanuni hizo yamekwishaanza kwa ushirikiano wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahakama na Mamlaka husika katika Halmashauri za Wilaya. Kanuni hizo zitakamilika na kuanza kutumika kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara inategemea kuimarisha zaidi suala la elimu kuhusu haki za Binadamu hasa katika Wizara, Idara na taasisi zetu za Serikali ili utendaji wetu uonekane kuwa na mtazamo wa kuzingatia masuala ya Haki za Binadamu zaidi. Hii inatokana na ukweli kwamba, lawama nyingi zinazotoka kwa wananchi katika kuilaumu Serikali zinazohusiana na ukiukwaji wa haki za binadamu katika utendaji wa maafisa wa Serikali wa kila siku. Aidha, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itaendelea kuongeza kasi ya uchunguzi wa malalamiko ya wananchi ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati (*Timely Justice*) na pia itatembelea Magereza na vituo vya Polisi katika Wilaya zilizobaki kuhakikisha kuwa haki za binadamu na misingi ya utawala bora inaheshimiwa na kulindwa.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo Wizara itaendelea kuyafanya katika kuimarisha Haki za Binadamu, ni uandaaji wa taarifa zinazohusu utekelezaji wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa juu ya Haki za Binadamu, kuendesha kesi za Kikatiba zinazofunguliwa katika Mahakama Kuu, kusimamia Serikali katika uchunguzi unaoendeshwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nchini, Tume ya Haki za Binadamu na Haki za Watu Barani Afrika na katika Tume ya Haki ya Binadamu ya Umoja wa Mataifa kutokana na Mikataba inayohusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi kirefu sasa yamekuwepo malalamiko kutoka kwa wanazuoni na baadhi ya wananchi kuhusu Sheria mbalimbali kuitwa na wakati na hivyo kuathiri haki za msingi za wananchi. Mionganis mwa Sheria hizo ni Sheria ya Ndoa, Sheria ya Mirathi na Sheria ya Watoto. Kwa kuwa jambo hili linahusu masuala ya kijamii, Serikali imeona umuhimu wa kupata maoni kutoka kwa wananchi kwanza. Wizara itasimamia shughuli ya kukusanya maoni kwa wadau mbali mbali kuhusu uboreshaji wa Sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara itaendelea na majukumu yake ya uandishi wa miswada ya sheria, sheria ndogo ndogo. Wizara, kwa kushirikiana na Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali inatarajia kufunga mitambo ya uchapishaji itakayounganisha Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mpango huu utarahisisha kazi ya utoaji wa nyaraka nyingi za Serikali ambazo zinafanyika kati ya Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Mafunzo yatatolewa juu ya uendeshaji wa mitambo hii kwa Waandishi na Warekebu wa Sheria. Ili kuboresha tafsiri ya Sheria katika lugha ya Kiswahili, kitengo cha tafsiri ya Sheria kitaboreshwu kwa kupatiwa mafunzo ya tafsiri za Sheria na kupatiwa nyenzo za kazi.

Mheshimiwa Spika, pia, Wizara kwa kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria itaendelea na utafiti, uchambuzi, na uhuishaji wa sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na utafiti wa Sheria ya Ukimwi (*HIV/AIDS*) na kukamilisha utafiti wa Sheria za *Flow of Justice* na Polisi na Magereza. Aidha, Wizara hii itaendelea kutoa ushauri wa kisheria kwa Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya Sheria za Kimataifa pamoja na kuiwakilisha katika mashauri mbali mbali ya madai.

Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Kati wa Programu ya Kurekebu Sekta ya Sheria (*Medium Term Strategy for the Legal Sector Reform Programme*), ulihuishwa kama nilivyoeleza awali. Mkakati huo unayo majukumu yafuatayo: Kurekebisha na kuhuishwa mfumo wa Sheria, kuimarisha Mfumo wa Utawala na Ushirikiano kati ya Taasisi za Sheria, kuimarisha mafunzo kabla ya ajira, kuimarisha utoaji wa haki kwa maskini na wasio na uwezo, kuboresha majengo na vitendea kazi katika Taasisi za Sheria na kuimarisha uendeshaji wa programu na kuweka Mfumo imara wa Usimamizi na Tathimini katika Sekta ya Sheria.

Hivyo, katika mwaka wa 2004/2005, Wizara itatekeleza majukumu machache ambayo yatakuwa ni kuimarisha usimamizi na uratibu wa utekelezaji wake kwa kushirikiana na asasi zote ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusika katika kutoa haki. Nia ni kuongeza kasi ya utoaji haki kwa kuhakikisha kuwa kila asasi inatekeleza jukumu lake kwa wakati na zinajumuika pamoja katika urekebu na kuimarisha uongozi, usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa programu.

Mheshimiwa Spika, asasi za kisheria zitakazohusika katika utaratibu huu ni pamoja Idara za Polisi na Magereza, Wizara ya Mambo ya Ndani, Idara ya Ustawi wa Jamii, Wizara ya Kazi, Vijana na Maendeleo ya Michezo pamoja na Mashirika yasiyo ya kiserikali. Utaratibu huu wa pamoja unajulikana kama *Sector Wide Approach*. Aidha, Wizara inalenga kuongeza uwezo wa asasi tekelezi katika kusimamia na kutekeleza majukumu yake katika kurekebu Sekta ya Sheria kwa kutoa mafunzo na kuandaa warsha na makongamano yanayohusu utekelezaji wa *Sector Wide Approach Programme* ikijumuisha na mkutano ya mwaka wa kisekta kwa ajili ya kutathmini utendaji na utekelezaji wa programu.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua kuwa urekebu wa Sekta ya Sheria ni jukumu pana na zito hasa ikizingatiwa kuwa Sheria ni muhimu katika kila badiliko na

kichocheo cha amani na utulivu nchini. Hivyo basi, Wizara inabidi kujizatiti ili kuongoza na kuratibu mabadiliko haya muhimu kitaifa kwa kuhakikisha kuwa kila mdau anashirikishwa katika hatua zote na kuelewa majukumu na malengo ya pamoja. Kwa kuzingatia haya, Wizara inalenga kuchukua hatua zifuatazo ili kufanikisha utekelezaji wa pamoja:-

- Kuandaa vikao vya ngazi mbali mbali vitakavyofanyika kati ya Julai na Septemba 2004. Vikao hivi ni vile vya viongozi watendaji wa asasi tekelezaji, warsha ya kitaifa ya Wadau, kikao cha ushauri na Wafadhili na kikao cha Kamati ya Uongozi. Lengo ni kuhakikisha panakuwa na ueleo na utekelezaji wa pamoja wa majukumu ili kuongeza kasi na kupata nyenzo kwa ajili ya utekelezaji;
- Maandalizi ya Mradi wa *ATIP* yanaendelea na mradi unafadhiliwa na Benki ya Dunia na utekelezaji wake utaanza taratibu za maandalizi zikikamilika;
- Ujenzi wa Mahakama za watoto Mbeya na Mtwara na ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mikoa ya Manyara na Arusha unakamilika chini ya Mradi wa *Quick Start*;
- Kutekeleza mradi wa Improving the Legal Framework for Economic Development utakaogharamiwa na Serikali za Ujerumani na Tanzania wenyе lengo la kuhuisha Sheria na mabadiliko ya kiuchumi ili kuongeza kasi ya uwekezaji nchini. Mradi utagharamia ushauri, vifaa vya ofisi na mafunzo ya ndani na ya nje ya nchi. Madhumuni ya mafunzo haya ni kuongeza ujuzi wa kuongeza mabadiliko (*Change Management*) kwa watawala wa vyombo vya kisheria, utafiti wa kisheria na maendeleo ya kisheria; na
- Kuanza utekelezaji wa mradi wa *Strengthening Good Governance in Delivery of Justice* unaofadhiliwa na Serikali ya Ubeligiji na Tanzania wenyе lengo la kuboresha utawala bora katika utoaji haki. Mradi utagharamia ushauri, samani na vifaa vya ofisi na mafunzo ya ndani na ya nje ya nchi. Ushauri utalenga katika uboreshaji wa mfumo wa usimamizi na utoaji haki, wakati mafunzo yatalenga katika kuboresha uwezo wa kuzingatia usimamizi na uwajibikaji kwa Watumishi wa vyombo vya kutoa haki hususan kubadili tabia na mwenendo ili kujenga maadili ya Wafanyakazi.

Yote haya yanalenga kuongeza kasi ya utekelezaji wa programu ikiwa ni pamoja na kuboresha utendaji katika asasi za kisheria ili kuongeza kasi ya utoaji haki sawa kwa wote kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara hii imelenga kuendelea na uboreshaji wa hadhi na uimarishaji wa vyombo vya utoaji haki nchini na kuvirudishia hadhi kama ifuatavyo:-

- Kuboresha mazingira ya kazi katika ofisi zote za Sekta ya Sheria yaani Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria;
- Kuanza utekelezaji wa Mpango Endelevu wa Mahakama za Mwanzo;

- Kuzipatia vitendea kazi muhimu Mahakama zote na ofisi zote; na
- Kuendelea kuboresha upatikanaji wa vyombo veya usafiri.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama, Wizara yangu inafanya jitihada mahsusizi za kuweza kukipanua Chuo hiki cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kiweze kukidhi mahitaji ya Sekta ya Sheria na pia kuwa Kitovu cha Mafunzo (*Centre of Excellence*) katika nyanja za Sheria katika Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki. Juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa ni pamoja na kuongeza majengo ya madarasa na mabweni na kuimarishe na kupanua Mitaala ya Masomo ili kupanua uwezo wa Chuo kutoa mafunzo, utafiti na ushauri wa Kisheria. Idara ya Mahakama inafanya mazungumzo na Shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*National Social Security Fund - NSSF*), ili Shirika hili liweze kugharamia ujenzi wa majengo muhimu kwenye Chuo hicho.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara itaimarisha juhudzi za kuongeza ufanisi katika Sekta ya Sheria kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa Wateja na Wananchi kwa ujumla. Hivyo, Wizara imedhamiria kufanya yafuatayo:-

- Kuwaongeza viwango veya elimu Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 68, Makarani wa Mahakama 20 na watumishi mbalimbali katika Sekta ya Sheria;
- Kuwasomesha Mawakili wa Serikali 10 katika viwango veya shahada ya uzamili, 28 katika mafunzo ya muda mfupi na watumishi wengine 20 katika mafunzo mbalimbali ya muda mfupi;
- Kuwapandisha vyeo watumishi wa ngazi mbali mbali na kuajiri watumishi wapya hasa Mahakimu, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine; na
- Kuboresha mazingira ya kazi na motisha kwa watumishi katika Sekta.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu sote, UKIMWI ni janga la kitaifa na dunia kwa ujumla. Janga hili limekuwa likiathiri utendaji na kupunguza nguvu kazi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara, kwa kushirikiana na Wadau wengine itaendeleza jitihada zake za kutoa elimu ya ukimwi kwa watumishi wake ili kukabiliana na janga la ukimwi. Aidha, Wizara yangu itaendelea kufanya utafiti juu ya Sheria ya UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni tatizo kubwa katika jamii yetu na madhara yake Kitaifa ni makubwa kwa sababu inavuruga mfumo wa haki na kusababisha kuvurugika kwa umoja, uwajibikaji na kuheshimiana kati ya wanajamii. Jamii imekuwa ikilipigia kelele sana suala hili la rushwa ambalo mara nyingi limekuwa likiigusa Sekta ya Sheria. Katika Mwaka wa Fedha wa 2004/2005, Wizara yangu imepanga kufanya yafuatayo: -

- Moja, Wizara, kwa kushirikiana na Taasisi husika, itaimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa;
- Pili, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyinginezo husika za Serikali itaiangalia upya Sheria ya Kuzuia Rushwa (*Prevention of Corruption Act, 1971*) na Sheria zote zinazohusiana ili kuzirekebisha na kuzipa makali kwa lengo la kuwadhibiti wale wanaojihusisha na rushwa ili kupunguza tatizo hilo na ikiwezekana kulitokomeza;
- Tatu, kufanya tathmini ya vyanzo vya rushwa kwa lengo la kuvibaini na kuweka mkakati wa kupambana na kuvidhibiti vyanzo hivyo;
- Nne, Wizara itaendelea kuendesha warsha mbalimbali kwa wafanyakazi wake juu ya kupambana na rushwa katika Sekta ya Sheria kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Majaji January H. Msiffe na Simon N. Kaji, walioteuliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Julai, 2003 kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani na Waheshimiwa Thomas B. Mihayo, Fakhi A.R. Jundu na Mariam S. Shangali, kuwa Majaji wa Mahakama Kuu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwatachia maisha mema, Waheshimiwa Majaji Nathaniel A. Mushi, Mathias D. Nchalla na Boniface P. Moshi, ambao wamestaafu katika utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hotuba yangu kwa kuwashukuru Viongozi na Watendaji Wakuu na Watumishi wote katika Wizara yangu ambao kwa kipindi kirefu wamekuwa wakinipatia msaada mkubwa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kuiongoza Wizara. Naomba niwataje kwa majina Mheshimiwa Jaji Mkuu Barnabas Albert Samatta, Mheshimiwa Jaji Kiongozi Hamis A. Msumi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew J. Chenge, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mheshimiwa Jaji Robert H. Kisanga, Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mheshimiwa Jaji Anthony Bahati na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Sheria Tanzania, Bibi Mwanaidi Maajar. (*Makofî*)

Aidha, nawashukuru Watendaji Wakuu wa vyombo mbalimbali viliyyo chini ya Wizara hususan Bwana Johnson P.M. Mwanyika, Naibu Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu wa Wizara, Bwana Augustine G. Mwarija, Msajili wa Mahakama ya Rufani Tanzania, Bw. Matty Chikawe, Kaimu Katibu Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Bw. Gad J. K. Mjemas, Katibu Mtendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Bibi Daria Bigeye, Kaimu Mshauri Mkuu wa Shirika la Sheria Tanzania. Msaada wao umenisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa nchi wahisani na taasisi za Kimataifa, ambazo zimeendelea kutoa misaada mbalimbali kwa ajili ya kuiendeleza na kuisaidia Sekta ya Sheria nchini. Naomba niwataje kwa majina, Serikali ya Canada, Denmark, Ujerumani, Ireland, Marekani, Uingereza, Finland, Norway, Uhlanzi, Sweden na Mashirika ya Kimataifa ya Benki ya Dunia, *UNDP, USAID, Ubelligji, CIDA* na *SIDA*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe mwenyewe, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza malengo na majukumu yake yaliyoainishwa kulingana na mwelekeo kwa Mwaka wa Fedha 2004/2005 na kama yalivyochambuliwa katika vitabu nya makisio, naomba Bunge lako Tukufu, likubali Wizara yangu ipatiwe jumla ya Shs.35,018,793,300/= ambazo kati ya hizo, Sh. 4,285,955,000/= ni fedha za nje. Mchanganuo wake ni kama ufuatao:-

- (i) Fungu 40: Idara ya Mahakama

| | |
|-----------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. 18,972,395,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo | Sh. 2,700,000,000/= |
| Jumla | Sh. 21,672,395,000/= |
- (ii) Fungu 41: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|-------------------------------|---------------------|
| Matumizi ya Kawaida | Sh. 5,336,708,700/= |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | Sh. 300,000,000/= |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | Sh. 4,133,455,000/= |
| Jumla | Sh. 9,770,163,700/= |
- (iii) Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

| | |
|---------------------|---------------------|
| Matumizi ya kawaida | Sh. 2,153,000,100/= |
| Jumla | Sh. 2,153,000,100/= |
- (iv) Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

| | |
|---------------------|-------------------|
| Matumizi ya kawaida | Sh. 501,459,100/= |
| Jumla | Sh. 501,459,100/= |
- (v) Fungu 64: Mahakama ya Biashara

| | |
|-----------------------------|-------------------|
| Matumizi ya kawaida | Sh. 611,252,400/= |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | Sh. 152,500,000/= |
| Jumla | Sh. 763,752,400/= |
- (vi) Fungu 90: Mahakama ya Ardhi

| | |
|---------------------|-------------------|
| Matumizi ya kawaida | Sh. 459,023,000/= |
| Jumla | Sh. 459,023,000/= |

Mheshimiwa Spika, Makusanyo ya Maduhuli kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2004/2005, Wizara hii imekisia kukusanya kiasi cha Sh. 1,846,333,271/= kama maduhuli ya Serikali kwa mchanganuo ufuatao:-

- Fungu 40: Sh. 482,404,000/=
- Fungu 41: Sh. 343,267,271/=
- Fungu 55 Sh. 662,000/=
- Fungu 59: Sh. -

Fungu 64: Sh. 1,000,000,000/=
Fungu 90: Sh. 20,000,000/=
Jumla **Sh. 1,846,333,271/=**

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wasemaji watano wa mwanzo watakuwa ni Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, akifuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekiffu, baada yake ni Mheshimiwa Ali Said Salim, baada yake ni Mheshimiwa Wilfred Lwakatare na wa tano ni Mheshimiwa Dr. William Shija. Sasa namwita Mwakilishi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Jenista Mhagama, awasilishe maoni ya Kamati. (*Makofî*)

MHE. JENISTA J. MHAGAMA (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kanuni Na. 81(1) ya mwaka 2004, naomba kutoa maoni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji na mapendekezo ya Matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2004/2005 ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, aidha, kabla sijafanya hivyo, naomba nichukue nafasi hii kwa mara nyingine, kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa na Wananchi wa Bariadi Mashariki kuwa Mbunge wao. Wananchi hao wameonesha imani kubwa walijonayo kwake, nasema Mheshimiwa Danhi Makanga karibu tena Bungeni. (*Makofî*)

Pia naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyesariki ghafla hapa Dodoma akiwawakilisha Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijiji, tarehe 24 Juni, 2004. Kifo chake ni msiba mkubwa kwa Bunge letu Tukufu na Jimbo alilokuwa analiwakilisha la Mbeya Vijiji. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, wanaainishwa katika kanuni ya 87(1)(2), Toleo la 2004 na kanuni ya 93(1), Toleo la 2004 na ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Athumani Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka

Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhan Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Pascal Degera na Mheshimiwa Nimrod Mkono.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala yameelezwa katika kanuni Na.93(2), Toleo la 2004 na yanatajwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kusimamia bajeti ya Wizara zinazohusika na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.
- (b) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara zinazosimamiwa na Kamati yetu.
- (c) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.
- (d) Kufuutilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kupitia utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2003/2004, Kamati ilipitia maagizo yake kwa Wizara, yaliyotolewa wakati wa kuijadili bajeti inayomalizika hivi sasa kama ifuatavyo:-

- (a) Mahakama zenyе hali mbaya zikarabatiwe na nyingine zijengwe, pia zipatiwe vitendea kazi na usafiri ili kufanikisha na kurahisisha kazi pamoja na kuimarisha shughuli za Ukgazi wa Mahakama za Mwanzo. Hali kadhalika madeni kwa Wazee wa Baraza wa Mahakama za Mwanzo ambao wanaidai Serikali yalipwe.
- (b) Mafunzo yatolewe kwa Idara ya Uandishi wa Sheria.
- (c) Wizara itenge fedha za kukarabati ofisi na kununua vifaa vya kisasa. Sheria ya Vizazi na Vifo ifanyiwe marekebisho ili iendane na mabadiliko yanayotokea nchini na nje ya nchi.
- (d) Katika marekebisho ya Katiba ya nchi yanayotarajiwa kufanyika, haki ya mtu kushiriki uchaguzi kama mgombea binafsi iangaliwe na kufanyiwa kazi, hususan kwa ngazi ya Ubunge na Udiwani.
- (e) Sheria za Mienendo ya Kesi za Madai na Jinai zitazamwe upya na kurekebishwa ili kuondoa mapungufu yaliyojitokeza. Pia Wizara isisitize ufuutiliaji wa taratibu zilizopo hususan kwa kutoa vifungo vya nje kwa makosa madogo ili kuondokana na tatizo la mlundikano wa mahabusu.

(f) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ifanye ziara pia katika Magereza ya Wilaya na kujionea ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu unavyofanyika huko.

(g) Kuwepo na utaratibu wa mihimili mitatu ya Dola yaani Serikali, Bunge na Mahakama, kugawana mapato ya Taifa kwa uwiano ili kila mmoja aweze kutekeleza malengo yake kikamilifu.

(h) Wabunge na Wadau wengine wawe wanashirikishwa katika hatua za mwanzo za maandalizi ya Bajeti ya Serikali ili wachangie maoni kuhusu maeneo ya kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa Wizara imejitahidi kutekeleza maagizo na maoni ya Kamati ingawa ufinyu wa bajeti umefanya utekelezaji huo kuwa mgumu. Kwa mfano, ukarabati wa Mahakama za Mwanzo haujatekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha. Katika maeneo kadhaa utekelezaji uko katika ngazi mbalimbali kufuatana na fedha zilizopatikana.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati kuhusu Wizara hii pia yatahusu Idara ya Mahakama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kurekebisha Sheria, Mahakama ya Biashara na Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia kwa makini sana utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2003/2004, hali kadhalika mapendekezo ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005 na kutoa maoni yafuatayo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kutokana na uchache wa Mahakimu, hasa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, mara kwa mara wamejikuta kila mmoja wao anahudumia zaidi ya Kituo kimoja, lakini watumishi hawa huwa hawana usafiri wowote wa kuaminika kuwapeleka katika vituo hivyo. Hali hiyo inawafanya kutofika au kucheleta kufika kwenye vituo vya ziada na hivyo watuhumiwa kucheleweshewa kesi zao.

(b) Mheshimiwa Spika, bado katika Magereza yetu kuna wafungwa na watuhumiwa wengi ambao kwa muda mrefu baadhi yao ama kesi zao hazijasikilizwa au hawajapata nakala ya hukumu zao. Hali hii inasababisha mlundikano katika Magereza yetu pamoja na malalamiko ya watuhumiwa kutotendewa haki.

(c) Mheshimiwa Spika, hali ya majengo ya Mahakama zetu nchini ni mbaya kwa Mahakama za Mwanzo na Mahakama za Wilaya. Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa mipango ya kukarabati majengo hayo inaendelea, lakini hali hii hajijonyeshi katika bajeti ya Wizara. Kwa bahati nzuri Kamati hii ilipata nafasi ya kutembelea Mahakama katika Wilaya za Mpwapwa, Dodoma na Lushoto, ambako majengo ya Mahakama zao zote yako katika hali mbaya sana.

(d) Kamati ilipotembelea Chuo cha Lushoto iligundua matatizo yafuatayo ambayo yanarudisha nyuma maendeleo ya Chuo: Ufinyu wa majengo kwa maana ya madarasa, Ofisi na mahali pa kulala wanafunzi, ufinyu wa bajeti ambao unasababisha upungufu wa wakufunzi, na vitendea kazi na wahitimu wachache wanaomaliza masomo kutokuajiriwa.

(e) Mheshimiwa Spika, mazingira ya kufanya kazi na Jengo la Kabidhi Wasii si ya kuridhisha na hasa ikizingatiwa kuwa, Ofisi hiyo inatunza kumbukumbu nyingi muhimu kwa Taifa. Bado njia za kizamani zinatumika katika kutunza nyaraka na vitendea kazi katika Ofisi hiyo ni za kizamani. Kamati imeridhika na kauli ya Mheshimiwa Waziri kuwa, mipango ya kulipanua na kulikarabati jengo hilo na kulipatia vitendea kazi vya kisasa inaendelea. Tunaihimiza Serikali ilishughulikie jambo hili haraka.

(f) Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2004/2005, Mahakama ya Biashara imepangiwa ruzuku ya Sh.76 milioni, kwa vile Mahakama hiyo itajiingizia fedha zake yenye kutoptera na ada kwa huduma zake mbalimbali . Kamati inatahadharisha kuwa pamoja na utaratibu wa *Retention Scheme*, baada ya marekebisho ya Sheria Na.4 ya 2004, upo wasiwasi wa Mahakama hiyo kukosa uwezo wa kujiendesha kwa ufanisi iwapo mapato yake hayatafikia kiwango cha matumizi ya Mahakama hiyo. Kwa mfano, Tawi la Mahakama ya Biashara Mjini Arusha, ambalo limeanza kujengwa na Wafadhili, halitaweza kutumika mwaka huu iwapo halitapata fedha zaidi kutoka Serikalini.

(g) Mheshimiwa Spika, ingawa Bunge hili lilipitisha Sheria Na 2 ya mwaka 2002 iliyounda Mahakama za Ardhi katika ngazi za Wilaya na Kata, Mahakama hizo bado hazijaanza kufanya kazi. Mheshimiwa Waziri ameieleza Kamati kuwa, liliuwepo tatizo la uchache wa Mahakimu, lakini sasa limetatuliwa kwa kupelekwa Mahakimu Wakazi 20 katika Wizara ya Ardhi ili waanze kazi yao mara moja. Ni matumaini yetu kuwa mchakato wa kisheria utaharakishwa ili Mahakimu hao waanze kazi haraka iwezekanavyo.

(h) Mheshimiwa Spika, yamejitokeza matatizo kadhaa katika kutekeleza baadhi ya miradi hususan katika mpango wa *Quick Start*, ambapo mradi umechelewa kuanza kutoptera na sheria ya manunuzi ya mwaka 2001 (*Procurement Act, 2001*), inayohusu manunuzi ya vifaa ambayo ina urasimu mkubwa. Tunafurahi kuwa Serikali imeliona hilo na kuahidi kuifanya marekebisho sheria hiyo kupitia Wizara ya Fedha ili isiwe kikwazo kwa utendaji bora. Ni matumaini yetu kuwa sheria hiyo italetwa Bungeni kwa marekebisho haraka ili isiendelee kudumaza juhudzi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni hayo, Kamati inatoa mapendekezo yafuatayo ili kuboresha utendaji kazi katika Wizara hiyo:-

(a) Kamati inashauri kuwa Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wapatiwe usafiri katika utaratibu uliotumika kwa Makatibu Tarafa. Vinginevyo basi utumike utaratibu wa kuwapatia mikopo.

(b) Ili kupunguza tatizo la ukosefu wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya, mkakati unaosubiri kutekelezwa katika Chuo cha Lushoto uanze kutekelezwa bila ya kuchelewa.

(c) Kwa kuwa baadhi ya wahitimu wa Chuo cha Lushoto wamekuwa wakikosa ajira, Serikali iiondoe dosari hii kwa kuwaajiri wahitimu wote wanaofaulu chuoni hapo.

(d) Idara za Mahakama na Polisi zishirikiane ili kuhakikisha kuwa hakuna msongamano wa mahabusu katika magereza yetu.

(e) Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu mahsus wa kukarabati Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo ili ziwe na sura ya Kimahakama ikiwa ni pamoja na kupeleka vitendea kazi kama vile makabati ya kuhifadhia nyara, samani nyinginezo, karatasi, kalamu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni na mapendekezo hayo, naomba sasa niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu ilipitia na kuidhinisha mapendekezo ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya jumla ya Sh.35.018,743,300/= kwa mgawanyo ufuatao:-

Fungu 40 - Mahakama: Matumizi ya kawaida Sh.18,972,395,000/=,
Matumizi ya maendeleo Sh. 2,700,000,000/=, jumla Sh.21,672,395,000/=.

Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Matumizi ya kawaida Sh. 5,336,708,700/=, Matumizi ya Maendeleo (Ndani) Sh. 300,000,000/=,
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh.4,133,455,000/=, jumla Sh.9,770,163,700/=.

Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora: Matumizi ya kawaida Sh. 2,153,000,000/=, Matumizi ya maendeleo hakuna, jumla Sh. 2,153,000,000/=.

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania: Matumizi ya kawaida Sh. 501,459,100/=, Matumizi ya maendeleo hakuna, jumla Sh. 501,459,100/=.

Fungu 64 - Mahakama ya Biashara: Matumizi ya kawaida Sh. 611,252,400/=,
Matumizi ya Maendeleo (Nje) Sh. 152,500,000/=, jumla Sh. 763,752,400/=.

Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi: Matumizi ya kawaida Sh. 459,023,000/=,
Matumizi ya maendeleo hakuna, jumla Sh. 459,023,000/=. Jumla Kuu ya Bajeti nzima ni Sh.35,018,793,300/=.

Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nitoe maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2003/2004 na mapendekezo ya bajeti ya 2004/2005.

Pia nachukua nafasi hii kuwashukuru Mheshimiwa Bakari H. Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa J.P.M. Mwanyika, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Katibu Mkuu, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, Mwenyekiti Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mwenyekiti Tume ya Kurekebisha Sheria, Mkurugenzi Mahakama ya Ardhi, Mkurugenzi wa Mahakama ya Biashara na Kabidhi Wasii Mkuu, pamoja na watumishi wote wa Taasisi hizo walioshiriki kuandaa taarifa zilizoletwa mbele ya Kamati, kwa ushirikiano wao na maelezo mazuri mbele ya Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Wajumbe wenzangu, kwa michango yao kwa lengo la kuboresha ufanisi na utendaji kazi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Nampongeza Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa na Wasaidizi wake, Ndugu Ernest Zulu, Ndugu Aggrey Nzowa na Ndugu Emmanuel Mpanda, kwa kazi nzuri ya kuihudumia Kamati hii hata kuweza kutoa taarifa hii, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda niseme kuwa, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naiunga mkono hoja na bajeti ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba pamoja na Taasisi zake zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. DR. WILBROD P. SLAA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani na ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kazi waliyofanya.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina jukumu kubwa la kusimamia utoaji haki kwa Wananchi, kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa, kuishauri Serikali kuhusu masuala ya sheria kwa lengo la kudumisha Utawala Bora, amani na utulivu na ustawi wa jamii, hali ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kambi ya Upinzani inadhani Wizara hii bado ina kazi kubwa katika kutekeleza majukumu haya.

Ni kweli kuwa kesi mbalimbali zinaendeshwa katika Mahakama za ngazi mbali mbali, Miswada mbalimbali ya sheria inawasilishwa Bungeni kwa nia na lengo la kupitishwa kuwa sheria, taasisi mbalimbali chini ya Mahakama zinajengwa, japo siyo kwa kasi ya kuridhisha. Lakini, kazi ya msingi ya Wizara hii, bado kabisa kutekelezwa na ndiyo maana kuna malalamiko kutoka kona mbalimbali za nchi yetu, kuhusu utekelezaji au uporaji wa haki mbalimbali. Kambi ya Upinzani inapenda kudodosa maeneo kadhaa ambako utekelezaji wa haki bado haujasimamiwa kikamilifu.

Ngazi ya kijiji ndiyo msingi wa Utawala Bora. Pamoja na kuwepo kwa sheria Na 7 na Na. 8, mambo yanayofanyika katika vijiji vyetu bado ni vya kutia aibu na kuchafua sifa njema ya nchi yetu. Kati ya Mwezi Januari na Aprili, 2003, katika Kijiji

cha Mang'aka Wilaya ya Masasi, kwa mfano, Viongozi wa Serikali ya Kijiji, walipigwa viboko mbele ya wake zao na wajukuu zao katika mikutano ya hadhara, kwa kilichoitwa kutotimiza amri ya Mkuu wa Wilaya, lakini hawakupelekwa kwenye chombo chocote cha sheria. Mkuu wa Wilaya kajichukulia jukumu la kutoa adhabu kana kwamba nchi hii haina sheria wala taratibu. Walipokwenda kuchukua *PF 3* walinyimwa na Polisi na Viongozi kutishwa na kuwekwa rumande. Hii ni hali ya hatari sana. Tafsiri sahihi ya amri halali ya Mkuu wa Wilaya, inahitajika haraka sana, ili haki za msingi zisikiukwe.

Katika Wilaya ya Karatu mwezi Juni, 2004, Viongozi wa Idara ya Afya, waliokwenda kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu, badala ya kutoa elimu waliwapiga Wananchi, tena hata wasiohusika na isitoshe licha ya kupigwa waliwatoza Sh. 3,000/= bila risiti na wengine licha ya kupigwa na kulipa Sh. 3,000/=, bado wamepelekwa Mahakamani. Nina hakika kuna taratibu za kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu, ikiwa ni pamoa na kuwapeleka Mahakamani wahalifu, lakini si kwa Watendaji kujichukulia jukumu la kupiga faini na au kuwapiga Wananchi wao wenyewe. Tunasikia kuna Tume ya *RAS* imeenda kufanya uchunguzi, lakini kazi imefanywa kimya kimya na wala wahuksika hawakuhusishwa wala kuhojiwa, yote ni kuonesha jinsi haki ya Wananchi inavyoweza kunyongwa mchana kweupe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi yametolewa dhidi ya Watendaji wa Vijiji (*VEOs*) na wa Kata (*WEOS*). Kada hii ya watumishi bado ni Miungu watu. Wana mamlaka ya kuweka watu ndani, hata kwenye ofisi ambazo kimsingi hazina mazingira ya kuweka binadamu mathalani kwenye *godown* ambako kuna mazao yaliyopigwa dawa. Wala maghala hayo hayana ulinzi wa kutosha kuwa mahabusu na kadha wa kadha. Haki za kupewa chakula waliohifadhiwa kwenye rumande hizo bandia mara nyingi zimeniyimwa, jambo ambalo ni kinyume na Haki za Binadamu. Mahali pengine hata watoto wadogo wasio na hatia wamewekwa rumande. Yote haya yanatokea kwa vile wanaoitwa "walinzi wa amani", wamepewa majukumu makubwa bila kupewa mafunzo ye yeyote angalau ya msingi katika mambo ya sheria au bila kupewa mwongozo wowote wa wajibu wa "mlinzi wa amani".

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kwa vile Serikali ni moja, ilete Bungeni Muswada wa Sheria unaoweka bayana majukumu ya walinzi wa amani na taratibu wanazopaswa kufuata katika kutekeleza majukumu yao. Wizara ya Sheria na Katiba pia itoe mwongozo ulio wazi, ili walinzi wa amani wawajibike kwa Mahakimu wa Wilaya au wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo yao kwa utaratibu unaoeleweka na wawe wanakaguliwa mara kwa mara kuona na kusimamia utendaji kazi wao.

Mheshimiwa Spika, Viongozi wa Serikali wa ngazi zote, wanatakiwa kuwa na uelewa wa sheria na taratibu za uendeshaji wa Serikali, angalau katika ngazi zao. Kila kiongozi ni lazima ajue mipaka ya kazi yake. Kutokuwa na uelewa wa sheria kunasababisha kuingiliana kwa mamlaka mbalimbali na kuleta vurugu isiyo ya lazima. Tatizo la maji Wilayani Karatu, limesababishwa kwa kiwango kikubwa chombo kilichoandikishwa kisheria yaani Bodi ya Maji ya *CAVIWASU* iliyoandikishwa chini ya Sheria ya Bodi ya Wadhamini (*The Trustees Incorporation Ordinance, Cap.375*), ambayo iko chini ya Wizara hii kuingiliwa na Viongozi wa Serikali bila kufuata taratibu

zilizowekwa na sheria na hivyo kuleta vurugu, ambayo nusura isababishe uvunjifu wa amani. Kambi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Viongozi wa Serikali kuheshimu mipaka ya kazi yao na kuwa walinzi wa sheria badala ya kuwa vianzio vya vurugu katika jamii. (*Makofi*)

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa mara nyingine tena, kuvunja ngazi ya Uongozi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya na Mamlaka yao iwe mikononi mwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa vile kuwepo kwa ngazi hiyo kunaleta mkanganyiko wa kazi. Kazi zote anazofanya Mkuu wa Wilaya, zimeainishwa kufanywa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa Kikatiba, Ibara ya 145 na 146 na Sheria Na. 7 kwa Serikali za Mitaa na Sheria Na. 8 kwa Mamlaka za Miji na Manispaa. Maendeleo hayawezi kuletwa mahali ambapo kuna mikanganyiko na Viongozi hawana mipaka iliyo wazi ya kazi. Mathalani, Sheria Na. 19 ya 1997, inatoa nafasi ya Wakuu wa Wilaya kama *facilitators* katika shughuli za maendeleo ambazo zote kimsingi ziko chini ya mamlaka ya Halmashauri za Wilaya au za Miji. Lakini kumekuwa na malalamiko katika Wilaya nyingi kuhusu kuingiliana kwa mamlaka za Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri wameacha kazi hizo kwa Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Katibu Tarafa ni kiungo muhimu sana kwa shughuli za maendeleo katika eneo la Tarafa. Aidha, Katibu Tarafa pia anatumika mara kwa mara katika kusimamia shughuli za ulinzi na usalama, uzalishaji mali na huduma za kiuchumi na huduma za kijamii katika Serikali za Mitaa. Wajibu wote huu unatekelezwa na Katibu Tarafa bila sheria yejote, bali Serikali imetoa tu mwongozo, ambao ndio umekabidhi majukumu makubwa kiasi hiki kwa Makatibu Tarafa. Kambi ya Upinzani inapenda kusositiza kwa mara nyingine tena, misingi ya Utawala Bora ni kuwa na sheria zilizo bayana na zinazoleweka kwa wote. Mwongozo uliotolewa unajulikana tu ndani ya Maofisi ya Serikali na umma ulio mkubwa hauna habari na majukumu ya kisheria ya Katibu Tawala. Makatibu Tarafa ni mionganoni mwa kada zinazolalamikiwa kwa kutokuwa na majukumu yaliyo bayana. Hivyo, ili kuepuka migongano na hasa migongano ya kisheria siku zijazo, tunaitaka Serikali kuwasilisha haraka Bungeni, Muswada utakaoainisha majukumu ya kisheria ya Katibu Tarafa. Utawala Bora ni pamoja na kuwa na miundombinu sahihi ya Utawala Bora, ambayo ni pamoja na kuwa na sheria zilizo bayana na zisizo na utata. Vinginevyo tunajidanganya tu. (*Makofi*)

Katika ngazi ya Serikali za Mitaa, Sheria Na. 7 na Sheria Na. 8 zinatamka kabisa kwa mfano, kuwa Serikali za Vijiji ni lazima zikutane kila mwezi na Mikutano Mikuu ya vijiji ni lazima ifanyike mara moja kila miezi mitatu. Katika vijiji karibu vyote Tanzania, hakuna sehemu sheria hii inatekelezwa na hakuna aliye tayari kuisimamia, wala siyo Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa, wala Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, wizi na ubadhirifu mwingi unafanyika katika ngazi hii. Mali nyingi za Wananchi, maduka, mashine za kusaga, matrekta, mashamba na miradi mingine mbalimbali imeteketea, kwa vile sheria hii haitekelezwi na hakuna anayeisimamia pamoja na kelele nyingi zinazopigwa na Wananchi kutoka kona mbalimbali za nchi, vijiji vingi, tangu vimeanzishwa taarifa ya mapato na matumizi, hajjawahi kutolewa hadharani na Wananchi wakidai inakuwa ugomvi kati ya Uongozi na wanakijiji.

Hali hii imedidimiza maendeleo ya vijiji vingi na kwa hakika itakuwa ndoto kupiga vita umaskini iwapo jambo hili halitarekebishwa na Serikali kwa maana ya Wizara inayohusika. Hapa inatakiwa kimsingi utashi wa kisiasa kwa vile malalamiko yako kutoka karibu nchi, kinachokosekana ni masikio makini ya kusikia na kufuatilia utekelezji wa sheria hii kwa lengo la kumletea mwananchi unaifuu katika maisha. Serikali inaelekea hajatambua kabisa umuhimu wa sheria katika kupiga vita umaskini, vinginevyo ingelikuwa tayari kuchukua hatua kamambe katika kukuza Utawala Bora katika ngazi za Vijiji, Kata, Tarafa na Wilaya, ambako ndiko kuna Wananchi walio wengi na raslimali zilizo nyingi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri basi misingi ya sheria ikitetereka au kama sheria zisiposimamiwa ipasavyo, utoaji wa haki unakwama. Katika vijiji vingi siku za hivi karibuni, tunasikia viongozi wa vijiji wamefungiwa nje au uongozi wa kijiji umeng'olewa na Wananchi wenye kwa kutumia kifungu cha 141 cha Sheria Na. 7 ya mwaka 1982. Mfano ni kijiji cha Endasak, Wilayani Hanang au Bassodawish, Wilayani Karatu, ambapo Wananchi wameng'oa Serikali nzima kwa madai ya ubadhirifu baada ya Uongozi wa Serikali ya Kijiji kuonekana kulindwa na viongozi wa juu wa Serikali. Amani na Utulivu haviteremki kutoka mbinguni, ni lazima kuilea. Namna thabiti ya kulea na kukuza amani na utulivu si hotuba za majukwaani bali kusikiliza kilio cha Wananchi na kusimamia utekelezaji wa haki zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Wizara hii vile vile inayo majukumu mazito ya kusimamia masuala yanayohusu utoaji wa Haki za Binadamu. Ni kweli Tume ya Haki za Binadamu chini ya Mheshimiwa Jaji Kisanga, inafanya kazi nzuri sana. Tatizo ni kuwa kasi ni ndogo sana na isitoshe Tume ina tatizo la fedha pamoja na Wafanyakazi wa kutosha. Pamoja na jengo zuri la Tume, lakini nafasi za ofisi bado ni finyu na ofisi zimetapakaa sana katikati ya Jiji la Dar es Salaam, jambo linalofanya utendaji kazi wao kuwa mgumu sana. Kambi ya Upinzani inapenda kutamka yafuatayo:-

Kwa utaratibu wa kawaida, Watumishi na Wafanyakazi wa Serikali wanapolalamikiwa husimamishwa kwa nusu mshahara, Watanzania wengi tumestushwa na hali iliyojitokeza ya Viongozi Vigogo waliothumiwa kwa makosa makubwa ya Haki za Binadamu, kama vile Mkuu wa Wilaya ya Serengeti, pamoja na Kamanda wa Polisi wa Wilaya hiyo. Naye Mkuu wa Wilaya ya Tarime anayo kesi mbele ya Tume hiyo. Katika hali ya kawaida, tungelitegemea Viongozi hao Wakuu wangelisimamishwa kazi wakati mashauri yao yanaendeshwa na au kuhamishwa maeneo mengine. Lakini Viongozi hao wameachwa katika maeneo hayo hayo na wameendelea na kazi zao za kawaida. Katika usikilizaji kesi za kawaida, watuhumiwa wakati mwagine huwekwa ndani ili wasipate nafasi ya kuingilia au kuvuruga ushahidi. Lakini kwa vigogo hao imekuwa tofauti. Kuna malalamiko na imeripotiwa kwenye vyombo vyahabari kuwa, Wananchi waliokuwa tayari kutoa ushahidi wametishwa kwa vitisho mbalimbali na vigogo hao. Jambo hili ni hatari na linatengeneza matabaka katika jamii yetu.

Iwapo sheria iliyounda Tume ya Haki za Binadamu hajafafanua jambo hilo vizuri, basi ni vyema Serikali ikaleta Bungeni marekebisho ya haraka, ili wahusika wa kesi kama hizo wasimame kama ilivyo kwenye kesi nyingine za jinai, kutoa nafasi kwa

Tume kufanya kazi zake vizuri na au wahamishwe basi eneo lingine. Isitoshe, wakati mwingine kama ilivyotokea kwa shauri la Haki za Binadamu la Serengeti na Tarime, wahusika wametuhumiwa kwa majina yao binafsi katika kesi kali kama hizo, bado ni kuikosea haki jamii kuendelea kumgharimia mhusika kwa fedha za walipa kodi, wakiwemo hao hao wanaolalamika. Watuhumiwa wa aina hiyo ni vyema wajigharimie wenyewe ili kuona uchungu na iwe fundisho kwao na kwa wengine wenye tabia hiyo ili wasirudie tena makosa ya aina hiyo katika maisha yao. (*Makofî*)

Hata hivyo, kwa watuhumiwa hao kubaki katika nafasi zao ni kuaibisha Serikali, wakati mambo mazito waliyoyafanya yanachunguzwa na wao wamebaki na vyeo vyao vikubwa na wakiendelea kutamalaki kana kwamba hakuna kilichotokea.

Hata kwenye kesi za jinai, wahusika ni watuhumiwa tu hadi pale wanapopatikana na hatia, lakini wanasmama kwa nusu mshahara. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuzingatia suala hilo ili haki ioneckane kweli inatendeka na siyo tu mchezo wa kuigiza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wananchi wasio na makosa kubambikiziwa kesi na sungusungu, ni kweli kuwa Sungusungu wanafanya kazi nzuri, lakini Kambi ya Upinzani imepiga kelele siku nyingi kuwa ni vyema Serikali iwapo inapenda Sungusungu kuendelea na kazi hiyo, basi itunge sheria yenyé kuonesha majukumu ya Sungusungu bayana. Kuna kesi nyingi ambazo zinatia mashaka na zina sura ya Wananchi kunyimwa haki za msingi na za binadamu na Serikali imefumba macho.

Mifano hai ni kama ifuatavyo: Tarehe 16 Februari, 1996 Bwana Raphael Merama wa Kijiji cha Soroneta, Kata ya Ngararo, Wilaya ya Tarime alikamatwa na Sungusungu sita waliodai kutumwa na Mwenyekiti wa Kijiji Bwana John Robert Sinyaro, Sungusungu wakiongozwa na Kamanda wao Bwana Joseph Ryoba Mwita, walichukua ng'ombe pamoja na fedha taslimu Sh. 160,000/=. Tarehe 16 Julai na 20 Agosti, 2003 katika Kijiji cha Nyanungu, watu wafuatao walikamatwa na Sungusungu na kupigwa na hatimaye kufa. Watu hao ni pamoja na Ryoba Bwaro Mwita, alikamatwa tarehe 16 Julai, 2003 na *IGP* alipoomba taarifa, akapotoshwa na Uongozi wa Polisi kama inavyoonekana kwenye taarifa, kumbukumbu inayoonekana kwenye *paper* yangu. Pamoja na taarifa ya Polisi kukiri kuwa Bwana Ryoba alikufa kutokana na majeraha aliyopata na jalada hilo linaloonekana linathibitisha hivyo, hadi leo hakuna hatua ye yote iliyochukuliwa na wahusika wanaendelea na shughuli zao kijijini kama desturi. Matatizo hayo pia yako kwenye Kijiji cha Goronga, ambapo Bwana Kerambo alichukuliwa Sh.150,000/= pamoja na wenzake. Tarehe 27 Novemba, 2003 Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi, Tarime, ilitoa barua kumbukumbu inayoonekana hapo kuhusu Bwana Wambura Mwita aliyedaiwa kwamba ameiba redio, lakini alikamatwa na kupigwa sana , hatimaye alifariki.

Mheshimiwa Spika, tumefanya utafiti wetu wa kina katika Wilaya ya Tarime, kwa vile ndiko kuliko na taarifa nyingi za mauaji. Lakini tunazo taarifa za mauaji ya aina hiyo hiyo Wilaya ya Kahama, Wilaya ya Geita na Mkoa wa Tabora. Ni dhahiri, maisha katika Wilaya hizo yamekuwa machungu na hawa bado ni Watanzania kama

wengine. Maisha ya binadamu yamekuwa kama ya kuku na hakuna hakika ya usalama hata ukiwa ndani ya nyumba yako na familia yako, kwani wengi wa watu hawa wamechukuliwa wakiwa majumbani mwao. Hata kama wangelikuwa wahalifu, sheria za Jamhuri ya Muungano bado zinataka kuwa wafikishwe mbele ya vyombo nya sheria ili tuhuma dhidi yao zithibitishwe na wapewe adhabu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge. Hali hii inatisha, Serikali inajua lakini imekaa kimya! Jukumu la Waziri la kusimamia Sheria ni dhahiri halitekelezwi kabisa katika eneo hili.

Kambi ya Upinzani, kulingana na uzito wa tatizo hili, inaitaka Serikali ichukue hatua mara moja kama ifuatavyo: -

(i) Ipige marufuku mara moja misako ya ovyo ovyo inayofanywa na Sungusungu. (*Makofi*)

(ii) Ilete mara moja Bungeni Muswada wa Sheria unaoainisha majukumu ya Sungusungu bayana, ikiwa ni pamoja na uwajibikaji wao, ngazi zao za uwajibikaji na mamlaka yao ya kutoa adhabu nayo pia yaainishwe. (*Makofi*)

(iii) Serikali iunde mara moja Tume ya Uchunguzi na kufanya *inquest* kuhusu mauaji haya na wizi huu wa dhati wa mali za Wananchi ambao Serikali inapaswa kulinda usalama wao na mali zao.

(iv) Serikali itoe maelekezo ya wazi kwa watendaji wake katika ngazi za Vijiji na Kata kuhakikisha wanasmamia, wanalinda na kutekeleza Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa manufaa ya Wananchi wenyewe.

(v) Polisi watakiwe kutekeleza sheria, kanuni na taratibu na siyo kufuata mapenzi yao na mbinu chafu zinazofanywa na Polisi wachache kuwanyanyasa Wananchi zikomeshwe mara moja kwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria zinazostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, tulipata matumaini kuwa matatizo mengi yanayoikumba nchi yetu hasa ya uhaba wa majengo ya Mahakama sasa yatapungua kutokana na mpango wa ujenzi wa majengo ya Mahakama kwa mpango wa *Quick Start*. Mpango huo ulizinduliwa na Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, mwanzoni mwa mwaka 2003. Kwa bahati mbaya, kilichoonekana kuwa *Quick Start* sasa imekuwa siyo tu *Late Start* labda imekuwa *Non Starter*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi huo ambao uko katika Mikoa ya Manyara na Arusha ulilenga kuhusisha Wananchi. Mradi wa *Quick Start* sasa umeishakuwa kero katika maeneo mengine kwa vile Wananchi walilengwa walishirikishwa tu katika kuchangia fedha na baada ya kuchanga hakuna anayejua nini kinaendelea.

Katika Wilaya ya Karatu mathalan, Wananchi walichanga fedha, tena mapema sana kufuatana na ratiba iliyotolewa. Lakini, hakuna anayejua kiwango kilichopaswa

kuchangwa kiliamuliwa vipi na baada ya kuchanga fedha zimehifadhiwa wapi na sasa kitu gani kinaendelea. Ni imani yetu kuwa, wakati wa kuhitimisha, Mheshimiwa Waziri atatoa rasmi fedha kiasi gani zimechangwa kwa Wilaya zote zilizoko kwenye *Quick Start*, fedha hizo zimehifadhiwa wapi, nani anayedhibiti matumizi yake na sasa ni lini ujenzi utaanza? Je, kwa mtindo huu, mradi huo ambaو ulitegemewa kuanza Mikoa ya Arusha na Manyara kama *pilot* utafika lini Mikoa 19 iliyobaki ili Wananchi wawze kupata manufaa ya Mpango huo? Ni vyema Mheshimiwa Waziri akalieleza Bunge lako Tukufu, mradi huu umekumbwa hasa na tatizo gani, baada ya kuwapatia matumaini makubwa Wananchi kama tulivyoleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya rushwa ni jukumu la kila mmoja wetu. Lakini Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, inayo nafasi pekee kabisa katika kufanikisha mapambano yetu dhidi ya rushwa. Ni kweli kuwa hatua kadhaa zimechukuliwa katika vita dhidi ya rushwa, lakini mafanikio ni kidogo sana na rushwa inazidi kujikita katika jamii yetu, kiasi kwamba, imeanza kula mifupa sasa kama kansa. Ni vyema Serikali ikaacha kutafuta visingizio na kujilinganisha na nchi nyingine. Watanzania tuna haki ya kupiga kelele kudai haki zetu katika nchi yetu, hata kama *Transparency International* au chombo chochote kingelieleza kuwa tatitizo la rushwa kwetu ni kidogo kuliko nchi zote duniani. Watanzania ndio wanaojua adha wanayopata kutokana na rushwa. Karibu huduma zote sasa zinanunuliwa, iwe mahakamani, polisi, hospitali au kwenye chombo chochote cha Serikali. Rushwa kubwa (*Grand Corruption*), imefikia hatua mbaya kabisa kiasi kuwa Serikali inaelekea kuihalalisha wazi wazi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inatoa mifano michache tu kuonyesha jinsi Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba inavyokuwa na jukumu kubwa katika vita dhidi ya rushwa.

Mara nyingi Serikali imejibu Bungeni kuwa mikataba hasa ya mauzo ya Mashirika makubwa kama vile ya Shirika la *TTCL*, *TANESCO*, *ATC* na kadhalika ni siri. Kwa sasa kufuatana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(2)(e), Mamlaka ya Bunge yanaishia katika kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa. Lakini Watanzania ndio walioiweka Serikali madarakani na ndio wamiliki wa mali na rasilimali zote za nchi hii. Wananchi hao hao, ndio pia waliowachagua Wabunge kama wawakilishi wao na kwa njia yao, kuisimamia Serikali na mamlaka yote ya Serikali yanatokana na Wananchi kama Ibara ya nane ya Katiba inavyotamka wazi.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri basi kwa utaratibu wa sasa ambapo Serikali ina uhuru wa kuleta tu Bungeni ile Mikataba ambayo Serikali inataka au inayoletwa kwa mujibu wa Ibara ya 63(2)(e) inapingana na dhana nzima ya Ibara ya 8 ya Katiba. Wananchi wana haki ya kushirikishwa kikamilifu. Kwa vile Wananchi hawawezi kushirikishwa moja kwa moja, ni lazima washirikishwe kuititia wawakilishi wao waliochaguliwa yaani Wabunge na au Kamati inayohusika ya Bunge kulinda mazingira maalum ya Mikataba inayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, iwapo, kikwazo ni Ibara ya 63(2)(e), Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwasilisha Bungeni haraka iwezekanavyo, marekebisho ya kipengele hiki ili Mikataba yote mikubwa na inayohusu maslahi ya nchi hii, yafikishwe katika Bunge hili Tukufu. Inapotakiwa, Bunge liweze kuhoji, kujadili, kutafakari vipengele mbalimbali vya Mikataba yote na kuielekeza Serikali ipasavyo. Dhana ni usimamizi na wala si Bunge kuingilia utendaji kazi kama Serikali inavyodai mara kwa mara. Bunge liwezeshwe kusimamia kama inavyotakiwa na Katiba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tatizo lingine ni la sheria zinazotungwa na Bunge bila uangalifu kuruhusu mianya ya rushwa. Mfano halisi ni Sheria ya *Public Procurement Act, 2001*, kifungu cha 14, ambacho japo Kambi ya Upinzani ilipinga kwa dhati kipengele hiki, lakini kilipitishwa kwa ushabiki wa kisiasa bila kujali maslahi ya Taifa. Kifungu hicho kimekuja kutumika katika kutengeneza Kanuni za Manunuzi ya Serikali za Mitaa kama ilivyo kwenye *GN 49* ya mwaka 2003, ambapo Waziri mwenye dhamana alitamka Bungeni tena kwa kutamba kuwa, Bunge ndiyo lililopitisha kifungu cha 14 cha *Public Procurement* ambacho kimempa mamlaka. (*Makofit*)

Madhara ya kifungu hicho sasa ni kuwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa, Mkurugenzi Mtendaji na Wakuu wake wa Idara, ndiyo wanaokuwa *Tender Board* ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya, bila kuwa na mtu yejote wa nje. Iteleweke hapa hoja siyo kwamba, Madiwani wawe kwenye *Tender Board*, bali sasa tumehalalisha mianya ya rushwa kwa vile taratibu zote za tenda, kuanzia kuandaa tenda mpaka kutathmini zinatolewa kwa watu wale wale ndani ya ofisi moja. Hakuna mtu yejote wa nje anayedhibiti (*check and balance*), hazipo tena na hata Baraza la Madiwani linapopelekewa taarifa linakuwa halina taarifa kamili na ikumbukwe kuwa, hata Diwani wa eneo mradi unapotekelezwa, hana mamlaka tena kutembelea mradi katika eneo lake isipokuwa kwa kibali cha Mkurugenzi Mtendaji, Kifungu cha 12 cha Kanuni *GN 49*. Je, kwa mtindo huo tumeziba *au tumetengeneza mianya ya rushwa?* *Serikali inawajibika kujibu.* (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilette Bungeni haraka iwezekanavyo, marekebisho ya Kifungu cha 14 cha *Public Procurement Act, 2001*, ili Waziri mhusika aweze pia kurekebisha vifungu husika vinavyomhusu. Ni vyema tukawahi kukinga kuliko kutibu, vinginevyo, Ripoti ya Tume ya Jaji Warioba iliyopendekeza kuziba mianya itabaki kuwa kwenye *shelf*, wakati nchi inaangamizwa na mdudu rushwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imefarijika na tamko la Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye kuwa, Soko la Kibaigwa si lake na wala shamba analohusishwa nalo katika eneo la Kibaigwa si lake, kama ilivyoripotiwa na vyombo vya habari siku alipozindua Soko la Kibaigwa, tumeferijika sana na tamko hilo. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inadhani tamko hilo limezua tafrani na maswali zaidi, kwani katika gazeti hilo hilo, wanaojiita Wananchi wa Kibaigwa wamekataa kauli hiyo, wameenda mbele zaidi kueleza kuwa Afisa Ugavi katika Idara ya Serikali ndiye anayelitunza shamba hilo. Je, ni kweli Wananchi wa Kibaigwa hawana macho na masikio? Wananchi wa Kibaigwa wana sababu gani ya kumsingizia Mheshimiwa Frederick

Sumaye? Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine tena, inamtaka Mheshimiwa Frederick Sumaye, kama anaitakia nchi hii mema, achukue jukumu la kuwajibika, akae pembeni ili *PCB* waweze kufanya kazi ya kuchunguza tuhuma hizi dhidi yake. Najua inauma, lakini ndiyo uongozi, aonyeshe njia ili wengine wafauate na ataona jinsi vita dhidi ya rushwa inavyokuwa rahisi katika nchi hii. (*Makofi*)

Haiwezekani kabisa kiongozi huyu mmoja atuhumiwe kutoka watu mbalimbali bila sababu, hata kama iko mbali sana. Haiingii akilini, mtu mzito hivyo kushutumiwa tuhuma nzito kama hizo, asichukue hatua ya kuwapeleka wanaomtuhumu Mahakamani kwa *libel* na *defamation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana haki sasa ya kujua ukweli kuhusu tuhuma hizo, aidha kwa Mheshimiwa Frederic Sumaye kuchukua hatua za haraka kuwapeleka Mahakamani wanaomchafulia jina lake au achukue jukumu la kuwajibika kwa kujiuzulu ili *PCB* ifanye kazi yake au la Mheshimiwa Rais, achukue hatua itakayoonesha nchi hii kuwa ana dhamira ya kweli kupiga vita rushwa. Ni vigumu sana kupiga vita rushwa ikiwa kuna wingu la giza nene linalosababishwa na Viongozi hao hao wanaotegemewa kuwa majemadari wa kupiga vita rushwa. Rushwa haitaisha kwa hotuba kali kali jukwaani, bali kwa hatua thabiti na madhubuti inayooonesha dhamira ya Taifa ya kumpiga vita mdudu rushwa. Vinginevyo, mabilioni tunayotumia kwa kuendesha semina za rushwa nchi nzima ni kazi bure. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaipongeza Tume ya Haki za Binadamu kwa kutoa Taarifa Maalum ya Ukaguzi wa Magereza. Hata hivyo, tuna mambo yafuatayo: -

Katika Magereza ya Isanga (Dodoma) na Ukonga (Dar es Salaam), kuna idadi ya Wafungwa 366 waliohukumiwa kunyongwa katika Magereza ya Maweni Tanga, Isanga, Morogoro, Litungu na Ukonga. Idadi hii inaweza kuwa kubwa zaidi kwa vile ukaguzi huu haukuhusisha Magereza yote nchini. Wako pia wafungwa waliohukumiwa kunyongwa wamekaa gerezani kwa karibu miaka kumi bila kujua hatma yao. Hakuna adhabu kubwa na mbaya kisaikolojia, kama kuhukumiwa kifo na kisha unaachwa kukaa bila kujua hatima yako huku kila asubuhi ukiamka unadhani kuwa siku yenyewe ndiyo leo. Kukaa peke yake kwenye hali hii ni adhabu ya kutosha. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta adhabu ya kifo mara moja kwa vile hata uzoefu umeonesha katika kipindi cha miaka kumi, adhabu ya kunyongwa haijawahi kutekelezwa. Tunaishukuru Serikali kwa kutotekeleza adhabu hii ambayo ni kinyume na haki za binadamu, lakini pia tunaitaka Serikali sasa iifute moja kwa moja ili ijulikane kwamba, adhabu hiyo kweli haipo katika vitabu vyetu nya sheria. (*Makofi*)

Wafungwa wameandika barua wakitaka zifikishwe kwa Mheshimiwa Rais. Inaonekana kuwa Mheshimiwa Rais, aidha, hapelekewi taarifa rasmi au zinachelewa sana. Kambi ya Upinzani inatoa rai kuwa wafungwa bado ni Watanzania, wana haki ya mawasiliano na Rais wao, hivyo, Kambi ya Upinzani inawataka wahusika wote kuhakikisha kuwa, jambo hilo linafanikishwa mara moja ili maamuzi muhimu kama ya kupunguza adhabu za wafungwa waliohukumiwa kunyongwa zichukuliwe mapema,

ikifahamika kuwa ni Mheshimiwa Rais peke yake ndiye mwenye mamlaka hayo. Mathalan, mfungwa mwenye kesi na 231/91 katika Gereza la Karanga alifungwa kwa kesi ya mauaji akiwa na umri wa miaka 17. Hadi sasa amekwisha kufikishwa miaka zaidi ya 34 gerezani na Mheshimiwa Rais peke yake ndiye mwenye mamlaka ya kutamka muda wa kutumikia kifungo kwa watoto wa aina hiyo. Zipo kesi nyingi za namna hii, ikiwemo Gereza la Maweni, Tanga. Tunamtaka Mheshimiwa Waziri, ampe Mheshimiwa Rais ushauri unaotakiwa ili utata ulioko uweze kuondoka na haki za watusika ziweze kupatikana.

Mheshimiwa Spika, katika Magereza yote yaliyokaguliwa na Tume ya Haki za Binadamu na hata kwa Kamati ya Bunge ya Sheria, wamebambikiziwa kesi na Polisi. Haiwezekani kabisa katika Magereza yote 45 yaliyokaguliwa, Magereza zaidi ya 30 yatoe lalamiko la aina moja la kubambikiziwa kesi na Polisi. Mbaya zaidi kesi wanazobambikiziwa ni kesi za mauaji, unyang'anyi wa silaha na dawa za kulevya ambazo ni vigumu kupata mdhamana. Kwa upande wa wanawake, hali inatisha kabisa, kwani aina ya rushwa iliyojitokeza ni rushwa ya ngono. Magereza yetu yana uwezo wa kubeba mahabusu na wafungwa 12,540 tu kwa wakati mmoja. Lakini yamekutwa wakati wa ukaguzi yakiwa na wafungwa 26,078, yaani mahabusu na wafungwa 13,538 zaidi au asilimia 108 zaidi.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ichukue hatua ya haraka na ya muda mfupi kuifanya kazi taarifa hii ili kubaini ukweli wa malalamiko haya na ikiwezekana jambo hili likomeshwe mara moja. Utawala Bora lazima uonekane kwa matendo si kwa hotuba nzuri na tamu za Mawaziri wetu. Polisi wachache wanaochafua jina la Jeshi letu la Polisi lazima wachukuliwe hatua zinazostahili. Watanzania wengi wamelalamika kuwa, Tanzania ukitaka kumfunga mtu unamfunga mradi pochi yako na ukitaka kumtoa muuaji unamtoa kwa pochi hiyo hiyo. Kumbe huu sasa inaonekana kwamba ni ukweli.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu vile vile imeangalia Haki za Wanawake na Watoto. Watoto hawa wana muda mrefu uliobaki katika maisha yao na ndiyo nguvukazi muhimu kwa Taifa letu. Magereza ya Watoto ni mahali ambapo watoto wanapata malezi na stadi mbalimbali za maisha ili wanapotoka gerezani wawe raia wema na waweze kulitumikia Taifa lao. Tunaitaka Serikali basi ikamilishe azma yake ya kutenga mabweni au majengo ya kuwafunga watoto tofauti na watu wazima ili kulinda hadhi yao, kuwapa malezi wanayostahili na kuwaokoa kutokana na manyanyaso wanayopata ikiwemo ya kutumika tofauti na hiari yao katika mambo ya ngono. Tukiwa na nia inawezekana, tutekeleze wajibu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda vile vile kuwapongeza Wanawake wa Tanzania kwa ujumla kuwa raia wema kwani wanawake walikuwa 209 na wanaume walikuwa 13,748 kati ya wafungwa waliokuwepo wakati wa ukaguzi, yaani asilimia 1.5 tu na kati ya mahabusu 12,121, wanaume walikuwa 11,666 na wanawake walikuwa 455 tu, yaani asilimia nne tu. Tunaitaka Serikali iendelee kuwalea waendelee kuwa raia wema wa nchi yetu na watulelee jamii yetu. (*Makofii*)

Lakini vile vile, tunaomba Serikali ifikirie kuwapunguzia vifungo vyao hasa wale wenye watoto wachanga na au wajawazito na angalau waachiwe kwa *parole* au kwa njia ya kifungo chini ya sheria ya *Community Service* ili kuwapa nafasi ya kuwalea watoto hao wasio na hatia, walioko bado tumboni au watoto wachanga ambaeo ni tegemeo la Taifa kwa siku zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda, nieleze tu kuwa, japo ndani ya Bunge hili limeishatoka jibu la Serikali kuwa, Magereza siyo hoteli ya kitalii na wakati tunakubali kuwa siyo hoteli ya kitalii kweli, lakini pia tukumbuke kuwa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano inataka mahabusu na wafungwa kutambuliwa na kuheshimiwa kama binadamu, kutoteswa na au kupewa adhabu inayodhalilisha utu wa binadamu na Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu inaonesha wazi wazi kabisa kuwa, katika Magereza mengi, wafungwa na mahabusu hutumia mitondoo au ndoo kujisaidia kwa haja kubwa na haja ndogo ndani ya mabweni. Hali hii ni dhahiri kuwa ni kinyume na kanuni za afya na pia ni kinyume na kanuni za kuheshimu utu na ubinadamu wa mwanadamu. Tunaiomba Serikali ihakikishe kwamba, suala hili linaondolewa mara moja, kwani hakuna kitu kinachodhalilisha utu wa binadamu kama kuvua nguo mbele ya wenzake na kujisaidia hadharani wakati wenzake wanamtazama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba nisipigiwe kengele, naomba niwasilishe na nimtake Mheshimiwa Waziri atupe majibu ya kuridhisha wakati wa ku-*windup* hotuba yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

MHE. DR. MASUMBUKO R. M. LAMWAI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kufungua mjadala wa jumla juu ya Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele yako katika mkutano huu, naomba nimpongeze sana ndugu yangu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni. Ushindi wake unaonesha wazi kwamba, udikteta wa Viongozi wa baadhi ya Vyama vya Upinzani kunyang'anya wapigakura, watu waliowachagua kihalali umepata jibu sahihi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba pia kwa wakati huu nikupe pole wewe, familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetete Mwalyego na wapigakura wake wa Mbeya Vijijini, pole kwa kifo chake cha ghafla hapa Dodoma. Tumepata hasara kubwa na ninaomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amina*.

Mheshimiwa Spika, katika kuanza mjadala huu, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote, kwa bajeti nzuri waliyotayarisha na pia nawapa pole kwa kufanya kazi katika mazingira magumu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunakumbuka kwamba, hii ni Wizara ambayo inaambiwa siyo Wizara ambayo ni *productive*, kwa hiyo, *ceiling* zake za bajeti zinakuwa ndogo.

Lakini ni Wizara ambayo ina kazi kubwa sana katika kuleta hali ya amani katika nchi hii, hali ya utulivu katika nchi hii na katika ku-regulate mahusiano ya binadamu na binadamu na mahusiano ya dola na binadamu ili hizo Wizara nyingine zilizo *productive*, ziweze kufanya kazi yake. Kwa hiyo, naweza nikasema kwamba, Wizara hii ni *productive* kuliko Wizara nyingine kwa kujenga yale mazingira ambayo watu wanaweza wakafanya *production* sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa hiyo, yote yaliyosemwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo nilishiriki, hivyo, nina machache ya kuongezea.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe kilio cha Wananchi kuhusu utoaji wa haki. Katika Mahakama zetu kwa sasa hivi hasa Mahakama za Chini, washtakiwa katika kesi za jinai wanateseka sana. Yako mambo manne ambayo yanatokea na nina uzoefu nayo. Kuna watu ambao wanajitia kwamba ni makuwadi wa kupata dhamana kwa niaba ya washtakiwa hasa Maaskari ambao ni wasaidizi kule Mahakamani. Hawa *literally* wamekuwa wanawanyang'anya watu pesa kwa ahadi kwamba, wataongea na Hakimu awapatie dhamana. Hii inatesa sana, siyo mijini tu hata vijijini na ukizingatia kwamba, wengi wa Wananchi wetu ni watu ambao hawajui sheria sawa sawa, hawajui ni nani anatoa dhamana na ni nani mwenye uwezo wa kumnyima dhamana. Hili suala linakuwa gumu sana na hiyo ndiyo inatokea, Mahakimu wanatuhumiwa kwamba wanapokea rushwa, lakini mipango ya rushwa kwa uzoefu wangu, haifanyiki kwa Hakimu, inafanyika hata kabla mshtakiwa hajafikishwa mbele ya Hakimu. Ningombwa suala hili lisimamiwe vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, kuna tatizo kubwa sana la kubambikiziwa kesi. Zipo kesi zinazoitwa kesi za zege. Ukiambiwa unapewa zege, maana yake ni kwamba, umekamatwa huko barabarani haijulikani umetenda kosa gani unafika pale Polisi unapewa risasi au unapewa bastola au unapewa vifaa vya kuvunja nyumba. Ndilo zege hilo na kesi nyingi sana zinaishia kwa watuhumiwa kuachiwa huru kwa kukosa ushahidi kwa sababu kesi nyingi sana ni kesi ambazo wamebambikiziwa, aidha, kwa sababu za kibinasi au kwa sababu watu wana pesa na wamekwenda kushawishi baadhi ya Maaskari kushirikiana nao kutesa Wananchi au kwa sababu nyingine ambazo hatuzielewi. Kesi hizi zinaendelea na hakuna mwenye uwezo wa kuzifuta mpaka Hakimu amalize ushahidi. Ninazo kesi ambazo zimeendelea zaidi ya miaka minane mtu anaishia kuachiwa na miaka minane mtu akiwa rumande. Naomba Wizara ishughulikie hili jambo zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hizi kesi za kubambikiziwa pia zinaendana na matumizi ya sheria za jinai kututua matatizo ya madai. Mara nyingi sana watu wanaodaiana mashamba mmoja anatangulia Mahakamani, mwingine anashtakiwa kwa kesi ya jinai na tunazo kesi nyingi sana za mashamba na za viwanja, kwa sababu hiyo. Mwenye pesa anatangulia Polisi, kesi inakwenda kama kesi ya jinai. Natambua Mahakama Kuu imeshatoa maagizo kwamba, kukawa na kesi za namna hiyo, ikiashiria kwamba kuna uwezekano mtu anadai haki yake, basi hiyo kesi washauriwe waende kwenye kesi za madai, lakini hii haitoeki mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kilio cha nne ni ucheleweshwaji wa kesi, huenda ikawa tunatafuta sababu ambazo siyo katika ucheleweshaji wa kesi. Ninakubali Mahakimu ni wachache, ninakubali pia kuwa Majaji ni wachache, lakini hasa katika Mahakama za Chini kuna ucheleweshwaji ambao unatokana na mfumo wa uendeshaji kesi wenyewe. Siyo Mawakili kulaumiwa, wala siyo washtakiwa kulaumiwa na wala siyo Mahakimu kulaumiwa, lakini kuna jambo linalotokea.

Mheshimiwa Spika, lalamiko langu kubwa ni kwamba, tangu uhuru tumerithi utaratibu wa uendeshaji wa mashtaka ambapo yule mkamataji anakuwa ndiye mshtaki. Ni kwamba, Polisi anakamata na kule Mahakamani Mwendesha Mashtaka anakuwa ni Polisi. Huyu Polisi kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai, anasemekana anapata maelekezo kutoka kwa Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, lakini wakati huo huo ni Askari ambaye yuko chini ya Mpelelezi Mkuu wa Wilaya au *RCO*. Anavaa magwanda yake ya kipolisi wakati anaendesha kesi na anapata maagizo hasa kutoka kwa *RCO*.

Mheshimiwa Spika, hilo nimeliona ni tatizo kubwa sana kwa sababu wakati ambapo kuna *interest* za kipelelezi huwezi kutekeleza tena *interest* za kutetea haki au za kutenda haki kama ipasavyo na kinachotokea ni kwamba, wale Maaskari wanamtii zaidi *RCO* kuliko wanavyofikiria jukumu lao la kumtii *DPP*. Nafikiri wale waliteuliwa wakati wa mwanzo wa uhuru kwa sababu ya upungufu wa wataalam katika *prosecution*, lakini kwa sasa ambapo tunao wengi wanaomaliza

Vyuo Vikuu tunawaona, tunao wengi wanaomaliza *diploma* zao, nashauri imefika hatua sasa kwamba, Ofisi ya *DPP* itenganishwe kabisa na Ofisi ya *RCO* kwa maana kwamba, kama kuna Askari anayetaka kuendelea kuwa Mwendesha Mashtaka, basi aachie ngazi Jeshi la Polisi na kama anataka kubaki Jeshi la Polisi, basi aachie ngazi asiwe *Public Prosecutor*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 35 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri, analiarifu Bunge lako Tukufu kwamba, utaratibu wa Mawakili wa Serikali kuendesha kesi hadi ngazi za Mahakama ya Wilaya unafanyiwa mipango. Lakini hili siyo jambo geni, Mawakili wa Serikali wamekuwa wanakwenda Mahakama za Hakimu Mkazi. Zipo kesi ambazo wamekuwa wanakwenda, zipo kesi nyingine ambazo zimeendeshwa Mahakama ya Wilaya na Mawakili wa Serikali.

Hoja siyo Mawakili wa Serikali kupata fursa ya kwenda huko, hoja ni kwamba, tunawataka watu ambao wanajibu moja kwa moja kwa *DPP*. Kule Mawakili wa Serikali kwenda mara moja haitoshi, naomba hili pendekezo la kwamba mpaka mwaka wa 2009, hii ofisi inaweza ikawa imeishafikia hatua ya kutenganishwa na Polisi, ni mbali mno huko, inatakiwa itenganishwe mapema iwezekanavyo na huku kuwa na kofia mbili katika *prosecution* katika Mahakama za Chini huenda ikawa ndiyo kunafungua mianya ya rushwa kwa kiasi kikubwa namna hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine juu ya Mabaraza ya Kata. Baadhi ya Viongozi wa Kata wanafanya maamuzi na wakati wale ambao wameathiriwa na yale maamuzi wanataka kwenda Mahakama ya Mwanzo kwa madai wanaambiwa waende kwenye yale Mabaraza ya Kata tena na wanakutana na wale wale watu ambao walifanya yale maamuzi. Mfano mzuri sana ni Kata ya Kibamba, wamegawa mashamba ya watu wakati watu wanakwenda kudai yale mashamba wanaambiwa nendeni kwenye Baraza la Kata, huko wanakutana na wale wale waliogawa yale mashamba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nipayendekeze kwamba Wizara ifikirie upya mahusiano kati ya Baraza na Kata na Mahakama ya Mwanzo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho ni jambo ambalo nisingependa kuliongelea lakini imebidi niliongelee. Hizi kelele za watu kujiengua wakati ambapo wametangazwa kuwa na rushwa au kufungua makesi ya kashfa. Ukubwa ni jalala na kama watu wangekimbilia mahakamani kila siku ambapo wanatuhumiwa basi mahakama zetu hazingewenza kufanya kazi. Mtu yoyote anaweza akasimama akamtuhumu mkubwa yoyote, kitu chochote hasa katika siasa za upinzani ambazo kwa kweli hazina lengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisingeshauri masuala binafsi ya watu awe mkubwa, awe mdogo yaletwe katika Bunge na uamuvi wa mtu wa kwenda mahakamani au kutokwenda mahakamani ni uamuvi wake mwenyewe. Katika hali yetu ambayo kila mtu ana haki ya kusema kila kitu bila kufanya utafiti wowote nisingeshauri kila mtu anayetuhumiwa aende mahakamani ikiwa ni pamoja na mimi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hayo, machache niliyosema naomba niseme tena kwamba kama nilivyounga mkono hii hoja wakati nikiwa kwenye kamati, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. (*Makofi*)

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe pamoja na Wizara ambayo leo inawasilisha Bajeti yake katika Bunge lako tukufu. Kwanza, nitambue hotuba nzuri na matayarisho mazuri ya Wizara na napenda kusema kwamba Mheshimiwa Mwapachu, ni kiongozi mwenye uzoeufu na sikushangaa kwa haya mazuri ambayo ameweza kuyatamka katika Bunge. Naamini hela hizi zitamsaidia. (*Makofi*)

Kwa kuwa nilikwisha pongeza na kutoa rambirambi naomba niende moja kwa moja katika hoja. Kwa heshima na taadhima niitambue kazi iliyofanyika na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Wizara hii na mapendekezo yake. Kamati inaonekana imefanya kazi nzuri na mimi ningependa nitamke kwamba mengi nitakayoyazungumza ni yale ambayo yameshatamka na kamati na kwa sababu ninaona kuna umuhimu yakazingatiwa na yakasisitizwa basi ninaamini kuna umuhimu wa kuyasema. (*Makofi*)

Kwanza nianze na tatizo la kutoa haki. Katika kutoa haki tunayo matatizo makubwa mawili/matatu. Kwanza inatambulika wazi uhaba wa Mahakimu na inaeleweka wazi kwamba liko tatizo, la vyombo vyaya kufanya kazi, Mahakimu na wale wote walioko katika kazi ya kutekeleza haki. Pia vile vile liko tatizo linalotokana na utendaji kazi wa

mtu binafsi mfano rushwa na kutozingatia utendaji wa haki. Sasa mimi nianze na suala hili la uimarishaji wa Mahakama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa ambao Waziri, alikuja nia ya kuvipa hadhi vyombo nya kutoa haki. Waziri alitamka hatua zinazochukuliwa katika kurekebisha miundo mbinu ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Katika hotuba yake alizungumzia kwamba zimetengwa shilingi bilioni 52 au mpango mzima utakuwa ni wa shilingi bilioni 52. Lakini mwaka huu ameeleza kwamba amepewa shilingi bilioni moja kwa ajili ya mpango huo. Sasa mpango wa urekebishi kama malengo ni shilingi bilioni 52 na wewe unapewa shilingi bilioni moja, utawezaji kufanya kazi? Kwa hiyo, itachukua miaka karibu 52 ili kutekeleza programu hiyo. (*Makofi*)

Sasa naomba Serikali kwa ujumla kama ilivyopendekezwa na Kamati ya Katiba, Utawala na Sheria, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba na hasa Idara ya Mahakama kama nguzo ya tatu katika nguzo tatu, ipewe haki yake na hadhi yake ya kuwa mhimili katika nchi hii. Mimi naamini kabisa matatizo yanayowakabili wananchi hasa katika Mahakama za Mwanzo ni makubwa sana. Mheshimiwa Dr. Lamwai amezungumzia mambo mengi ambayo kwa kweli ni ya msingi sana. Ameweza kuyazungumza kwa kina kwa sababu yeye anahusika moja kwa moja katika utekelezaji na uteteaji wa haki. Ninaloliomba Serikali kwa kweli itambue umuhimu wa nguzo hii ambayo kazi yake ni kutekeleza haki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo ambalo litatusaidia katika kutekeleza haki ni eneo la mafunzo. Mimi eneo hili ndiyo kwa kweli lililonishawishi niamke kuzungumza katika Wizara hii. Tunacho Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto, chuo hiki ndicho kinaweza kutoa jibu katika tatizo la uhaba wa Mahakimu. Kwa mwaka huu wako wananchi 706 ambao wameomba kujiunga na chuo hiki.

Katika waombaji hao 574 walikuwa na (*qualifications*) sifa za kuweza kujiunga na chuo hiki. Walioruhusiwa kupata nafasi ni wanafunzi 132 tu. Katika hao 84 ni stashada na 32 ni cheti. Sasa tunapozungumzia tuna uhaba wa Mahakimu na tunapozungumzia kwamba haki haitendeki na kuna uhaba wa Mahakimu siyo chini ya 600 kwa sasa tunapozungumza japo Waziri, hakutamka hili pengo tutalizibaje bila kupanua uwezo wa chuo? Namshukuru sana Waziri kwa kutoa kauli kwamba yako mazungumzo kati ya Chuo na NSSF ili chuo hiki kiweze kupewa uwezo wa kujengewa majengo.

Sasa mimi naiomba rasmi Serikali, ichukua njia hiyo kwa haraka na linalohitajika hapa ni hazina kukubali *ku-guarantee NSSF* wakubali kuweza kukijengea chuo hiki majengo na kiweze kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo, ninaloliomba katika Serikali ni kwamba kwa matamshi ya Waziri, basi Waziri wa Fedha, akubaliane kwa kushirikiana na Waziri wa Sheria na Katiba, kukubali mpango huu ili tuepukane na tatizo la uhaba wa Mahakimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni katika eneo la haki za binadamu. Mheshimiwa Lamwai, alizungumzia suala la ubambikizwaji wa kesi.

Mimi ninao mfano hai na ninaomba Waziri auchunguze na atoe kauli, atoe maelezo kumetokea nini? Huko Shinyanga kesi namba 3 ya mwaka 2004 wako akina mama 4 wamewekwa ndani kwa tuhuma za mauaji. Katika kesi iliyotokana nafikiri na wizi au mauaji yaliofanyika huko Bulyanhulu. Akina mama hawa wamewekwa ndani kwa sababu waume zao wametoroka. Kuanzia Januari, 2004 mpaka leo kutokana na kutoroka kwa waume zao, wao wako ndani. Sasa Serikali inatamka nini juu ya kukiuka haki kiasi hicho? Jana kesi yao imeahirishwa mpaka mwezi ujao, Agosti, 2004. Wengine ni walimu, wengine ni wafanyakazi, sasa hebu fikiria mwalimu anayewekwa ndani kwa kosa la mume wake, kwa sababu mume katoroka, haki iko wapi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, kwa kweli ninaomba hilo liangaliwe, yapo maelezo ya kutosha kama Waziri angependa nitampa. Asubuhi nilimwuliza Mwanasheria kama sheria ipo kama mume au mke akitenda kosa mwingine awekwe ndani kwa makosa ya mume wake na uchunguzi uendelee kufanywa. Nyumba zao wamekwenda ku-search hawakukuta kitu chochote kilichohusiana na wizi uliofanyika. Sasa hawa wana makosa gani? Wakina mama wengi na wananchi wengi wasiojua haki zao wanateseka. (*Makofi*)

Tume ya Haki za Binadamu tumeitwisha mzigo mkubwa sana. Ukweli uliopo ni kwamba uwezo wake bado ni mdogo. Tume hii bado ni changa haina matawi. Katika taarifa ya tume tumeambiwa kwamba tume ina kesi karibu 5000 iliyotokea mwaka jana. Kweli kesi 5000 hata kama ungekuwa ni efficient utawezaji kuzishughulikia zote kwa wakati mmoja? Huna tawi, huna chombo cha kufanya kazi, unategemea haki itatendeka? Sasa kwa heshima tuliyonayo katika nchi yetu mimi naomba mapendekezo aliyotoa Mheshimiwa Lamwai kwa sababu yuko kwenye hicho chungu yaangaliwe. (*Makofi*)

Yako mambo machache yaliyopendekezwa na wenzetu wa Kambi ya Upinzani yanaweza yakafikiriwa. Mimi naamini Waziri anakubali. Yale ambayo siyo ya msingi kama ya kumtuhumu mtu kwa sababu tu ya mambo binafsi, uje useme aachie ngazi hiyo, tunasema haiwezi kuruhusiwa lakini yale mazuri kwa kweli ni vizuri yaangaliwe. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninachoshauri na ninachoomba ni mambo matatu kwanza tuimarishe sana vyombo vyetu hivi vya kutenda haki na nguzo hii ya Idara ya Mahakama, ipewe haki yake na hadhi yake na zitengewe fedha kama nguzo muhimu, kama nguzo zingine zinavyotengewa fedha. Si halali hata siku moja Serikali, kama chombo kinachogawa mapato ya Serikali kutamka na kuangalia kwamba eneo la kutekeleza haki siyo eneo muhimu na bahati nzuri imetambuliwa sasa kwamba sekta ya haki, nayo ni ya kipaumbele katika kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Sasa hatuoni sababu kwa nini kama sekta zingine kwa mfano za sekta za elimu na afya zimetengewa shilingi bilioni 85, bilioni 100, hii inatengewa shilingi bilioni, eti ijenge Mahakama, inunue vyombo vya kudhibiti na kukagua Mahakama mimi nadhani tunafanya mchezo, haki haiwezi kutendeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Mwapachu, naomba niseme kwamba ametoka Mvi zaidi katika kipindi hiki cha miaka kumi alichelewa Waziri kuliko

huko nyuma. Lakini ni matatizo ya Wizara hii, mambo hayaendi na hayaendi kwa sababu Serikali kwa ujumla hajatoa kipaumbele katika sekta ya sheria. Kwa kweli leo ukiangalia katika Wilaya ya Lushoto jinsi mtu anavyotembea karibu kilometa 20 kwenda kupata haki. Kitu cha kuchekesha ni kwamba mwingine inabidi aje ye ye mwenyewe ili ahukumiwe. Mtu anatoka Bumbuli aje Soni kusikiliza kesi au anatoka Mlalo aje Dochisikilize kesi yake.

Kwa bahati mbaya mtu huyo anafungwa na amekuja na mtu mmoja kumsindikiza. Sasa akihukumiwa pale kufungwa yule anarudisha kilio nyumbani na ndiyo pale pale Mahakimu wanaambiwa wamekula rushwa maana aliyeshudua haki ikitendeka pale, wala maelezo ya hakimu kumfunga au kumwachia hayakueleza, pale pale inaonekana kwamba haki haikutendeka mzigo mzima anatupiwa Hakimu. (*Makofî*)

Lakini kwa kweli kama Mahakama ingekuwa mahali jirani wananchi wakaenda kusikiliza watajua kweli kama huyu katenda kosa au hakutenda kosa. Lakini mpango wa Waziri na katika mpango wa Serikali kwa ujumla hakuna mpango ambao kweli unatamka wazi kwamba ikifika mwaka fulani tatizo la uhaba wa Mahakama, uhaba wa Mahakimu tutalitatua. Kila mwaka tunaambiwa programu zipo Hoja ndiyo sijui ya *start*, sasa baadaye wenzetu kule wataipa jina jingine na kweli unafuatana na ukweli kwa sababu umekwenda kuanza, kwenda huendi, hutamki kama unakwenda, kwa nini usiambiwe ume-*stop*? Umesimamia kwa hiyo, ni *none start*.

Mimi sisemi nakubaliana naye lakini programu tunapoziweka ni lazima zilingane na utekelezaji. Tukiweka programu ambazo haziwezi kutekelezeka hatutafanikiwa. Mimi nasema tatizo siyo Waziri, wala tatizo siyo Wizara. Lakini wafadhili siku zote nimesema tuwaangalie sana. Wanakuja kwa malengo siyo mengi ni mazuri, mengi ni kutuyumbisha. Tuwe na msimamo wa kusema hili tulitekeleze na tukishakubaliana nalo twende kwa wananchi. (*Makofî*)

Kwa hiyo, naomba chuo changu cha Lushoto cha Mahakama kiwekwe katika programu hii kwa sababu kama chuo hakitaweza kuongeza majengo bado tatizo la Mahakimu litakuwepo. Kama kweli hatutakuwa na programu ya dharti ni lini tutatatua tatizo la majengo ya Mahakama? Tutakuwa bado na tatizo la Mahakimu ambao wanakula rushwa kwa sababu hawana nafasi ya kujieleza kwa wahusika moja kwa moja, wanajieleza katika maeneo ya ugenini. Nchi yetu itaonekana haitendi haki. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mimi nashauri na naomba sana baada ya kuunga mkono hoja niombe yale yalitamkwa, ambayo kwa kweli ni ya maana sana yazingatiwe na tupate ratiba kamili ya kutatua tatizo la utekelezaji wa haki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nichukue nafasi hii, nimshukuru Mola ambaye amewezesha asubuhi hii, kuamka nikiwa na afya na kuweza kushiriki katika shughuli hizi pamoja na sisi wote tukiwa katika hali ya afya njema. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, pili, nichukue nafasi hii, kukushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia machache katika hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Nataka nichukue nafasi hii kuwatanabaisha Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwamba wamebebesewa jukumu zito, jukumu ambalo wanatakiwa watanze na kutetea haki za watu. Hili ni suala zito kwa sababu ni suala ambalo linabeba mamlaka, linabeba haki za watu jambo ambalo haliishii hapa duniani, lakini utendaji wake pia unaisha baada ya maisha haya kumalizika. Kwa hiyo, ni vema wakazingatia haya na wakafanya kazi zao kwa uadilifu mkubwa sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo machache sana ya kuzungumza ni mawili/matatu tu. La kwanza nataka niende katika kifungu cha 7 ni napenda ninukuu hapa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, inasema kwamba: “jukumu la Wizara yangu ni kusimamia suala zima la utoaji haki, udumishaji wa haki za binadamu na kuishauri Serikali katika masuala ya sheria kwa lengo la kudumisha amani, utulivu na kuweka mazingira mazuri ya maendeleo. Hii ndiyo azma moja kubwa ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, bila kuwepo amani na utulivu maendeleo ya nchi hayawezi kupatikana. Sasa napenda kuchukua nafasi hii kushauri Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kuangalia uwezekano wa kuweka hali ya amani na utulivu kwa upande wa Zanzibar, hasa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 kuzingatia hali halisi ya siasa ya Kisiwani Zanzibar. Nilikuwa nashauri katika kutekeleza hilo Wizara iangalie uwezekano wa kuweka marekebisho makubwa katika sheria au katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, itakayowezesha vyama hivi vya CUF na CCM kwa upande wa Zanzibar, kuunda Serikali ya pamoja katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005.

Hili si jambo jipya hata kwenye muafaka imeleewa kwamba baada ya kumalizika uchaguzi mdogo vyama vya CCM na CUF, vilipatana kufikiria vipi wanaweza kuanzisha Serikali ya pamoja. *Logic* yake hasa hii nafikiria kusema kwamba kwa hali ya siasa ya Zanzibar ilivyo ni ukweli usiofichika kwamba mtu anakuambia kwamba Zanzibar hakuna CCM tukiacha ushabiki kisiasa huyu atakuwa kwa kweli anaongopa. Hali kadhalika atakaye kuambia kwamba Zanzibar CUF hakuna tabu huyu pia atakuwa anaongopa. Sasa katika hali hiyo, kwa kweli iko haja Serikali ya Muungano kukaa chini na kutafakari sana ili kulinda amani na kuleta umoja wa kweli, basi iko haja kubwa sana ya kufikiria kufanya mabadiliko makubwa ya Katiba ambayo yataapelekea kuundwa kwa Serikali ya pamoja kati ya CCM na CUF. Hili likifanyika nakuhakikishia hizi chokochoko zote pamoja na uhasama ambaou upo kwa kweli huu utaondoka. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, haiwezekani asilimia 49 ya wananchi ukaweka pembeni kwamba wao hawahusiki katika Serikali na ninyi watu 51 mkajifanya nyie wenye mamlaka yote unatarajia pawe nini hapa? Haiwezekani. Sasa nashauri sana katika hili basi kaeni Viongozi wa Serikali ya Muungano mfikirie kwamba katika kuleta amani kwa upande wa Zanzibar, suala la kuundwa kwa Serikali ya pamoja ni la msingi sana. suala hili sisemi mimi tu, suala hii imezungumzwa kutokana wetu wa vyama viwili ambayo

imo ndani ya muafaka na ndiyo utamaduni wa nchi nyingi za Afrika kuweza kuweka watu mahali pamoja. Nawahakikishieni Waheshimiwa Wabunge, kwamba hili kama hamtalitekeleza uchaguzi wa mwaka 2005 tutakwenda salama salmini na tutakaa pamoja na maslahi ya taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini hivi sasa pana muafaka, lakini unamsikia kiongozi wa juu wa Serikali anamwita Kiongozi wa Upinzani, mwongo na tuna muafaka zinaenda kweli kauli hizi zinaashiria nini? Mheshimiwa Rais Karume, kasema tumechoka na hizi kauli zinazoashiria shari. Mimi kila nikitazama huko mbele katika uchaguzi wa mwaka 2005 sioni mwanga naona kiza, pamoja na muafaka naona kiza. Sasa kiza hiki mwenye mamlaka na jukumu la kuziondoa kiza hiki ni Serikali ya Muungano. Nadhani pamoja na uchanga wangu katika siasa kwani ni mtoto mdogo sana, lakini nadhani ni vyema mkafikiria na kuzingatia haya mawazo ambayo tunayota na mkidhani kwamba ni ya muafaka na mkayashughulikia siku za mbeleni mtakuja nikumbuka. La mkiona kwamba huyu ni mtoto mdogo masihara yake hayana mpango wowote, nawakikisheni ipo siku moja siku za baadaye huko mtakuja kukumbuka kwamba siku yuko kijana aliyeitwa Ali Said Salim, Mbunge wa Ziwani alizungumza suala hili. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Longa longa.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Spika, lingine nataka niseme tumekuwa na matatizo mengi. Kila siku manung'unico ya upande huu wa Muungano kulalamikia upande mwingine wa muungano kwamba sera/muundo au utekelezaji wa Muungano umekuwa ni wa mashaka. Sasa nilikuwa nashauri kwa nini Serikali ya Muungano haifikirii kuunda mahususi kabisa Mahakama ya Katiba? Kuundwa kwa Mahakama ya Katiba kutasaidia kupunguza kwanza malalamiko ya mambo ya Muungano. Malalamiko yote ya mambo ya Muungano yatakuwa yanashughulikiwa na Mahakama hii ya Katiba. Mahakama ya Katiba, sina hakika kwamba kwenye Katiba inaruhusu au hairuhusu.

Lakini hata kama hairuhusu bado uwezo wa kufanya mabadiliko ili tukaruhusu kuundwa kwa Mahakama ya Katiba uwezo upo. Kama hamna katika kipengele cha Katiba zote ya Zanzibar na Muungano, basi ni vyema tukafikiria kuweka kipengele ambacho kitaruhusu kuanzishwa kwa Mahakama ya Katiba. Mahakama hii itashughulikia kwa mfano masuala ya Muungano. Lakini mbali ya shughuli hizo, baada ya kumaliza uchaguzi kunakuwa na kesi nyingi sana zinazohusiana na uchaguzi na kesi hizi hurundikana katika mahakama zetu na zinachukua muda mrefu. (*Makofii*)

Sasa kama tutakuwa na Mahakama ya Katiba hata hizi kesi zote za bara na visiwani zinazohusiana na uchaguzi zitaratibiwa chini ya Mahakama ya Katiba. Hii itasaidia kupunguza hata mlundikano wa kesi nyingi ambazo ziko kwenye mahakama zetu za Kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, uzoefu unatuonyesha kwamba kesi za uchaguzi zinapokuwa kwenye mahakama zetu za kawaida zinachukua muda mrefu sana kumalizika, mfano hai ni kesi inayohusu Wawakilishi wa CUF sita wa Zanzibar ambayo ilifunguliwa lakini hadi leo kesi ile bado inaendelea, inapigwa kalenda. Nawahakikishia kesi ile itafika mwaka

2005 bado haujapatikana uamuzi. Sasa kama tutakuwa na Mahakama ya Katiba, kesi zote za Uchaguzi zitahamishiwa katika Mahakama hii, basi naamini katika muda mfupi kesi zile zitapata ufumbuzi na wenyewe haki watapewa na wasio na haki hawatapewa.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo nataka niseme ni suala la rushwa hasa katika Idara ya Mahakama. Kwa kweli tumekuwa na malalamiko mengi sana kwamba Idara ya Mahakama rushwa imekithiri. Kwa hiyo, watu amba ni maskini siku zote kwa kuwa hawapati haki zao kupitia mahakama. Hili ni tatizo kwa sababu hata mazingira yenyewe ya rushwa yanapotolewa yanatolewa katika hali ya usiri sana. Siri rahisi kuweza kubaina kwamba hapa pametokea rushwa. Sasa siku moja nilipendekeza hapa na nataka nirudie tena kusema kwamba kutoa madawa katika masuala ya kukabiliana na rushwa si katika Idara ya Mahakama tu, lakini katika Idara na Wizara na shughuli zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, dawa yenyewe ni hivi, sisi sote ni binadamu tuna sifa moja kwamba tunaamini amini sana dini zetu. Kama ni Mkristo basi utaamini Biblia kweli kweli kama ni Mkristo kweli. Kama ni Muislam kweli kweli basi utaamini msaafu hasa katika kukabiliana na hili suala la rushwa.

Kwa nini, hatulipeleki mpango wa dini kabisa kabisa. Ni kuwekwa kwa Misahafu na Kitabu cha Biblia katika Mahakama na katika ofisi zetu na hasa Mahakama asubuhi, kama tunavyofanya sisi hapa katika kuomba dua basi dua ya kwanza wafanyakazi wote Waislamu wakakamata Msaafu kwamnba tunaapa hatutachukua rushwa kwa leo.

Pia Wakristo wote wataapa kwa Bibilia hii hatutachukua rushwa na tukichukua rushwa Mungu tuhukumu. Nawahakikishieni rushwa itaondoka taratibu. Vinginevyo tutamaliza karne rushwa bado iko pale pale. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri Mheshimiwa Bakari Mwapachu na Mheshimiwa Chenge katika kulinda, kuitetea haki ili wananchi wote waweze kupata haki zao kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri na pia nimpongeze yeye pamoja na watalaaam kwa kuwasilisha bajeti yao vizuri. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Pia naomba nitoe pole kwa familia ya Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, naiombea kwa Mungu familia yake iweze kuwa na subira na Mwenyezi Mungu amlaze marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa labda nianzie kwenye suala alilozungumza Mheshimiwa aliyemaliza kuzungumza hapa kwamba namna ya kuondoa rushwa ni

watumishi wote kukamata Misahafu au kukamata Biblia. Sasa Mheshimiwa mmoja akawa anauliza na Wapagani je? Nikawa nasema, kwa hali ya rushwa jinsi ilivyo, mimi naamini dini ya Wapagani itapata wafuasi wengi iwapo utaratibu huo utaanzishwa kwa namna mambo yalivyo katika nchi yetu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nitoe shukrani kwa Wizara na Idara zake na Serikali kwa ujumla kwa kukubali kilio chetu cha siku nyingi cha kuanzisha Mahakama Kuu katika Mkoa wetu wa Kagera pale Bukoba. Nawapongeza sana kwa sababu imepunguza kero nyingi ambazo kimsingi tulikuwa tunazilalamikia muda mrefu. Pia, nishukuru kwamba hata ndani ya Bajeti hii nafikiri imetengwa fedha za kujenga jengo zuri tu la Mahakama pale Bukoba.

Naamini kama ambavyo imeanza kuonekana mandhari ya eneo lile la Mahakama litaendelea kupendeza na litapendezesha Mji wetu wa Bukoba. Kama Waziri na Wataalam wake wanavyofahamu, Bukoba pamekuwa na Chuo, pamekuwa mahali pa kupitia watu wengi ambao wamekuwa aidha wanatumikia Mahakama au wanatumikia Idara mbalimbali za Serikali ambapo sisi kazi tunayoifanya pale ni kuwa-*train* na kuwatayarisha kukamata madaraka ya nafasi kubwa zaidi. Kwa hiyo, suala la kuimarisha Mahakama yetu na Taasisi zetu za pale Bukoba Mjini zinatusaidia kwa kiasi kikubwa na kusaidia Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo kuhusiana na uanzishwaji wa Mahakama ya Ardhi. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Utawala na mwakilishi wetu, Mzungumzaji wa Kamati amelizungumza wazi. Kwa kweli limekuwa ni suala ambalo kidogo Serikali naamini haijalitilia mkazo kulifanyia kazi ipasavyo na matokeo yake kutoanza kikamilifu kwa *system* nzima ya Mahakama ya Ardhi kuanzia ngazi za chini mpaka juu. Kwa kweli imekuwa ni kero na inasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Mimi nilifika mahali, nafikiri kwenye Kamati nikazungumza wazi kabisa kwamba ni vyema Serikali inapokuwa haijajiandaa vizuri isikurupuke kuanzisha vitu ambavyo haiwezi kuvisimamia na haiwezi kuviweka katika utekelezaji ulio makini na sahihi. Tunaposhindwa kusimamia kitu au kupanga mipango yetu ikiwa kamili, matokeo yake inakuwa ni kuwaumiza wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutoanza kufanya kazi kwa Mahakama ya Ardhi kuanzia ngazi za chini, hivi sasa kumetoa *loophole* kwa watu wajanja wachache kuitumia nafasi hiyo kuweza kuwahangaisha watu na kuwanyima haki na kuweza kuwadhulumu hata mali. Yameshatokea matukio mbalimbali ambapo mtu pamoja na kuwa na kiwanja chake, anaweza akashtukia nyumba inajengwa ndani ya wiki moja na asiwe na jambo lolote la kufanya. Anashtukia asubuhi asubuhi mtu anamwaga mchanga, anapima msingi wake wa nyumba, ndani ya wiki moja mtu ameshasimamisha nyumba mpaka hata kwenye *level* ya *renter*. Lakini watu hao wanafanya hivyo kwa sababu wanajua kwamba bado kuna *loophole*, *system* yetu ya Mahakama ya mtu kulalamikia mambo ya viwanja bado iko *weak* na haipo. Kwa hiyo, matokeo yake ndiyo hizo vurugu ambazo tunazing'amu na zinatokea kila wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kama ambavyo ushauri umetolewa na Kamati kwamba maadam umeshatokea uteuzi wa Mahakamu Wakazi, kwa kweli tungeomba Mahakama hizi zianze haraka kadri inavyowezekana na hasa ngazi za chini. Hii Mahakama ya juu ambayo tayari imeanza kufanya kazi, naamini imeanzishwa kwa ajili ya wakubwa, isije ikawa kwamba hata kuanzishwa kwa Mahakama ya Ardhi tuliianzisha tu kwa kukurupushwa na Wafadhili au Wawekezaji wakubwa. Mimi ningeomba kwamba maadam nchi hii walio wengi ni wananchi wa kawaida, lazima tuwe na *system* ya kuweza kuwasaidia na kuwapa haki zao za msingi.

Tatizo hili la mambo ya ardhi kama unavyofahamu kwa maeneo ya Bukoba, Kagera na Kilimanjaro ndio maeneo makubwa ambayo kwa kweli yana matatizo na kesi nyingi sana za ardhi. Kwa hiyo, kuharakisha kufanyia kazi jambo hili kutawasaidia wananchi wangu, wapigakura wangu wa Bukoba Mjini, pamoja na wananchi wa Kagera na mikoa mingine kama nilivyosema kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie pia suala la Mahakama zetu. Kama tunavyofahamu, mwaka kesho tunaingia katika kipindi cha Uchaguzi na mwaka huu mwishoni kama ambavyo ilizungumzwa hapa Bungeni kutakuwepo na Chaguzi za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kutenga pesa nyingi kwa Wizara ya Mambo ya Ndani tena wakazungumza *specifically* kwamba tunatoa pesa kwa sababu mwaka kesho ni kipindi cha uchaguzi na tukapitisha tukawapa, lakini kutoa pesa Wizara ya Mambo ya Ndani bila kutoa pesa kwenye *system* ya Mahakama ambayo kimsingi mambo yanayokuwa yamefanyiwa kazi na Polisi mwisho wake yanapelekwa kwenye Mahakama, nafikiri tunakuwa bado hatujasaidia chochote. Vinginevyo kwenye kipindi cha Uchaguzi tutakuwa na matukio mengi ambayo yatashughulikiwa na Polisi na yataishia Polisi na watu wanyimwe haki kwenye *system* zetu za Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha uchaguzi huwa kunakuwa na mambo chungu nzima yanayolalamikiwa dhidi ya taratibu na wakati mwingine hata vyombo vy'a dola vinaweza kuingilia shughuli hizo za uchaguzi kwa kuwakamata watu mbalimbali. Sasa kama hatujaandaa utaratibu mzuri na *network* nzuri ya kufanyia kazi mambo mbalimbali ambayo yatakuwa yamechukuliwa hatua na Polisi, mimi naamini utakuwa ni uchaguzi wa vurugu kwa sababu watu wakishanyimwa haki zao, watu wakishanyimwa fursa ya kupelekwa kwenye vyombo vy'a kuweza kuwasikiliza na kutoa maamuzi haraka, naamini mwisho wa yote itakuwa ni vurugu tupu.

Mheshimiwa Spika, jambo nililokuwa naliomba kwa Serikali ni kwamba umuhimu ulionekana kwa upande wa kutoa fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa minajili ya kuwa na uchaguzi ulio mzuri, ulio na utulivu na haki, vile vile suala hili lingeweza kufanyika kwa Wizara hii ili iweze kusimamia haki katika kipindi hicho cha uchaguzi.

Pia nimwombe Mheshimiwa Jaji Mkuu awapange Mahakimu wake vizuri. Ngazi zote zipangwe vizuri kwa sababu kumekuwa na matukio mbalimbali ambapo Mahakimu kwenye maeneo mbalimbali hizi kesi za kisiasa wengine wanaziogopa kuzitolea

maamuzi. Sasa nilikuwa naomba, pamoja na Serikali kwamba imeona umuhimu wa kulizungumzia suala la kuwa na Tume ya Uchaguzi inayoshirikisha Vyama vingi kwa minajili ya kuwa na Tume inayoonekana huru zaidi, lakini ili tuwe na Mahakama ambayo ni *independent*, Mahakama ambayo inaweza ikawa na heshima, ikajijengea heshima ya kwamba ni mhimiili anayejitegemea, ningewomba Jaji Mkuu aweze kuwapanga Mahakimu wake vizuri na vile vile Semina maalum itolewe kwa Mahakimu wetu namna gani ya kuweza ku-deal na hizi kesi hasa zinazohusiana na mambo ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kuhusiana na marekebisho ya Katiba. Tunashukuru kwamba suala hili limeanza kufanyiwa kazi na bila shaka wakati wowote tutaletewa marekebisho ya Katiba. Sasa ningeomba Serikali ya CCM ambayo kimsingi ndio watayarishaji wakuu wa suala hili, ni vizuri wakatumia nafasi hii vizuri wakafanya marekebisho ya Katiba ambayo ni more serious na ambayo yanagusa jamii yetu katika mambo mbalimbali ambayo yanalamikiwa au mambo mbalimbali ambayo yanaweza yakaifanya nchi yetu iweze kukaa katika hali ya utulivu na amani.

Vile vile ni nafasi yao pekee ambayo wanaweza wakafanya marekebisho ya Katiba yanayoweza kuwasaidia hata tukishawaondoka madarakani mwaka kesho. Kwa sababu nchi nydingi ambazo zimeingia kwenye Uchaguzi na wenyewe wanajua, pindi Upinzani unapochukua Serikali, wengi wanapenda Katiba isibadilike kusudi sheria hizo hizo mlizozitunga tuzitumie kuwashughulikia. Imetokea Zambia, imetokea Kenya.

Kenya pamoja na kwamba Serikali ya *NARC* kabla haijaingia madarakani ilikuwa inalilia Katiba kubadilishwa, lakini baada ya kuchukua madaraka, suala la kubadili Katiba limekuwa ni ngoma nzito. Sasa kwa wenzetu wa CCM, Serikali ya CCM ni bora ikajifunza kutoka kwa majirani zao kwa sababu msipobadili, mambo yote tunayoyalalamikia kwamba yarekebishwe, hayo hayo yatakuwa msumari mzito wa kuwapiga kuanzia utosini. Kwa hiyo, tungeomba suala hili, kama ambavyo tumeamua kuwa na Tume huru, lakini vile vile mambo ya msingi ambayo yamekuwa yakilalamikiwa yarekebishwe, muyarekebishe kabla moto haujawa mkali. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, nisipigiwe kengele ya pili, naomba kumpongeza Waziri na kisha ajaribu kuangalia mambo ambayo tumeweza kuyazungumza.

MBUNGE FULANI: Unga mkono.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Ah, siwezi kuunga mkono, kwanza wamempa pesa njiwa, sasa nitaungaje? Ahsante sana. Nashukuru. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLIAM J. SHIJA: Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya leo ili niweze kuzungumza machache juu ya hoja ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote bado naendelea kuwaombea na kumwombea Marehemu Mwalyego kwamba Mwenyezi Mungu ampumzishe mahali pema Peponi na tunawapa pole sana ndugu zetu wa Jimbo la Mbeya Vijijini. Nilikwishesem, lakini naona ni vyema tu nirudie.

Mheshimiwa Spika, utangulizi wangu katika kuzungumzia hoja hii, napenda nirejee ukurasa wa 38 wa hotuba ya Waziri ambapo wanazungumzia haki za binadamu, utawala bora na mambo ya Katiba.

Ni kweli kwamba Wizara hii ni Wizara mojawapo ya msingi katika kutoa haki kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba na Sheria zilizowekwa na katika kudumisha utawala bora nchini. Kwa hiyo, isipofanya kazi vizuri kwa kushirikiana na Wizara nyingine, tutaona kwamba wananchi hawataweza kufanya kazi vizuri na kwa uhuru katika kujiletea maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, kuna Mwandishi mmoja ameandika kitabu kinachoitwa Taifa, Sheria na Maendeleo. Kwa Kiingereza, *The State, Law and Development*. Mwandishi huyu kwa watu waliosomea mambo ya Sheria bila shaka wanamfahamu, lakini hoja yake katika kitabu kile anasema kwamba, kama Taifa halitaendesha mambo ya sheria vizuri, watu watakosa haki na kwa msingi huo watu hawatafanya maendeleo ya uhakika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napenda nianzie hapo kwa kusema kwamba mwaka 1995 Mheshimiwa Rais aliteua Tume ya Warioba juu ya suala la rushwa. Je, hatima ya Tume hiyo ya Warioba juu ya rushwa iliishia wapi? Kuna nini baadaye ambacho hasa kilitekelezwa katika kufuatilia Tume ya Rushwa ya Warioba? Hilo napenda niliseme kama utangulizi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza ambalo nataka kulisema katika mazungumzo yangu ni kwamba napenda niwaunge mkono Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliozungumza na kulalamika juu ya hali ya wananchi Vijijini na Mjini kubambikiziwa kesi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa hoja ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nilizungumzia hili, lakini leo nimekuomba nafasi niweze kulirudia tena ili kusudi Serikali isikie kwamba mimi kama Mbunge wa Sengerema, nalalamikia juu ya wananchi wangu kubambikiziwa kesi. Suala hilo liko ndani ya yale ambayo Warioba aliyapata katika Tume yake ya Rushwa kwa sababu tunafahamu katika Tume ya Warioba ya Rushwa alizungumzia juu ya Polisi na Mahakama kukithiri katika rushwa.

Sasa suala hilo bado lipo na linaendelea kuumiza wananchi kwamba katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Tabora, Mara, Kagera na maeneo yake na hata Dodoma kwa watani zangu, kwa sababu wananchi wengi wana maisha ya kuwa na mifugo, huwa wanabambikiziwa kesi na hali hiyo inawaathiri sana wananchi, inawaathiri wanawake, watoto na familia mbalimbali zinashindwa kufanya mambo ya maendeleo kwa sababu

wapo wenzetu wachache au wengi ambao wamezama katika hali ya kubambikizia wananchi kesi na hasa kesi za mauaji. (*Makofi*)

Yupo mwananchi mmoja John Wanzalima pale Kasungamire, nimekwenda kukagua Gereza la Kasungamire nikakuta maelezo ya wengi wa mahabusu walikuwa wanalamika wamebambikiziwa kesi.

Mheshimiwa Spika, hiyo imetokea mahali pengi sana. Wapo wananchi wanalamika sana, wanakuja kwa Wabunge usiku na mchana, wengine wanakuja kutukabidhi familia tuwasomeshee watoto wao, wengine wanakuja kulia akina mama kwamba mume wangu amebambikiziwa kesi, sio kweli na aliyofanya yanafahamika Kijijini kwa Viongozi wa Vijiji na Viongozi wengine lakini bado unakuta mtu anasota katika mahabusu.

Mheshimiwa Spika, suala hili ni zito, naomba Bunge lako Tukufu na Serikali ilipokee ilifanyie kazi kikamilifu. Wananchi Vijijini wanabambikiziwa kesi ili waliwe rushwa na wanateseka! (*Makofi*)

Nafahamu sehemu za wafugaji, wavuvi, wakulima wa kawaida, wafanyakishara wadogo wadogo, wananchi wanabambikiziwa kesi. Mimi nina masikitiko makubwa sana juu ya hili, kwa sababu wananchi wanapokuja kukueleza mmoja mmoja, wanakueleza mambo ya kukusikitisha kweli! Sasa inatokeaje mpaka tabia hii iwe imeota mizizi! Imekuwa kama imezoeleka, imekuwa kama ndio tabia ya Watanzania kwa wananchi kubambikiziwa kesi!

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alishapita baadhi ya Mikoa na Mkoa wa Mwanza aliwahi kufika akachunguza baadhi ya maeneo, akapita kwenye Magereza yetu, naomba aendelee na ninaomba Serikali kwa ujumla ifanye juhudi maalum kuweza kuhakikisha kwamba jambo hili sasa linaachwa. Hatuwezi kupata maendeleo ya kweli kama wananchi wanasota na kesi ndogo ndogo lakini kwa sababu wanabambikiziwa kwa sababu wana mali.

Mheshimiwa Spika, mimi narudia, nimeshapata nafasi au bahati ya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Nilichunguza kwa wakati wangu na nikajua kwa uhakika juu ya tabia hii ya watu wengine wanaomba hata kuhamishiwa Mwanza au Shinyanga katika kazi zao ili waende wakavune mali kwa kubambikizia kesi wananchi. *Yes! I know it!* Nina uhakika! Ndiyo maana ninaomba Serikali hili jambo kupitia Polisi au Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria au Wizara nyingine na Serikali kwa ujumla, Serikali yetu inafanya mambo mengi mazuri lakini yanachafuliwa na watu wachache wanaokwenda Vijijini kuwaonea wananchi bila sababu *and then they feel terrorised*. Kwa Kiswahili, wanahofishwa wananchi Kijijini pale, akichukuliwa tajiri mmoja basi wanakaa wana hofu hawawezi kufanya kazi katika ujumla wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana suala hili tulifanyie kazi kama Watanzania ili suala la kubambikizia kesi wananchi likomeshwe. Pendekeso langu nasema kwamba pamoja na kwamba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora bado ni ndogo lakini tungeunda Mabaraza ya Haki za Wananchi Wilayani pale ili Tume ikawa inatumia Mabaraza hayo kuweza kuchunguza na kupunguza hali hiyo ya watu kulalamika kwamba wamebambikiziwa kesi. Mabaraza hayo yatasaidia sana. Sasa namna ya kuyatungia utaratibu, hilo naliacha kwa wataalam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni juu ya Kesi za Uchaguzi. Mwaka kesho tutakuwa na Uchaguzi Mkuu, tunamwomba Mwenyezi Mungu wale ambao watakuwepo awajalie tuendeshe Uchaguzi wetu vizuri ili Tanzania iendelee kuwa na utulivu wake na amani kama tulivyozoea. (*Makofi*)

Lakini naomba nitoe hoja leo kwamba tuna Majaji wetu wazuri kabisa wana uzoefu, wana maadili wapo wengi pamoja na uteuzi ambao umefanywa kwa mfano kuingia katika Mahakama ya Rufaa kwa baadhi ya Majaji wetu, tunawapongeza sana.

Lakini mimi nilikuwa nasema kwamba ifike mahali tubadili sheria ili Mbunge asiweze kuondolewa kwenye Ubunge wake mpaka jopo la Majaji watatu wakae. Kuondolewa kirahisi rahisi kwa Mbunge na Jaji mmoja. Je, kama amehongwa utajuaje?

Hatupendi kusema kwamba labda kuna hisia Jaji anaweza kuomba hongo, lakini kibinadamu kuna baadhi ya Majaji wanahongwa na katika kesi hizi hata za wananchi wa kawaida utakuta kama Jaji atahongwa, basi mwananchi atakosa haki yake. Katika haki, kama Mbunge amechaguliwa na watu 40,000, 50,000 au 30,000. Sasa inakuwaje kirahisi rahisi aje aondolewe na Jaji mmoja akikaa kwenye *Bench*?

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hoja yangu ya msingi kabisa na ninajua naungwa mkono na ndugu zangu wengi tu hapa ndani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hoja ni kwamba si kwamba Wabunge hapa utachukulia tu kwamba wameingia kwa rushwa, hapana. Au utasema katika Afrika Uchaguzi haukufanyika vizuri. Haukufanyika vizuri namna gani ndani msimamizi kwa timu ya *African Union*. Nimeona matatizo ni yale yale kama ambayo tunayapata Tanzania.

Sasa Uchaguzi kama utasema ulikosea, eti maboksi hayakufika mapema; hayakufika mapema wapi? Visiwani! Visiwani kama maboksi hayakufika mapema ndiyo hali yetu ya Afrika, ndio hali yetu ya maendeleo! Sasa ndio nasema, kwa kweli kuna haja ya kutazama kwa nini Mbunge anayechaguliwa kwa halali na wananchi aweze kutolewa katika Ubunge wake na Jaji mmoja?

Naomba wawe Majaji watatu na Majaji watatu tunafahamu kabisa katika ngazi ya Mahakama ya Rufaa bila hata kuomba Mahakama ya Rufaa lakini kesi hizo zisimamiwe na Majaji watatu. Najua haki itatendeka na Taifa hili litaepukana na hukumu ambazo zinaingiza Taifa hasara tu badala ya kupeleka maji kwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho napenda niseme kwamba katika sheria kuna suala ambalo hata Mheshimiwa Waziri amelizungumza vizuri juu ya Elimu ya Sheria. Hebu tujizatiti katika kutoa Elimu ya Sheria Vijijini ili wananchi waelewe kinachofanywa na Sheria zinazopitishwa Bungeni.

Sisi Wabunge tunafanya kazi hiyo lakini hatutoshi. Tutengeneze vipeperushi mara kwa mara tuvipeleke Vijijini vielezee juu ya sheria mbalimbali wananchi wapate Elimu ya Sheria tunazozitunga na kazi hii ni kazi ya Wizara hii, tusiendelee na usemi wa Waingereza, *ignorance of the law has no excuse* na Walatini wanaongezea ignorance has juris known as skusat.

Sasa kama kutojua sheria hakuna kinga yoyote, tuondoke huko twende sasa katika hali ya kuwasaidia wananchi Vijijini waweze kujua sheria, waweze kufuatilia mambo mbalimbali ya haki zao. Hivyo tutakuwa tunawasaidia wananchi; tutakuwa tunajenga mshikamano wa pamoja ili kusudi wananchi washughulike katika kufanya mambo ya tija yawe ni ya kilimo, uvuvi au kwa wafugaji, yaweze kufanywa na wananchi wote kwa tija tuendelee kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, napenda niseme namwunga mkono Mheshimiwa Waziri hoja yake na ninamtakia kila la kheri. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. GEORGE F. MLAWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba.

Kwanza kabisa sina matatizo kumwunga mkono Waziri wetu katika hoja hii na ninaunga mkono hoja. Vile vile ningependa kumpongeza Waziri kwa kazi njema anayoifanya katika Wizara hii pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Watendaji wote katika Wizara hii. (*Makofi*)

Vile vile ningependa niipongeze kwa namna ya pekee Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora chini ya Uongozi makini wa Mheshimiwa Jaji Kisanga. Kuna mambo mengine nitakayoyazungumzia yanayotokana na taarifa iliyotolewa na Tume hii.

Kwanza kabisa naungana mkono na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba fedha inayotolewa kwa Wizara hii ni kidogo mno na kwa kweli tunafanya makosa kutoa fedha kidogo kiasi hiki kwa Wizara ambayo ina dhamana ya kutoa fedha hizi kwa Mahakama. Mahakama ni chombo chenye mamlaka ya utoaji haki. Hii ni kazi kubwa na ni mamlaka kubwa katika nchi.

Sasa tunapokuwa tunagawa hela kiholela tu, yaani hakuna *formula* maalum ya kuhakikisha kwamba Mahakama kama Mamlaka katika hizi Mamlaka tatu kwamba kuna *formula* gani kuhakikisha kwamba Mamlaka hii ya tatu inapewa fedha ambazo angalau itafikisha *above 50 percent* ya majukumu yake, lazima kweli kuna namna fulani ya

kupima na sio tu kupanga tu kwamba na Wizara hii, na Wizara hii, kwa hiyo na Mahakama inachanganywa kama Idara tu mojawapo hivi.

Nafikiri tunafanya makosa sana na ndio maana kunakuwa na matatizo makubwa sana katika Mahakama zetu. Kama Mahakama za Mwanzo, yaani kabisa ukienda kwenye Mahakama zetu za Mwanzo ambako ndiko waliko Watanzania wengi, kuna hali mbaya sana ya *staffing*, majengo na *facilities* mbalimbali za kuendeshea Mahakama hiso.

Kwa hiyo, ningeomba upande wa Serikali inapoleta Bajeti Bungeni, kabla hawajafanya maamuzi au kutenga fedha, watengeneze *formula* fulani hata kama ile *formula* ambayo imeshawahi kuzungumzwa huko nyuma juu ya mapato ya Serikali, hiyo inakuwa ni ngumu kidogo kuiweka lakini kuwe na *formula* fulani ya kitaalam ambayo inahakikisha kwamba majukumu muhimu ya Mahakama yanakuwa *taken care of*.

Halafu ningependa kuzungumzia juu ya taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ambayo imezungumziwa sana juu ya mahabusu na wale ambao wanahukumiwa katika kesi za mauaji ambao wako wengi huko ndani ya mahabusu na ndani ya Magereza. Kwanza ni juu ya kesi za mauaji, ni nyingi sana! Mimi mwenyewe kwa vile zamani nilikuwa Wakili wa Serikali, kwa hiyo ninaelewa juu ya suala hili uzito wake ni mkubwa sana.

Kwa hiyo kwanza huwa kunakuwa na matatizo ya Mahakama kupewa fedha ili kuhakikisha kwamba zile *High Court Sessions* zinakuwa nyingi iwezekanavyo ili Majaji waweze kufanya kazi zao. Kwa hiyo , fedha inakuwa ni kidogo. Vile vile Majaji wanakuwa ni wachache.

Ukitazama Wanasheria wanaoendelea kutoka Vyuo Vikuu unakuta wengi sana wanaapishwa kuwa Mawakili wa Kujitegemea kwa sababu inaonekana huko ndiko kuliko na *more incentives*.

Kwa hiyo, lazima tuweke *incentives* ambazo zitafanya watu waingie Uhakimu kwa wingi ili wapende kazi ya Uhakimu, baada ya hapo tuwe na Majaji wa Mahakama Kuu wengi iwezekanavyo wanaoweza waka-*handle* kesi nyingi sana za mauaji nchini na vile vile Mahakama ya Rufaa.

Baada ya kuwa watu waliokuwa na kesi za mauaji wameshahukumiwa hasa wale ambao wanahukumiwa wametiwa hatiani, kwa kuua kwa makusudi ambapo adhabu ni moja tu kisheria kwamba akitiwa hatiani hukumu yake ni kunyongwa mpaka afe. Ndiyo ilivyo. Sasa hapa panakuwa na tatizo kubwa sana la kiutekelezaji. Maana ukiingia katika Magereza unakuta wako watu wengi sana ambao wamehukumiwa lakini hukumu zao bado hazijatekelezwa na kwa hiyo watu kama ilivyozungumzwa huko nyuma kwamba wanakuwa wanakaa miaka mingi bila hukumu zao kutekelezwa. Hili jambo ni gumu kwa kweli. Maana sasa anayetakiwa atekeleze ni kiongozi mmoja tu, naye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwamba sasa asaini mtu anyongwe mpaka afe. Kwa kweli hili ni jambo gumu, tena ni gumu sana. Lakini Rais amepewa *alternative* ya ku-

commute sentence ili mtu acae maisha au miaka kadhaa, thelathini na kadhalika. Kwa hiyo, ningeshauri kana kwamba baada ya kuwa kesi zimeshafikia kiwango hicho, hata Mahakama ya Rufani iseme ahukumiwe, amehukumiwa kunyongwa, basi vile vile uamuzi wa utekelezaji wa hukumu hiyo ufanyike mapema. Kama inakuwa ni vigumu basi iwe *commuted* basi ili mtu yule ajue kana kwamba kesi kwangu mimi sasa imeisha. Kwa hiyo, nitakaa gerezani kwa maisha, basi aendelee kuishi bila kuogopa kwamba anaweza akahukumiwa muda wowote. (*Makofi*)

Lakini vile vile kama tunakuwa na ugumu wa kutekeleza hukumu ya kifo, basi ni vema sasa tuanze kulizungumzia suala hili. Je, haingekuwa jambo bora Sheria ibadilike ili tufute hukumu ya kifo? Ni suala ambalo ni lazima lianze kuzungumziwa, kwa sababu kunapokuwa na ugumu wa kulitekeleza maana yake ni kwamba dhamira za Watanzania zinaanza kubadilika. Kwa hiyo, hata yule kiongozi aliye pale juu anaona ngumu kulitekeleza. Kwa hiyo, ni jambo la kuanza kulizungumzia. (*Makofi*)

Ni jambo gumu, maana mimi nimeendesha kesi za mauaji nyingi sana na nimeshuhudia ushahidi wa ukatili wa kutisha sana. Kwa hiyo, nikiulizwa juu ya hukumu ya kifo naweza kusisitiza kabisa iendelee.

MBUNGE FULANI: Ndiyo!!

MHE. GEORGE F. MLAWA: Kutokana na *experience* yangu hiyo, lakini hili ni *subjective*. Ni jambo linalojadilika, linaweza likajadiliwa. Wenzetu wa *European Union* hatakuwa *member* wa *European Union* lazima uwe umefuta adhabu ya kifo ndiyo nchi iweze kuwa mwanachama wa *European Union*. Lakini unakuta Marekani bado wanashindwa kufuta *State* zote kufuta hukumu ya kifo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo ni gumu, lakini tuanze kulijadili kitaifa. Ningombwa Serikali, Mheshimiwa Waziri tulitazame suala hili kwa makini. (*Makofi*)

Sitoi maoni yangu kwa sababu ni Mhehe hapana. Vile vile ukitazama tumekuwa kutokana na mmomonyoko wa maadili watu wengi sana wanafanya makosa haya ya kutisha sana kama ya kubaka, kubaka vitoto vidogo na hata vichanga. Watu wengi sana wamejaa magerezani kwa sababu wana hukumu hizo za miaka mingi sana. Kwa hiyo, nafasi za kuwaachia wenzao ili wanaoingia wapya wapate nafasi hazipatikani kwa sababu wengi sana wana hukumu hizo.

Kwa hiyo, magereza yanazidi kujaa sana sasa hivi kutokana na watu wenye hukumu za vifungo vya muda mrefu sana. Hili ni tatizo ambalo nalo italazimu tulitazame juu ya kujaa kwa magereza yetu hapa nchini. Aidha, kwamba tufanye maamuzi makubwa ya kuendelea kujenga magereza kwa wingi iwezekanavyo.

Kuna jambo lililozungumzwa juu ya Tume ya Uchaguzi kwamba iwe ina wawakilishi wa Vyama vya Siasa. Kwa heshima nimewahi kuwa nilipokuwa Katibu wa Bunge pale mwanzoni nilikuwa vile vile ni Mkurugenzi wa Uchaguzi nchini. Kwa hiyo, nina kauzoefu kadogo juu ya jambo hili. Tume ya Uchaguzi inatakiwa kweli iwe huru ili ifanye maamuzi yafaayo kwa mujibu wa Sheria. Lakini ukiweka tena wawakilishi wa

Vyama vyaa Siasa, maana yake ni kwamba hao watakuwa kila mmoja anakwenda kupigania haki za chama chake. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mnaweza mkafika mkakuta wananchi wameshafanya uamuzi lakini Tume ya Uchaguzi inashindwa kutamka nani aliyeshinda kwa sababu wao wanagombana wanashindwa kufanya maamuzi. (*Makofî*)

Kwa hiyo, mnaweza mkachelewesha hata Uchaguzi wa Rais. Rais ameishapatikana lakini kuna mvutano ndani ya Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo mkawa mna shida kumpata Rais kutoptana na mivutano ya ndani ya Tume. Hili ni jambo ambalo lazima litazamwe, pamoja na kwamba Zanzibar imewekwa katika hali hiyo. Lakini isiwe kwamba lazima tui-copy moja kwa moja. Kuna mazingira yake kule Zanzibar ndiyo maana wamefanya maamuzi hayo. Lakini kwa Jamhuri nzima ya Muungano hili jambo litazamwe kwa makini sana. Rais anaweza akashauriana na upinzani, watu wenye *integrity* ni akina nani ambao wanakubalika pande zote, wenye *integrity*, lakini yule mtu akiingia ndani ya Tume asiwe mwakilishi wa chama. (*Makofî*)

Hapo ndipo inapowezekana Tume ya Uchaguzi ikawa Tume iliyo huru, inayoweza ikafanya maamuzi na yakaheshimika katika nchi. Kwa hiyo, hili jambo ningependa niliweke hivyo ili tuendelee kujadili maana inaonekana kama vile tayari tumeshakubaliana wote kwamba Tume ya Uchaguzi iwe na wawakilishi wa vyama vyaa siasa.

WABUNGE FULANI: Ndiyo!!

MHE. GEORGE F. MLAWA: Najua wenzangu kule ndivyo wanavyoamini. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo sijui kama nina muda wa kutosha kidogo. Nilikuwa nataka kuzungumzia juu ya *Legislative Programme*. Sasa hivi kuna mambo mengi sana ambayo yanatakiwa yatungiwe Sheria kutoptana na mabadiliko ya kiuchumi na kadhalika. Kwa hiyo inatakiwa kwa mfano kama Ofisi ya CPD, iwe na Wanasheria wengi zaidi wa ku-draft Miswada kulingana na maamuzi ya Baraza la Mawaziri na vile vile na *Law Reform Commission* inavyozidi kuleta mapendelekezo mbalimbali.

Kwa hiyo, ningependa niishauri kabisa kwamba kuwekwe mara baada ya uchaguzi mkuu, kwa mfano chama kinachoshinda kina Ilani ya Uchaguzi, kwa hiyo lazima *legislative programme* tujue kwa mwaka huu tunagemea walau Sheria kadhaa au ngapi na aina gani tuzipitishe.

Kwa hiyo, vile vipindi ambavyo huwa tunakaa kama Bunge, siyo hiki cha Bajeti, pengine ingefaa tuwe tunakaa badala ya wiki mbili iwe wiki tatu, ili tupitishe Miswada mingi iwezekanavyo kulingana na mahitaji. Naona *pressure* inakuwa ni kubwa sana na kwa siku hizi ambazo Kamati za Bunge zinakaa wiki mbili kwa hiyo zina uwezo wa

kuchambua Miswada mingi iwezekanavyo ili Miswada mingi iweze kupidishwa na Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naona muda wenyewe karibu unamalizika. Ningependa niishie hapo, lakini ni *emphasize* sana juu ya suala la Tume ya Uchaguzi kwa masuala ya kimsingi. Tufuate *principles*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HASSAN C. KIGWALILO: Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Wizara hii ambayo ni muhimu sana katika nchi yetu. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam wake kwa kuandaa Bajeti hii vizuri ambayo leo hii mimi naiunga mkono mia kwa mia. (*Makofi*)

Lakini kuna kitu kimoja ambacho kimenistaajabisha katika kabrasha hili la taarifa maalum kuhusu hali ya majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo nchini. Nimejaribu kuangalia sijaiona Liwale wala Wilaya ya Liwale. Sasa ikawa sielewi kama Wilaya yangu imefutwa Kikatiba au viperi.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kabisa baadaye katika majumuisho yake aweze kunieleza kunatendeka nini huko Liwale. Kwani Liwale tuko mbioni kuboresha Mahakama. Kibutuka wananchi wamejitlea kujenga Mahakama ya Mwanzo na imefikia katika ngazi nzuri na pia nimejaribu kuzungumza na Mheshimiwa Waziri kuona kiasi gani yeye ataweza kutusaidia ili tuweze kumalizia Mahakama hiyo.

Mheshimiwa Spika, Liwale ni eneo gumu kwa maana kwamba hatuna mawasiliano yaliyo rahisi aidha kwa njia ya barabara au kwa njia ya simu. Kwa hiyo, Hakimu aliyoko kule kusema kweli yuko katika hali ngumu sana na nadhani hata alipokuja Jaji Mkuu ambaye ninamshukuru sana alifanya ziara katika Wilaya yangu aliyona hayo.

Mheshimiwa Spika, ni Hakimu tu wa Wilaya ya Liwale ndiye hana gari ambalo lingeweza kumsaidia kuangalia matukio mbalimbali wakati shughuli za Mahakama zinafanyika, wakati Wizara zingine zote wamejaribu kutoa gari kwa ajili ya wafanyakazi wao. Ningekuomba Mheshimiwa Waziri kwa Wilaya ya Liwale ambayo imezungukwa na wanyama na pia ni *Selous almost fifty percent* ya eneo lake, *thirty nine thousand square kilometers*.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba kwamba ujaribu kutoa nafasi nzuri kwa Hakimu ambaye anaweza kukaa maeneo kama ya Liwale na yuko mmoja tu kwa hivi sasa akisaidiwa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Hali inayojitokeza ni kwamba kila wakati wanaomba msaada kutoka sehemu mbalimbali. Wakati mwengine Wizara zingine au Idara zingine zimekuwa *committed* na shughuli zao.

Kwa hiyo, wanakosa msaada. Kwa hiyo, shughuli zao huwa zinazorota. Nakuomba kwa heshima na taadhima Mheshimiwa Waziri jaribu kuwatengea gari hata kama ni ka-Suzuki au gari la aina yoyote ile liweze kukaa Liwale kwa ajili ya manufaa ya Mahakama ile. Kwa umuhimu wa Wizara hii, kwani hata Rais wa Jamhuri anaapishwa na Jaji Mkuu, naomba Serikali ijaribu kutilia maanani Bajeti ya Wizara hii kikamilifu. Na ijaribu kuwasaidia iwezavyo na tuzidi kuiboresha Bajeti ya Wizara hii mwaka hadi mwaka. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine kwa mfano jimbo langu la Liwale, hakuna huduma ya uandikishaji wa Vizazi na Vifo. Ningombaa kabisa Msajili ajaribu *ku-decentralize* hizi huduma ziende mpaka Wilayani. Kwa kuwa hali iliyojitokeza sasa hivi mtoto akizaliwa maeneo kama yale ya Liwale unakuta hana *Birth Certificate* na inakuwa kero sana kwa mzazi kufuutilia kupata *Birth Certificate* mpaka aje DSM.

Hatimaye inatokea wengine wanamaliza *Form Four* wanapotakiwa kuajiriwa bado wanakuwa hawana *Birth Certificate* ambapo *condition* mojawapo ya kuajiriwa ni kuwa na cheti cha kuzaliwa. Naomba kabisa zichukuliwe hatua za dhati za Serikali ili kujaribu *ku-decentralize* shughuli za Idara hiyo ili ziweze kufika vijijiini ili wananchi wetu waweze kunufaika kama ilivyo sehemu zingine. Vinginevyo haki za watoto zitakuwa hazitendewi haki kila mahala kama vile inavyopaswa.

Mheshimiwa Spika, ninaelewa mwaka jana palikuwa na fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya *uniforms* za Mahakimu. Pia ningependa kupata taarifa kama kweli Mahakimu waliboreshewa shughuli zao au maslahi yao pia kwa kupatiwa *uniforms* hizo au fedha ambazo walizotengewa kweli zinawafikia Mahakimu kwa ajili ya shughuli hizo.

Kwa kuwa hatua mojawapo ambayo ilizungumziwa katika kuzuia rushwa hasa katika Idara ya Mahakama iliyozungumziwa na Tume ya Warioba ni kuboresha hali za Mahakimu na Mahakama zilizopo nchini. Sasa kama hali hiyo bado haijaboreshwa au inalegalega kuboreshwa, mimi sijui sababu za msingi na ningetaka kupata maelezo ambayo hadi hivi leo yamefikiwa katika kuboresha maslahi ya wafanyakazi katika Mahakama na Idara zingine zote za Wizara hiyo.

Vinginevyo *Anti-Corruption* huwa wanalipwa vizuri sana. Sioni sababu kwa nini haya masuala ya *Anti-Corruption* baadaye yanapelekwa Mahakamani watu ambao hawalipwi vizuri. Sasa kwanza tunawatendea vipi Mahakimu au Majaji wetu katika suala hili. Ningeshukuru kama Wizara ingelivalia njuga suala la kuboresha haki na hali za wafanyakazi au watumishi wake katika Wizara ya Sheria na Katiba.

Ningependa kupata mikakati ambayo sasa hivi inafanywa ili kuona kila Wilaya inatarajiwa kuwa na Mahakimu wangapi wa Wilaya na Mahakimu wangapi wa Mahakama za Mwanzo. Kwa kuwa kinachofanyika sasa hivi ni ufuatiliaji tu. Ukiweza kufuutilia kupata Hakimu ndiyo huyo huyo. Hali hii nadhani sio nzuri. Nadhani tuwe na mikakati ya kujua tunatakiwa tuwe na Mahakimu wangapi kila Wilaya na wafanya kazi wangapi, ikama iwe imekamilika na pia wawe wenye mafunzo mazuri.

Pia suala la wazee wa Baraza. Hawa Wazee wa Baraza kazi zao ni nzuri. Lakini baadhi yao hawajui majukumu yao. Sijui kama wanapewa semina zozote hasa za kuhusu mambo ya rushwa maana yake unakuta wanatengwa kabisa. Wanakaa tu pale Mahakamani baadaye wanatoka. Ningefikiri kwamba ni wakati muafaka hata kama ni kiwilaya, wapewe mafunzo ya aina fulani hawa Wazee wa Baraza, hata posho yao iwe *reviewed* mwaka hadi mwaka. Hali ya maisha ni ngumu na wakati mwingine wanalazimika kukaa Mahakamani, badala ya kwenda mashambani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo narudia tena kwa kusema kwamba naunga mkono hotuba ya Wizara hii mia kwa mia. Ninachokiomba katika majumuisho yake nipate sababu ambazo zimefanya Liwale isionekane katika mpango huu uliotolewa katika kabrasha hili. Ahsante sana. (*Makofî*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja hii ambayo ni muhimu sana katika kutenda haki ya kila mtu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa ujumla kwa kazi ngumu wanayoifanya kwa kuweza kuimudu kwa kiwango cha kuridhisha. Nimpongeze Waziri, Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wote Wizarani, kazi yenu ni ngumu hivyo ni vyema tukawapongeza kwa kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe maelezo ni kwa nini Misungwi haijapewa Hakimu wa Wilaya na ni kwa nini Mahakama haijengwi katika Wilaya hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Misungwi na Wilaya ya Misungwi kwa ujumla tunasikitika kwa kutotendewa haki na Serikali yetu, Wilaya yetu ilianza mwaka 1997 sawa na Kongwa, Sikunge lakini baadhi ya Wilaya ujenzi umeanza. Jem Misungwi mmpanga kuanza lini? Je ni sahihi mtu kufuata haki zaidi ya kilometra 120 mfano ni Mahando - Kwimba, hii siyo kuruhusu rushwa?

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zote za Wilaya hii ya Misungwi hazijapata pesa yoyote ya ukarabati, hii ni kutendewa haki? Naomba Waziri wakati wa kuhitimisha hoja yake hii nipate majibu, amenipangia nini katika Wilaya hii?

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wilayani Misungwi hasa ukizingatia umbali na pia kuwasilisha taarifa mbalimbali Wilayani Kwimba badala ya Misungwi naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuzidiwa na matatizo ya mateso wanayopata wananchi kufuata haki kwa umbali huo inanifanya tujione tu wanyonge ndani ya nchi yetu ni vyema nikaelezwa ni nini nifanye ili figa la tatu lipatikane Misungwi yaani Bunge

lipo, Serikali ipo na imekubali kuleta *OCD*, Mahakama haipo, watu wa Misungwi wanaonewa, hawapati haki yao. Bila majibu mazuri nakuwa mzigo kuunga mkono.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, Idara ya Mahakama, kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mpwapwa na Viongozi Wakuu wa Idara ya Mahakama walifika Mpwapwa akiwemo Jaji Mkuu na kuona jengo hilo, je, mpango huo umefikia wapi? Naomba jibu.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri afike Wilayani Mpwapwa ili aone jengo hilo kwa Wilaya ilioanza mwaka 1905 lakini bado haina jengo la Mahakama ya Wilaya na kutumia jengo dogo la shule ya msingi ya Mtejela. Kiwanja cha kujenga jengo hilo kipo tayari.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kuna migongano kati ya Mabaraza ya Kata na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ipo haja kwa Serikali kuwapatia mafunzo angalau ya muda mfupi Makatibu wa Mabaraza ya Kata na hii itasaidia Makatibu hao kujua majukumu na mipaka yao ya madaraka.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihakikishe kwamba Mahakimu wa Wilaya na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanapatiwa usafiri ili kurahisisha utendaji wao wa kazi hata kama ni mkopo kama watumishi wengine wa Serikali wanavyopewa mikopo.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Mahakimu na Mawakili wa Serikali yaboreshwe, mishahara wanayolipwa ni kidogo na wanayo majukumu makubwa ya kutetea haki za watu. Mawakili wengi wa Serikali wanaacha kazi Serikalini kwa vile maslahi ni duni Serikali iboreshe maslahi yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Mahakama Lushoto kiimarishe kwa kutengewa fedha za kutosha za uendeshaji, pia Serikali iongoze idadi ya wanafunzi ili kupunguza tatizo la upungufu wa Mahakimu hapa nchini. Kwa kuwa nafasi za kukaa Chuoni ni chache, wanafunzi waruhusiwe kukaa nje ya Chuo na Serikali itafute majengo mengine nje ya Chuo ili kuongeza idadi ya wanafunzi Chuoni.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa kutuma wataalam wake kuja Jimboni Nanyumbu kufanya tathimini ya Majengo ya Mahakama za Mwanzo. Tathmini hiyo imeonyesha hali mbaya ya Majengo ya Mahakama za Mwanzo za Mangaka, Nanyumbu na Nakopi, hivyo kuhitaji kupanuliwa na ukarabati wa majengo yaliyopo. Hivyo naiomba Serikali kuhakikisha kuwa majengo hayo yanafanyiwa ukarabati mkubwa na kupanuliwa ili kuepusha madhara yoyote yanayoweza kutokea kutokana na ubovu wa majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa hiyo ya wataalamu sikuona maelezo yoyote juu ya Mahakama ya Mwanzo ya Michiga. Mahakama hiyo bado inafanya kazi, ndiyo

tegemeo pekee kwa wananchi wa Mji mdogo wa Michiga na wananchi wa Kata za Likokona na Lumesule kumekuwepo na habari kuwa Mahakama ya Mwanzo ya Michiga inaondolewa na kurudishwa Nakopi, jambo ambalo siyo la haki kwa vile eneo ambalo Mahakama hii ipo ni eneo lenye watu wengi kuliko Nakopi ambako watu ni wachache sana. Sababu ya uchache wa watu ndiyo iliyopelekea huko nyuma kuhamisha Mahakama ya Mwanzo Nakopi kwenda Michiga.

Mheshimiwa Spika, hivyo siyo haki kuhamisha tena Mahakama ya Mwanzo ya Michiga kwenda Nakopi kwani italeta usumbufu mkubwa kwa wananchi wengi wa eneo hilo.

Naomba Serikali kuhakikisha Mahakama ya Mwanzo ya Michiga inabaki Michiga na Mahakama ya Mwanzo Nakopi nayo inafufuliwa kukidhi mahitaji ya wananchi wa Nakopi na Kata ya Napacho. Kutokana na ukubwa wa Kata ya Napacho nina hakika itakidhi mahitaji ya Mahakama ya Mwanzo ya Michiga ili iweze kuhudumia wananchi wanaozunguka Mji mdogo wa Michiga.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ambayo imesahaulika ni eneo la Kata za Maratani, Nandete na Mikangaula. Eneo hilo halina Mahakama ya Mwanzo hivyo hulazimika kusafiri safari ndefu hadi Masasi Mjini kupata huduma ya Mahakama. Naomba Serikali ijenge Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Maratani ili kuhudumia Kata hizo tatu za Maratani, Nandete na Mikangaula. Hali hiyo itawaondolea wananchi wa Kata hizo adha ya kusafiri masafa mrefu kutafuta huduma ya Mahakama. Ni imani yangu kuwa Serikali italionia hili na kuzingatia.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo nimalizie kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. AZIZA SLEYUM ALI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabaraza ya wazee, mabaraza ya wazee yana madai chungu nzima katika kipindi kirefu sana na hasa ukizingatia wazee hao hawana ajira nyingine ya kuweza kuwasaidia wao kujikwamua kimaisha, pia hata hiyo posho yenyewe ni ndogo zaidi, naomba Mheshimiwa Waziri na Serikali iangalie hayo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi hawaelewi sheria zao wenyewe ambazo zingewasaidia kujua haki zao wenyewe ambavyo mtu hushindwa kudai haki yake au kuogopa Kiswahili au lugha zao kikabila lakini zaidi huongea kiswahili. Je, utamdaije mtu kuwa amevunja sheria na wakati mtu huyo sheria yenyewe hana, haijui na lugha haielewi hiyo ni mojawapo ya kumnyima haki yake ya kujua sheria ambayo inamwongoza?

Mheshimiwa Spika, kuhusu uelimishaji wa sheria,haki za binadamu, suala hili ni muhimu sana kwa wananchi kwa sababu kuwa na kipindi cha kumwendeleza na kumwelimisha Mtanzania haki zake. Sheria anayotakiwa kufuata ni suala muhimu sana na itamtoa Mtanzania gizani kwa kuelewa sheria ya nchi yake na mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mirathi, suala la mirathi ni tatizo sana kwa wananchi hapa Tanzania hasa kulingana na janga la UKIMWI, wazazi huondoka kwa kufariki na kuacha mke au mume na watoto lakini Mahakama huchelewa sana kuzungumzia haraka masuala hayo ya mirathi na watoto na mke huendelea kusumbuka na hata wengine nao hupoteza maisha yao na bado mirathi hiyo bado haijasikilizwa, Je, hiyo ndiyo haki ya binadamu kweli?

Mheshimiwa Spika, mwisho, natoa maoni kuwa masuala haya yaangaliwe kwa ukaribu zaidi, wananchi wengi hupata matatizo na kuwakilisha kwa wawakilishi wao ambao ndiyo sisi Wabunge. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ayaangalie haya kwa undani zaidi.

MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS: Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali katika kulitatu tatizo la Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo ni vyema Serikali ikaongeza juhudi za haraka kutanua Chuo cha Mahakama Lushoto ili chuo kiweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi na hatimae kuziba mapengo ya nafasi za Mahakimu katika Mahakama mbali mbali nchini.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kuanzisha *White Paper* kwa ajili ya kupata maoni ya wananchi juu ya uanzishwaji wa Mahakama za Kadhi, nadhani huku ni kurudi nyuma, kazi hii katika hatua ya tafiti, mahojiano na wadau mbali mbali, uzoefu wa nchi mbali mbali, tafiti hizo zote zimeshafanyika na kwa kutumia fedha nyingi za Serikali aidha, kwa sasa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala inaendelea na kazi hiyo ambayo ipo katika hatua za mwisho kukamilisha kazi hiyo. Hivyo siyo vyema kurudi nyuma kwa kuanza tena kutafuta maoni kazi ambayo imeshafanyika karibu miaka kumi sasa. Nashauri Serikali isubiri maoni ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala na Serikali ifanyie kazi maoni hayo na siyo kuanzisha *White Paper*.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa azma yake njema ya kutaka kuleta mabadiliko ya Katiba, nashauri mapendekezo ya mabadiliko ya Katiba yatolewe mapema na yachapishwe mengi ili wananchi wengi zaidi waweze kuyapata mapema, kuyasoma na kutoa mapendekezo yao. Vile vile wakati wa *public hearing*, zitengwe siku za kutosha zisizopuingua sita ili kukusanya maoni mengi zaidi. Aidha, kati ya siku hizo angalau siku mbili kazi hiyo ifanyike Zanzibar ili kupata maoni ya upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi wakati Bunge linapokuwa katika mjadala wa Miswada ya sheria zinazotumika Tanzania nzima, kumekuwa na tatizo la kutoshirikishwa kwa upande wa pili wa Muungano (Zanzibar) katika Miswada hiyo, hivyo nashauri wakati kwa kutayarisha hizo *Bills*, Wanasheria wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar wawepo ili kuona kwamba endapo *Bill* hiyo itapitishwa na Bunge isiwe na matatizo ya kiutekelezaji kwa Tanzania nzima. Hali tuliyonayo hivi sasa zipo sheria zilizopitishwa na Bunge kwa lengo la kutumika Tanzania nzima ikiwemo na Zanzibar lakini utekelezaji wake haupo hivyo. Msingi mkuu wa tatizo hilo ni kukosekana kwa ushirikiano wakati wa utayarishaji wa Sheria hiyo. Nashauri tuachane na tabia hiyo katika utendaji wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ABDULA S. LUTAVI: Mheshimiwa Spika, naipongeza hotuba nzuri ya Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na nafasi hii niitumie kumpongeza yeye mwenyewe na wasaidizi wake kwa maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninayo machache ambayo ningeomba Wizara iyaangalie kwa karibu. Kwanza, hatuna Mahakama ya Wilaya Tandahimba na sioni ndani ya hotuba hii mipango ya Wizara kulikabili tatizo hili ili kuinusuru Wilaya yetu na tatizo hili la kulazimika kuelekeza Rufaa zote kwenye Wilaya ya jirani ya Newala. Tandahimba ni Wilaya iliyoanza 1997 lakini idara zingine za Uendeshaji wa Serikali zote zimeweka ofisi zake pale isipokuwa Idara ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo kubwa la kufuatilia haki za wananchi kwa kuharibika taratibu katika Idara ya Mahakama. Imekuwa kero iliyokomaa sasa kwamba mwananchi akilalamika, Mahakama ya Mwanzo kwa dhuluma inayofanywa na mwananchi mwingine analazimika mlalamikaji kugharamia usafiri wa askari wa kumpeleka mtuhumiwa Mahakamani pamoja na gharama zao za kujikimu. Mtuhumiwa akitakiwa kuwekwa *remand prison* siku hizi inakuwa ni kwa gharama za mlalamikaji kwa mahabusu hao kupata chakula kwa muda wote wanapobaki mahabusu.

Mheshimiwa Spika, inaaminika hali hii imetawala sasa kutokana na wazabuni wengi wenyewe jukumu la kulisha mahabusu kususia kazi hiyo kwa kutolipwa ankara zao kwa muda mrefu sasa. Jambo hili lazima litazamwe na lipatiwe ufumbuzi ili kuirejesha nidhamu inayotarajiwu kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanalamikia hali mbaya ya rushwa katika Mahakama hasa Mahakama za Mwanzo ndani ya nchi yetu. Tatizo hili limefikia hatua ya wananchi kukata tamaa na kuamua kutopeleka kabisa mashauri yao Mahakamani hasa wakiamini kwamba anayelalamikiwa ni mtu mwenye uwezo kiuchumi kuliko mlalamikaji. Hali hii ya kukata tamaa na kupuuzia ufuatiliaji wa haki zao za msingi imetawala katika maeneo ya vijiji. Lakini mbaya zaidi ni pale ambapo sasa tumezoea na tunashuhudia wananchi, hasa mijini, wakichukua sheria mkononi, wanaua watuhumiwa kwa visu, mapanga na hata kuwachoma moto watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, huu ni mwenendo mbaya na kamwe hali haitabadilika kama rushwa katika Idara ya Mahakama haitadhibitiwa na wananchi wakarejeshewa imani juu ya chombo hiki muhimu katika utoaji wa haki ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. THADEUS M. LUOGA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ni Wizara muhimu sana inayosimamia haki za wananchi. Wizara inashindwa kukamilisha majukumu yake kikamilifu kutokana na matatizo mbali mbali yakiwemo upungufu wa watumishi, uhaba wa vifaa, majengo na vitendea kazi kwa jumla. Ili Wizara hii iweze kufanya majukumu yake vizuri, naishauri Serikali itoe fedha

za kutosha kwa Wizara hii ya Sheria na Mambo ya Katiba ili iweze kufanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna upungufu wa Majaji na Mahakimu katika Idara ya Mahakama ikiwa upungufu huu wa watumishi Serikali haifanyi jithada ya kuondoa na haki haiwezi kufanyika bila watumishi kwa hali hii tunawanyima haki wananchi. Kwa mfano, katika Mahakama za mwanzo kuna upungufu wa Mahakimu 1,560. Mwaka 2004/2005 Wizara itaa jiri Mahakimu wa Mwanzo 55 na kama itaendelea kwa kiwango hicho hicho kwa kuajiri kila mwaka itachukua miaka 28 kumaliza upungufu huu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze ajira nyingi zaidi za Mahakimu wa Mwanzo ili upungufu huu umalizike baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni maombi yangu mawili kwa Mheshimiwa Waziri:-

Kwanza, nina Tarafa mbili katika Jimbo langu haina Mahakimu wa mwanzo hivyo naomba tupewe.

Pili, kwa kuwa Idara ya usajili wa vizazi, ndoa na vifo haipo kila Mkao, naiomba Wizara ifungue Idara hii kila Mkao kwa lengo la kupunguza usumbufu wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya machache naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri mia kwa mia. Asante sana.

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyiningine, Mahakama za Mwanzo Jimboni Nkenge zipatiwe Mahakimu. Mahakama za Mwanzo ninazoombea Mahakimu ni Mahakama za Mwanzo za Kanyigo, Gera, Minziro, Kayanga, Ndwaniro - Buiyango na Kasambya na *Kagera Sugar*.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kunasababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi. Kwa mfano, wananchi (walalamikaji) wanalazimika kusafiri umbali mrefu zaidi ya kilometra hamsini na wakati mwingine wanalazimishwa kutoa fedha za kusafirisha watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba njue ni nani anawajibika kuwahudumia mahabusu? Naomba maelezo ya kina. Naulizia huduma za chakula kwa mahabusu nani anawajibika kuwapa chakula mahabusu kwenye Mahakama za Mwanzo?

Mheshimiwa Spika, sheria iliyoanzisha Chuo Kikuu Mzumbe ilitoa nafasi ya mwakilishi wa Wabunge mmoja kwenye *Council* ya Mzumbe. Wakati huo huo, Wabunge tunawakilishwa na Wabunge watatu, watatu, kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Naomba maelezo yaliyopelekea Chuo

Kikuu Mzumbe, Bunge liwakilishwe na Mbunge mmoja wakati *UDSM* na *SUA*, Bunge linawakilishwa na Wabunge watatu, watatu. Naomba maelezo ya kina.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria ya kuanzisha Mzumbe inatoa nafasi kwa Makamu Mkoo wa Chuo kukaa vipindi viwili tu vya miaka mitano mitano kwa Vyuo vya *UDSM* na *SUA*. Makamu Wakuu wa Chuo wanakaa muda usiokuwa na mwisho, je, busara iliyotumika kuweka kikomo cha Makamu Mkoo wa Chuo kwa Chuo Kikuu cha Mzumbe, kwa nini haikutumika kurekebisha Sheria za Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na *SUA* ili Makamu Wakuu wa Vyuo hivyo nao wakae si zaidi ya miaka kumi ili kuondokana na tatizo la mtu mmoja kukaa kwenye nafasi nyeti ya Umakamu Mkoo wa Chuo kwa zaidi ya miaka kumi jambo linaloweza kusababisha muhusika kulewa madaraka na kuharibu kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo, naunga mkono hoja lakini naomba maelezo ya kina kuhusu hoja nilizotoa hapo juu.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara hasa Mheshimiwa Waziri, watalaam wake kwa kazi nzuri ya kusimamia sana sheria kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee naomba nizitoe kwa Mwanasheria Mkoo wa Serikali, kwa kuisaidia Serikali kwa mambo ya kisheria ndani ya Bunge na nje ya Bunge na nimpongeze kwa kushika wadhifa huo wa *Attorney General* kwa muda wa zaidi ya miaka 13. Yote hayo ni kwa sababu ya umakini. Namtakia kila la kheri.

Mheshimiwa Spika, naomba nilete ombi langu kwa mara ya tatu kuhusu karani wa Mahakama ya mwanzo iliyoko Jimboni kwangu, Mahakama ya Nyamikoma, karani huyo Mheshimiwa Waziri nilishamwandikia kuhusu utendaji wake wa kazi, si mwaminifu, ni mla rushwa, anajifanya Mungu Mtu, hata Mahakimu wa Mahakama za mwanzo wanafanya kazi naye wanamfahamu na inawezekana taarifa hupelekwa zinazohusu utendaji wake wa kazi lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, si tabia nzuri sana kukaa tunalalamikia suala hilo kila mara, ingekuwa vizuri zaidi kama mtumishi huyo hata kama anapendwa sana na uongozi wa Wilaya, apelekwe sehemu nyingine ili wananchi wa maeneo hayo wapumue.

Mheshimiwa Spika, katika taarifa ya watalaam kuhusu hali ya majengo ya Mahakama imeeleza kuwa katika Mahakama za Mwanzo za Nyamikoma imeandikwa *Demolition and New Construction*, Nyambiti imeandikwa *Extension and Rehabilitation*, Malya pia imeandikwa *Demolition and new construction*.

Swali langu ni kwamba majengo hayo yatakarabatiwa, yatavunjwa na kujengwa upya au tayari shughuli hizo zimeishafanyika? Kama ni ndiyo nasema kuwa shughuli za ujenzi hazijafanyika. Lakini kama bado basi tunaipongeza Serikali kwa kufikiria

kuyafanya ukarabati na kujengwa upya hasa zile Mahakama za mwanzo za Nyambiti, Malya, Bungulwa, Ngulla na Nyamikoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kuwa naunga mkono hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Jaji Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wenyeviti wa Tume na Bodi zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri walizozifanya katika kipindi cha mwaka uliopita. Naunga mkono hotuba ya Waziri wa Sheria na Mamabo ya Katiba kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zilizofanywa katika kipindi chote hicho, bado yapo maeneo ambayo kwa jimbo langu la Sumbawanga Mjini ni kero. Nitaanza na majengo:-

Jengo la Mahakama Kuu lilonunuliwa limebaki gofu tu. Hivi ni kwa nini hakuna hata jitihada za kuanza marekebisho ya majengo hayo yaliyonunuliwa toka Benki ya Taifa miaka miwili iliyopita? Tupewe maelezo.

Mheshimiwa Spika, jengo la Mahakama ya Mwanzo Mjini Sumbawanga ni mali ya shule ya sekondari ya Sumbawanga Mjini kwa hivi sasa ambalo linatakiwa likarabatiwe ili liwe darasa. Nazidi kuiomba Wizara ikamilishe jengo lake la Hakimu Mkazi ambalo litatumika pia kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo. Kazi hii imeanza, naomba kasi isipunguzwe ya ujenzi wa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri aone uwezekano wa kuwasaidia usafiri Mahakimu wetu. Umuhimu wa usafiri unaojulikana hasa katika maeneo ambayo hayana usafiri mbadala na umuhimu wa kutoa mafunzo kwa watumishi walio katika Mikoa inayodhaniwa haipendwi na watumishi kwa kigezo cha kuwa mbali na Makao Makuu ya nchi. Ni vizuri wakapewa vivutio ili viwasaidie kupenda kuishi katika maeneo kama hayo ya Rukwa, Kigoma, Lindi, Mtwara na hata Kagera.

Mheshimiwa Spika, ombi la kuimarisha utoaji wa haki kwa haraka zaidi upewe kipaumbele kwa kuwa watuhumiwa wengi na hasa walioonewa, hukaa gerezani au mahabusu kwa muda mrefu sana bila maamuzi kufanyika. Ni wajibu wa Waziri na NGOs zinazotetea haki za binadamu kuweka mtandao wa ushirikiano wa karibu ili kuona njia rahisi ya kupunguza baadhi ya maonevu yanavyotendeka nchini bila ya Serikali kujua. Naunga mkono hoja hii.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri kwa jitihada zake za kusimamia Wizara hii ngumu na yenye kugusa watu wengi. Amefanya kazi nzuri, nami nampongeza yeche pamoja na watumishi wote wa Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Ardhi, wananchi wengi bado hawaelewi sheria ya ardhi. Naomba Elimu ya kuwaeleza wananchi juu ya sheria hii kwa

lugha rahisi ifanywe. Mahakama ni mpya kwa watu, wananchi waelimishwe kuhusu kazi za Mahakama ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usajili wa vifo na vizazi, iwapo ni kweli tutaanzisha Daftari la Wapigakura, basi wananchi wahimizwe au waelimishwe na Wizara yako umuhimu wa kusajili watoto wanapozaliwa na wanao kufa wasajiliwe pia. Waelimishwe kuhusu usajili wote wajue faida zake, Elimu ni muhimu. Wizara yako isihukumu tu bali ielimishe watu pia.

Mheshimiwa Spika, utafiti kuhusu sheria za ndoa, watoto na mirathi.

Mheshimiwa Spika, mwanaume anapokufa mali yake hugaiwa kwa watoto, wazazi pengine na mjane. Je, mke kama alikuwa mfanyakazi sheria inasemaje juu ya wazazi wake? Hupata fungu gani? Mnapoangalia upya sheria hiyo ya mirathi na hilo linaangaliwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kurithi mali ya wanandoa watoto waliozaliwa nje ya ndoa ni kuwaonea watoto na mke wa ndoa. Wanawake wanaozaliwa nje ya ndoa wanapendelewa huyo bwana akiwa hai vipi asilazimishwe kuwaandalia maisha yao. Mke mfanyakazi anashiriki kujenga maisha katika ndoa. Huyo wa nje anatoa yaliyo ndani kutoa nje. Je, ni vipi mali iliyochumwa ndani ya ndoa ilithiwe na watu nje ya ndoa vipi? Sheria inamlindaje huyu mke wa kwenye ndoa? Baba awaandalie wanawe wa nje ya ndoa kabla hajafa.

Mheshimiwa Spika, mwisho napongeza kuweka mikakati ya kufundisha Mahakimu kule Lushoto.

Mheshimiwa Spika, naomba namba ya wanafunzi iongezwe ili Mahakama zipate watenda kazi. Naunga mkono hoja.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wahusika wote wa Wizara hii ya Sheria na pia Wahusika na Watendaji wa Mahakama zetu nchini.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwa nchi yetu katika kuwapatia wananchi wa nchi hii haki zao na pia kuonesha sura halisi ya utawala bora katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kufuatia umuhimu wa Wizara hii katika kusimamia na kuwapatia haki Watanzania, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kuisimamia ipasavyo Wizara hii ili kuwapatia haki zao wananchi wanapozidai katika vyombo vyetu nje ya sheria hapa nchini ili kuwapatia haki zao za msingi kwa ajili ya usalama wao na maendeleo yao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara hii kwa kuwa na dira sahihi ambayo imeelezwa katika ukurasa wa tano katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, dira hii inasema kuwa Wizara imejizatiti kutekeleza majukumu yaliyoainishwa kwa kuongozwa na dira ya haki kwa wote na kwa wakati. Kwa kweli naipongeza sana Wizara hii kwa kuwa na dira hii ambayo itatekeleza majukumu yake katika kutoa haki kwa wote na wakati.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kutekeleza majukumu yake haya naiomba Wizara hii ihakikishe kuwa suala la mahabusu wanaosubiri mashtaka yao yashughulikiwe haraka iwezekanavyo ili kuwapatia haki zao raia hawa amba wanakabiliwa na shutuma mbalimbali hasa tukizingatia kuwa wapo wengi amba makosa yao ni madogo madogo na ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, pia lile suala la kuwepo Hakimu mmoja kuhudumia zaidi ya Wilaya moja au nne (2 mpaka 4) liangaliwe sana kwani inaonyesha kuwepo wananchi wengi wanaokaa katika mahabusu mbali mbali hapa nchini wakisubiri hukumu zao na huku wakiwa wamekaa kwa miaka mingi katika Magereza yetu wakiwa ni mahabusu tu na wala sio kama ni wafungwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 18 ambaoumeelezea haki za binadamu, utawala bora na mambo ya Katiba ambapo inasema kuwa kama mlivyosema katika utangulizi, eneo lingine muhimu ambalo linashughulikiwa na Wizara ni lile linalohusu masuala ya Katiba na haki za binadamu. Kwa kweli ni imani yangu kuwa suala hili litakapokamilika halitabakia katika nyaraka za Serikali tu na kubakia ofisini, bali litafanyiwa kazi ipasavyo kwa faida ya kuwaelewesha wananchi juu ya haki zao na Sheria za nchi yao inavyofanywa kazi kwa misingi ya haki na utawala bora.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 34, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, ameelezea juu ya kuimarisha uendeshaji wa kesi na kupunguza mlundikano wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake hii kulitekeleza hili la kuimarisha uendeshaji wa kesi na kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu hapa nchini. Kwa kweli suala hili limekuwa kero kubwa sana kwa wananchi wetu pamoja na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri katika kulisimamia na kulifanikisha hili.

Mheshimiwa Spika, pia nachukua fursa hii kumwomba sana Mheshimiwa Waziri wakatia atakapokuwa analishughulikia jambo hili walifanye kwa haraka itakavyowezekana pamoja na kuwfanyia haki wale wote amba wataonekana kuwa wamewekwa magerezani kwa kubambikiziwa kazi na kuwa na makosa madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi na ya muda mrefu mionganini mwa wananchi kuwa wametiwa hatiani kwa kubambikiziwa kesi. Serikali haina budi kulishughulikia suala hili na kuwapatia haki zao za msingi wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, pia tumeelezwa kuwa wapo baadhi ya wananchi ambao wamejikuta wakiingizwa katika mashtaka na kuwekwa ndani wakiwa mahabusu au wafungwa kwa kugeuziwa kesi baada ya kutoa taarifa au kupinga jambo fulani lisifanyike kwa sababu ni kosa.

Mheshimiwa Spika, kati ya watu hao ambao wanalamikiwa wapo wale waliopinga masuala ya ukeketaji ndani ya familia zao au maeneo yao wanayoishi.

Mheshimiwa Spika, watu hawa wanapokwenda kulalamikia suala hili kwenye vyombo vyao vya Serikali au vya Sheria baadaye wanajikuta ni wao wanaoingizwa hatiani kwa kubadilishiwa kesi kwa kuwepo hongo fulani kutoka ule upande wa pili kama kumkomoa kwa hatua zake hizo za msingi alizozichukua.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara hii pamoja na Serikali Kuu kuliangalia suala hili kwa kina na kuwanusuru na kuwapatia haki zao wananchi hawa ambao hawana hatia.

Mheshimiwa Spika, asante, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na naomba Wizara hii kuishauri kama ifuatavyo:-

Kwanza, kwa bahati mbaya Mwenyezi Mungu alimchukua Hakimu wa Wilaya, sasa ni Marehemu Tua, mwaka huu na hivyo kwa sasa yupo Hakimu mmoja tu wa Wilaya ambaye hawezi kusikiliza mashauri mengi kwa kuzingatia kuwa Babati mbali ya kuwa Wilaya ni Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu ya Halmashauri ya Mji wa Babati.

Pili, Wilaya ya Babati ina Mahakimu wachache sana wa Mahakama za Mwanzo na wananchi wanalamikia kusafiri na kutumia gharama kubwa kwenda kwenye Mahakama zenye Mahakimu. Nafahamu kwamba tatizo hili litakwisha baada ya mradi wa *Quick Start* kumalizika. Lakini naona itachukua muda mrefu kwa mradi kukamilika. Hivyo ni vema Wizara ikafanya juhudzi za muda za kutatua tatizo hili.

Tatu, kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wazee wa Mahakama za mwanzo kuwa wamekuwa wakibadilishwa bila kufuata utaratibu. Hivyo ni vema Mheshimiwa Waziri akatumia nafasi ya kueleza utaratibu wa kuteua wazee wa Mahakama za Mwanzo na hivyo hivyo taratibu za kuwaondoa. Hii itasaidia kuondoa manung'uniko yaliyopo.

Nne, Idara ya Mahakama kwa ujumla haina usafiri unaoaminika na magari madogo ya Waheshimiwa Mahakimu wa Wilaya wengi sasa ni mabovu sana. Hivyo ni

muhimu kukawa na utaratibu wa kununua magari walau moja kwa kila Wilaya na yawe magari mazuri na visuzuki vidogo kama ilivyo sasa.

Tano, nashauri kuwa utoaji wa mafao ya mirathi kupitia Mahakama za Mwanzo unatoa mwanya wa urasimu mrefu na ucheleweshaji kutokana na Mahakama kutokuwa na vifaa vya mawasiliano ya kuaminika kati yao na warithi. Ni vizuri eneo hili likatizamwa upya ili kuondoa urasimu uliopo.

Mheshimiwa Spika, namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri katika kukabiliana na changamoto iliyopo.

Mheshimiwa Spika, naunga tena mkono hoja hii.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Makatibu Wasaidizi wote walioshiriki katika kuandaa Bajeti hii nzuri. Napongeza sana na wote kwa ujumla nasema hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwanza ni kuhusu vyeti vya kuzaliwa, vina urasimu mno. Naomba na naishauri Serikali kukasimu madaraka ya Kabidhi Wasii karibu na wananchi kama vile, Kanda au Mikoani ili kurahisisha upatikanaji wa vyeti hivyo.

Pili, uwepo mpango madhubuti wa kupunguza kesi zilizopo hivi sasa kwani, zipo kesi za miaka kumi, minane na kuendelea. Aidha, waliopo mahabusu wakisubiri upelelezi ni wengi mno kiasi kwamba hao ni kama wanatumikia kifungo tayari. Hii ni kero kubwa.

Tatu, mishahara ya watumishi wa Mahakama ni midogo sana. Naishauri Serikali kuboresha maslahi ya Majaji, Mahakimu Wakazi na Mahakimu wa ngazi zote ili kupunguza makali ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, wapeni vifaa vya kufanya kazi kama vile magari na pikipiki pia vitendea kazi. Inasikitisha kuona Mwanasheria wa Kanda hana vitendea kazi, hata mshahara wake uko chini ya shilingi 200,000/=. Hii ni kuwafanya washawishike kuomba rushwa katika kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nne ni kuhusu Wazee wa Mahakama wapewe posho yao kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, napenda mipongeze Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa

uwasilishaji mzuri wa hoja. Aidha, naipongeza Wizara na watendaji kazi wote katika Wizara hiyo kwa jitihada za kutekeleza majukumu yao kwa mwaka uliopita wa fedha. Nawaasa kuongeza jitihada kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni yangu kwa machache yafuatayo:-

Kwanza, nafasi za mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo zipanuliwe. Chuo cha Lushoto ni kidogo mno ukilinganisha na idadi kubwa inayotakiwa kukidhi mahitaji ya Mahakimu wa Mahakama za mwanzo nchini. Nafasi 60 ni chache mno kwa nafasi zaidi ya 700 tunayotakiwa kujaza.

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana vyuo vingine vipewe nafasi ya kufundisha na kutoa vyeti nya wahitimu wa vyeti nya Uhakimu kwa Mahakama za Mwanzo.

Pili, nashauri wahitimu wa Chuo cha Mahakama Lushoto waajiriwe moja kwa moja toka Chuoni badala ya kusubiri nafasi kutangazwa na kufanyiwa usaili wa kujaza nafasi hizo.

Tatu, nashauri vitendea kazi hasa usafiri kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, hasa pikipiki ili warahisishiwe kazi kutoka kituo hadi kituo hali itakayopunguza wingi wa kesi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nne, haki isimamiwe kwa mahabusu wasihukumiwe bila kusikilizwa ama kuwekwa mahabusu muda mrefu (miezi 6 na zaidi) bila kusikilizwa kwa madai ya kukosa usafiri. Kwa msingi huo, Serikali ihakikishe Magereza haikosi magari ya wafungwa, mafuta ya magari na ukarabati wa mara kwa mara ili wapelekwe kusikilizwa kesi zao.

Tano, naomba watoto wanaofungwa na mama zao waangaliwe haki zao. Haki ya mtoto ya kuwa huru iangaliwe ili asitumikie kifungo na mama yake. Akinamama wenye watoto wafikiriwe kubadilishiwa adhabu ili watoto wawe huru.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua maendeleo ya ujenzi wa Mahakama Kuu ya Kanda ya Bukoba umefikia wapi? Naishukuru Serikali imetuletea Jaji wa Kanda ya Bukoba, lakini hajapatiwa jengo linalolingana na hadhi ya Mahakama Kuu ya Kanda ya Bukoba.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe jibu wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa hotuba nzuri, nina maoni machache yafuatayo:-

Kwanza, naishukuru Serikali kwa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya unaoendelea vizuri kule Kongwa.

Pili, Sheria inayowaruhusu *WEO*, Katibu Tarafa, *DC* na kadhalika kuwaweka watu ndani kwa muda mfupi kama walinzi wa amani iangaliwe upya. Sheria hii kama bado iko inatumika ovyo ovyo. Wilayani Kongwa Wenyeviti wa Vijiji, walimu, wananchi wa kawaida wamekuwa wakitiwa ndani ovyo ovyo.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Kongwa, Wenyeviti wa Vijiji, Walimu, wananchi wa kawaida wamekuwa wakitiwa ndani ovyo ovyo kwa kisingizio cha kuwepo hiyo Sheria.

Mheshimiwa Spika, kama ipo sheria hiyo nashauri itazamwe upya haraka. Inatumika vibaya sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara kusaidia kukarabati au kujenga majengo mapya ya Mahakama za Mwanzo katika maeneo ya Kongwa Mjini, Kibaigwa, Sagara, Mlali, Mkoka, Mbande na Mтанана.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Hakimu wa Wilaya Kongwa mwaka huu pia tunaomba gari moja kwa ajili ya ukaguzi wa Mahakama na kila hakimu apewe au akopeshwe pikipiki ya kumsaidia kuhudumia Mahakama za mbali. Hii itapunguza mlolongo wa kesi na uahirishaji usioisha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Pamoja na ufinyu wa bajeti, lakini tunaomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tulikwisha omnia tupatiwe Mahakama Kuu Mkoa wa Shinyanga, kwani watu wanahangaika sana kufuatilia haki zao Mahakama Kuu, Tabora. Majengo yapo ya kutosheleza kwa makazi ya Jaji, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wahusika wote.

Mheshimiwa Spika, kesi ni nyingi zinarundikana, ambazo zinahusu Mahakama Kuu hasa za mauaji ambazo nyingi ni kutoka Wilaya ya Bariadi. Hilo haliwezekani kwa hivi sasa, basi Wilaya ya Bariadi iruhusiwe kushughulikiwa na Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza kwa sababu ndiyo karibu, ili kupunguza usumbufu.

Mheshimiwa Spika, mlundikano wa mahabusu katika Gereza la Bariadi unasababishwa na watu ambao wamekamatwa na nyara za Serikali au kwa kukomoana au kweli, lakini kesi zao zinahitaji Mahakama Kuu (Jaji) ambao wako Tabora na ni wachache sana. Kwa nini Mahakimu Wakazi wa Wilaya wasipewe Mamlaka ya kusikiliza kesi hizo na kuamua? Wapo mahabusu wengi sana na wana miaka mingi hadi miaka nane. Ni muhimu sana tukawatendea haki watu hawa.

Mheshimiwa Spika, kesi zinazosikilizwa na Mahakama za Mwanzo ziruhusiwe kuwekewa Mawakili kwani wananchi walio wengi hawawezi kujitetea na wanaonewa sana. Wengi hawapewi haki mpaka watoe rushwa. Hiyo rushwa ingeweza kutumika kulipia Wakili wa kutetea kesi zao na haki ikapatikana. Tena kuweka Wakili, ingekuwa rahisi kuliko kutoa rushwa ambayo ni kubwa na inaleta umaskini.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa hotuba nzuri sana ya bajeti na mipango mizuri sana ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu, wanafanya kazi nzuri sana. Wafanyakazi wa Wizara hii ni wachache kwa sababu ya maslahi duni, lakini wanafanya kazi kubwa sana kwa ufanisi sana. Napenda kwa dhati kabisa niwapongeze na kuiomba Serikali iangalie upya mishahara na marupurupu ya Wanasheria wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, Mahakama zetu zinafanya kazi katika hali ngumu sana. Wote tunalifahamu tatizo hili na sina nia ya kurudia kulielezea. Hata hivyo, kwa mzigo ambao Mahakama zetu zinaubeba, napenda nimpongeze Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa heshima kubwa aliyo nayo nchini na nchi za nje. Yeye na Majaji wetu wa Mahakama ya Rufaa na Majaji wa daraja zote za Mahakama Kuu ya Tanzania, wanafanya kazi nzuri sana ya kutoa haki nchini mwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hali ilivyo, ni vyema tukawapongeza sana na kuwashukuru kwa kujitolea kwao kulitumikia Taifa letu na kwa kuwa kazi ya Ujaji ni ngumu sana, pongezi, shukrani zake ni za nadra. Tungekuwa na utaratibu wa kutambua kazi zao. Tuwape nishani za Taifa za Utumishi Bora pale wanapotekeleza majukumu yao vyema mbele ya wenzao na pale wanapokaa kazini muda wa miaka mitano, kumi, ishirini na kadhalika. Nishani hizi ziwe pamoja na tuzo ya fedha taslimu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara kwa kutusaidia kukamilisha ujenzi wa Mahakama ya Kagongo, Kata ya Lang'ata, eneo la Nyumba ya Mungu. Tunawashukuru sana kuleta Hakimu wa Mahakama hiyo na wafanyakazi wanaohitajika. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hali ya Mahakama katika Wilaya yangu ni ngumu sana. Tunaye Hakimu wa Wilaya, Bwana Msigit, anayefanya kazi yake kwa juhudzi za pekee na uadilifu mkubwa. Lakini anao wafanyakazi wachache sana. Hakuna Hakimu hata Mahakama za Mwanzo za Tarafa za Usangi, Ugweno, Lembeni na Jipe-Ndea. Mtu mwenye shauri la Mahakama, sharti aende Mwanga kwa kulipa nauli ya shilingi 3,000/= kwa ajili ya kwenda na kurudi ama akajibu mashtaka, kutoa ushahidi au kuhakikisha anapata haki.

Mheshimiwa Spika, chonde, tupatieni hata Mahakimu wawili tu.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba na timu yake kwa kuandaa na kutoa hotuba nzuri ya bajeti ya Wizara. Naiunga mkono hoja hiyo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa Wizara kwa kushirikisha Jimbo langu kwenye mpango wa *Quick Start* (Ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo *Usa River*). Ni kwa kudra ya Mwenyezi Mungu tu, jengo la Mahakama ya Mwanzo la *Usa River* halijaanguka na kuleta maafa au ajali nyingine mbaya, tunashukuru sana. Tunashukuru pia kwamba Mahakama ya Mwanzo Mbuguni na Maji ya Chai, zimetajwa kwenye taarifa ya wataalam kuhusu hali ya majengo ya Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo nchini.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Arumeru Mashariki lina Mahakama za Mwanzo nane, tatu (*Usa River*, Maji ya Chai na Mbuguni) zimetajwa kwenye taarifa ya Wwataalam. Je, hizo zipo zote kwenye *Quick Start*? Tano (Nkoanrua, Poli, Nkoaranga, King'ori na Ngarenanyuki) hazimo kwenye taarifa ya wataalam wala taarifa nyingine yoyote ya Wizara, tuliyo nayo. Je, Wizara itakuwa na mpango gani wa kufufua huduma kwenye Mahakama hizi tano? Naunga mkono hoja.

MHE. KHERI KHATIB AMEIR: Mheshimiwa Spika, mimi naunga mkono hoja hii moja kwa moja. Bila Wizara hii, hakuna Serikali wala Vyama vya Siasa. Lakini kwanza niwapongeze wote, Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, bila ya kuwasahau Jaji Mkuu, Mheshimiwa Barnabas Samata na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge.

Mheshimiwa Spika, kama inavyoleweka kwamba nchi yetu imegawika katika nguzo tatu Kisheria na Kikatiba, moja ya nguzo hizo ni Mahakama. Mahakama ni mhimili mkubwa mno wa utulivu na mtengamao katika nchi. Katika kufahamu hivyo, ndio maana bila ya kuwa na chombo madhubuti cha Sheria na Mahakama, hakuna mhimili wa pili (Serikali) wala wa tatu (Bunge), kwani kama hali itakuwa hivyo, itakuwa vurugu tupi, hakuna nchi. Kwa maana hiyo basi, mimi nakubaliana na wale walio na mawazo ya kuwa na kasma kubwa na ya kutosha, itengwe kwa Wizara hii ili itekeleza majukumu inayojipangia.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri, Wizara na wahusika wote, wajitahidi kupunguza mlundikano wa kesi na mahabusu Mahakamani na Magerezani. Labda kwa hili, pangeandaliwa utaratibu maalum wa uchunguzi na mtindo wa uendeshaji wa kesi Mahakamani ili kesi zisichukue muda mrefu na kwa wale ambao mashauri yao yana utata, basi wasiwekwe mahabusu. Kuwaweka watu ndani kwa sababu za kiuchunguzi au ushahidi haujatimia, kunawakosesha haki si mshtakiwa au mtuhumiwa tu, bali hata wale wanaomtegemea kama watoto, mke, mume na pengine wazazi.

Mheshimiwa Spika, nashauri vile vile kwamba ili kulinda haki za binadamu watoto (mahabusu na wafungwa) watengwe au wawekwe mbali na Magereza ya watu wazima. Kwa kweli kitabia, wafungwa wengi wanakuwa na tabia zisizo maadili na baadhi yao walishindwa kuishi katika mazingira ya watu wa kawaida. Lakini si hivyo tu,

wanajengeka na tabia ya kuvunjika moyo kimaisha ya baadaye, tofauti kabisa na watoto ambao wana nafasi kubwa endapo watawekwa vyema, kubadili tabia na kufuata maadili mema na baadaye kuwa raia wazuri. Watoto kuwekwa kwenye mazingira ya kutu uzima, na hasa ya wafungwa wazee, ni kuwadumaza kiakili kimawazo na huenda wakaona kumbe hayo ndiyo maisha yenyewe.

Mheshimiwa Spika, sheria zina haja ya kutazamwa upya hasa kwa akinamama wajawazito. Pangetafutwa kipengele cha akinamama wajawazito walio mahabusu au kifungoni, ama wakatolewa kwa muda katika muda wa kabla ya kujifungua na baada ya kuzaa. Kuendelea kuwa kifungoni, tunawatesa watoto wanaozaliwa, kwa kosa ambalo wao haliwahu. Asante.

MHE. JUMANNE H. NGULI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii. Kabla ya kuanza kuchangia, naomba nitamke kuwa naunga mkono hoja hii. Lakini naomba nichangie haya machache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho ya wazee wa Mahakama za Mwanzo. Mpango wa wazee wa Mahakama kulipwa posho ya shilingi 1,500/= kwa kesi, ulianza katika mwaka 2002/2003 na ilitegemewa kuharakisha kesi. Lakini tegemeo hili halijawezekana mpaka leo kwani bado tuna kesi nyingi kila Mahakama. Badala yake, mpango huu umeleta matatizo kwa wazee wa Mahakama kwa kutopata posho zao, kwani kesi haziishi kwa haraka ilivyotegemewa na kwa kuwa wazee hawapati posho, sehemu zingine wazee wameanza kupuza kwenda Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, kesi haziendi haraka kwa sababu mbalimbali ikiwi ni pamoja na upelelezi kutokamilika na kutopatikana kwa mashahidi wengine. Hakimu haathiriki, kwani ye ye anapata mshahara wake. Pia Mahakimu ni wachache na wanasmamia Mahakama zaidi ya moja. Hivyo, uwezekano wa kesi kwisha haraka ni ndoto. Kwa hiyo, nashauri Serikali irudishe mpango wa zamani wa kuwalipa wazee wa Mahakama kwa siku anayohudhuria, ila posho hiyo ipandishwe ili wazee hawa wasipoteze muda bila posho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu urekebishaji wa majengo ya Mahakama ya Mwanzo. Mahakama na vyombo vyake vyote vikiwa na sura nzuri machoni mwa raia, ndiyo vinaonyesha utawala bora. Mambo yakienda hovyo hovyo katika sekta hii mbele ya raia, kwa kweli inaonyesha matatizo juu ya utawala. Majengo ya Mahakama za Mwanzo yafanyiwe ukarabati, na sehemu zingine yajengwe upya ili yalete heshima ya Mahakama. Hata kama raia anahukumiwa, aone anatendewa kweli.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na wataalam wote. Hotuba hii imeandalika vizuri sana. Lakini kama itatekelezwa vizuri, basi mambo yote yatakuwa mazuri sana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuiomba Serikali iangalie upya mishahara na marupurupu ya Waheshimiwa Majaji na Mahakimu. Hawa Waheshimiwa wanafanya

kazi katika mazingira magumu sana na mishahara yao ni midogo yenyе vishawishi vya rushwa. Hii iwe pamoja na kuboresha ofisi. Mfano, nchi yetu hadi leo ndiyo mahojiano ndani ya Mahakama hayarekodiwi. Hivyo, ningependekeza kwamba mahojiano yote yarekodiwe badala ya kuendelea kuandika na bila kutunzwa vizuri (*record*). Vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki, baiskeli na kadhalika wapewe wafanyakazi ili kurahisisha kazi zao.

Mheshimiwa Spika, sheria zilizo nyingi zimepitwa na wakati. Kwa mfano, Sheria ya Matunzo ya Watoto wa nje ya ndoa (*Affiliation Ordinance*) ya mwaka 1949 ambayo inatoa haki za huduma za matunzo kwa watoto wa nje ya ndoa. Lakini sheria hii imepitwa na wakati. Mfano, mpaka sasa baba wa mtoto huyu wa nje ya ndoa anapaswa atoe shilingi 100/= kila mwezi kwa ajili ya matunzo ya mtoto wake.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Makosa ya Kujamiana Na. 4 ya mwaka 1998, imeharamisha ukeketaji kwa mtoto wa kike. Chini ya kifungu cha 169 (1) cha sheria hiyo, ukeketaji kwa mtoto wa kike ni moja kati ya vitendo vya kikatili. Lakini sheria hiyo haiku wazi kama ni kosa kumkeketa mwanamke mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi ni kuwa sheria nyingi zinahitaji marekebisho na nyingi ni za kuiga toka kwa wageni. Ningombwa iwepo sheria pia ya kutoa msaada wa kisheria kwa wafungwa ambao wapo Gerezani kwani wengine wanafungwa kwa sababu ya kukosa watetezi kwani siyo wote walio Magerezani wametenda makosa (hawana uwezo kifedha).

Mheshimiwa Spika, kuna Watanzania wengi sana wapo Magereza ya nje ya nchi na wengi wamefungwa kwa sababu ya kushindwa kupata msaada wa kisheria, kwani wengi wameshindwa kujieleza kwa lugha za kigeni na kwa makosa hayo hayo, wenyeji huachiwa au kufungwa vifungo vidogo. Hivyo, kuna Watanaania wengi wamefungwa vifungo vikubwa sana nje.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mapendekezo ya kisheria. Ikiwa mfungwa aliyefungwa nje ya nchi ameshatumikia nusu au zaidi ya kifungu chake katika nchi aliyohukumiwa, lakini kwa vyovoyote vile ameshatumikia miaka mitano huko nje, Waziri anapewa uwezo wa kumwachia huru mara atakaporudishwa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, pia ikiwa mfungwa amehukumiwa kifungu cha maisha katika nchi aliyokamata na kwa kosa hilo hilo hapa nchini kwetu, adhabu yake isiwe kifungu cha maisha na ikiwa ameshatumikia kifungu hicho kwa zaidi ya miaka mitano huko nje, basi Waziri apewe uwezo wa kumwachia huru mara afikapo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ikiwa mfungwa aliyekamatwa nje ya nchi na akahukumiwa kifungu huko na hatakuwa na uwezo wa kuomba kurudishwa nyumbani kwa vile yuko ndani (mahabusu), basi ndugu zake waruhusiwe kumwombea kurudishwa nyumbani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza swali moja, je, ni nani anayepaswa kulipia gharama za kumtunza mahabusu kati ya Serikali, mshtaki, mshtakiwa na kijiji?

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe pongezi kubwa kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tume hii imefanya kazi kubwa na kurahisisha kazi nyingi za Mahakama. Tume hii imezunguka sehemu nyingi Tanzania kuelimisha jamii tena vizuri. Hivyo, ningeomba sana Tume hii itengewe fungu la kutosha ili kuendelea kuelimisha jamii kujua haki zao. Naomba Tume hii ifanye ziara nyingine katika Wilaya mpya ya Kilolo.

Mheshimiwa Spika, Wizara zote zina mipango mizuri ya kuhakikisha angalau katika Makao Makuu ya Wilaya zote, kufanya kitu cha maana. Wilaya ya Kilolo ni mpya, suaona mpango wowote wa kujenga Mahakama ya Wilaya na Mahakama ambazo zipo, ziko kwenye hali mbaya sana. Mfano, Mahakama ya Mahenge haina hata bati moja na nyingine za Kilolo na Mazombe zinahitajika kujengwa upya. Nitaunga mkono hoja hii baada ya kupewa maelezo ni lini Mahakama zitajengwa?

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya sheria ni kulinda haki za wanajamii na sheria haiwezi kufanya kazi yenye bila jamii kuikubali sheria hiyo na kufikisha masuala ya kisheria katika vyombo vinavyotoa haki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%, lakini nitaomba nielezwe lini Mahakama za Kilolo zitapewa fedha za ujenzi.

MHE. MUSA A. LUPATU: Mheshimiwa Spika, natoa pole sana kwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, kwa kazi nzito ya matayarisho ya bajeti. Hoja yake ameiwasilisha kwa ufundi mkubwa na imeeleweka vizuri. Hongera sana, nampongeza pamoja na wataalam wake wote.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuainisha na kuwasilisha orodha ya hali za Mahakama zetu kwa nchi nzima. Katika jedwali la orodha hiyo kwa upande wa Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Korogwe, Mahakama ya Mwanza ya Vugiri haikutajwa. Lakini Mahakama hii ilijengwa pamoja na Mahakama ya Mwanza ya Bungu. Zote mbili zinafanana, zinalingana, ni ndogo na zimezeeka sana.

Kwa hiyo, kama ilivyopendekezwa kwa Mahakama ya Mwanza ya Bungu, naomba Mahakama hiyo ya Vugiri nayo iongezwe katika orodha hiyo na ijengwe mpya kama ilivyopendekezwa kwa ile ya Bungu. Ili Mahakimu waweze kufanya kazi zao vizuri, naomba kwa Mahakama za Bungu na Vugiri ambako hakuna nyumba za kupanga, wajengewe nyumba za kuishi Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu. Ahsante.

MHE. JOSEPH J. MUNGAI: Mheshimiwa Spika, sisi Wahehe chini ya Mtwa Mkwawa, hukumu ya *murder* ilikuwa kulipa ng'ombe kati ya 50 na 200, kulingana na utajiri wa aliyeua. Adhabu ya kifo ilikuwa kwa kosa la *treason* peke yake. Ndugu Mlawa hakujibu mapigo.

MHE. JOHN E. SINGO: Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa kazi ngumu wanayofanya katika kujengea nchi yetu msingi mzuri wa Utawala wa Sheria na Katiba ya nchi. Mazingira ya kazi hii ni magumu na hivyo wanastahili kupongezwa kwa mafanikio na mipango ya maendeleo, iliyotolewa katika hotuba ya bajeti yao yamwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu unalenga katika eneo la huduma ya Mahakama Wilayani Same, rushwa katika Mahakama nchini na Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto.

Mheshimiwa Spika, huduma za Mahakama katika Wilaya ya Same ni duni mno na uduni huo unazidi kuwa mbaya kwa sababu ya mazingira mabaya ya barabara na mawasiliano ya simu. Wilaya ya Same kijiografia ina ukanda wa milima ambayo ndipo 80% ya wananchi wa Same wanaishi. Ukanda wa tambarare inaishi sehemu nyingine ya wananchi 7%. Sasa tatizo kubwa ni kwamba Mahakama za Mwanzo nyingi ziko kwenye tambarare, milimani kuna Mahakama moja tu kule Kata ya Mamba na ambayo mara nyingi haina Hakimu.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya milimani ya Kata za Mbagga, Suji, Chome, Vudee na Gonja, yote haya hayana Mahakama za Mwanzo na ni ya ukanda wa milimani. Jambo la pili ni Mahakama zetu kuwa na majengo machakavu na sehemu nyingine hata jengo la Mahakama hakuna. Namshukuru Waziri kukubali kukarabati Mahakama ya Kisiwani. Lakini hii haitoshi kwa sababu ile ya Makanya imechakaa sana na baada ya Waziri kupita katika ziara yake Same, Mahakama hii iliezuliwa na upepo. Sasa ningombwa Waziri atoe upendeleo maalum, Mahakama hii ya Makanya ijengwe upya.

Mheshimiwa Spika, kule katika Kata ya Hedaru, hakuna jengo la Mahakama. Kata ya Hedaru ndiyo yenye idadi kubwa ya wananchi katika Wilaya ya Same. Kwa mujibu wa takwimu za sensa za mwaka 2002 ina wakazi wapatao 19,600. Naiomba Wizara ikubali Kata hii ijengewe Mahakama ili kutoa huduma inayostahili idadi ya wananchi niliyoitaja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili unahu su tatizo la rushwa kwa Mahakimu na Watumishi wa Mahakama, pia Wazee wa Mabaraza ya Mahakama. Nakubaliana na Mheshimiwa Waziri juu ya mikakati ya kupambana na rushwa katika ukurasa wa 47 wa kitabu cha hotuba yake. Jambo moja ambalo ningemshauri akaliwaze na kulifanyia kazi ni kuangalia *scheme of service* ya Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, tofauti kubwa ya mishahara na maslahi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Wilaya, Mkoa na ya Majaji, ni kubwa mno. Tofauti hii, sisi tunaoishi na wananchi wakiwepo Mahakimu, imepelekeea Mahakimu kula rushwa. Mazingira haya haya yamepelekeea Idara zingine za Serikali kama Polisi, kuhusika na ulaji wa rushwa. Kulingana na taarifa ya Jaji Warioba, Idara zote zilizoonekana kuongoza kwa rushwa, naziona pia kuwa na *scheme of service* na maslahi duni mno.

Watumishi wa idara hizo wanajiuliza, kulikoni nikistaafu, nikifa au nikifukuzwa kazi, hatima yangu na ya familia yangu ikoje? Namshauri Mheshimiwa Waziri alitafakari hili na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa mwisho unahu Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto. Pamoja na chuo hiki kuwepo, bado idadi ya wanachuo wanaohitimu hapo haitoshelezi mahitaji ya Mahakimu nchini. Pamoja na juhudzi za kukipanua chuo hiki, juhudzi ambazo nazipongeza, namshauri Mheshimiwa Waziri afikirie kufungua/kujenga chuo cha pili cha uongozi wa Mahakama. Hii itasaidia kutoa Mahakimu watakaotosheleza pengo la Mahakimu lililopo na la wale ambao wanapungua kutokana na vifo au ajali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ifikirie kuweka chuo cha pili hapa Dodoma katika moja ya majengo ya Serikali au Mashirika ya Umma yasiyotumika au ambayo hayajakamilika. Kuwepo kwa chuo cha pili cha Mahakama, kutapunguza uhaba wa Mahakama katika nchi, msongamano wa wafungwa Magerezani, msongamano wa kesi katika Mahakama mbalimbali na mwisho Wizara itaweza na kufaulu kuboresha Utawala Bora na haki za binadamu kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa Mahakimu katika Mahakama zetu ni upungufu mkubwa katika Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Mheshimiwa Waziri, huwezi kuwa na gari lisilokuwa na dreva. Sasa Wizara yako inakuwaje na Mahakama ambazo hazina Mahakimu? Naomba hili lifanyiwe marekebisho hasa kule katika Wilaya yangu ya Same.

Mheshimiwa Spika, mwisho nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Mkuu, kwa kazi nzuri na hotuba nzuri. Naunga mkono hoja.

MHE. PAUL N. MAKOLO: Mheshimiwa Spika, kuhusu posho za wazee wa Mahakama, utoaji wa posho hizi haueleweki. Hivyo, umezua malalamiko makubwa kwa wazee wa Mahakama. Hivi tatizo la posho hizi ni upatikanaji au namna ya kuzitoa?

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa wazee hawa ndio wanaotegemewa kusimamia na kutoa haki. Sasa inakuwaje Wizara inasuasua kutoa haki zao? Jambo hili linaleta aibu kubwa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, samani katika Ofisi za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hali ni mbaya sana. Tunaitaka Wizara ihakikishe mazingira wanayofanyia kazi Mahakimu sasa inakuwa nzuri. Meza, viti, karatasi na kadhalika vinapatikana na viwe na hali nzuri. Inamfanya Hakimu naye afanye kazi vizuri na kwa moyo.

Mheshimiwa Spika, pia suala la usafiri kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni muhimu. Hivyo, naishauri Serikali iwanunulie au kuwakopesha pikipiki ili waweze kusafiri kwa urahisi katika kuleta ufanisi wa utendaji kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ISAAC M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, magereza yetu yana mahabusu wengi kuliko wafungwa. Wengi wa mahabusu hao ni watu ambao wamebambikwa kesi. Katika hali halisi, kuna uhusiano mkubwa wa kubambikiza kesi unaofanywa kati ya Polisi na Hakimu wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ni mara nyingi sana wananchi wamekamatwa vijiji, wakapelekwa Kituo cha Polisi bila kuelezwu wamekosa nini. Wanapofika Mahakamani, wanasomewa kesi ya mauaji. Wakati mwingine mtuhumiwa anakamatwa kwa kutishia kwa maneno. Akifika Mahakamani, anasomewa shitaka la mauaji, hapa aliyetishiwa kuuawa, haonekani Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, raia huyo anakaa rumande kwa kesi ambayo hawezu kuwekewa dhamana. Matokeo yake, ndugu wa raia huyo wanaombwa watoe chochote ili waweze kufutiwa kesi. Watu wa namna hiyo wasipotoa chochote, wanasota rumande bila kupelekwa Mahakamani, kwa kisingizio cha upelelezi haujaisha.

Mheshimiwa Spika, uhusiano uliopo kati ya *PP* na Hakimu, mara nyingi wanakaa pamoja, wanajadili kesi na hata kukubaliana mtuhumiwa akae rumande kwa kumkomoa tu. Lakini pia chanzo kingine cha kuwa na mahabusu ambao hawapati dhamana, ni pale viongozi kama *DC* anapoingilia shughuli za Mahakama na kuagiza Hakimu asitoe dhamana kwa watuhumiwa na mara kadhaa *DC* anaagiza kuwa mtuhumiwa lazima akae rumande hata kama kesi yake inaruhusu kupata dhamana. Haya yanatokea Wilayani kama Bariadi.

Mheshimiwa Spika, raia wa kawaida hana mahali pa kupata haki zaidi ya Mahakamani. Kimbilio la haki ni Mahakama ambayo tunayo imani ya kutenda haki. Raia anakosa haki hiyo inapotokea Mkuu wa Wilaya anapoingilia kwa kutumia wadhifa wake, kuzuia Mahakama isitoe dhamana. Mara nyingi *DC* ameonekana akisaka watuhumiwa, akiagiza Polisi na Mahakama wasitoe dhamana.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kitendo kibaya kwa Wakuu wa Wilaya kuingilia shughuli za Mahakama na ni kinyume cha haki.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali itoe kauli kuzuia *DCs* wasiingilie shughuli za Mahakama. Mahakimu wanaruhusiwa kuangalia mwenendo wa kesi na pale ambapo kesi inaonekana ni *fineable*, basi atoe dhamana kwa watuhumiwa. Pale ambapo wapo Polisi kwa muda mrefu wameshindwa kupata ushahidi au upelelezi haukamiliki, basi Mahakama iwaachie huru watuhumiwa. Hiki ni kitendo ambacho Hakimu anaruhusiwa.

Mheshimiwa Spika, wale ambao wataonekana wamebambikiwa kesi, wasaidiwe kuwashtaki wale waliowatengenezea shtaka la uongo. Kitendo hiki kitakomesha mtu kubambikizwa kesi.

MHE. FETEH SAAD MGENI: Mheshimiwa Spika, kwanza nachukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa juhudi yako kubwa ya kuliongoza Bunge hili katika hali ya usalama na utulivu.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu, Wataalam na Watendaji wote wa Wizara, kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nilikwisha toa pole kwa wafiwa pamoja na Wabunge waliofiwa na maafa mbalimbali pamoja na kutoa hongera kwa Wabunge waliopata fursa mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa, kwa hiyo, naomba kutoa mchango wangu moja kwa moja katika baadhi tu ya maeneo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanzia upungufu wa Mahakama. Naomba sana kuongezwa Mahakama hasa za Mwanzo. Hizi ni chache mno na zinasababisha kurundikana kesi nyingi. Aidha, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni kidogo na wanahitaji kuimariswa kielimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wazee wa Mahakama. Nashauri wazee hawa wasaidiwe zaidi katika kupewa elimu na semina mbalimbali ili waweze kumsaidia vizuri Hakimu. Aidha, waangaliwe vizuri katika ile posho ya shilingi 1,500/= ambayo ni kidogo hata kwa sabuni. Vile vile fedha hizi walipwe kwa wakati, kwani wanadai kwa vipindi virefu sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuboresha Mahakama, naomba Wizara ichukue juhudi kubwa katika kufanyiwa matengenezo Mahakama zetu, kwani nyingine ni mbovu sana na ni aibu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwekewa Mahakama za Watoto walio chini ya miaka 18, ni muhimu sana, kwani kutokana na kuhukumiwa katika Mahakama za watu wazima, ndiyo maana wanafungwa katika Magereza ya watu wazima. Nashauri kwa imani kabisa, Gereza la Watoto lazima liwepo. Hali iliyopo sasa kwa wafungwa watoto ni kukiuka haki za binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri kuwa wafungwa ni watoto wetu, ndugu zetu na ni binadamu wenzetu, sisi tumewaweka Gerezani kwa lengo la kuwarekebisha tu hali zao, ili wawe raia wema na waweze kulitumikia Taifa letu hili katika hali bora na nzuri.

Mheshimiwa Spika, ninachokusudia kusema ni kwamba sasa umefika wakati wa kurekebisha haraka hali ya Magereza yetu. Chakula kiwe bora zaidi, kuondoa viroba haraka na sasa kupewa hizo kaunda suti na viatu ambavyo tumeshazungumza hapa Bungeni. Kuharakisha kupatiwa magodoro na kuondolewa haraka vikeka wanavyolalia. La mwisho kabisa, ni kuondolewa haraka mitondoo, kwani kibinadamu si vizuri hata kidogo kwa nchi kama hii inayotekeleza vyema haki za kibinadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kuona juhudini nilizofanya katika Jimbo langu la Uchaguzi ili kazi za Mahakama ya Mwanzo ziwe bora, lakini zikakwamishwa na Ofisi ya Jiji Mfawidhi Kanda ya Magharibi Tabora.

Mheshimiwa Spika, jengo likakamilika, Kituo cha Polisi kikaanza kazi. Nikasubiri muda wa miezi sita, hakuna Hakimu aliyepelekwa Igalula. Idara ilipoamua kupeleka Hakimu, wananchi wahalifu wakawa wamebomoa milango na madirisha kwa kutoroka Mahakamani kutokana na uhalifu.

Mheshimiwa Spika, Hakimu huyo akaenda Tabora na kusema hakuna jengo na anaomba aende Kijiji cha Goweko, akingoja ukarabati wa jengo. Uongozi wa Kijiji cha Igalula ukaanza kukarabati jengo. Uongozi na Idara ukapeleka barua Igalula kueleza kuwa Hakimu huyo akaripoti Goweko hadi Mahakama ya Igalula itakapokuwa tayari. Sasa yapata miezi zaidi ya sita, hakuna dalili za kupeleka Hakimu Igalula na wakorofii wakaenda kubomoa milango tena.

Mheshimiwa Spika, hapo Igalula ndipo Makao Makuu ya Jimbo. Vyombo vyaa Ulinzi na Usalama ni muhimu, lakini watendaji wanatoa visingizio. Huko Goweko, hakuna jengo la Mahakama wala nyumba ya Hakimu, sababu ni kuwa Goweko ni *centre* kubwa, ina wafanyabiashara wengi na wa kulanguliwa wengi. Sasa hii ni haki?

Mheshimiwa Spika, Polisi wa Igalula wakiwa na kesi, waipeleke Kigwa ambako ni umbali wa maili 14 au Goweko maili 18. Hii ni haki? Mazingira ya kufanyia kazi Hakimu ni mazuri kuliko Goweko. Sasa wananchi wapoteze nguvu zao hadi lini kwa kuwabembeleza Mahakimu?

Mheshimiwa Spika, naomba Idara ya Mahakama inieleze kama Mahakimu wanachagua sehemu ya kufanyia kazi au ni wajibu kufanya kazi mahali popote? Nini maana ya utii katika kazi?

Mheshimiwa Spika, kama hakuna atakayekwenda, nguvu za wananchi za kutengeneza Mahakama, zilipwe na Idara yako? Wananchi wa Igalula wamechoshwa na urasimu wa Idara yako kutowatendea haki wananchi hao. Naomba jibu ili nikawaeleze kuwa Idara haitambui usalama na haki yao Kikatiba.

Mheshimiwa Spika, Hakimu aliyeko Mahakama ya Mwanzo ya Kijiji cha Kigwa, aitwaye Katuku, ni kero kwa wananchi wa Jimbo la Igalula. Malalamiko mengi ya rushwa tangu akae hapo zaidi ya miaka kumi, ni himaya yake. Anathubutu kutoa hata *judgment*, nakala yake kuwapa watu ili wapatie mradi wa kula. Tuhuma hizo ziko kwa DC Uyui na Diwani wa Kata ya Lutende anafahamika wanavyoshirikiana naye kutoa nakala za hukumu ili kutafutia pesa.

Mheshimiwa Spika, malalamiko mengi, lakini Idara yako ya Mahakama imemlinda na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Sasa naomba kama ni mtu maarufu sana katika Idara ya Mahakama, basi mtoeni Jimboni kwangu aende sehemu nyingine. Nchi hii ni kubwa na ninyi bado mnamhitaji. Basi tuondoleeni kero hiyo ili wananchi wangu waishi kwa amani na wafanye kazi zao salama.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Igalula tumechoshwa na tuhuma za Hakimu Katku wa Kigwa. Mchukueni kwa manufaa yenu, lakini hatufai kwa Jimbo la Igalula. Nawasilisha kwa hatua.

MHE. PAUL E. NTWINA: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba kwa hotuba yake muhimu kwa Wizara hii. Pia nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi zake nzuri, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, mimi sina maneno mengi, lakini ni vyema ukaelewa suala zima la ukosefu wa Mahakama pale Kijiji cha Mbwayuni, palikuwa Mahakama ndogo, lakini mara baada ya Hakimu kukamatwa kwa tuhuma ya kudai rushwa, hajapatikana Hakimu wa kubadili nafasi hii. Hivi sasa jengo limeanguka, wananchi wanakwenda Mkwajuni ambapo ni mbali sana na ni kero wakati watuhumiwa wanateseka sana kwenda Mkwajuni Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, licha ya tatizo hilo, Hakimu anayetumika ni yule wa Wilayani. Huyo hutumia muda mwangi kutoka Chunya kwenda Mkwajuni. Naiomba Wizara hii kutupatia Hakimu pale Mkwajuni na pia tusaidiwe kujengwa kwa Mahakama ndogo pale Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri atupatie gari la Wilaya, hatuna kabisa gari la Mahakama. Suala hili nimekwisha omba sana huko nyuma, ingawa sasa kazi inakuwa ngumu sana kwa Hakimu kusafiri.

Mheshimiwa Spika, hata wananchi kupigwa pingu na kusafirishwa kwa kuvuka Mto tena kwa kupita kwenye Mto uliojaa maji au kuzunguka kuititia darajani ambako ni mbali zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hata hivyo, kwa lengo la kuboresha, napenda nichangie maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, idadi ya Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo ni ndogo kiasi kwamba hakuna haki inayotendeka katika maeneo hasa ikiizingatiwa kuwa kesi zinacheleweshwa sana. Nashauri pawepo na *crush programme* ya kufundisha Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo, kwa sababu afadhali kuwa na Mahakimu kuliko kukosa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Bunge tayari limekwisha hamia Dodoma, nashauri Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, ionyeshe mfano. Jaji Mkuu awe wa kwanza kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Spika, rushwa Tanzania ipo katika mfumo wa sheria na utalawa. Kwa hiyo, inakuwa vigumu kwa mtuhumiwa kunaswa. Kitengo kinachohusika na mikataba, kinabidi kuangaliwa upya hasa kwa kuzingatia mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia. Hatma ya vita dhidi ya rushwa hasa *general corruption*, ipo mikononi mwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali nikiwa na maana ya Ofisi. Sheria zetu zitungwe kiasi kwamba hata kama kiongozi atachaguliwa kwa njia chafu, basi mfumo umbane asiendeleze rushwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri Serikali iangalie upya mishahara ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Mahakimu Wakazi. Mishahara na marupurupu ya waamuzi hao wa haki, wapewe upendeleo kama ile ya *TRA* au Wabunge.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima napenda kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Manasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Majaji, Mahakimu na wataalam mbalimbali wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa naiomba Serikali ikumbuke kwamba nchi yetu ni ya Utawala wa Sheria. Haiwezekani kuimba wimbo wa Utawala Bora, lakini bado Mahakama hazitoshi, Mahakimu hawatoshi na vifaa muhimu vya kutendea kazi havipo. Kwa mantiki hiyo, naiomba Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

- (i) Jitihada zifanyike kukarabati Mahakama zetu za Mwanzo za Wilaya.
- (ii) Mahakama pekee bila Mahakimu haitoshi, idadi ya Mahakimu iongezwe.
- (iii) Vifaa muhimu vya kusaidia utendaji katika Idara ya Mahakama, viongezwe kama magari, *stationery* na kadhalika.
- (iv) Kwa ujumla wake Wizara hii iongezewe fedha ili kukidhi matakwa ya kuimarisha demokrasia nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maombi maalum ambayo ni kero sugu katika Wilaya ya Korogwe, ni jambo la kusikitisha sana Wilaya ya Korogwe ina Mahakama za Mwanzo tatu tu na kwa bahati mbaya hata hizo tatu ni chakavu mno na zipo mbalimbali sana. Zaidi ya Mahakama tano ambazo ni *Old Korogwe*, Mombo, Makuyuni, Magoma na Mnyuzi, majengo yake yamebomoka kabisa na hayatumiki kabisa. Hali hii imeleta usumbufu, na wananchi kukosa haki zao kwa sababu ya usumbufu wa umbali.

Mheshimiwa Spika, naomba Mahakama hizo zikarabatiwe ili ziweze kutoa huduma. Hapa nashauri hata kama haiwezekani kukarabati zote, zikarabatiwe chache hasa za Mashewa, *Old Korogwe* na Mnyuzi kwa maana ya Hale.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Hale, hivi kuna tatizo gani la hadi leo hii Mahakama ya kisasa ya Hale kutokumalizika na kuanza kazi? Naomba sana nipatiwe maelezo, hivi tatizo ni nini? Mahakama hii ingeweza kuondoa tatizo la Mnyuzi, Kwagunda, Potwe, Songa, Kabuku, Michungwani na kadhalika, ipo mahali pazuri ambapo kipo Kituo cha kisasa cha Polisi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 niliahidiwa kwamba Mahakama hiyo itakamilika na kuanza kazi mara moja. Lakini cha kushangaza hadi leo hii hakuna dalili za Mahakama hiyo kuanza kazi. Naomba maelezo, hivi ni lini Mahakama hiyo ya kisasa kabisa itaanza kutumika?

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara hii iendelee kutafuta mkakati wa kupunguza muda wa mahabusu kukaa muda mrefu katika mahabusu. Kisingizio ni bado upelelezi unaendelea. Matokeo yake, kesi ni kupigwa tarehe tu. Leo hii ukienda katika Magereza, mahabusu ni wengi kuliko wafungwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri, yapatikane magari ya kuwapeleka Mahakimu kwenye Mahakama za Mwanzo pale ambapo hakuna Hakimu, kwa kuzingatia siku iliyopangwa katika Wilaya, Mahakimu wapatiwe usafiri. Gari ya Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Korogwe ni bovu sana, hivyo ndivyo ilivyo katika Wilaya zote nchini. Serikali hivi haionti hilo? Ni jambo la kusikitisha kwa mtu anayetoa haki kukosa usafiri.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono 100% hotuba hii muhimu.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, kumpongeza Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa msaada mkubwa anaoutoa kwa Wizara na hivyo mambo kwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchukua fursa hii kukumbushia ombi langu la muda mrefu la kuongezwa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo za Sanya Juu, Barazani Mae, Ngarenairobi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. MAUA ABEID DAFTARI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Majaji Wakuu na wengine kwa kazi zao nzuri na nzito. Ninayo maoni yafuatayo:-

- (i) Ucheleweshaji wa kusikilizwa kesi za madai (juhudu ifanywe zaidi).
- (ii) Bado wako Waheshimiwa Majaji (wachache) ambao wanakubali kughiribiwa kwa chochote na kuwanyima haki wengine.
- (iii) Maslahi ya Waheshimiwa Majaji yaboreshwe.
- (iv) Mawakili wapenda rushwa na wale *double-standard*, wamulikwe na wafichuliwe.
- (v) Shughuli za kutoa haki mikoani, lipewe kipaumbele. Bado ipo kazi ya kusafisha eneo hilo.
- (vi) Watuhumiwa kuwekwa ndani kwa muda mrefu, tatizo hili lipatiwe ufumbuzi.
- (vii) Ipo haja ya kuboresha majengo ya Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Hongereni na kazi njema.

MHE. JUMA S. KIDUNDA: Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, imeelezea mambo mengi ya msingi yaliyotekelizwa na yanayotarajiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Ni hotuba inayodhirisha maendeleo makubwa ambayo Wizara imekuwa inayafanya katika kuboresha utoaji wa haki nchini, pamoja na upungufu mkubwa wa fedha ambazo umeikabili Idara hii kwa miaka mingi mfululizo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia upungufu huo wa bajeti ikilinganishwa na majukumu, nianze kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake kwa jitihada zao kubwa katika ngazi zote hadi Mabaraza ya Kata na hivyo kulazimika kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nizungumzie hali ya mtandao wa Mahakama katika Wilaya mpya ya Kilindi, Mkoani Tanga. Moja ya sababu kubwa zilizoishawishi Serikali kuianzisha Wilaya ya Kilindi ni umbali wa Makao Makuu yake

pale Songe kuwa mbali na Mahakama ya Wilaya ya Handeni (zaidi ya kilometra 100) na zile za Kilosa na Kiteto kuwa mbali zaidi. Kwa sababu ya tatizo hili la Wilaya hii mpya, napenda kutoa maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iweke katika programu yake, mpango wa ujenzi wa Mahakama ya Wilaya pale Songe (Makao Makuu), ili tuanze uhamasishaji wa wananchi kushirikiana na Serikali katika kazi hiyo ya ujenzi, ikiwa ni pamoja na nyumba ya Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, haja ya kuboresha mtandao wa Mahakama za Mwanzo Wilayani Kilindi ni kubwa. Ili kupunguza adha ya wananchi kusafiri mwendo mrefu, tunapendekeza msambazo wa Mahakama za Mwanzo uanishwe ifuatavyo:-

- (i) Mahakama ya Mwanzo - Mswaki (ipo, ikarabatiwe au kujengwa upya).
- (ii) Mahakama ya Mwanzo - Kimbe (ijengwe upya).
- (iii) Mahakama ya Mwanzo - Mgera/Kwediboma (ijengwe).
- (iv) Mahakama ya Mwanzo - Kwekivu (ikarabatiwe).
- (v) Mahakama ya Mwanzo - Songe (ikarabatiwe au ijengwe upya).
- (vi) Mahakama ya Mwanzo - Kikunde (ijengwe).
- (vii) Mahakama ya Mwanzo - Kilindi (ijengwe).

Mheshimiwa Spika, baadhi ya majengo ya Mahakama hizi yapo na yanahitaji ukarabati wa kawaida ingawa baadhi yanahitaji ukarabati mkubwa na sehemu nyingine hazina kabisa majengo kama nilivyoainisha katika mapendekezo yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kusitiza kuwa jiografia ya Wilaya hii mpya kuwa ya milima mingi, kuna lazimisha uzingatiaji wa huduma ya Mahakama kuwa angalau katika kila Tarafa kama nilivyopendekeza.

Mheshimiwa Spika, nimalizie mchango wangu kwa kuipongeza Idara ya Mahakama kutekeleza vyema majukumu ya kugawa haki, pamoja na mazingira yao ya kazi kuwa magumu sana.

MHE. MARTHA M. WEJJA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa 100%. Pamoja na kuunga mkono, naomba niweze kutoa ushauri wangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama. Kazi inayofanywa na Mahakama ni nzuri, lakini inasikitisha sana kuona rushwa bado inachukua nafasi kubwa. Rushwa inaanzia kwa askari, hudai kwamba wao wasipopewa chochote, wanaweza kumbambikia mtu kesi nzito mhusika. Hivyo, mwananchi analazimika kutoa rushwa ili kesi yake isimwumize. Pia kesi hucheleweshwa kwa madai ya kutokukamilika ushahidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kesi, mshtakiwa kwenda mara kwa mara Mahakamani bila kesi kwisha, hata pale mshtaki hafiki Mahakamani, kesi haisikilizwi. Kila leo mshtakiwa huenda Mahakamani bila kusikilizwa na mhusika hafiki Mahakamani na kesi haifutwi hadi kesi inachukua miaka mingi. Je, Mahakama haina sheria ya kuona kama mshtaki haji kwenye kesi na kesi hufutwa? Ninao ushahidi wa jambo hili, niko tayari kuthibitisha. Ni mateso sana. Hamwoni hiyo ni moja ya mianya ya rushwa? Mshtakiwa atahonga wangapi kati ya Hakimu, askari na Karani? Naomba Wizara isimamie suala hili, wananchi wanaonewa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchache wa Mahakama, kutokuwa na Mahakimu wa kutosha kwenye Mahakama, kunasababisha ucheleweshaji wa kesi nyingi na hakuna Hakimu wa kulaumiwa kwa hili, kwani kesi ni nyingi na Mahakimu wachache. Kwa hali hiyo, unaruhusu mianya ya ulaji rushwa kuwa mkubwa. Naishauri Wizara iliangalie hili suala upya ili kunusuru jamii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mishahara. Mishahara iongezwe kwa Mahakimu na Makarani. Hii itasaidia kupunguza tamaa ya kupokea fedha nje ya mapato ya kawaida kwani mtumishi ataona bora afanye kazi kwa uadilifu ili aendelee kupata haki yake halali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho ya Wazee wa Mahakama. Tafadhali waongezwe posho ili kuwapunguzia tamaa ya kupokea rushwa hawa Wazee wetu wa Mabaraza na ili wafanye kazi zao kwa uadilifu.

MHE. PHILIP A. MAGANI: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza tena Waziri na wataalam wa Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa kuendelea na azma ya kuboresha shughuli za Wizara, hususan katika kuhakikisha utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, katika shughuli za uboreshaji wa mazingira, nafurahi kuona katika hotuba ya Waziri, azma yake ya kuongeza ukubwa na kukarabati Mahakama za Mwanzo za Mnacho na Ruangwa katika Wilaya ya Ruangwa.

Nichukue fursa hii kukumbusha kwa mara nyingine tena kwamba Wilaya ya Ruangwa ina Mahakama za Mwanzo tatu ambazo ni Ruangwa, Mnacho na Mandawa. Aidha, Mahakama ya Mandawa imekaa kwa muda mrefu bila kupatiwa Hakimu, tangu alifariki aliyekuwa Hakimu wa Mahakama hii zaidi ya miaka kumi iliyopita. Suala hili nilishazungumza na Waziri Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu na vile vile Mheshimiwa Jaji Mkuu Barnabas Samata, wakati wa ziara yake Wilayani.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa masikitiko ya wananchi wa Ruangwa kwa kutokuwepo kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Wilaya. Tatizo hili linasababisha uchelewaji mkubwa kwa wananchi kupata haki zao kwa vile Hakimu Mkazi wa Lindi hafanyi ziara za kikazi ili kusikiliza kesi mbalimbali. Aidha, hali hii husababisha mlundikano katika jela na gereza za rumande. Nimeangalia programu ya ujenzi wa Mahakama za Wilaya, lakini sioni mahali popote ambapo pameonyesha nia ya Serikali ya kujenga Mahakama ya Wilaya hii mpya.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iwe na jicho la huruma kwa wananchi wa Ruangwa ambao wanalazimika kusafiri masafa marefu kuelekea huko Lindi kufuatilia haki zao za Mahakama. Hali ya barabara ni mbaya na pengine kwa sababu za ufukara, wananchi inawapasa kusafiri kwa miguu kupitia misitu yenyе samba wala watu (hususan wakati wa masika) wakienda Lindi kutafuta haki. Tunaomba Wizara ijenge Mahakama ya Wilaya na imteue Hakimu Mkazi wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumalizia mchango wangu, napenda kukumbusha tena kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Mnacho, Bwana Kapinga, amekaa kwa muda mrefu katika kituo hicho, kiasi cha kuwa *ineffective* kwa vile amezoeana kupita kiasi na wakazi wa hapo. Hali hii inaleta mazingira ambayo pengine haki haitolewi bila upendeleo na hivyo kupelekea kero na malalamiko ya rushwa kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, ningependekeza Hakimu huyu abadilishwe mara moja. Aidha, nakumbusha tena umuhimu wa kupatiwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Mandawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba.

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, kuhusu Idara ya Mahakama ya Wilaya ya Mbulu. Toka Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Dongobesh ahamishwe (baada ya kunung'unikiwa na wananchi na kutuhumiwa kwa rushwa), Mahakama hiyo iliyokuwa ikihudumia wananchi 150,000 sasa haina Hakimu. Anahitajika Hakimu haraka, hasa kwa vile wananchi wenyewe ndio waliojenga majengo ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi mwaka huu imetengewa shilingi milioni 459. Mahakama hiyo haitakuwa na rufaa za kushughulikia kwa vile Mabaraza ya Ardhi ya Kijiji na Mabaraza ya Kata hayajatengewa fedha na Wizara husika. Hivyo, katika ngazi hizo hakutakuwa na mashauri yatakayosikilizwa na ikimbukwe kuwa Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya, ambayo hupewa fedha kidogo sana kutoka Wizara ya Ardhi, hushughulikia rufaa kutoka Mabaraza ya Kata na Vijiji pekee (*have no original jurisdiction*). Waziri aelezee namna ya kushughulikia tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kituo cha Haki za Binadamu, kimekuwa kikiwaandaa wananchi na vikundi vyta wasaidizi wa sheria (*Para-Legals*) katika Vijiji vyta Mikoa ya Morogoro, Manyara, Mara na Arusha. Hii ni kazi nzuri na inafaa zoezi hili kuendelea nchi nzima. Pamoja na mambo mengine, Wizara iratibu zoezi hili katika muda mfupi na

Tume ya kurekebisha Sheria ifanye uchunguzi ili kuona kama kuna haja ya kuwa na sheria itakayowatambua rasmi Wasaidizi wa Sheria Vijijini (*Para-Legals*).

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru sana Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, kwa hotuba yake nzuri juu ya Wizara yake. Pia nimshukuru kwa dhati Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andew Chenge, kutokana na kushiriki kwake. Ninayo imani kwamba ameboresha sana hotuba hiyo. Kwa pamoja, naomba sana niwashukuru na kuwapongeza Watumishi wa Wizara kwa kushiriki kwao kwenye maandalizi ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee mambo matatu kwenye hotuba hii.

Kwanza, naomba kukumbushia kurudisha Mahakama ya Mwanzo ya Kirumba, Jijini Mwanza. Kata ya Kirumba sasa hivi, wakazi wote wa Kirumba na maeneo yote ya Kata ya Kitangiri, Kata ya Nyamanoro, Pansiansi na pia Isamilo, wanatumia Mahakama ya Mwanzo ya Ilemela.

Mheshimiwa Spika, kufuatana na hali halisi ya kesi, inawawia vigumu sana wakazi wa maeneo hayo kutimiza mambo yao ya Mahakama kwa kutumia Mahakama ya Ilemela ambayo ni mbali. Kesi mpaka kwisha inapitia mambo ya kuahirishwa au kupangiwa muda mwingine. Jambo hili naona ni kero sana na wananchi wengine kuacha kesi zao kufuatana na matatizo hayo. Nimeandika barua Wizarani juu ya jambo hili. Je, sasa Wizara itanipa matumaini gani?

Mheshimiwa Spika, pili, nashukuru sana kwa hatua ya mwanzo ya kufanya matengenezo Mahakama yetu ya Mwanza ya Mkoa ya Hakimu Mkazi, pamoja na Mahakama Kuu iliyoko Mwanza Mjini. Kwenye kifungu cha mwaka huu, je, Wizara itaendelea na matengenezo zaidi ya Mahakama hizi? Matengenezo yanatakiwa sana kwenye sehemu ya ndani ya majengo yote, kwani hatua ya matengenezo ya kwanza ilielekezwa kwenye sehemu za nje tu za majengo hayo. Tafadhali sana matengenezo yaendelee mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba niongelee juu ya matatizo yanayowapata wananchi wa Mwanza Mjini kutokana na kubambikiziwa kesi mbalimbali ambazo kwa kweli zinawaumiza sana na pia kujaza Gereza la Butimba na mahabusu wengi. Naomba Mahakama ijiondoe kwenye tabia hii mbaya. Wananchi wamekuwa na matumaini kwamba wanapokamatwa na Polisi na kubambikiziwa kesi, Mahakama ingewatendea haki wananchi hawa na kuwakemea Polisi.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo ni kwamba Mahakama na Polisi wanashirikiana kwenye zoezi hili la kumbakikiza kesi wananchi, ndiyo maana jambo hili limeendelea kwa muda wote huu. Naomba Mahakama ijiondoe kwenye zoezi hili ambalo ndani yake uchafu wa rushwa mbalimbali unaendeshwa na kama tunavyofahamu ni kwamba rushwa isiachiwse mianya ya aina yoyote.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itoe msimamo wa kuzuia Mahakama kuendeleza tabia hii mbaya. Wananchi wetu tuwatendee haki zao sawasawa. Wananchi wengi sana wanalamikia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, sasa Jijini Mwanza, tunalo tatizo kubwa la nyumba za kukaa Mahakimu na Majaji. Wizara inatoa maelezo gani kuhusu tatizo hili la nyumba za Mahakimu na Majaji kwenye kituo cha Mwanza Jijini? Kuna Majaji ambao wamekaa hotelini kwa muda mrefu sasa na bado wako hotelini. Taarifa na takwimu za *Mwanza Hotel* zinatosha kabisa kutoa ushahidi wa muda na wangapi wanaishi hotelini hapo. Naomba Wizara itoe maelezo ni namna gani tatizo hili litamalizwa.

Mheshimiwa Spika, ninayo imani kubwa kwamba kwa kupitia kwako, nitapata majibu kwenye mambo haya niliyoyatoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. ALI SHEHA MUSSA: Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, siyo vibaya kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa rambirambi zetu za dhati kwa niaba ya wananchi wangu wa Mkwajuni, dhidi ya Marehemu Mheshimiwa Yeteh Malyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijiji. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake pema peponi. *Amin.*

Mheshikiwa Spika, hotuba hii ni nzuri iliojaa mambo mengi muhimu kwa nchi yetu, yenye lengo la kuangalia haki na sheria, jambo ambalo ni kama gumzo kwa wananchi walio wengi. Ukiangalia katika hotuba hii kuanzia ukurasa wa 35 pale chini, kuna para inasema: "Mwanasheria Mkuu wa Serikali (SMT) atafungua Ofisi zake katika Wilaya 20 hadi ifikapo mwaka 2009." Sasa ningependa kufahamu. Je, upande mwingine wa nchi yetu hii, Mwanasheria Mkuu huyu atatusaidia nini? Kwa sababu Mwansheria Mkuu huyu ni wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Katiba yetu, kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa tulipo. Pamoja na kusikia kwamba huenda ikafanyiwa marekebisho, ingawa ni mapame kuongelea jambo hili, nashauri na kusisitiza kuwa na uelewa na ufahamu, jamani tusije tukajitumbukiza kwenye mambo magumu, kwani mimi mwenyewe nimekuwa kiongozi wa ngazi niliyofika

Mheshimiwa Spika, kutokana na Katiba iliyopo kuendelea kuwekwa viraka siyo jambo bayo, lakini tusije tukafika mahali pabaya. Ingawa hivi sasa mitaani kule Zanzibar, kuna maneno yasemayo: "Tumechoka na sura ya Katiba, lugha ya "wewe" kuwa Rais na mimi ni Makamu," yaani kwa maana ya misingi inayokubalika na wananchi walio wengi au Katiba ya kuwezesha.

MHE. REMIDIUS EDINGTON KISSASSI: Mheshimiwa Spika, napenda kuiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na nampongeza sana kwa juhudhi kubwa zinazofanywa na Wizara yake kwa kuimarisha majengo na kuwapa motisha Majaji wa ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kuchangia dogo lifuatalo nalo ni kuhusu matatizo ya kesi za wajane na hasa waliofiwa na waume zao kutokana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, kesi hizi zinachukua muda mrefu sana na hivyo kuongeza maumivu kwa wajane na warithi wengine. Hivyo, naomba Wizara hii iliangular sana suala hili ili taratibu maalum zitafutwe ili wajane wapate haki zao kwa haraka kama inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nahimiza watu wajijengee utamaduni wa kuandika wosia ili warithi wasipate usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kusema tena kuwa naunga mkono hoja hii. Ahsante.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, kwana kabisa naomba nianze kwa kumpongeza Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Andrew Chenge, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa bajeti yenyenye mpango mzuri wa kutetea haki na maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, niitumie fursa hii kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na kuwatakia utekelezaji wenye mafanikio kwa raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Wizara kuwa na mikakati mizuri ya kuhakikisha Mahakama zetu zinatenda haki kwa raia wake, bado kuna mapungufu madogo madogo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi. Mfano, kumekuwa na tatizo la ucheleweshaji wa kesi nyingi bila sababu yoyote ya msingi na kuwafanya Watanzania wengi kupoteza muda mwangi wa uzalishaji mali kwa kufuatilia kesi. Kwa kuwa lengo la Serikali siyo hilo, naomba tatizo hilo likomeshwe.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo la walalamikaji wengi kutokutendewa haki hasa Mahakama za Mwanzo na nyinginezo. Tatizo hili limekuwa likiwapatana sana wanawake wajane, walioachika au wanaonyanyasika kwa waume zao au katika ndoa zao na kufanyiwa maasi mbalimbali mfano, kupigwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, matatizo haya yote niliyoainisha hapo juu, yanapatikana tu kwa kuwa Mahakimu wetu wengi wametawaliwa na suala zima la rushwa na watoa rushwa walio wengi ni akina baba kwa kuwa wao ndio wana uwezo wa kuhodhi mali za familia kama zao peke yao yaani mfumo dume.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lengo la Serikali ni kutimiza ahadi ya binadamu wote, ni sawa. Naiomba Serikali iwamulike Mahakimu wanaoendeleza rushwa nchini katika sehemu zao za kazi, kwa kuwapa adhabu kali wale wanaobainika. Mfano, kufukuzwa kazi pamoja na kifungo.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea suala la rushwa, tunatakiwa pia kujadili chanzo cha rushwa, ikiwa ni pamoja na kuangalia mishahara na maslahi ya Mahakimu wetu na watumishi wote kwa ujumla wa Wizara hii. Ni matumaini yangu kuwa watendaji hawa wakiboreshewa vipato vyao, inawezekana ikawa dawa ya kupunguza rushwa kwa kiasi kikubwa. Daima nitaendelea kutoa mfano kwamba, Mtoto ale, ashibe, ili asidowee kwa jirani.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nizungumzie suala la Wazee wa Baraza. Pamoja na Bunge hili kupiga kelele siku zote juu ya posho za Wazee wa Baraza, bado Serikali haijaongeza posho za wazee, kiasi cha kukidhi haja kulingana na wakatu tulipo. Naiomba Serikali itazame upya suala la posho za Wazee wa Baraza kwani bila kufanya hivyo nina hakika hata Wazee wa Baraza wataingia kwenye mkumbo wa kupokea rushwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile nataka niikumbushe Serikali kwamba Wazee wa Baraza walio wengi wanatoa ushauri wa Mahakama kwa kutumia uzoefu. Hivyo basi, ni matumaini yangu kuwa ni wakati muafaka wa kutoa semina mbalimbali kwa Wazee wa Baraza, kwa lengo la kuwaongeza upeo wa uelewa na kujua sheria za makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mahakama zetu bado zinakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitendea kazi. Mfano, vifaa vya ofisini, mawasiliano, usafiri na kadhalika, jambo ambalo linadhoofisha ari ya kazi kwa watendaji wetu. Nitashukuru kama Mheshimiwa Waziri atatamka lolote juu ya hili, ili kufufua ari ya kazi kwa watendaji wote. Nina hakika Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba ana upungufu mkubwa wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo. Naiomba Serikali ione umuhimu wa kuongeza Chuo kingine cha Sheria kwa mafunzo ya Cheti (*Certificate*), ili tuweze kupata Mahakimu wengi wa kutosheleza Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, nadhani pia itakuwa vyema kama Serikali itatoa nafasi za masomo ya juu kwa Mahakimu wenye nia, kwani wengi wao wameanza kuitwa na wakati na pia sheria nyingi sana zinabadilika.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama zetu, yamekuwa machakavu na ya muda mrefu. Naiomba Serikali ifanye mkakati na juhudzi za makusudi ili kurudisha hadhi ya chombo chenyewe, kwa kukarabati ama kujenga majengo mapya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa lugha ya Kiswahili sasa inatambulika Kimataifa, hivyo sioni sababu ya Mahakama zetu kuanzia ngazi ya Mkoa mpaka Mahakama ya Rufaa, kuendesha kesi kwa lugha ya Kiingereza ambayo inawanyima haki Watanzania

wengi na kusababisha wengi kukosa haki zao kwa sababu tu ya kuchengwa na lugha. Ningeshukuru kama Mheshimiwa Wairi angetoa majibu kwa hili.

Mheshimiwa Spika, sasa nirudie tena kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mpaka hapo ndiyo tumefikia mwisho wa kikao cha asubuhi. Waliojiandikisha kusema kwa mdomo wote wamepata nafasi. Nina hakika wengine wengi wamechangia kwa maandishi, ndiyo utaratibu wetu unakwenda vizuri. Tutakaporejea kipindi cha mchana kabla ya watoa hoja wenyewe hawajaanza kuhitimisha hoja yao, tutampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa sababu michango iliyotolewa iligusia Magereza, Polisi ni vizuri majibu yakatoka kwenye Wizara husika, yeche atakuwa wa kwanza halafu ndiyo tutakuja kwenye Wizara yenyewe tukianza na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, halafu mtoa hoja mwenyewe. (*Makofî*)

Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.43 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nikushukuru kwa nafasi uliyonipa ili na mimi nichangie hoja iliyio mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu, nitajaribu kugusia yale mambo ambayo baadhi ya wachangiaji walipokuwa wakichangia waligusa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya jambo ambalo limesemwa na wengi kuanzia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kambi ya Upinzani na wachangiaji wengi tu, ni suala la Polisi kubambikiza kesi kwa watuhumiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimamo wa Wizara kuhusu jambo hili ambalo hata huko uraiani, kwenye magazeti na sehemu mbalimbali kwa kweli linazungumzwa sana, ni kwamba kwa askari kumbambikizia mtu kesi ya uwongo ni kosa kubwa na adhabu yake ni kufukuzwa kazi na kushtakiwa kwa matumizi mabaya ya cheo chake. Jambo hili Polisi wote katika vikao mbalimbali vya Mabaraza tunawaeleza kwamba ni jambo ambalo halikubaliki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachoomba kwa raia, inapotokea amebambikiziwa kesi atupe taarifa na sisi tutachunguza. Kama ni kweli huyu askari kumbambikizia kesi tunasema hili ni kosa kubwa adhabu yake ni kufukuzwa kazi na kushtakiwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane kuwaeleza wananchi wetu badala tu ya kulalamika kwenye magazeti, watuarifu, tutachunguza na tutachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile uko upande wa pili wa shilingi huu ni upande wa kwetu sisi tunashughulikia hilo, uko upande mwingine tu wa binadamu kukataa kukiri kwamba kafanya kosa. Wapo watu ambao wanasema nimebambikiziwa, nimebambikiziwa ili aonekane kwamba hakufanya kosa, hakubali. Kwa kawaida binadamu hakubali kwamba amefanya kosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano lile Gereza alilolitaja Mheshimiwa Dr. William Shija, *Kisungamile Prison* kule Sengerema. Mwaka 2003 nilitembelea Gereza lile na mimi nilielezwa haya haya kwamba hapa tunabambikiziwa kesi. Katika ziara yangu nilikuwa nao ni pamoja na *DC* wa Sengerema, nikawaambia wale wafungwa yejote yule ambaye kwa dhati kabisa anajua kabambikiziwa kesi, yuko hapa *DC* mpelekeeni taarifa tutachunguza na *DC* atatupa taarifa. Baada ya kumaliza ziara yangu ile ilikuwa mwezi Aprili mpaka Mei mpaka sasa hatujapata ripoti ya mtu aliyejkenda kwa *DC* au ndugu zake kwenda kutoa taarifa na ushahidi kamili kwamba mimi nilibambikiziwa kesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, liko hili la watu tu kutokukubali kwamba nimefanya makosa anasema nimebambikiziwa japo kafanya makosa. Huko kwenye Magereza ukitembelea hakuna anayekubali haraka haraka kafanya makosa, huo ni upande wa pili. Lakini upande unaotuhusu sisi ni ule upande wa Polisi wenyewe tabia hiyo. Hilo nataka kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge ni kosa ambalo tukipata ushahidi wake tutawaadhibu Polisi wote ambao wanaendekeza tabia hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, lilielezwa sana kwenye Kamati lakini vile vile na baadhi ya wasemaji kuhusu wajibu wa Polisi kwamba wao ndio wakamataji na wao ndio waendesha mashtaka, wenyewe ndio wanafanya *arrest* na wenyewe kule Mahakamani ndio wana-*prosecute* kama *PP*. Nataka kuliarifu Bunge hili kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, tumeshakubaliana kimsingi kwamba Polisi tunawaondoa kwenye jukumu hili la kuendesha mashtaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi kwanza sio kazi yao ni kazi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*). Miaka ya nyuma sijui ilitokeaje wakapewa Polisi ikazoeleka kwamba ni moja ya kazi za Polisi, lakini kusema kweli sasa tunarudi kwenye misingi, hii sio kazi ya Jeshi la Polisi, tunajiondoa. Lakini wenzetu wametuumba hasa Ofisi ya *DPP* kwamba msijiondoe haraka lazima apate muda, apate na yeye ma-*PP* wa kutosha nchi nzima, apate vitendea kazi, anataka muda wa kufanya maandalizi. Kwa hiyo, tuko kwenye mpito ya kuwaondoa Polisi katika suala hilo *DPP* akishakuwa tayari hata kesho sisi tunaondoka kwa sababu Polisi tumewapa kazi nyingine nyingi ambazo sio zao sasa tunaondoa moja ni hii ya uendesha mashtaka, tunawaondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko nyingine ile ya kuwatoa Gerezani mahabusu na kuwapeleka kwenye Mahakama na kuwarudisha Gerezani kwa kutumia makarandinga. Huduma ya makarandinga inafanywa na Polisi, nayo vile vile tunawaondoa itafanywa na Jeshi la Magereza. Kwa hiyo, bajeti ya mwakani tunataka Jeshi la Magereza waseme wanataka vifaa gani, tuwaongezee askari wangapi wa kufanya kazi hiyo ili jukumu hili vile vile tuliondoe kwa upande wa Polisi kwa sababu tumekuja kuona kwamba tumewapa Jeshi la Polisi kazi nyingi mno na nyingine ambazo haziwahusu. Kwa hiyo, wao watabaki na zile *core functions* za Jeshi la Polisi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai na wote mlizungumzia jambo hili, tuko njiani kuwaondoa Polisi kwenye *prosecution*, wenyewe watakamata wahalifu, habari ya kuendesha kesi Mahakamani itakuwa ni shughuli itakayofanywa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu linahusu haki za binadamu kwenye Magereza. Ni kweli Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilitembelea Magereza, ikatuletea ripoti yake. Kimsingi tunakubaliana na yale yote ambayo Tume iliyaona. Matatizo yalikuwa mengi ya msongamano, mitondoo, ya huduma za Magereza na kadhalika. Matatizo hayo yalitokea kwa sababu huko nyuma fedha za kuendesha Magereza kusema kweli na Majeshi yote zilikuwa zinatoka zile za mshahara tu lakini za mambo mengine haya ya kuendeleza Majeshi zilikuwa hazitoki kwa miaka kumi. Kwa hiyo, matatizo haya yakarundikana katika Majeshi yetu yote sio Magereza tu hata Polisi na kwingineko. Sasa maadamu katika miaka hii kuanzia mwaka 2002, 2003 na mwaka 2004 Waheshimiwa Wabunge mmeshaanza kutupatia fedha za kufanya kazi za maendeleo, tutaanza kubadilisha mambo huko.

Sasa hivi kwenye Magereza tunafanya mabadiliko makubwa sana. Habari ya mitondoo, wanajisaidia kwenye ndoo, kesho asubuhi wachukue, wakamwage nje, ni kweli ni suala la fedheha, sio haki, sio ubinadamu. Sasa hivi tunayo programu ya *ku-phase out* jambo hili. Tunafanya ukarabati katika Magereza yetu yote na jambo moja ambalo tunalifanyia ukarabati ni kuwa na vyoo vya kutumia maji yaani vya *ku-flash* ili kuondokana kabisa na suala la mitondoo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi chakula Magerezani tumeboresha, ni safi kabisa, wanapata lishe ya kutosha, kila kinachohitajika mtu apate kama ni matunda, nyama, wanga, mboga za majani sasa hivi wanapata vizuri. Mwaka 2003 tulitumia bilioni 9 kulisha Magereza tu. Kwa hiyo, kwa kweli tumeshaondokana na utaratibu wa zamani ambapo ukishafungwa wewe mwaka mzima unakula dona na maharagwe ambayo hayakuungwa, hapo tumeshaondoka. Sasa hivi wanakula na wali, mboga iliyo na mafuta, *diet* ni nzuri kwa sababu sasa fedha tunazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matibabu sasa hivi yamekuwa mazuri sana katika Magereza. Kila Gereza tunayo *Dispensary*, wanapata dawa kama kawaida hata baadhi ya raia walio nje, jirani na Magereza vile vile wanapata dawa katika Zahanati zile. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sare, tumezoea wafungwa wanavaa vikaptura na vishati nya mikono mifupi, kaki nyeupe. Ndio sare tuliyorithi wakati wa mkoloni, tumeendelea nayo lakini tumekuja kuona kwamba nayo vile vile inadhalilisha. Mtanzania huyu, mtu na heshima zake amefungwa sasa unakwenda kumvisha kaptura. Kama nilivyoleza juzi sasa hivi sare tunabadilisha watakuwa sasa wanavaa suruali na shati la mikono mirefu, imeshonwa kwa mtindo wa kaunda suti na viatu japo hatutakuwa na viatu vizuri lakini hata makubazi tu ya kumsitiri miguu yake maana zamani walikuwa wanapekua, watakuwa na viatu, huyu ni Mtanzania ambaye vile vile ana haki zake za binadamu. Rangi tunabadilisha ile rangi nyeupe tunaondoa sasa rangi za sare zao zitakuwa ni machungwa (*orange*).

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika Magereza sasa hivi tunawapa uhuru wa kupata habari. Sasa wanapata magazeti, sasa kila Gereza tunaweka redio ili waweze kusikiliza taarifa za habari na sasa hivi tumeanzisha programu ya kupeleka *television* katika Magereza ili waweze kupata habari mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tumeruhusu kusoma, mfungwa anaweza kujiunga na *Open University* akasoma akiwa Gerezani. Sasa hivi tumeshafufua kile Chuo cha Ufundı pale kwenye Gereza la Mbeya tunawapeleka wanasoma, wanapata vyeti nya *VETA* ili hata akimaliza kifungo chake anaweza kujiajiri mwenyewe. Yote haya ni mabadiliko makubwa kabisa katika Jeshi la Magereza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na moja la Sungusungu.

Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alisema hapa mna kitu kinaitwa Sungusungu hakitambuliwi katika sheria, kinafanya mambo kienyeji, sheria iletwe.

Sasa usahihi ni kwamba Sungusungu inafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Tunayo *Act 9* ya mwaka 1989, hii ni *act* ambayo *people's military* (mgambo), Sungusungu, inawapa na *powers* ya kukamata na kupeleka kwenye vyombo nya Polisi, inawapa na haki kama wakiwa katika shughuli ambazo wametumwa rasmi watapata fidia, kwa hiyo, sheria ipo.

Sasa kama mnataka tuiboreshe kwa sababu hakuna sheria ambayo ni *static*, ni jambo lingine lakini Sungusungu wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, sio kweli kwamba ni watu tu ambao wanafanya kazi kienyeji, sheria haiwatambui, madaraka yao hayatambuliwi, mipaka yao haipo hata kidogo, sheria hii inawapa madaraka, mipaka na vile vile inawapa haki zao wanapokuwa kazini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nichangie hayo, nakushukuru tena na naunga mkono hoja iliyo mbele yetu. (*Makofî*)

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, *Assalaam alaikum?*

WABUNGE FULANI: *Waalaikum salaam.*

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii adhuhuri hii ili niweze kusema machache kwa maana ya kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, ilio mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kufanya hivyo, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetete Mbalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini aliyefariki tarehe 24 Juni, 2004 tukiwa hapa Bungeni. Nasema kwa masikitiko sana kwa sababu marehemu nilifanya naye kazi sana katika miaka ya 1980 mpaka mwanzoni mwa miaka ya 1990 pamoja na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati ule mimi nikiwa mshauri wa sheria katika Wizara ya Nishati na Madini. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii na kama nilivyosema naiunga mkono asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitafanya mafupi kwa lengo la kupalilia njia ya mtoho hoja Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba. Nitajielekeza katika yale ambayo yana sura kidogo ya kisheria sheria na yeze nitamwachia yale yenye sura ya kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa ufanuzi alioutoa sasa hivi. Hiyo ndio azma ya Serikali katika maeneo yote aliyoagusia nitayagusia kidogo katika maelezo yangu kwa lugha yangu lakini huo ndio mwelekeo wa Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili swali liloulizwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kuhusiana na tafsiri sahihi ya amri halali ya Mkuu wa Wilaya ni ipi?

Napenda niseme amri halali ni amri ambayo inatolewa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Kwa msingi huu, mipaka ya mamlaka zote imeainishwa katika sheria na kanuni na kanuni hizo huwa zinawekewa pia taratibu zake. Hivyo amri halali hutolewa na mamlaka hizi kwa kuzingatia mipaka iliyowekwa na sheria. Hilo sidhani kama lina utata na naomba tu tuelewana kwa maana hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja unaweza kuiona ni ya mzaha mzaha kidogo lakini Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, wakati akichangia alisema marekebisho ya Katiba yanayopendekezwa na Serikali ni vyema yakalenga katika maeneo ambayo yanalamikiwa na wananchi, hakuyataja lakini akaendelea kusema Serikali isipofanya hivyo yaani ninyi ambaa mmeingizwa hapa na Serikali kupitia Chama cha Mapinduzi ndio mtakaoumizwa na sheria hizo, alisema maneno kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niliambie Bunge lako Tukufu kwamba Serikali haitungi sheria za kuwagandamiza wananchi wala Vyama vyta Upinzani. Sheria

za nchi yetu zinazingatia misingi ya haki na ninaamini inshallah Mwenyezi Mungu atakapowezesha Kambi ya Upinzani kuongoza nchi hii...

MBUNGE FULANI: Haiwezekani.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Watazikuta sheria hizi na watazitumia vizuri na sio kwa lengo la kutisha viongozi kwamba ninyi ndio mtazitumia sheria hizi kuwagandamiza, ni vyema tukaelewana na hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ifanyiwe marekebisho ili kuwezesha Serikali ya mseto, ya umoja Zanzibar. Jamani, mimi nawaachieni. Wanaoamua pawe na ushirikiano, pasiwepo na ushirikiano ni Vyama vile ambavyo vimeshiriki katika Uchaguzi Mkuu na matokeo yalivyotokea huwezi kulazimisha. Ndio maana Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaliweka tu hili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba yawezekana tukafika hapo, fursa hiyo ipo. Sasa kwa Zanzibar mimi siwezi kusemea masuala ya Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo hayamo katika masuala ya muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Mheshimiwa Dr. William Shija, viongozi hawa wanachaguliwa na wananchi ni vizuri basi katika kesi za uchaguzi Jaji mmoja asikae na kuengua. Ni hoja nzuri, tumeisikia, tutaifanyia kazi. Niseme tu kwamba ni kama mnavyotushauri kila wakati hapa kuhusiana na kesi zinazohusu Katiba ndio utaratibu uko hapo kesi yoyote inayogusa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania lazima isikilizwe na jopo la Majaji watatu. Sasa mnasema mnawachukua Majaji watatu, inachukua muda kuwapata, wanaoacha shughuli nyingine zile lakini ndio hivyo. Sasa hili acha tulichukue kama itaonekana kwamba kuna busara ya kuchukua utaratibu huo unaofanana na mtu anayehoji Katiba au sheria inayohojiwa kwamba vifungu fulani vinakinzana na Katiba basi acha tukalifanyie kazi tuone kama tutalifika nalo mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa aligusia Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo kama alivyo sema ni sahihi kabisa, Ibara hiyo ndio inayoipatia Serikali ya Jamhuri ya Muungano madaraka na mamlaka yake yote yaani yanatoka kwa wananchi, mamlaka yote na madaraka yote ya Serikali uhalali wake ni wananchi wenyewe, sawa kabisa.

Lakini Katiba hiyo hiyo na kifungu hicho hicho kinasema kwa mujibu wa Katiba hii. Sasa Katiba ya Jamhuri ya Muungano imegawa madaraka yale ya Bunge, Serikali na Mahakama. Kwa upande wa Serikali Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Rais Mtendaji (*Executive President*) na Serikali yake inatokana na Wabunge waliochaguliwa na wananchi waliomo humu Bungeni kumsaidia katika kuendesha Serikali yake. Kwa hiyo, lazima tulielewe hilo unaposema mamlaka yanatokana na wananchi ndio maana hiyo na Rais ni sehemu ya Bunge hili huwezi ukajiona kwamba mimi ndio Mbunge uhalali wangu na uwakilishi wangu ni huo tu kwamba Serikali yenyewe haipaswi kuyafanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ya mikataba ambayo yametajwa katika Ibara ya 63(2)(a) ni mikataba ya Kimataifa ambayo Serikali ya Jamhuri ya Muungano kama nchi inaingia na nchi nyingine au na taasisi za Kimataifa. Hiyo ndio inayoongelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongelea kuridhia maana ya kuridhia ndio hiyo kwamba hatua ya kwanza lazima iwe hati hiyo imepata saini, huwezi ukaliomba Bunge liridhie kitu ambacho Serikali hajaweka saini. Sasa anakuja na pendekozero kwamba iende kwenye Kamati. Sasa masuala ya biashara ndio kazi ya Serikali, mikataba ya biashara ni kazi ya Serikali. Sasa pale ambapo inaonekana wazi kwamba mkataba fulani Serikali ilitetereka ndio kazi ya Bunge hili kuihoji na kuishauri Serikali. Lakini mkianza kusema kwamba kama anavyopendekeza kuingia jikoni mambo yanapoharibika utakuja kuhoji nini?

Kwa hiyo, naomba hilo tulielewa kuna hiyo dhana ambayo ni ya wazi kabisa kwamba lazima kwanza mkataba usainiwe na tunapoongelea kifungu hicho alichokitaja cha 63 kinahusu mikataba ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aligusia adhabu ya kifo, mimi nitasema tu mawili. Adhabu ya kifo kwa *statement* yake aliyotoa Bungeni anasema adhabu hiyo inaenda kinyume na haki za binadamu. Mimi sikubaliani na hilo maana haki za binadamu kwa mujibu wa Katiba wa Jamhuri ya Muungano ni zile ambazo zimeainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kama tunavyooleza kila wakati ukizisoma kwa makini na ndio maana tumekataa kabisa wazo la kusema kwamba tuingize katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwenye eneo la haki za binadamu yale yote yaliyomo katika tangazo la dunia kuhusu haki za binadamu na hakuna nchi duniani iliyofanya namna hiyo. Sisi tunasema haki ambazo tunazitambua ni zile ambazo zimo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano sasa haki ya kuishi imetajwa. Sasa nauliza anaposema haki ya kuishi ilindwe, mtu asinyongwe sasa yeze anaiona upande mmoja tu wa sarafu yule aliyeuawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunasema hivi suala hili linazungumzika lakini hatuwezi kuja humu Bungeni kwa ujanja ujanja na lugha nyepesi nyepesi na kusema kwamba Serikali ilete mapendekozero ya kufuta adhabu hiyo, hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyo sema yeze mamlaka na madaraka ya Serikali yanatoka kwa wananchi sasa sisi tunapendekozero kama ilivyo na maamuzi mazito yanayohusu sera ya nchi yetu yaende kwa wananchi. Kama nilivyokumbusha mwaka jana wakati najibu swali humu Bungeni tulishasema tumeshawahi kuifanya hivi. Tume ya Kurekebisha Sheria miaka saba iliyopita tuliiomba ifanye kazi hiyo. Imepita nchi nzima kupata maoni ya wananchi kuhusu adhabu ya kifo na wananchi walio wengi wakati huo walisema iendelee kuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la Sungusungu, nashukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani amenisaidia, sheria ipo. Lakini walisema iundwe Tume kufanya uchunguzi. Nchi yetu ina Sheria hii ya *Inquest* tuliiufuta Sheria ya *The Inquest Proceedings Ordinance* ambayo imekuwa na sisi tangu wakati wa Ukoloni Bunge likatunga Sheria ya *Inquest* nadhani ya mwaka 1980. Lakini Serikali haionti msingi

wa hoja iliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwenye eneo hili la kutaka uchunguzi wa vifo ufanywe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hilo kwa sababu Sheria ya *Inquest* inaweka utaratibu wa nini kifanyike na lini kifanyike. Sheria hiyo inatamka wazi kabisa ni pale ambapo kuna utata kuhusiana na mazingira ya tukio la mauaji. Hasa katika haya aliyoyasema hatuamini kwamba kuna sababu ya kuunda Tume ya Uchunguzi kwa vifo vinavyofanywa na Sungusungu lakini tunakubaliana na yeze na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba Sungusungu pamoja na Polisi lazima wazingatie sheria, kanuni na haki za binadamu na sio kufanya kazi na majukumu yao kwa mapenzi yao. Hilo ni la wazi na tungependa sana lizingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ni muhimu kwa watendaji wote wa Serikali za Vijiji, Kata, Tarafa na kadhalika kusimamia, kulinda na kutekeleza sheria za nchi kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Hayo nimeona niyazungumzie kwa sababu ni msingi imara sana katika utawala bora na hasa *component* hiyo ya utawala wa sheria na pia utawala bora kwa maana ya kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwanza namshukuru sana. Ameongea kwa uchungu sana kuhusiana na akinamama kuhusishwa na kesi za mauaji baada ya waume zao kutoroka, ametusaidia sana ametupatia na kesi Na. 3 ya mwaka 2004. Nasema hivi kama ni kweli aliyoyasema Mheshimiwa Henry Shekiffu na mimi sina sababu ya kutomwamini kiongozi.

Nataka niseme hivi kitendo hicho ni kinyume kabisa na sheria za nchi yetu, ni ukiukwaji wa haki za binadamu na ni ulevi wa madaraka wa hali ya juu ambao lazima uchunguzwe mara moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ndio kwanza malalamiko haya yametufikia, tayari nimewaagiza wasaidizi wangu wafuatilie malalamiko haya mara moja ili hatma ya akinamama hao ijulikane mapema iwezekanavyo na ikibidi tukiwa hapa Bungeni.

Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Henry Shekiffu, kwamba malalamiko kuhusiana na akinamama hao yatapewa ufumbuzi kama nilivyo sema, labda naamini siku saba kuanzia sasa. Tunamshukuru sana. Tunaomba radhi kwa wale walioguswa na yote haya lakini tutajitahidi kupunguza makali kwa yote waliyoyapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ameligusia vizuri sana Mheshimiwa Kepteni John Chiligati suala la uchunguzi na *prosecution* kwamba ni vizuri sasa tukatofautisha majukumu haya. Niliseme hili limekuwepo tangu taarifa ya Mheshimiwa Pius Msekwa ya mwaka 1977. Limekuja kurudiwa kwa nguvu sana katika taarifa ya hivi karibuni ya Jaji Bomani na tunalifanya kazi, uamuzi wa Serikali ni wazi kwa sababu ni vema tukalifanya. Kama mtakavyoona katika mwaka huu wa fedha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imepanga kuajiri Mawakili wengi na kuwapa mafunzo ili waweze kuendesha mashtaka chini ya mfumo mpya ambao unaandaliwa. Kutokana na umuhimu wake

mpango huu utatekelezwa mapema lakini tutaufanya hatua kwa hatua kwa kutegemea upatikanaji wa raslimali.

Waendesha Mashtaka waliopo sasa na ambao wanafaa kuendelea katika mfumo mpya watapewa uhuru ama wa kuijunga na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na kuacha kazi ya Jeshi la Polisi au kubaki kwenye Jeshi hilo na kufanya kazi ya upelelezi tu. Huo ndio mwelekeo wa Serikali katika eneo hili. Tunao ma-*DPP* wazuri tu, lakini huwezi kumlazimisha mtu kwamba katika utaratibu huu sasa uje huku, hiari ya moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu watuhumiwa kubambikizwa kesi. Hata mimi lazima nikiri kwamba, ofisi yetu inapokea malalamiko mengi sana kuhusiana na eneo hili. Kesi nyingi ambazo tunafuutilia tunakuta kweli wananchi wameonewa. Sisi tunaendelea kuipongeza Polisi kwa kazi nzuri inayofanya katika mazingira magumu lakini tufike mahali kero kama hizi tuzipunguze kama siyo kuziondoa kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na *Home Affairs*, pale wanapobainika watu wa namna hii hatuwalazii damu hata kidogo, tunawachangamkia na tutaendelea kuhangaika nao pale wanapobainika. Lakini mlinisikia majuzi nikijibu swali kwa niaba ya Waziri wa Sheria kwenye eneo hili.

Nadhani sasa tufike mahali tuiangalie upya Sheria inayosimamia Mwenendo wa Makosa ya Jinai (*Criminal Procedure Act*) kwenye eneo hili. Ni vizuri tulitafakari sote hapa na ninyi Waheshimiwa Wabunge mnawenza kutusaidia. Lakini tunachosema kwa makosa mazito ambayo hayana dhamana kama mauaji na kukutwa na madawa ya kulevyta na makosa mengine ukiondoa kosa la uhaini, tunapendekeza tuweke muda kwamba kazi ya Polisi wafanye uchunguzi wao kwa sababu ndio kazi yao wana majukumu sita chini ya Sheria ya Polisi, lakini kubwa ni hilo la kufanya uchunguzi kwa makosa ambayo yanatuhumiwa kutokea. Tutapendekeza ni kipindi gani, lakini nasema ndani ya kipindi hicho, Ofisi ya Msimamizi wa Makosa ya Jinai nchi nzima wawe wanatoa taarifa kwa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maana ya *DPPs office* na siyo kutuambia tu kwamba uchunguzi unaendelea lakini itabidi watueleze ni nini kinachoendelea katika hatua hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tukiridhika kweli hatua na jitihada nzuri zinaendelea lakini tuweke ukomo kama baada ya miezi sita hakuna uchunguzi uliokamilika basi *DPP* atatumia mamlaka yake na kuifuta hiyo kesi ili wahusika waachiwe huru, lakini Polisi waendelee na kazi yao ya kufanya uchunguzi. Wakipata ushahidi unaothibiti, sheria inaruhusu sasa kumkamata mara moja, *stage* hiyo ni kumpeleka Mahakamani na kesi kuanza kusikilizwa. Narudia, hawa wenye mchezo huu wa rafu kuchezea haki za binadamu wenzao ni watu wabaya na siwaonei huruma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimegusia yale ambayo muhimu yaliyosemewa kwa nguvu sana na Waheshimiwa Wabunge na niseme tumewashukuru sana kwa hayo walijotusaidia na waendelee kutusaidia kwa sababu wanapotoa ushauri na mara nyingine hata wanapotoa kwa nguvu, tunaamini wanatuimarisha kwa sababu nia

yetu na lengo letu ni moja, kuwatumikia wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, namheshimu sana lakini mambo mengine unafahamu ukifika katika ngazi ya uongozi hii hupendi kufanya mizaha mizaha. Sasa mimi nimemsikiliza sana asubuhi, viongozi aliokuwa anawataja kwenye Vijiji vile ambavyo viro katika *statement* yake Manyata, mimi nawafahamu na nilibahatika tu hata wakati ule hili *group* la wazee hawa kutoka huko walikuja hapa Dodoma na kutoa ukweli kwamba Waziri Mkuu wetu, walisema wazi kwamba hana shamba. Sasa hawa ni wananchi, wamekuja hapa kusema, jamani tunasikia *story* gani hii, lakini kwa sababu amelleta, mimi nasema tunapokuwa humu Bungeni, nilitaka kusimama pale lakini nikasema basi mara nyingine unamezea tu haya masuala, lakini mimi inanisumbua sana unapokuja na *sweeping statements* ambazo kusema ukweli hazina, lakini mimi huwa najiuliza kuwa hivi mimi Andrew John Chenge, kuwa na shamba ni dhambi au nkipata shamba nimelipata kwa njia ya rushwa? (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Hapana.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Watu wanahangaika sana usiku na mchana kuangalia maslahi yao na ya watoto wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunachokataza kwa maadili na sheria za nchi hii ni kutumia nafasi yako kujineemesha wewe na familia yako na wajomba zako na wote wale, lakini kwenda kuhangaika kuomba kwa taratibu za Kiserikali katika Kijiji, mfano, Kibaigwa, wakakubali wakasema bwana Chenge tutakupa shamba hili, kuna ubaya gani, dhambi iko wapi? Nawaomba Waheshimiwa Wabunge hasa sisi viongozi tuonyeshe njia, tusiwe malofa, lazima tufanye kazi na moja ya kiongozi mzuri ni kuwa na shamba la mfano, wakifika pale wanaona kweli huyu anaonyesha njia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema itapendeza kama Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, atakwenda kwenye Kijiji kile akaonyeshe lile shamba liko wapi. Ni vizuri kwa sababu *you know* huyu ni Waziri Mkuu wetu. Inatusumbua sana baadhi yetu kuona anatupiwa madongo tu, madongo tu. Lakini nimeona niliseme hilo kwa sababu nilitaka kusimama kuulizia utaratibu, lakini nikaona niliache hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena sana kwa kunipa nafasi hii na nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja hii mia kwa mia na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hotuba yangu.

Kwanza kujibu hoja mbalimbali kutokana na michango ambayo imetolewa na Waheshimiwa Wabunge na ningependa nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kutoka Chama Tawala na Vyama vyta Upinzani kwa jinsi walivyopokea hotuba yangu. Kwa hiyo, napenda niwashukuru kwa hilo na sisi kwa kweli tumepokea

kwa upande mwingine shukrani zao pamoja na pongezi zao kwa mikono miwili. Maelekezo yenu na maoni yenu tumeyazingatia na tungependa kuahidi kwamba tutayafanya kazi katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichukue fursa hii kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa namna ya pekee kwa jinsi walivyotoa maoni yao na kwa jinsi Mheshimiwa Jenista Mhagama aliviyowasilisha maoni yao siku ya leo. Maoni hayo pia tumeyapokea na tutayafanya kazi. Hali kadhalika nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kwa upande wa Upinzani kwa maoni yao, nasema sisi tumeyasikia na tumeyapokea na tutayafanya kazi. Baadhi ya majibu nitayatoa baadaye lakini mengi yamekwishajibiwa na *Attorney General*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, kwa majibu aliyotoa kutokana na maelezo au maoni hasa ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, asubuhi ya leo.

Mwisho ningependa nimshukuru Mheshimiwa *Attorney General* kwanza kwa maelezo yake fasaha katika kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge na pia nimshukuru kwa kuunga mkono hoja yangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nichukue nafasi hii ya kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia maoni yao kwa kuzungumza humu Bungeni, nao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mheshimiwa Kepteni John Chiligati na Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tumeyapokea maoni yote hayo na naahidi kwamba tutayafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi ni arobaini na tatu, nao ni, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Tatú Ntimizi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Rhoda Kahatano.

Wengine ni Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ali Sheha Mussa, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Juma Khamis, Mheshimiwa Jumanne

Nguli, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Joseph Mungai, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Diana Chilolo na Mheshimiwa Remidius Kissassi. Hao pia tunawashukuru sana kwa michango ambayo wameitoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo na ili kuokoa muda ningependa kwanza kuzungumzia masuala ambayo yamejitokeza wakati Mwenyekiti wa Kamati hii akitoa maoni yake kwa niaba ya Kamati hiyo na kwa mara nyingine ningependa niwashukuru sana kwa mapendekezo yao mazuri na ya kina. Yote haya yatatusaidia katika kuboresha shughuli zetu za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwepo suala la Mahakimu wa Wilaya na Mahakama ya Mwanzo kukopeshwa pikipiki. Hili ni suala ambalo tumekuwa tukilifuatilia kwa muda mrefu na kwa mwaka huu wa fedha tutajitahidi kuzungumza na wakala mbalimbali pamoja na Wizara ya Fedha ili kuona kama tunaweza kuwapatia pikipiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango endelevu wa Chuo cha Lushoto. Majadiliano yanaendelea kama nilivyosema asubuhi ya leo kati ya Idara ya Mahakama na NSSF ili kupanua Chuo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa wahitimu wote wa Chuo cha Lushoto. Niseme tu Serikali imekuwa ikiwaajiri wahitimu wa Chuo cha Lushoto. Hata hivyo sifa za kuajiriwa kuwa Hakimu zinazingatia pia maadili na tabia ya mwajiriwa kwa ujumla. Hapa ningependa nimnukuu Mwalimu ambaye aliwahi kusema kwamba: “kuna kazi ambazo zinaweza kufanywa na kila mtu lakini Uhakimu siyo moja ya kazi hizo.”

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni msongamano wa mahabusu, nadhani Mheshimiwa AG amelizungumza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukarabati wa Wilaya na Mahakama za Mwanzo nimezungumza asubuhi ya leo katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna masuala ambayo yamezungumziwa na Kambi ya Upinzani. Moja, ni kutozingatiwa kwa Sheria Na. 7 na Na. 8 za Mwaka 1982 wakidai kwamba uwepo uwazi na kuhakikisha unazingatiwa. Ningependa tu kusema kwamba Wizara kuititia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora itawasiliana na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, kuhusu Kijiji hicho cha Mangaka, Wilaya ya Masasi ili kupata undani wa malalamiko hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilizungumziwa kwenye Kambi ya Upinzani ni kasi ndogo ya utendaji wa kazi wa Tume ya Haki za Binadamu kutokana na upungufu wa fedha na watumishi. Hii ni sahihi, lakini kwa sasa hivi hatua zimekwishachukuliwa ili kuweza kuwaajiri wafanyakazi 123 na kuajiriwa wengine 103 hapo baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo lilizungumziwa na Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa ni *Quick Start Project* sio tu kwamba ni *late start* bali ni *non starter*. Niseme malengo ya mradi wa *Quick Start* ni kama nilivyoainisha katika aya ya 32 na 34 ya hotuba na itakumbukwa kwamba mradi huu ulibuniwa ili kuainisha majukumu ya wadau kwa kufanya tafiti, kuandaa mpango wa kuboresha haki za watoto watukutu na majaribio katika Mikoa ya Arusha na Manyara. Napenda kueleza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi walijulishwa kinachoendelea, si sahihi kwamba hawakushirikishwa na mimi mwenyewe nimetembelea katika Mikoa hiyo miwili ya Manyara pamoja na Arusha. Nimekutana na viongozi katika Wilaya na tumezungumzia masuala haya, kwa hiyo nimejionea mimi mwenyewe kwa kweli kiasi ambacho wananchi wameshirikishwa katika suala hili la mradi wa *Quick Start*. Lakini ni kweli pengine taarifa hazijatolewa mahsus kuhusu michango ambayo wananchi wameifanya.

Kwa hiyo, tumemwagiza *coordinator* wetu mama Mdundo kwenye tarehe 28 Julai, 2004 aende Karatu kuweza kukutana na uongozi ikiwa ni viongozi wa Halmashauri pamoja na *DC* na wengine kuweza kulizungumzia suala hili na tukiri kwamba michango kweli ni mikubwa, kwa upande wa Mkoa wa Arusha michango imefikia shilingi milioni 27 na upande wa Mkoa wa Manyara shilingi milioni 120. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wa Mikoa hiyo kwa kuitikia wito wa Serikali kujihusisha na mradi huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni *Juvenile Justice*, watoto kufungwa pamoja na wakubwa. Hili ni tatizo ambalo nadhani Mheshimiwa Kepteni John Chiligati, amelizungumza, tunalo tatizo lakini tutajitahidi kuweza kulitatua. Nadhani haya ndiyo yalikuwa masuala makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilikuwa ni uhaba wa Majaji. Hili ni tatizo ambalo tunalo, lakini kwa sasa hivi hata tukiteua Majaji wengi tatizo ni uhaba wa maofisi na *Court Rooms*. Kwa hiyo, masuala haya lazima kwa kweli yaende sambamba, lakini tumelipokea suala hilo na tatalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na michango mingi kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Abdula Lutavi, wameongelea kuhusu ukiukwaji wa maadili ya kazi kwa misingi ya rushwa Mahakamani. Hili ni suala ambalo tunalifahamu na zipo taratibu za kuweza kuwachukulia hatua wale wafanyakazi wote na Mahakimu ikiwa ni pamoja na Majaji ambao wanakiuka taratibu hizo.

Kwa hiyo, nasema tumelipokea, lakini tungeomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kushirikiana na Bodi za Mahakama kama kuna watu ambao wanakiuka maadili hayo, basi kuweza kuwasiliana na uongozi wa Mkoa au Wilaya ili hatua za kinidhamu ziweze kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwasilisha mambo kama hayo kwenye Wizara yenyewe ya Sheria na Mambo ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Jacob Shibili na Mheshimiwa Ruth Msafiri, wao wamezungumzia tatizo la usafiri. Tunasema hili ni tatizo ambalo tunalifahamu, lakini tumeanza kulishughulikia katika kipindi cha mwaka 2003/2004, kwa kununua magari 25 na katika kipindi cha mwaka 2004/2005, tunatarajia kununua magari mengine 30 ili kuweza kuwapa usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Philip Magani, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa John Singo, Mheshimiwa Musa Lupatu, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Jumanne Nguli, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, wamezungumzia upungufu wa Mahakama, uchakavu wa majengo na ujenzi wa Mahakama mpya. Suala hili nasema tunalipokea na tumelizungumzia kwa kina katika hotuba na tumewapa *inception report* ambayo inaonyesha maeneo ambayo yanahitaji Mahakama hizo kufanyiwa ukarabati ama kufanyiwa upanuzi ama kubomolewa kabisa na kujengwa kwa Mahakama mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Phillip Magani, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Paul Ntwina, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Ruth Msafiri na Mheshimiwa George Mlawa, wamezungumzia upungufu wa Majaji na Mahakimu. Hilo nasema pia tumelipokea. Tatizo ni kwamba, ikama yetu imekuwa ni ndogo. Sasa hivi tunawasiliana na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri ambaye anashughulikia masuala ya Menejimenti ya Utumishi ili kuona kwamba ikama hii inakuwa ni kubwa zaidi. Kwa hiyo, tunaweza kuajiri Mahakimu wengi zaidi na wafanyakazi ikiwa ni pamoja na Makarani kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mrundikano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Hili ni suala ambalo tunalifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ucheleweshaji wa kesi. Ni suala ambalo tunalifahamu na kama tulivyozungumza asubuhi ya leo, tunaunda Kamati ya Kusukuma Kesi Kitaifa ambayo itakuwa na viongozi wa juu ili kuweza kufuatilia masuala haya katika ngazi ya Mkoa na ngazi ya Wilaya ikiwa ni pamoja na mbinu nyingine kama utaratibu wa *ADR* na kuwaongezea vitendea kazi na kadhalika.

Kuhusu sheria ya UKIMWI hili limezungumziwa na kwa kweli tuko mbioni kulishughulikia suala hilo kuweza kuandaa sheria ambayo itaendana na tatizo hilo.

Kuhusu mpango endelevu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama tumeshalizungumzia. Uhamisho wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni kweli tuna tatizo hilo, lakini kitu kinachogomba hapa ni gharama kubwa ya kuwahamisha Mahakimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wazee wa Baraza malipo na uteuzi, hili suala tumekwifanyia kazi, tuliongeza viwango vya posho kutoka shilingi 200/= hadi shilingi 1,500/= kwa kesi ambazo wanazisikiliza na kuzikamilisha, nadhani wazee wamelifurahia suala hili. Lakini kuhusu mambo ya uteuzi watakuwa pale kwa muda gani, wawe na umri wa miaka mingapi, masuala haya tunayatizama upya ili kuandaa *regulations* mpya kuhusu masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya mirathi hili pia tumekuwa tukilijibu humu Bungeni jinsi Wizara ya Fedha inavyolishughulikia suala hili. Lakini litashughulikiwa vizuri zaidi katika ile *Whiter Paper*, Waraka Maalum ambao utaangalia sheria ya Ndoa, Watoto pamoja na Mirathi. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge mvute subira.

Kuhusu usikilizaji wa kesi kwa faragha, huu ni utaratibu ambao tunaona unahu su watoto wenye umri mdogo. Kwa hiyo, mashauri yao husikilizwa katika *chambers* na pia masuala ya ubakaji haya pia kisheria na kiutaratibu katika Mahakama zetu yanatakiwa masuala haya yasikilizwe katika *chambers*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tafsiri ya sheria kuwa katika Kiswahili hili nasema tumelipokea, ni suala muhimu tunalifanyia kazi, tumekwifatafsiri baadhi ya sheria zetu na tunaendelea kufanya hivyo kwa kuimarisha kitengo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upungufu wa Mawakili Serikalini ni kweli upo upungufu wa Mawakili na Wizara inachukua hatua za kupunguza upungufu huo kwa kuajiri Mawakili wapya kila tunapopata kibali na kwa sasa hivi tumeboresha maslahi ya Mawakili, ni mategemeo yetu kwamba wataendelea kuwa na sisi katika Wizara na katika Taasisi zingine ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la adhabu ya kifo hili limezungumziwa na *Attorney General*, Mheshimiwa Andrew Chenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo masuala ambayo nimeona kwamba ni muhimu yaliyozungumziwa asubuhi ya leo. Kama nitakuwa nimeacha majina mengine ya Waheshimiwa Wabunge basi mtaniwia radhi. Lakini kwa hayo ambayo mnaona kwamba pengine tungeyatoa majibu tutakuwa tayari kuweza kupokea hoja zenu na sisi kuweza kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa mara nyingine nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kuweza kufanya majumuisho haya na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa mara nyingine kwa michango yao mizuri na ninaahidi kwamba michango yote hiyo tumeipokea na tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 40 - Mahakama

Kifungu 1001- *Administration and General* 3,501,545,300/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe hii ni Idara ya Mahakama.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. *Vote 40* ambayo inahusu Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilieleza matatizo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na nikatoa ushauri kwamba Vyuo vingine vingeruhusiwa kuweza kutoa mafunzo kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kuweza kuona namna ya kupunguza huu wingi wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanaotakiwa.

Pia nikashauri kwamba watu binafsi nao waruhusiwe kuweza kuanzisha Vyuo kama tumeruhusu sasa hivi hata Mashirika kuanzisha Vyuo Vikuu. Ni kwa nini Vyuo vya Mahakimu wasiruhusiwe wale wenye sifa na wenye ujuzi ili waweze kuanzisha Vyuo vya Mahakama za Mwanzo? Nataka maelezo hayo.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na nakubaliana na yeche kwenye kwamba ingekuwa ni vizuri tukawa na Chuo zaidi ya kimoja na nikiwa ni Muislam tena mzuri tu tunaruhusiwa kuoa mpaka wanawake wanen. Kwa hiyo, mimi naafiki kabisa kwamba ingekuwa ni vizuri tukawa na Vyuo zaidi ya kimoja, lakini la msingi ni uwezo wetu wa kuweza kuwa na Vyuo zaidi ya kimoja ni mdogo. Kwa hiyo, hiki Chuo ambacho tunacho sasa hivi pia tuna matatizo nacho, Bajeti haitoshi na bado tuko katika harakati za kutafuta mikopo ya aina mbalimbali na ruzuku kutoka Serikalini ili kuweza kukiendesha Chuo cha Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watu binafsi kuanzisha Chuo kama hiki, mimi nadhani hakuna matatizo yoyote, tungeweza kupata maoni ama maombi kutoka kwa watu ambao wana *interest* za namna hiyo tukaweza kuyafikiria.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na vyuo anavyovitegemea kuvianzisha kwa jinsi alivyovielewa yeche, lakini nataka kuzungumzia vyuo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utaratibu, ningetegemea pengine Wizara au Mheshimiwa Waziri mwenyewe awasilishe basi utaratibu wa namna ya kuanzisha vyuo binafsi kwa ajili ya Mahakimu wa Mahakama wa Mwanzo. Ndiyo hilo tu.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwamba mimi sina matatizo. Tatizo langu kubwa sasa hivi ni kutosheleza mahitaji ya Chuo ambacho tunacho sasa hivi cha Lushoto. Sasa nitakuwaje na utaratibu mwengine. Kama Mheshimiwa Ruth Msafiri, kwa kweli anao muda na wakati tutashukuru kupata mawazo ya jinsi gani ambavyo tunaweza kuanzisha hicho Chuo cha binafsi. Kwa sasa hivi *headache* yetu ni Lushoto.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi langu ni ndogo. Lingine nitakuja kulizungumzia kwenye mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Lakini hili linalohusu Mahakama nilikuwa nataka kupata maelezo, Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto hakina fungu linaloelewka katika kitabu hiki. Kwa hiyo, fedha zake zinapopatikana zinakuwa zinatengwa kama fadhila. Kwa hiyo, zinamegwamegwa. Sasa nataka njue Chuo cha Lushoto fedha zake zimetengwa wapi katika kitabu hiki? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo sahihi kwamba Chuo hiki kwa kweli kinatengewa fedha kwa misingi ya fadhila. Chuo hiki kinajitegemea, kina Bodi yake, kina Bajeti yake, kina mkakati wa muda mrefu na muda wa kati na wanawasiliana na Idara hiyo ya Mahakama ikiwa ni pamoa na Jaji Mkuu mwenyewe na sisi kama Wizara hukaa kwa kweli tukayafikiria haya na kuyachukua mpaka katika ngazi ya Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, si sahihi kusema kwamba ni Chuo ambacho kinaendeshwa kwa fadhila, hapana. Fungu ambalo linatumika ni katika masuala ya utawala.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nililokuwa nazungumzia ni kweli amesema kwamba ni fungu la utawala. Lakini tunapojadili shughuli kwa mfano za maendeleo, fungu la Maendeleo linapelekwa Mahakama kwa ujumla. Kwa hiyo, badala ya Chuo cha Mahakama kutengewa fungu lake kwamba kwa maendeleo labda *vote* namba fulani, hapana. Fedha zote zinapelekwa Mahakama na kule Mahakama kutokana na lile fungu kama ni milioni 400 ndiyo wanasesma basi pengine tuwatengee Chuo cha Uongozi wa Mahakama milioni 20. Sasa sisi tunachotaka ni Serikali itenye fungu linalojulikana ambalo Chuo cha Uongozi wa Mahakama kinaeleweka kwa fungu gani?

MWENYEKITI: Kwa hiyo, huo ni ushauri Serikali itenye fungu kwa maana ya ushauri.

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Kweli ikiwa hivyo inaweza ikafaa.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kifungu hicho hicho 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mwaka 2003 nilisimama tu kwenye hoja ya bajeti hii kutaka kupata ufanuzi na nina uchungu kidogo na nitajaribu tu kujitahidi kueleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na vijana ambao niliwaeleza hapa Bungeni kwamba walikamatwa Serengeti na askari waliokuwa wakifuata mifugo. Vijana walikuwa wanachoma nyama kiasi cha kilo nne. Lakini ng'ombe waliokuwa wakifuatwa walikuwa 40, hao vijana walipelekwa mpaka Meatu wakahukumiwa, bahati mbaya sana hakukuwa na mkalimani. Kwa hiyo, walihukumiwa wakafungwa miaka 40 kila mmoja, walikuwa vijana watatu. Waliletwa mmoja akafungwa kwenye gereza hili la Dodoma, wawili wakapelekwa sehemu nyingine ambayo hajulikani mpaka leo. Wazazi wao wamekaa miaka mawili bila kujuwa kwamba vijana wao wako wapi? Mpaka siku moja huyo aliyepo hapa Dodoma akamsikia Mbunge wake akizungumza Bungeni ndiyo akatuma habari kwamba mwambieni niko hapa. Ndiyo akaanza kufahamika kwamba huyo kijana yuko hapa lakini wengine hawajulikani waliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza hapa Bungeni nikashika kifungu. Tulizungumza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tulizungumza na Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, nadhani Waziri alifika mpaka akaenda kumwona huyo kijana Gerezani Isanga lakini hakuna hatua iliyo chukuliwa mpaka sasa. Bahati mbaya sana wale wawili wazazi wao walisema kwamba wamekufa kwa sababu hawajulikani waliko. Kwa hiyo, ningependa kupata ufanuzi.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, anayozungumza Mheshimiwa Lekule Laizer, ni sawa kabisa. Hawa vijana walituhumiwa kwa makosa ya jinai na wakafungwa kwa majibu wa sheria na taratibu za Kimahakama.

Lakini baada ya mimi kusikiliza kilio chao *I went out of my way* na nikaenda na Mheshimiwa Omar Kwaangw' mpaka gerezani kumwita yule kijana mbele ya Afisa wa Magereza na yeze kujieleza na katika msafara ule nilikuwa na msaidizi wangu na *State Attorney In-charge* wa kanda hii ya Dodoma. Nikawaachia wafanye utafiti kuhusu suala lile na majibu ambayo niliyapata ilionekana kwamba hakuna njia mimi kama Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ama *Attorney General* tungeweza kufanya kumtoa yule kijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikawajulisha Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Lekule Laizer pamoja na Mheshimiwa Omar Kwaangw', kwamba wanachoweza kufanya pengine ni kuzungumza na Mheshimiwa Omar Ramadhan Mapuri, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuona kama ana tabia nzuri pengine akaweza kupata msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuja kusema sijafanya lolote na kama mimi nitakuwa nasikiliza mambo ya kila mtu humu ndani ama nje kwenda magerezani na kuwakomboa ndugu zao hiyo siyo kazi yangu. *I better resign, is not my job.*

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu kuuliza Serikali kwamba hivi kumfunga mtu bila kujua kosa lake, hivi ni haki ya binadamu?

La pili, naomba kuuliza Serikali kwamba wale vijana wengine wawili wako wapi? Kwa sababu anayejulikana aliko ni huyu mmoja na yeye alisema kwamba wametengwa yeye ameachwa hapa Dodoma na wengine wakapelekwa nisikokujua. Kwa hiyo, naomba kuuliza Serikali kwamba hao vijana wako wapi?

La tatu, hivi kilo nne ya nyama inaweza kuwa sawa na ng'ombe 40? Kwa sababu hao ng'ombe hawajapatikana mpaka leo. Kwa hiyo, ningependa labda nitoe shilingi unipe dakika hizo tatu ili niweze kuongea nisipoteze muda. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Sasa utoe shilingi ya mshahara wa nani au kifungu gani?

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hiki ninachozungumzia.

MWENYEKITI: Kwa Mheshimiwa Waziri bado kifungu chake hii ni Mahakama.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nipaye majibu ya hayo niliyoyaongea.

MWENYEKITI: Sawasawa.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa kiti.

MWENYEKITI: Ndiyo, mwongozo.

MHE. OMAR S. KWAANGW': Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametaja jina langu, lakini nadhani amechanganya siyo mimi niliyekuwepo kwenye sakata hilo. Nadhani ni Mbunge mwagine Mheshimiwa Lekule Laizer, amseme ni nani lakini siyo mimi. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Sasa umetaka maelekezo ya kiti. Mimi nafikiri Mheshimiwa atafafanua ni nani alikuwepo kwenye msafara huo au Mheshimiwa Lekule Laizer mwenyewe, aseme ni nani walifuatana kwenye msafara huo. Sasa sijui nimwachie Mheshimiwa Waziri ajibu hayo ya Mheshimiwa Lekule Laizer, lakini katika kujibu pia anaweza kutaja ni nani alikuwa kwenye msafara huo.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwamba niliyefuatana naye ni Mheshimiwa Mathew Taki-Ole Timan, Mbunge wa Ngorongoro, ndiye tulifuatana naye. Naomba radhi kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini narudia kusema kwamba masuala haya yanahu su Mahakama na lazima kwa kweli tuheshimu maamuzi ya halali ambayo yanatolewa na Mahakama. Mimi sikuwepo nadhani na Mheshimiwa Lekule Laizer, hakuwepo maana pia alikuwa hajui wako wapi. Ni hapo majuzi tu ndiyo amekuja kufahamu kwamba yuko wapi na kuweza kunichukua mimi kunipeleka Isanga na kuweza kuzungumza na kijana yule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama ameiba kilo nne au ng'ombe 40 hayo ni masuala ambayo yanaamuliwa na Mahakama na hukumu imekwishatolewa. Kwa hiyo, mimi ningemshauri tu Mheshimiwa Lekule Laizer, aendelee kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuona ni vipi wanaweza kuwasaidia hao kijana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ufanuzi wa ziada.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Lekule Laizer, atupatie hayo majina ya vijana wawili ambao hajui wapo katika gereza gani, akishatupatia hayo majina na kesi yao hiyo basi tutatumia Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Magereza ili aweze kutazama katika Magereza yake wako wapi ili tumuarifu Mheshimiwa Lekule Laizer. (*Makofî*)

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri mwenyewe anayo majina.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lekule Laizer, mimi nafikiri ungekubali tu kama unayo umpelekee yaishe au huwajui majina.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikatai, lakini hii imekuwa danadana kwa sababu kwanza Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe anayo hayo majina, Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba, anayo hayo majina. Natagemea kwamba hata Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi anayo hayo majina tumeyapeleka kwao. Sasa akiniambia nifuutilie, nifuutilie wapi? Hao vijana sijui wako wapi? Wao ndiyo wanajua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lekule Laizer, naomba sana uridhike tu kwamba wewe una shida ya hao vijana na unawafahamu pengine wanatoka katika Jimbo lako na majina yao unayajua. Anachosema Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi basi mpatic hayo majina ukishampa ye ye atawatafuta pengine kwa muda mfupi utawajua wako wapi. Nadhani kwa hili tuishie hapo kama unataka kujua wako wapi. (*Makofî*)

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wewe. Isipokuwa nataka ieleweke tu kwamba vijana hao siyo wa Jimbo langu ni wa Jimbo la Mheshimiwa Mathew Taki-Ole Timan, lakini inatuumma wote hata Waheshimiwa Wabunge walioko hapa inawauma, kila mwananchi akifungwa bila kosa. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Nakushukuru, ni kweli wote hapa inatuumma, lakini lazima ufuate taratibu ili ujue wako wapi?

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua kwamba tunahimiza Utawala Bora na unaposema Utawala Bora ni pamoja na kumwezesha mwananchi akiibiwa mali yake apate sehemu ya kwenda na kuwasilisha malalamiko yake. Sasa katika Jimbo la Nkenge tulikuwa na Mahakama za Mwanzo zaidi ya 10. Hivi sasa ninavyoongea imebaki Mahakama ya Mwanzo moja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati anatoa maelezo amesema tatizo ni kwa sababu ya udogo wa Ikama, mimi nakubaliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hoja hiyo si ya msingi kwa sababu kama Mahakama tayari zilikuwepo na zilikuwa na Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo huwezi ukaniambia leo hii kwamba hakuna Mahakimu kwa sababu ya Ikama, kwa sababu tayari walishaajiriwa walikuwepo kwa sababu moja au nyingine wakahamishwa.

Sasa nataka nijue ni lini atanipa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa sababu wananchi wanansumbuka, wananchi wanalazimika kugharimia fedha za wale waliowaibia ili waende kwenye Mahakama za mbali, wananchi wanansafiri zaidi ya kilometra 100 kwenda kwenye Mahakama za Mwanzo na wananchi wanalazimika kutoa fedha za kugharamia chakula kwa ajili ya mahabusu. Sasa hii inaonyesha kwamba Utawala Bora tunaoongea ni wa juu siyo wa ngazi ya chini. Naomba anihakikishie ni lini atanipa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. (*Makofî*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetuwa na mawasiliano na Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kuhusu tatizo hili kwa muda siyo safari hii, lakini kwenye vikao vya mikutano iliyopita na pia ameniandikia barua kuhusu suala na mimi nimewasilisha hoja zake katika Idara ya Mahakama na hivi majuzi tu tulizungumzia suala hili na tukakubaliana kwamba punde watakapokuja viongozi wa Idara ya Mahakama basi tukutane pamoja ili tuone ni vipi tunaweza kulishughulikia suala hili.

MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri ambayo yanaonyesha kwamba nimevumilia vya kutosha. Ni kweli tumewasiliana zaidi ya miaka miwili sasa, vingineyo ningekuwa sijalifutilia kwa muda mrefu nisingesimama hapa na alisema kwamba wataalam wa Idara ya Mahakama watakuja na nina hakika leo hii tunapoongea wapo na wamekuja.

Sasa nataka kujua walipokuja, akakutana nao, wamekubali kunipa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo au wamekataa maana tayari wapo hapa hapa wanatuangalia kule kwenye vioo? (*Makofî/Kicheko*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu hoja ya Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuweza kuzungumza nao kwa sasa hivi kwa sababu nilikuwa nasubiri kwanza Bajeti hii ipite maana ukitaka kuwapata hao inabidi uweze kuwapa posho ya usafiri na kadhalika. Lakini ningependa tu nimuahidi kwamba wapo Mahakimu kama 10 sasa hivi amba wanangojea *post* na nimepata taarifa kwamba baadhi ya hawa tunaweza kuwapeleka huko. Nashukuru.

MWENYEKITU: Ahsante. Mheshimiwa Mbunge umeishapata ahadi bado tena?

MHE. DR. DIODORUS B.KAMALA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuweka sawa. Sote ni wanasiisa ukiwemo wewe na Mheshimiwa Waziri, mtu anaposema kwamba anaweza kupata maana yake nyingine ni kwamba anaweza kukosa. Naomba angalau anihakikishie niwe na uhakika wa kupata Mahakimu wawili na uwezekano wa kupata zaidi ya wawili. (*Makofî*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ye ye kimsingi nia ipo, sababu ya kufanya ipo na uwezo unaonekana upo upo. Kwa hiyo, tutazungumza lakini hatuwezi kuyapanga haya moja kwa moja humu ndani ya Bunge. (*Kicheko*)

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Ahsante Mwenyekiti, kifungu hiki cha 1001 mshahara wa Mahakimu.

Katika mchango wangu wa maandishi niliomba sana kuhusu matatizo yanayowapata wajane hasa wale ambao waume zao wameathirika na UKIMWI. Kesi zao zinapigwa danadana na zinachukua muda mrefu sana.

MWENYEKITU: Mheshimiwa Remidius Kissassi, hilo usingelipeleka kwenye Wizara, maana hapa ni Mahakama peke yake.

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Siwezi kumkamata Jaji hapo?

MWENYEKITU: Unamkamata wa nini sasa?

MHE. REMIDIUS E. KISSASSI: Naogopa kufungwa.

MWENYEKITU: Hiyo ni Waziri mwenyewe anahuksika.

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama.

Nieleze kwamba nimeshazungumzia mara nyingi katika Bunge hili Wilaya ya Simanjiro kutokuwa na Mahakama ya Mwanzo wala ya Wilaya. Kwa miaka kumi sasa wananchi kama kesi inahuksika Mahakama ya Wilaya itabidi asafiri sio chini ya kilometra 150 kwenda Kiteto. Sio chini ya kilometra 200 kwenda Arusha. Kwa hiyo, mwananchi

wa Simanjiro hapo ameshanunua haki na hakuna usafiri wa kuaminika. Kwa hiyo, anajiandaa kwa wiki nzima na mara nyingine anafika tarehe imeshapita anaambiya mpaka wakati mwingine na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Mwanzo tuna Mahakimu watatu tu kwa Wilaya nzima. Waziri aliwahi kunipa ahadi kwamba kutokana na ahadi aliyotoa Mheshimiwa Rais kwamba itajengwa Mahakama ya Wilaya Simanjiro, alisema kwa mradi wa *Quick Start* watatumia nafasi hiyo kujenga. Wamekuja kweli, wametuelimisha namna ya kushiriki kwenye mradi huo. Wananchi na Wilaya wamekamilisha yale waliohitajika kuyafanya bado sehemu ya Serikali na yejote yule anayehusika, lakini sio Wilaya wala sio wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashangaa kwa sababu inaelekeea hatuna umuhimu wa kwanza. Sasa Waziri leo anieleze kwamba Serikali itajenga Mahakama au wanatuambia kwamba tutumie sheria za jadi. Lakini siku hizi tuna mchanganyiko wa watu. Wilaya ya Simanjiro wako Wachaga, Wapare, Wasegeju na kadhalika. Sasa utatumia sheria ipi ya jadi katika Mahakama ya jadi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atueleze kama Mahakama hiyo itajengwa ama haitajengwa. Kama haitajengwa sisi Simanjiro tupate wapi haki?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nikiri kwamba tatizo hili tunalifahamu na tumekuwa na mawasiliano na Mheshimiwa Parseko Kone. Lakini niseme kwamba ni Wilaya nyingi ambazo hazijapata Mahakama hasa Wilaya ambazo ni mpya.

Kwa hiyo, kama nilivyozungumzia katika hotuba yangu ni kwamba chini ya mradi wa *ATIP* na kama tulivyoonyesha katika ukurasa wa kwanza wa taarifa hii ya majengo kwa Mahakama Hakimu Mkazi Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mwanzo. Ni kweli kabisa Wilaya ya Simanjiro ina matatizo makubwa na tumeonyesha kwamba kote humo inabidi tujenge Mahakama mpya, wala sio suala la kubomoa wala la kukarabati. Lakini narudia tena kusema kwamba kinachogomba hapa sasa hivi ni suala la fedha. Lakini *priority* kwa kweli ipo na tunatambua usumbufu ambaeo ndugu wananchi wa eneo hilo wanaoupata katika kutafuta haki zao.

Sasa nitamwomba tu kama ilivyo kwa upande wa Karatu basi *co-ordinator* aweze kukutana na viongozi ili waweze kuona ni vipi tunaweza kuharakisha ujenzi wa Mahakama ya Wilaya na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo katika maeneo hayo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Parseko Kone, azidi kutupa wasaa kuweza kuyatekeleza hayo.

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Mwenyekiti, wasaa huo nitatoa, lakini Waziri naye aahidi kwamba tuwape muda gani?

MWENYEKITI: Wakupe muda gani kujenga? (*Makofi/Kicheko*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Kwa sasa hivi Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwisha panga Bajeti kwa kipindi hiki cha mwaka 2004/2005. Lakini tukizungumza na wenzetu kwa upande wa ufadhili kama tunaweza tukaharakisha suala hili basi tutafanya hivyo mapema iwezekanavyo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Parseko Kone, tuendelee kuwasiliana. Lakini ningependa nimhakikishie kabisa katika bajeti ya mwaka 2005 tukielekea kwenye Uchaguzi Mkuu nadhani itakuwa tumefika mahali pazuri.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi. Kwanza kabisa nilitaka kuuliza *High Court* ya Shinyanga kama ambavyo tumekuwa tukilalamika na kusema muda wote kwamba wananchi wa Shinyanga wanapata adhabu kali sana, wanakwenda mpaka Tabora kutoka Bariadi ni kilometra 360. Tulishaongea na Jaji hapa na ye ye akakubali, majengo yako tayari ya Jaji na Wanasheria. Sasa kinachogombaa kuleta *High Court* Bariadi ni kitu gani?

MWENYEKITI: Bariadi au Shinyanga?

MHE. DANHI B. MAKANGA: Eeh, Shinyanga, lakini nikasema kama basi hili suala linachukua muda mrefu basi sisi Bariadi kwa sababu tuko karibu na Mwanza basi tupelekwe *High Court* ya Mwanza iweze kushughulikia masuala ya Bariadi. (*Makofi*)

Lingine la pili, nilisema kesi ya mlundukano wa mahabusi katika Wilaya ya Bariadi ni kesi za nyara ambazo nyingi ni za kusingiziwa hazina kitu chochote. Hizi zinahitaji Jaji na Jaji yuko Tabora. Sasa watu wanakaa pale hata miaka mitano au sita wanakamatwa na mkia wa nyumbu tu au kangozi ka sungura. Mimi nikafikiri kwa nini basi hizi kesi za namna hii wasipewe Mahakamu wa Wilaya wakazisikiliza na kuzimaliza badala ya kusubiri Jaji. Mimi nafikiri hizo ni *arrangements* za Kimahakama tu.

Lingine nikasema kesi zinazoendeshwa Mahakama za Mwanzo ni tatizo sana. Watu wengi hawajui kujenga hoja na kujitetea, kwa nini tusiruhusu basi waajiri Mawakili ili wawze kujengewa hoja na kutetewa katika Mahakama za Mwanzo badala ya sasa wanazimika kutoa rushwa kubwa. Sehemu kidogo ya kumwajiri Wakili ingetosha na akabaki na hela. Rushwa inaleta umaskini.

Lingine nikasema katika kabrasha hili la majengo ukurasa wa 18 ambapo anazungumzia Bariadi. Sasa kama hao ni watafiti kweli aliwatumaa sisi hatuna Mahakama ya Mwanzo Bariadi Mjini. Sasa wao waliipata wapi hii ambayo imeandikiwa lazima ibomolewe na ijengwe majengo mapya, pale Bariadi Mjini? Mahakama za Mwanzo Somanda ambazo ni kilometra moja na nusu kutoka Bariadi Mjini au wanataka kujenga.

Lakini lingine ambalo anasema ameeleza katika orodha hii kuna kubomoa na kujenga. Lakini majengo haya Mwenyekiti si ya kwao ni Halmashauri. Wao kama Mahakama hawana majengo haya. Sasa wanataka kubomoa majengo yetu bila ya ruhusa yetu au wanataka kufanyaje? Ahsante.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu masuala ya Mheshimiwa Danhi Makanga, kama ifuatavyo:-

Kwanza inawezekana kabisa kwamba katika kufanya utafiti huu yakawepo makosa fulani fulani. Sasa kwa hili tumelipokea, tutalifanya kazi na ningeomba Waheshimiwa Wabunge wengine watupe taarifa kama kuna makosa mengine ndani ya ripoti hii.

Kuhusu majengo kilichopendekezwa kwa sababu kwa sasa hivi Idara ya Mahakama ndiyo inatumia hayo majengo. Kama ni ya Halmashauri ama ni watu wengine. Walichofanya hawa wataalamu ni kusema kwamba majengo yale hayafai. Kwa hiyo, wametuachia sisi tuzungumze ama tutafute njia ya kutafuta viwanja, lakini wameona kwamba majengo haya hayafai yanafaa kubomolewa na Mahakama mpya kujengwa.

Kuhusu ujenzi ama kuwepo kwa (*High Court*) Mahakama Kuu Shinyanga. Hili suala tunalifahamu. Mimi nimekwishafika Shinyanga wakati Mheshimiwa Babu akiwa ni *Regional Commissioner* tukalizungumzia suala hili. Jaji Mkuu amekwishatemebelea. Kimsingi ni kwamba tunakubali kabisa na sasa hivi yako maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba tujenge Mahakama Kuu katika Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo tutalifuatilia suala hili.

Kuhusu suala la mahabusu basi tungependa tupate orodha kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, ni mahabusu ya namna gani, majina yao kesi namba zao ili tuweze kuyafuatilia masuala haya.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni swali dogo tu. Labda hakunipata vizuri Mheshimiwa Waziri, nilisema hao mahabusu ni kesi za kukamatwa na nyara porini kule tuko karibu na Serengeti. Sasa hizi zinahitaji Jaji? Hivi hamwezi kufanya *arrangement* za Kimahakama mkakasimu madaraka kwa Mahakimu wa Wilaya waweze kuwasikiliza hawa watu wasisote rumande kwa muda mrefu wakaleta hasara ndani ya Serikali? (*Makofi*)

Lakini lingine kutumia Wakili katika kesi za wananchi wetu katika Mahakama za Mwanzo. Hili la Mahakama Kuu tangu nikiwa Upinzani, nikiwa *UDP* ni siku nyingi tumerudia kuzungumza hili mpaka nimerudi CCM huku sijalionna hili kama linatekelezwa. Sasa tuambie si suala la kujenga. Majengo yapo na nyumba za kuishi Jaji hata Wakili wa Serikali na ofisi zipo. Tatizo ni nini? Si kujenga ni kuweka bajeti tu Jaji ahamie na Wakili ahamie pale tuendeleee?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu masuala haya mawili. Kwanza kuhusu Mahakama ya Mwanzo kuweza kuhudumia na Mawakili. Hilo swala bado kwa sababu mpaka sasa hivi Mahakimu wetu hawana uwezo wa kuweza kukabiliana na hoja kutoka kwa watu ambao ni wasomi zaidi yao. Tunatambua kwamba hii ni kuwapunja haki zao ama kuwanyima haki zao wananchi. Ndiyo jitihada ambazo tunafanya katika kujaribu kupanua Chuo cha Lushoto ili Mahakimu ambao wana sifa zinazostahili waweze kuendesha shughuli za mashauri katika Mahakama za Mwanzo na pindi hilo likifanyika basi tutaruhusu Mawakili kufanya kazi hiyo. Lakini pamoja na hayo ni kwamba wanao uhuru wa kuweza kwenda kwenye Mahakama ya Wilaya kama wanaona kwamba watahitaji kutetewa na Wakili.

Kuhusu kuongeza mamlaka kama nilivyozungumza hapo mwanzo, ningependa Mheshimiwa Danhi Makanga, atupatie orodha tuone uzito wa shughuli yenyewe ili niweze kumwandikia Jaji Mkuu aweze kuwapa mamlaka Mahakimu wa Mahakama za Wilaya kushughulikia kesi hizi.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechangia kwa maandishi. Nimezungumzia masuala hasa ya Mahakama ya Mwanzo. Waziri amejibu majibu ya jumla. Lakini hasa nilitaka kupata ufanuzi kwa sababu jambo hili nimekaa nikilifuatilia, nimekuwa nikiiandikia Wizara pia kuhusiana na kituo cha Mahakama ya Mwanzo eneo la Kirumba Mjini Mwanza. Nashukuru kwamba kwa Mahakama ya eneo la Mkuyuni sasa imekwishaanza kufanya kazi. Sasa nilitaka tu kujua kama hili jambo amelichukua linaweza kutekelezwa, tulifanye lini ili huduma ile irudishwe pale kwa sababu sasa wananchi wa eneo lile pamoja na Kata zake za Kitangiri, Nyamanoro na sehemu ya Isamilo inabidi waende Ilemela ambako ni mbali na huduma inakuwa ngumu kwao? Wakati mwingine mpaka wanashindwa kuendeleza kesi wanaacha tu kwa sababu ya umbali wa Mahakama iliko.

Pia nilishukuru nikasema suala moja kuhusiana na matengenezo ya majengo ya Mahakama Kuu pamoja na Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mwanza ambayo imeanza kufanyiwa matengenezo. Nilitaka kujua kama mwaka huu pia wataendelea kwa ajili ya sehemu ya ndani, kuna mabadiliko makubwa kwa nje sasa lakini kwa ndani bado sio pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine cha mwisho ambacho nilitaka tu kupata ufanuzi ni kuhusiana na Majaji wanapokuja Mwanza, waliohamia pale wanakaa hotelini mpaka sasa. Sasa sijui kwamba nyumba zitapatikana au wataendelea kukaa pale? Hili pia nilitaka kupata majibu yake niweze kuelewa.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali ya Mheshimiwa Stephen Kazi, kama ifuatavyo.

Kwanza nimpongeze kwa kufuatilia haya masuala kwa ukaribu na kwa kweli Idara ya Mahakama imejitahidi sana. Mimi mwenyewe nimetembelea Mkoa wa Mwanza na kujionea mimi mwenyewe hali ya *High Court* ilivyokuwa. Nashukuru kwamba ukarabati umefanyika sasa hivi ni jipya na ukarabati wa ndani ya Mahakama yenyewe

unaendelea na katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha unaokuja tutakuwa tumekamilisha kazi hiyo. Makuyuni nako hali ni nzuri na pia Mahakama ya Hakimu Mkazi imefanyiwa matengenezo.

Sasa naomba tu kwa hili la Kirumba kwamba linahudumia eneo kubwa, naomba Mheshimiwa Stephen Kazi, avute subira. Pindi tutakapokuwa na fedha za kutosha basi na hili tutaweza kulishughulikia. Lakini kazi kubwa kweli imefanyika katika kipindi kifupi katika kuimarisha na kuboresha sura za majengo ya Mahakama zote pale Mjini Mwanza.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika kifungu hicho hicho cha 1001, Mahakama.

Katika mchango wangu wa maandishi nilielezea suala la Mahakama ya Wilaya Misungwi, bado kuna mateso kweli. Mtu kutoka Mahando kwenda Kwimba ni umbali wa kilometra 100 na zaidi, ni muda mrefu. Mtu kutoka Bukumbi mpaka Kwimba ni mbali kweli. Mheshimiwa Waziri alipata nafasi akaja, siaona mabadiliko yoyote. Lakini nimshukuru Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Naibu Waziri, yeye ameshatekeleza kwa maana kwamba atakuwa na *OCD* tayari. Nataka nipate maelezo basi kwamba vipi anasemaje kuhusu ujenzi wa Mahakama ya Wilaya yetu ya Misungwi ili angalau wananchi waendelee kupata haki zao katika eneo lao la Wilaya yao? Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti. *Tukwibona anze. (Kicheko)*

Tutayazungumza na Mheshimiwa Jacob Shibiliti masuala haya. Nakiri kwamba hii ni Wilaya ambaye imekuwa pale kwa muda mrefu na kwa kweli hatujaweza kuishughulikia.

Kwa hiyo, tutazungumza na wenzetu wa Idara ya Mahakama. Niseme anayozungumza ni kweli kabisa na mimi nimetembelea Gereza la Kwimba kuzungumza na mahabusu na wafungwa waliniimbia nyimbo za Kisukuma kweli kweli kwa maana ya kujaribu kuniwezesha kuelewa matatizo yao na gereza hilo la Misungwi kujengwa kwa sababu kuna mbanano mkubwa kweli kweli. Watu wamebanana kweli. Upo msongamano wa karibu sana katika gereza hili la Kwimba. Kwa hiyo, tutazungumza na wenzetu wa Mahakama, tuone ni jinsi gani tunaweza kulitatu tatizo hilo. (*Makofî*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila ya mabadiliko yoyote)*

| | |
|---|-----------------|
| Kifungu 2001 - <i>High Court</i> | 378,747,500/= |
| Kifungu 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i> | 382,692,100/= |
| Kifungu 2003 - <i>Arusha Zone</i> | 672,293,800/= |
| Kifungu 2004 - <i>Dar es Salaam Zone</i> | 1,333,792,400/= |
| Kifungu 2005 - <i>Dodoma Zone</i> | 543,126,700/= |

Kifungu 2006 - *Mbeya Zone* 917,930,100/=
Kifungu 2007 - *Mtvara Zone* 495,886,800/=

(*Vifungu viliyyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2008 - *Mwanza Zone* 842,575,000/=

MHE. KISYERI W. CHAMBIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu namba 2008 *Mwanza Zone*, amana ya Mahakama ya Mwanzo katika Mji wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bunge la Bajeti kama hili niliuliza swali kwa Waziri kwamba Mahakama ya Mwanzo ya Tarime ambayo iko Nyamisangura kuna mtu alijitolea kwamba yeze aichukue halafu eneo lile alitumie kwa matumizi yake ajenge Mahakama nyingine. Kwa hiyo, wakati ule nililalamika kwamba ingawa Wizara yake ilikubaliana na hayo maoni kwamba jengo lililokuwa linajengwa lilikuwa na *quality* ya chini kuliko jengo linalochukuliwa. Kwa hiyo, pamoja na hayo malalamiko nikaandika barua kwa Waziri. Barua ambayo mpaka leo hajajibu.

Sasa mimi nilikuwa nataka nielewe kwamba kama Mbunge anamwandikia Waziri barua, tena ya malalamiko inatakiwa Mbunge atoe nini kusudi aweze kujibiwa hiyo barua? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijibu swali la Mheshimiwa Kisyeri Chambiri, kama ifuatavyo:-

Kwa kweli tunajitahidi sana kila tunavyoweza kujibu na kwa usahihi kabisa masuala kama hayo. Sisi ndio watu ambao tunasimamia Utawala wa Sheria, Haki za Binadamu, masuala ya utu kuheshimiana. Kwa hiyo, kama hatujajibu basi sio kwa nia mbaya. Niseme tu kwamba hiyo barua mimi sijaiona. Kwa hiyo, wanachowenza kufanya ama tunachowenza kufanya ni kuonana uso kwa uso ama kunikabidhi barua hiyo ili tuweze kulifanyia kazi suala hilo.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2009 - *Tabora Zone* 1,092,519,400/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 2010 - *Tanga Zone* 360,862,500/=

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka tu nipaye ufanuzi kwa suala ambalo nimeliuliza mwaka 2003 na mwaka 2004 kwa

Mahakama ya Hale ambayo imejengwa ni moja ya Mahakama nzuri sana katika nchi hii. Lakini mpaka leo haijakuwisha na bado haijaanza kazi. Hilo ni moja.

Lakini la pili, nilitaka tu na mimi niweze kujenga hoja kwamba katika Mkoa wetu wa Tanga baadhi ya Tarafa nyingi hazina Mahakimu kama Tarafa ya Magoma, Bungu na Mlalo, hakuna Hakimu kabisa, je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu suala hilo?

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali ya Mheshimiwa Joel Bendera kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba Mahakama ya Hale imechukua muda mrefu na ipo njiani, ninapokwenda Jimboni na ninapokwenda nyumbani na ninaporudi Dar es Salaam, nimekuwa kwa kweli na tabia ya kupita. Nimekwishapita mara moja au mara mbili na tumekwishazungumza na Idara ya Mahakama na tulikuwa tuna matatizo na *contractor*. Kwa hiyo, nitaendelea kuwasiliana na Idara ya Mahakama ili kufahamu tatizo ni nini. Lakini ni *finishing touches* tu ambazo zimebakia pale. Kwa hiyo, nitalifuatilia hilo suala na wenzetu wa Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hakimu basi namwomba Mheshimiwa Joel Bendera, naye atuandikie tuweze kuona katika hawa kumi tunaweza kusaidia kwa njia moja au nyingine.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2011- Primary Court 4,396,428,600/=

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 2011 - Primary Courts, nilikwishachangia na hata kwa mwaka 2003 nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba katika eneo langu la Nkasi; Wilaya nzima, ingawa kifungu hicho kitafuata baadaye, lakini sizungumzii hicho, nazungumzia hiki kilichopo, licha ya kusema tu kwamba hakuna Hakimu wa Wilaya, lakini pia Wilaya nzima ina Hakimu mmoja tu kwa Mahakama ya mwanzo na ukitazama katika vituo, kwenye jedwali lake la utafiti licha ya kusema majina mengine yamekosewa humu, huyu Hakimu mmoja wa Mahakama ya Mwanzo anashughulikia vituo 13 ambapo ni zaidi ya watu 200,000. Je, hii ni haki kukosa Hakimu wa Wilaya au hata Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo awe huyu mmoja? Unakuta kesi ziko nyingi hawezi kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Waziri, katika majibu yake anasema tutakazana, je, anasema nini kuhusiana na suala hilo na anaahidi nini kupunguza tatizo hilo kwenye Wilaya hii ya Nkasi? (*Makofi*)

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujibu maswali ya Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema tu kwamba, nadhani sisi sote humu ndani ya Bunge tunatambua kwamba tuna tatizo hili ambalo limekuwa ni la muda mrefu la upungufu au uchache wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na ndiyo maana tumejenga hiki chuo, lakini nacho idadi ya wanaoomba ni kubwa na uwezo wetu wa kufundisha na kuwapata Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni mdogo. Lakini nasema tutaendelea na jitihada hizi za kuweza kupanua chuo hiki ili kiweze kukidhi mahitaji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kama nilivyozungumzia wakati wa kuhitimisha hotuba yangu, nasema tutaendelea kuwasiliana na Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, ili kuweza kuongezewa Ikama hii kwa sababu ni kweli kwamba wanaofuzu pale ni wengi ukilinganisha na wale ambao wanapata ajira. Sasa itabidi tukae na wenzetu Ofisi ya Rais, Utumishi ili kulitazama kwa kina ni vipi tunaweza kuwatumia hawa wachache ambao wanatoka katika chuo hiki cha Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba tunawanyima haki hawa wenzetu ambao hawahudumiwi na inabidi wasafiri kwa muda mrefu ili kuweza kupata haki zao. Hili tunalitambua ni tatizo nasema la Kitaifa, lakini mwelekeo wetu ndiyo huo, ukisema kwamba tutakuwa na *Crush Program*, fedha zenyewe tulizotengewa kuweza kuturuhusu kufanya hivyo nazo hazipo.

Kwa hiyo, tunaendeleza mazungumzo na wahusika wanaopanga Bajeti ili kutupangia Bajeti ambayo ni kubwa na suala hili limezungumzwa kwa kirefu na kwa kina na Kamati ya Mheshimiwa Athumanji Janguo, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na humu ndani na Waheshimiwa Wabunge jinsi ya kuweza kutafuta mbinu mbalimbali kuhakikisha kwamba hizi *Primary Courts* zinapata Mahakimu wa kutosha.

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu hayo. Lakini kwa vile nchi yetu ina utaratibu wa kuwatumia wastaafu pale inapoonekana kwamba kuna tatizo na imekwishafanya hivyo kwenye Wizara ya Elimu kwa kuajiri Walimu wastaafu ili kuziba mapengo hayo.

Je, Mheshimiwa Waziri huoni kwamba kwa wakati huu ambapo kuna tatizo la kuwasomesha hao kutohana na tatizo la chuo, wale Mahakimu wa Mwanzo waliostaafu na ambao wako kwenye Wilaya zinazohusika zenyе matatizo kama hayo mnaonaje mkiwa tayari kuwapa mkataba wa miaka miwili, mitatu wakati mnasomesha wale wengine ili waje wazibe mapengo hayo? (*Makofî*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo kwa ufanuzi aliotaka Mheshimiwa Ponsiano Nyami, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Serikali imejua eneo la Mahakama kama ilivyo Sekta ya Elimu na Sekta ya Afya ni eneo ambalo linataka Serikali itoe kipaumbele.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge akubaliane na sisi kwamba tumeshaanza utaratibu wa kutoa kipaumbele kinachotakiwa ili kama siyo kuondoa basi kupunguza matatizo ambayo yako kwene Sekta ya Mahakama. (*Makofii*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2012 - *District Courts* 2,700,477,600/=
 Kifungu 2013 - *Kagera Zone* 425,289,300/=
 Kifungu 2014 - *Ruvuma Zone* 479,882,300/=
 Kifungu 2015 - *Moshi Zone* 448,345,600=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kifungu 1001 - Administration and General 1,140,379,000/=

MWENYEKITI: Ahaa, ngoja tuwaandike. Pengine kabla sijaanza kuwaita majina niwatahadharishe tu kidogo kwamba, siyo nia ya kubana uhuru wa kila mtu hapana, lakini ni kuwataaarifu tu, hii ni moja ya Wizara yenyeye vifungu vingi sana. Kwa hiyo, naona hilo niwatahadharishe mapema. Kama tunaweza kufanya haraka tukaenda *specific* kwenye tatizo tutakwenda haraka sana.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu 1001, mshahara Waziri. Katika kitabu cha hotuba yake ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, umesema ni mshahara wa Waziri, lakini kifungo ni cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 16 wa kitabu cha Bajeti, nimeona mambo mazuri ambayo yanatakiwa kuzingatiwa, lakini katika mambo ambayo nataka kuzungumzia ni kisehemu kile cha Ustawi wa Mtoto pamoa na Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania, Sheria ya Mirathi na Urithi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifafanuliwe sheria hii itakapoletwa kujadiliwa katika Bunge hili, maana Waziri alipokuwa anajibu swali moja mapema alisema tusubiri mpaka *bill* hii itakapoletwa. Lakini nataka tu labda niambiwe katika sheria hii itazingatia sawa mambo ya kurithi kwa jinsia zote mtoto wa kike na mtoto wa kiume. Hii naona ni nzuri na naomba wakaiweke sawa sawa ili hata watu wa vijijini baadaye waweze kufundishwa na kuelimishwa ili watoto wetu warithi.

Lakini vile vile imesema kwamba, mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa apate kurithishwa kwa sababu ni kweli watoto waliozaliwa nje ya ndoa wanasumbuka. Nilikuwa najiuliza, katika sheria ya mwaka 1971 kuna mali ya ndoa ya mke na mume ambayo wanachuma pamoja, huyu mtoto wa nje ya ndoa atarithi mali ipi, iliyochumwa na mke wa ndoa au iliyochumwa na ile nyumba ndogo? Kwa sababu nadhani watoto wanaozaliwa nje ya ndoa ni wale wa nyumba ndogo tunazozisikia mitaani nyumba ndogo, nyumba ndogo. Sasa atarithi mali ya nani, ya mke wa ndoa aliyetafuta mali na huyo mume wake aliyekuwa na nyumba ndogo au watatayarisha sheria na itagawa vipi mirathi ya hawa mabwana wanaozaa nje ya ndoa? Kwa sababu mwanamme mmoja anaweza akawa na ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, imeeleweka.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Imeeleweka?

MWENYEKITI: Imeeleweka.

MHE. RHODA L. KAHATANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, nadhani umeelewa pia.

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Nimeelewa na tumeyazingatia. Hiyo ilikuwa ni mifano tu, lakini tutazingatia hizo hoja za Mheshimiwa Rhoda Kahatano. (*Makofit*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye Fungu hilo hilo 1001. Wakati Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani anajibu alielezea suala la Sungusungu kwa kutumia sheria namba 9.

Kwanza nataka nimhakikishie kwamba sheria hiyo naijua na niliisoma kabla sijaandika hotuba yangu. Lakini Waziri amejibu hoja ambazo ni nje ya hoja ambazo tuliziweka za msingi. Hoja yetu ilikuwa inataku tuhakikishiwe kwamba Sungusungu wanaundiwa utaratibu, sheria namba 9 haitoi utaratibu wa kufanya kazi zao, haitoi utaratibu wa namna wanavyotoa adhabu, haitoi utaratibu wa namna wanavyowenza kuwapeleka watuhumiwa wale kwenye ngazi za juu. Sasa tuliomba atupe utaratibu huo utaandaliwa lini? Hatujapata jibu hilo na hii ni kero. Kwa hiyo, nadhani tulichotaka ni sheria namba 9 ifanyiwe utaratibu, Waziri anatoa kauli gani juu ya hilo?

La pili juu ya hilo hilo ni kwamba, hawa tuliotoa majina ni watu walioua, walioua tumewataja kwa majina, barua zinazohusika zikiwemo za Polisi tumezitaja *references* zake. Sasa hawa walioua wako nje, hawajakamatwa, hawajashughulikiwa, je, sheria namba 9 inaruhusu Sungusungu kuua? Tulichotaka ni Waziri atusaidie hawa walioua ni

kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria kama sheria zingine zinavyotaka kwa sababu siyo sheria moja tu na naunganisha na lile la *inquest*.

Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema sababu za *inquest* hazzioni, lakini hapa kuna watu ambao wameuawa, Polisi wakati mwingine wanatoa sababu kwamba ni watuhumiwa kwa hiyo, waachiwe. Sasa unauliza hata wangekuwa watuhumiwa, je, ni kweli waachiwe? Watuhumiwa si wanapelekwa wanakostahili? Sasa kwa kuwa wameuawa na hakuna kitu kilichofanyika na waliowaua wako nje ndiyo sababu tulikuwa tunadai *inquest* ifanyike kwa sheria ya *inquest* ambayo ameitaja Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni kuhusu hiyo moja, naomba niliache hili la Sungusungu. Sasa niingie kwenye hili la Kibaigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana rafiki yangu Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema ananiheshimu na mimi namuheshimu sana pia na yeye. Lakini pia nataka niseme kwamba, hapa hatufanyi mzaha, tuko hapa kwenye kazi nzito, kama yeye anavyotetea Serikali, mimi kazi yangu ni kutetea hoja za upande wa Upinzani. Kwa hiyo, si suala la kwamba tunafanya mzaha.

Sasa nataka nimweleze hoja si kwamba Mheshimiwa aliyetuhumiwa hatutaki awe na shamba au yejote mwingine asiwe na shamba, suala si kuwa au kutokuwa na shamba. Hoja inayojitokeza sasa hivi ni kwamba, shamba hilo lilipatikanaje? Ndiyo sababu inaunganishwa na rushwa na yule aliyetaja suala la rushwa kule awali. Lakini ya pili tukasema tumefarijika kwa sababu mhusika amekanusha na baada ya kukanusha ikatokea hoja kwamba si kweli.

WABUNGE FULANI: Uthibitisho, uthibitisho!

MHE. DR.WILLBROD P. SLAA: Naomba majibu ya hoja hizo.

MWENYEKITI: Hebu tusikilize kwanza.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hili la Sungusungu, kwanza nirudie kama nilivyosema. Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, amepongeza kazi nzuri inayofanywa na Sungusungu na nataka niunganishe hapo hapo. Huwa najiuliza sijui hali ingekuwaje kama Sungusungu hawa wasinge kuwa wanafanya kazi hiyo ya ku-*supplement effort* ya Polisi. Tunawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, ametoa orodha ya wale ambao yeye anadai wameua. Mimi siwezi kusema kwamba wameua, yeye ametumia maneno wameua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo yana taratibu zake za kimahakama. Sisi kama Serikali tunachowenza kusema ni kwamba tutafuatilia hayo aliyoorodhesha katika *statement* yake, tutapata ukweli tu. Lakini tusije hapa tukaanza kuwahukumu watu, hapana, twende kwa utaratibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kuhusu hayo niliyosema ya Kibaigwa. Narudia kwa moyo wa dhati kabisa, nilisema hivi eneo hilo kwa sababu siku ile mimi nilibahatika tu kuwa hapo ule uongozi wa Kijiji wa Manyata ulipokuja wakaeleza yale wanayofahamu kwamba eneo la pale ukitaka wanakodi. Miaka miwili na nusu iliyopita nilikuwa nakodi ardhi Kiteto kwa Mheshimiwa Benedict Losurutia, kwa ajili ya ulimaji wa mahindi pamoa na dada yangu Mheshimiwa Martha Wejja, tunalima huko, tunafanya kazi Matui kule. (*Makofi*)

Sasa nilichosema kuhusiana na Manyata ni kwamba kuna ardhi pale inakodishwa na wale wanaotaka kwenda kukodisha wapo tulionyeshwa na risiti wanazolipia. Ukitaka unaenda unafuata utaratibu unapewa eneo, unalipia *rent*, unalima na napenda sana Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, naye alime akipenda. (*Makofi*)

Lakini la mwisho nimemalizia kusema hivi, ule uongozi wa Kijiji ni uongozi, tuuheshimu kama alivyo yeze na nikasema basi yeze aende pale kwenye Kijiji kile cha Manyata akatuonyeshe shamba hilo ambalo anadai ni la Kiongozi wetu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimemalizia hilo tu. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Nadhani yaliyotakiwa ndiyo hayo aliyosema, kwanza kwa sababu tulikuwa tunanong'onezana hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikuwa anamnong'oneza nataka nikiri kwamba ninalijua hilo shamba...

WABUNGE FULANI: Aaah! Una uhakika na unayoyasema?

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti ...

MWENYEKITI: Hebu kaa chini Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa.

Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize. Tumsikilize vizuri, amesema analijua hili shamba, lipi? Basi tumruhusu aendelee mjadala ufungwe.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri tatizo letu ni huwa tunawahi sana, huwa hatuna uvumilivu na ndiyo maana tunaoneana aibu katika nchi hii. Nimesema nalifahamu shamba hilo liko Kijiji kinachoitwa Hogolo, liko kilometra kama 20 kutoka barabarani. Kwa kuwa kuna lalamiko la wazi hadharani na anayetuhumiwa ni Kiongozi wetu, nilifikiri tulitakiwa kupongezwa kwamba tunamtafutia namna ya kumsafisha jina.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Sasa ili kusafisha jina na ili sisi tuweze kutekeleza wajibu wetu, ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba kilichosemwa kinatamkwa hadharani kwamba si kweli na kwamba shamba hilo ambalo liko na mimi nimekwenda

pale na nimeonyeshwa na mtu yejote akifika pale Kibaigwa uliza suala la shamba la fulani utapelekwa.

Baada ya kupelekwa pale tunataka kujua taratibu hizi zilizosemwa kama si za kweli hoja yetu ya msingi asubuhi ilikuwa kwa nini wahusika wasipelekwe Mahakamani na usipofanya hivyo kwa taratibu za kawaida ni kwamba kuna wingu unalijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tulichotaka ni hicho na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, amesema kwamba shamba inawezekana limekodishwa, sisi tutachukua hilo kwamba limekodishwa, tutaendelea kufanya utafiti wetu.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* 240,503,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 1003 - *Policy and Information Services* 481,205,000/=

MHE. PARSEKO V. KONE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwamba katika kifungu 1001 kuna wengi tuliojiandikisha majina kuchangia na hatujatajwa ili kupewa nafasi hiyo.

MWENYEKITI: Sikuwa na orodha hiyo hapa, kwa hiyo, tutaendelea na vifungu vingine. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 - *Administration and General* 570,807,000/=

Kifungu 2002 - *Public Prosecution* 1,646,897,000/=

Kifungu 2003 - *Legislative Drafting* 421,206,000/=

Kifungu 3001 - *Civil and International Affairs* 492,072,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 4001 - *Constitutional Affairs* 343,639,700/=

MHE. HENRY D. SHEKIFFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 4001 na fungu dogo linalohusu mishahara 250100, fungu hili linahusu Katiba. Wakati nachangia nilizungumzia suala la kuvunjwa kwa haki za binadamu na namshukuru sana Mwanasheria Mkuu wa Serikali alijibu hili kwa uchungu sana. Sasa kutokana na ahadi yake kwamba suala hili linaweza kupata jibu katika muda wa siku saba, nafikiri ni vizuri

pia ingetamkwa, hivi ikidhihirika kwamba hawa wamefanya makusudi kuwatesa wale akinamama kwa miezi karibu nane watachukuliwa hatua? Nafikiri Wananchi wangependa kujua Serikali inasema nini kuhusu hilo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Henry Shekiffu, awe na subira. Ni yale yale tusijaribu kuwa *judgemental*, sisi tunaenda kwa uchunguzi tuyaone kwanza yale ithibitike kweli hayo uliyosema yamefanyika halafu tuanzie hapo sasa, mtendewa na mtendaji. Kwa hiyo, namwomba atupatie muda huo tuifanye kazi hii.

MHE. ALI SAID SALIM: Nimesimama.

WABUNGE FULANI: Hapana.

MHE. ALI SAID SALIM: Nimesimama.

WABUNGE FULANI: Hapana.

MHE. ALI SAID SALIM: Nimesimama nasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa, kaa chini. Sisi hapa watatu hatukukuona, isipokuwa tutakupa nafasi maana kwa kweli hatukukuona.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu 40, *sub vote 4001* inahusu *Constitutional Affairs*, Mambo ya Katiba. Nilipokuwa nikichangia asubuhi nilizungumza kwamba iko haja ya Wizara kufikiria kuanzishwa kwa Mahakama ya Katiba ambayo itashughulikia pamoja na mambo mengine, lakini kero, manung'uniko au mambo yanayobishaniwa katika pande mbili za Muungano na pia kwa kuwa kunakuwa na msongamano mkubwa wa kesi baada ya uchaguzi, basi na kesi zote za uchaguzi zihamishiwe kwenye Mahakama ya Katiba. Wakati Mheshimiwa Waziri anafanya majumuisho sijapata maelezo yoyote kuhusu suala hili. Ningombwa nipate maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili katika sehemu hiyo hiyo ya Katiba nilizungumza kwamba kutokana na hali ya siasa za Zanzibar zilivyo, basi katika kujenga mazingira mazuri ni vyema Wizara ikafikiria kurekebisha Katiba ili kuwe na Serikali ya pamoja kuanzia chaguzi zinazokuja, kuanzia 2005, sikupata maelezo yoyote. Naomba maelezo.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimjibu Mheshimiwa Ali Said Salim, maswali yake mawili, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge alichangia katika hayo maeneo mawili, lakini lile la kwanza la Serikali ya Mseto nililijibu.

MHE. ALI SAID SALIM: Bado.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Nililijibu.

MWENYEKITI: Alijibu, pengine ulikuwa hujaingia.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili napenda tu nimuelekeze Mheshimiwa Mbunge kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 125 mpaka 128. Maeneo haya ya sehemu ya saba ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano yanaweka uwezekano wa kuundwa kwa Mahakama maalum ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na majukumu haya yameainishwa, lakini lengo lake hasa ni pale ambapo kunakuwa na kitu kinachobishaniwa kati ya Serikali zetu mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa upande mmoja na Serikali ya Mapinduzi. Kwa hiyo, kwa maana ile alioisema kwamba ifanye shughuli hizi tayari Katiba imeweka utaratibu huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na wazo kwamba Mahakama ya Katiba hiyo aliyokuwa nayo katika mawazo yake ifanye pia kusikiliza kesi za uchaguzi. Tunasema itakuwa ni *superfluous* kwa sababu Katiba hii hii imeipatia Mahakama Kuu jukumu hilo la kusikiliza kesi za uchaguzi kwa ngazi hiyo ya Wabunge. Kwa hiyo na lenyewe halina utata la kutaka kuwepo na chombo kingine kufanya kazi hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimeyajibu yote sasa. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 55 -Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

Kifungu 1001 - *Administration and General* 2,153,000,100/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 59 - Tume ya Kurekebisha Sheria

Kifungu 1001 - *Administration and General* 501,459,100/=

Fungu 64 - Mahakama ya Biashara

Kifungu 1001- *Administration and General* 611,252,400/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 90 - Mahakama ya Ardhi

Kifungu 1001 - *Administration and General* 459,023,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 40 - Mahakama

| | |
|---|-----------------|
| Kifungu 2001 - <i>High Court</i> | 400,000,000/= |
| Kifungu 2002 - <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i> | 1,000,000,000/= |
| Kifungu 2011 - <i>Primary Courts</i> | 1,050,000,000/= |
| Kifungu 2012 - <i>District Courts</i> | 150,000,000/= |
| Kifungu 2013 - <i>Kagera Zone</i> | 100,000,000/= |
| Kifungu 2015 - <i>Moshi Zone</i> | 2,700,000,000/= |

(*Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 41 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kifungu 1001 - *Administration and General* 4,433,455,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 - Mahakama ya Biashara

Kifungu 1001 - *Administration and General* 152,500,000/=

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba kwa mwaka wa fedha 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali Makadirio haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofisi*)

WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba
kwa mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge kuna tangazo moja dogo. Mheshimiwa Maria Watondoha, anaomba Waheshimiwa Wabunge wote mbaki humu kwa dakika kama tano baada ya kuahirisha Bunge anataka kuelezea kuhusu Usiku wa Mwanawake wa Tanzania. Baada ya tangazo hilo dogo...

WABUNGE FULANI: Ni wanawake tu au wote?

NAIBU SPIKA: Ni Waheshimiwa Wabunge wote, siyo wanawake tu, yanawahuhsu wanawake, lakini Wabunge wote wabaki. Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.33 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi
tarehe 22 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*